# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

**Kikao cha Arobaini na Tano – Tarehe 12 Juni, 2017**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2016 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 pamoja na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na Mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2016, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2017/2018

pamoja na Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea. Katibu.

**NDG. LAWRANCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Kipindi cha maswali na swali letu la kwanza, swali 364 linaelekezwa Ofisi ya Waziri Mkuu na linaulizwa na Mheshimiwa Ester Michael Mmasi. Kwa niaba yake linaulizwa na wajina wake, Mheshimiwa Ester Mahawe.

Na. 364

### Juhudi za Serikali Kuinua Kiwango cha Ajira Zisizo Rasmi

**MHE. ESTER A. MAHAWE (K.n.y. MHE. ESTER M. MMASI)** aliuliza:-

Serikali imekuwa na juhudi mbalimbali za kuinua kiwango cha ajira zisizo rasmi nchini.

Je, nini mpango wa Serikali katika kuwawezesha vijana wahitimu waweze kuingia rasmi kwenye sekta ya kilimo na ufugaji?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu Swali la Mheshimiwa Ester Michael Mmasi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali katika kuwawezesha vijana wahitimu waweze kuingia rasmi kwenye sekta ya kilimo na ufugaji ni kama ifuatavyo:-

(i) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kutekeleza mkakati wa Kitaifa wa kukuza ujuzi nchini ambao umelenga kutoa mafunzo ya kukuza ujuzi kwa wahitimu, wakiwemo wale wanaopenda kujiunga katika kilimo na ufugaji. Kupitia programu hii ofisi yangu imetenga fedha kuwezesha vijana, wakiwemo wahitimu, kupatiwa mafunzo ya kilimo cha kutumia kitalu nyumba *(green house).* Mafunzo haya yatafanyika katika Mikoa yote Tanzania Bara na tayari tumetoa maelekezo kwa Ofisi za Mikoa kuhamasisha vijana kujiunga katika vikundi kwa lengo la kuwawezesha kupatiwa mafunzo hayo katika maeneo maalum yaliyotengwa na mikoa yao kwa shughuli za vijana.

(ii) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuboresha mazingira bora ya uwekezaji katika sekta zenye uwezo mkubwa wa kuzalisha ajira, hususan kilimo biashara. Aidha, katika hili Serikali itajikita zaidi kuhamasisha na kuwezesha uwekezaji kwenye viwanda vidogo vidogo, vya kati na vikubwa, ili kufikia lengo la asilimia 40 ya nguvu kazi nchini kuwa katika sekta ya viwanda ifikapo mwaka 2020. Kupitia Mpango wa Pili wa Maendeleo wa miaka mitano, mwaka 2016/2017 na mwaka 2020/2021.

(iii) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendelea kuimarisha utekelezaji wa mfumo wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na mifuko mingine ya uwezeshaji wa wananchi kiuchumi, ambayo inalenga kuwasaidia vijana kuweza kujiajiri na kuajiri wenzao kwa kuwapa mikopo yenye masharti nafuu na mafunzo ya ujasiriamali kupitia kwenye *SACCOS* za Vijana ambazo zimesajiliwa. Aidha, Serikali kupitia Halmashauri zote nchini inaendelea kuhamasisha kutengwa kwa asilimia tano ya mapato yake kwa ajili ya kuwakopesha vijana, ili kujiajiri na kuajiri vijana wengine.

**MHE. ESTER A. MAHAWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wahenga wanasema samaki mkunje angali mbichi. Nakumbuka zamani tulikuwa tunajifunza masomo ya kilimo katika shule za msingi na

sekondari nchini, lakini kwa bahati mbaya sana masomo hayo yakafutwa. Sasa labda tupate Kauli ya Wizara ya Elimu ni kwa nini masomo haya yalifutwa na tunategemea vijana baada ya kumaliza vyuo vikuu ndio wanaoweza kupata sasa ajira kupitia kilimo na ufugaji wakati hawakuandaliwa tangu mwanzo?

Swali la pili ambalo linasema ni maeneo gani hasa yaliyoandaliwa na yaliyotengwa kwa ajili ya kilimo kwa ajili ya vijana hawa wanapohitimu masomo yao ya Vyuo Vikuu na kukosa ajira katika maeneo mengine? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajibu swali la pili, la kwanza atajibu Mheshimiwa Waziri wa Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ameuliza kama kuna maeneo ambayo yamekwishakutengwa kwa ajili ya shughuli hizi za vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2014 Novemba, Ofisi ya Waziri Mkuu ilifanya kikao na Wakuu wa Mikoa wote wa nchi nzima hapa Dodoma. Katika kikao hicho iliamuliwa kwamba kila Mkoa uende kutenga maeneo maalum ambayo tutayaita *Youth Special Economic Zones,* ni Ukanda Maalum wa Uchumi kwa ajili ya Vijana, lengo lake ni kuwafanya vijana hawa wahitimu na vijana wengine wote wa Kitanzania ambao wangependa kufanya shughuli ya ujasiriamali, lakini wanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa maeneo ili kupitia utaratibu huu waweze kupatiwa maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka hivi sasa tayari Mikoa mingi imekwishatenga maeneo haya na zimekwishatengwa tayari ekari 85,000 nchi nzima kwa ajili ya shughuli za vijana.

**MWENYEKITI:** Waziri wa Elimu Mheshimiwa Profesa Ndalichako.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Ester Mahawe, kuhusiana na Serikali kufuta masomo ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali haijafuta masomo ya kilimo, masomo ya kilimo bado yanafundishwa shuleni na hata katika matokeo ya wanafunzi wanaoenda Kidato cha Tano ambayo Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI ameyatangaza juzi wapo wanafunzi waliochaguliwwa kwenda kusoma *combination* zenye kilimo. Vilevile Serikali na Chuo Kikuu Maalum cha Kilimo cha Sokoine na Serikali ina mpango wa kuendelea kuimarisha masomo ya kilimo katika ngazi zote ikiwa ni pamoja na kuongeza udahili katika vyuo vikuu kwa sababu tunatambua kwamba, kilimo ndio uti wa mgongo wa maendeleo ya Taifa hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Khenani, nitende haki halafu Mheshimiwa Lyimo halafu Mheshimiwa Richard.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Kwa kuwa swali la msingi linazungumzia ajira kwa vijana, kumekuwa na utaratibu wa baadhi ya makampuni kuajiri watu kutoka nje, yakiwemo makampuni ya ulinzi na kuwafanya vijana wa Kitanzania kutengwa kuonekana kwamba, wao hawana uwezo.

Je, Serikali haioni kuendelea kuajiri watu kutoka nje ni kuweka nchi yetu hatarini, badala ya kuajiri vijana wa Kitanzania?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, imetungwa Sheria ya Uratibu wa Ajira kwa Wageni ambayo na sisi kama Wizara, tunaisimamia. Nataka nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika utekelezaji wa sheria hii tunahakikisha nafasi

nyingi sana zinashikwa na wazawa, ili kuweza kulinda ajira za Watanzania. Kama kuna jambo lolote limetokea kinyume chake hapo, basi tutaelekeza Maafisa wetu wa kazi waende kufanya ukaguzi na wale wote ambao wameingia kinyume cha utaratibu waweze kuchukuliwa hatua ili vijana wetu waweze kupata nafasi za ajira.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lyimo halafu Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba uchumi wa nchi yetu ungekua zaidi kama tungewekeza kwenye kilimo, lakini tunaona kwamba kilimo chetu kinaendelea kuporomoka. Huko nyuma kilikuwa kinaingiza asilimia nne, lakini sasa hivi kimeshuka mpaka asilimia 1.7. Sasa nilikuwa naomba kujua Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba, vijana hawa wanajiajiri kwenye mashamba ili kuweza kukuza uchumi wetu? Kwa sababu vijana wapo wamezagaa, lakini mapori, mashamba yako makubwa, lakini hakuna chochote kinachoendelea. Je, Serikali kupitia ofisi yako ina mkakati gani?

**MWENYEKITI:** Ahsante umeeleweka. Mheshimiwa NaibuWaziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu tumeandaa mpango mkakati wa Kitaifa, *it is a national strategy* ya kuwaingiza vijana katika kilimo. Katika mpango huu malengo makubwa ni kuyatumia yale mashamba makubwa ya Serikali ambayo hayatumiki kwa ajili ya shughuli za kilimo kwa vijana.

Kwa hiyo, tunaamini kabisa katika mpango huu kwa muungano huu kati ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Kilimo, tutafanya kazi pamoja ili maeneo haya sasa tuweze kuwapatia vijana wa nchi hii wakafanye shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikisema, narudia mara nyingine tena leo ya kwamba moja kati ya kazi ambayo tunaanza nayo mapema kabisa tumeamua katika eneo la Mkulazi na Mbigili pale Morogoro ambako Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya *NSSF* na *PPF* wanakwenda kujenga Kiwanda cha Sukari tutawafanya vijana wa nchi hii kuwa ndio *out growers* ambao watasaidia kulima miwa kwa ajili ya kukilisha kiwanda. Kwa hiyo, tunaamini kabisa kwa kupitia mkakati huu vijana wengi zaidi watapata ajira na waweze kujiajiri.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Asilimia 67 ya Watanzania wako kwenye ajra ya kilimo na kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu kuna mikopo inayotolewa na ndani ya Halmashauri tunatenga asilimia tano kwa ajili ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua upande wa Serikali ni lini watabadilisha hiyo sheria ili ukomo wa umri kwa vijana katika kukopa usiwepo kwa sababu, kumekuwa na changamoto, wengine wamefikia miaka 45 miaka 50, lakini bado wanahitaji mikopo, lakini wanakwamishwa na suala la umri. Ni lini Serikali itabadilisha hiyo sheria?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kuhusu lini tutabadilisha umri, hili ni suala la kisera. Siwezi kulisema hapa moja kwa moja, lakini *definition* ya kijana si ya Tanzania peke yake ni *definition* ya kidunia na sisi tunakwenda katika *definition* ambayo inazungumzwa na *ILO,* lakini kama kuna mahitaji hayo nafikiri baadae, kupitia sera na mahitaji mbalimbali, jambo hilo linaweza likaangaliwa upya, lakini kwa sasa bado tunabaki kuwa na umri huo kuanzia miaka 15 mpaka 35.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la uwezeshaji; kwenye uwezeshaji ukiacha Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ambao ndio una-*limit* umri, mifuko mingine bado iko zaidi ya mifuko 19 ya uwezeshaji ambayo yenyewe haiangalii umri. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Mbunge uendelee tu kuwapa elimu wananchi waelewe mifuko mingine ya uwezeshaji ili waweze kuitumia kwa ajili ya kuweza kujiwezesha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali linalofuata namba 365 linaulizwa na Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 365

**Fedha kwa Ajili ya Ujenzi wa Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino**

**MHE. FELISTER A. BURA** aliuliza:-

Mkandarasi anayejenga Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino anaidai Serikali shilingi bilioni tatu kwa ajili ya kukamilisha jengo la Halmashauri.

Je, ni lini Serikali itamlipa mkandarasi huyo kiasi hicho cha fedha ili ujenzi huo uweze kukamilika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum, kutoka Mkoa wa Dodoma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, madai ya Mkandarasi aliyejenga Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, mpaka sasa ni shilingi milioni 758.2 yakiwemo madai yaliyohakikiwa ya shilingi milioni 368.0 na madai ambayo hayajahakikiwa ya shilingi milioni 390.2 ambayo yanaendelea

kufanyiwa kazi. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri hiyo imepokea shilingi milioni 700 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi. Vilevile katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 600 kwa ajili ya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zinapaswa zitumike kulipa deni ambalo Mkandarasi anadai kabla ya kuendelea na kazi nyingine. Serikali itaendelea kutenga fedha kila mwaka ili kuhakikisha ujenzi wa jengo hilo la Halmashauri unakamilika.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Bura maswali ya nyongeza.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino ilianzishwa zaidi ya miaka Kumi iliyopita na Halmashauri hii Makao yake Makuu yako karibu sana na Chamwino Ikulu. Kwa hiyo, nilitegemea Serikali ingeliangalia hili suala kwa jicho la kipekee kabisa. Idara za Halmashauri hii zimetawanyika, ukitoka Ofisi ya Mkurugenzi hadi Ofisi ya Ardhi ni kilometa tano.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa uliza swali.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitoka Ofisi ya Mkurugenzi hadi Idara nyingine ambazo nyingine ziko kwenye shule za msingi, nyingine ziko kwenye nyumba za watu binafsi kwa hiyo, ufanyaji kazi na huduma kwa wananchi uko katika hali ngumu kabisa kutokana na jengo lile kutokamilika. Halmashauri waliwafuata *TBA* wakafanya tathmini wakaona kwamba, zinahitajika shilingi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa uliza swali! Wamekuelewa, uliza swali.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa shilingi bilioni 2.3 na Serikali imetenga shilingi milioni 600 tu kukamilisha lile jengo.

Je, ni lini sasa Serikali itatoa fedha za kutosha kwa ajili ya lile jengo la Halmashauri na likamilike kwa wakati, japo *floor* ya chini, ili watumishi wahamie wakafanye kazi pale?

Swali la pili, Halmashauri ya Chemba iliomba shilingi milioni 950 kwa mwaka huu wa fedha na wamepata shilingi milioni 450 tu. Je, shilingi milioni 500 zilizobaki watapata lini ili waendelee na ujenzi wa jengo la Halmashauri?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu ya hayo maswali kwa kifupi tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, watumishi wa Halmashauri ya Chamwino wanapata shida kubwa sana na hili tunalijua wazi. Ninajua kwamba mkataba wa kwanza wa mkandarasi wa kwanza umevunjwa lakini *commitment* ya Serikali iko pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali mpaka hivi asubuhi na-*cross check* pale tumeshapeleka shilingi milioni 750 hivi sasa. Kama ulivyosema tathmini iliyofanywa na *TBA* imeonekana kumaliza lile eneo la *ground floor* peke yake karibu ni shilingi bilioni mbili. Hata hivyo, nimeongea nimeongea na Kaimu Mkurugenzi pamoja na *Engineer* leo wafike ofisini kwangu kuangalia *way forward* tunafanyaje kwa sababu tathmini iliyofanywa gharama yake ni kubwa, lakini *Engineer* na timu yake wanasema kwa kutumia wao utaalamu wao pale ile shilingi milioni 750 wataweza kumaliza ile *ground floor* na hivi sasa tunajielekeza kuangalia jinsi gani fedha zitumike vizuri.

Kwa hiyo, nimemuagiza Kaimu Mkurugenzi na *Engineer* leo hii wanakuja kukutana na wataalam katika ofisi yetu tuangalie tufanye nini ili tumalize ile *ground floor.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la ujenzi pale Chemba, ni kweli tumepeleka shilingi milioni 500 mpaka hivi sasa, tunachotaka kufanya ni kuhakikisha kwamba, fedha tunazipeleka maeneo haya na maeneo mengine tofauti, lengo kubwa ofisi hizi ziweze kukamilika na watumishi wetu wapate maeneo mazuri ya kufanya kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililopo Chamwino ndiyo tatizo lililopo Manispaa ya Tabora. Ofisi mpya ya Halmashauri imekwama kwa muda mrefu sasa kukamilika kwa sababu ya ukosefu wa fedha. Kwa kuwa ombi maalum kupitia Hazina Serikali iliahidi kutoa shilingi bilioni mbili ili kuweza kukamilisha ujenzi huo pamoja na kumlipa mkandarasi anayedai karibu shilingi bilioni moja *Masasi Construction.*

Je, Serikali ni lini italeta pesa hiyo kwenye Halmashauri ya Manispaa ya Tabora ili jengo hili liweze kukamilika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Lini mtatoa pesa hizo ili jengo likamilike? Basi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli lilikuwa ombi maalum, lakini tutaenda kulifanyia kazi. Siwezi kutoa *commitment* hapa lakini tutaenda kulifanyia kazi tuangalie kwamba lile ombi la awali limefikia wapi halafu tutapeana mrejesho nzuri na Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu najua ni kweli Manispaa ya Tabora wanapata shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tutakwenda kuangalia jinsi gani tutafanya.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ntimizi.

**MHE. MUSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la Halmashauri ya Chamwino linafafana na tatizo la Halmashauri ya Tabora Uyui. Tuna zaidi ya miaka kumi tumeamia Isikizya, lakini jengo la Halmashauri yetu lina zaidi ya miaka mitano halijakamilika kutokana na kutoletewa pesa.

Je, ni lini Serikali itatusaidia ili kumalizia ujenzi wa jengo hilo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo ni kwamba maombi haya ya Halmashauri yako katika maeneo mbalimbali na ni kweli Mheshimiwa Mbunge nimefika kwako Uyui tulikuwa pamoja siku ile, kikubwa zaidi tutaangalia kipindi hiki kutokana na bajeti zilizotengwa katika mahali ambapo pesa ambazo hazijapelekwa basi tutafanya harakati ziwezekanazo mradi tuweze kupeleka fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niweze kusema kwamba *commitment* ya Serikali ni kuhakikisha kwamba kama tulivyofanya mwaka huu hivi sasa tumepeleka takriban bilioni 30 kwa Halmashauri mpya na Halmshauri mbalimbali kwa hiyo tutajitahidi kwa kadri iwezekanavyo kuwezesha mpango huu wa Serikali ambao tumeupanga katika bajeti zetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea na swali 366 linaulizwa na Mheshimiwa Sixtus Raphael Mapunda, Mbunge wa Mbinga Mjini.

Na. 366

**Kukamilisha Jengo la Mkuu wa Wilaya ya Mbinga**

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA** aliuliza:-

Kwa zaidi ya miaka kumi sasa Serikali imejenga jengo la ghorofa moja kwa ajili ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mbinga lakini jengo hilo bado halijakamilika, ujenzi umesimama kwa muda mrefu hali inayosababisha jengo hilo kuharibika na kuanza kupoteza ubora wake.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa jengo hilo?

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sixtus Raphael Mapunda, Mbunge wa Mbinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukamilisha ujenzi wa jengo la Ofisi ya Wilaya ya Mbinga, Serikali imetenga shilingi milioni 250 katika bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018. Fedha hizo zitatumika kukamilika ujenzi wa tanki la maji, uwekaji wa mfumo wa maji safi na maji taka, ujenzi wa uzio, ufungaji wa mfumo wa umeme,vifaa vya kuzuia moto, upigaji rangi na kukamilisha kazi ya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwasihi kwamba fedha hii itakapotolewa wahakikishe jengo hili linakamilika na kuanza kutumika mara moja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mapunda swali la nyongeza.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze Serikali kwa kutenga hiyo milioni 250 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya. Kutenga fedha ni jambo moja na kulipeleka ni jambo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba mwaka wetu wa bajeti unaanza mwezi Julai, unaisha mwezi Juni, kuchelewa kuipeleka hiyo pesa kwa namna yoyote ile kutaathiri ujenzi wa hilo jengo hasa ikizingatiwa gharama zinaweza zikabadilika.

Je, Serikali inawahakikishia vipi wananchi wa Mbinga kwamba pesa hii itakwenda kwa wakati na ndani ya mwaka wa bajeti wa 2017/2018 jengo likatakamilika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge mwenyewe na wananchi wa Mbinga, kwa sababu Mbunge unakumbuka ulikuja mpaka ofisini kwangu kwa shida kubwa sana za Jimbo lako na eneo lako. Mwaka huu umepambana mpaka umepata shilingi milioni 250 ambayo kutokana na maombi yako tumeiweka katika bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni *commitment* ya Serikali, kwamba tutakapofika mwezi wa Saba mpaka kipindi ambacho tutakachoenda nacho hicho sasa nikuhakikishe kwamba Serikali itajitahidi kwa kadri iwezekanavyo *In Shaa Allah,* tutajitahidi fedha zitaenda na nikuombe kwamba usimamizi uwe karibu kama ulivyokuwa makini jengo hilo liweze kukamilika kwa ajili ya wananchi wa Mbinga.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Selasini atafuatiwa na Mheshimiwa Sakaya.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwwenyekiti, Serikali inapochelewesha kupeleka fedha ambazo ziko kwenye bajeti kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi mbalimbali za Serikali kama Ofisi za Wakuu wa Wilaya na za Halmashauri inasababisha *variation* katika ujenzi wa ofisi hizi na kwa sababu hiyo Serikali inaingia katika matumizi makubwa zaidi katika kumalizia.

Je, kwa nini Serikali isitoe kwa mkupuo fedha hizo ofisi hizo zikamalizika zote kwa pamoja ili Halmashauri pamoja Wilaya hizo zikawa na ofisi na Serikali ikaokoa kiasi kikubwa cha fedha kwa njia ya *variation?*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo la Mheshimiwa Selasini ni wazo zuri na ndiyo maana nimesema mwaka huu tumetoa karibu shilingi bilioni 30 kwa ajili ya ujenzi huo, lakini unaangalia jinsi gani kila sehemu ina eneo lake la kimkataba la ujenzi. Ndiyo maana hapa tukusema kila Mbunge ataanza kupinga kelele.

Kwa hiyo, ni wazo zuri tutaenda kulifanyia kazi lengo kubwa ni kwamba tumalize haya matatizo yote ya ofisi wananchi na wataalam wetu waweze kupata huduma kwa hiyo ni wazo zuri na Serikali tunaendelea kupeleka fedha kwa kadri tunavyokusanya na mimi naamini kwamba utafika muda ofisi nyingi zitakamilika na Watendaji wetu watakuwa katika mazingira mazuri ya kufanya kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Magdalena Sakaya halafu Mheshimiwa Ndaki wa mwisho.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kaliua haina Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Wilaya anatumia Ofisi ya Tarafa ambayo ina hali mbaya na ni chumba kimoja kidogo

wanajibana pale. Ofisi ya Wilaya imeanza kujengwa tangu mwaka 2012 na imesimama mwaka 2014 mpaka leo haijaendelezwa. Naomba kujua Serikali ina mpango gani wa kutoa fedha ya kutosha ili Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ikamilike na Mkuu wa Wilaya aweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, ni lini mtapata pesa mkamilishe?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, alichosema Mheshimiwa Sakaya ni kweli na ndiyo maana nimesema kwamba sasa hivi tunajitahidi kupeleka fedha na hata katika Halmashauri yake anafahamu tumeshapeleka milioni 700 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Halmashauri Kaliua. Hiyo ni *commitment* ya Serikali kwa Kaliua. Angalia kipindi hiki cha muda mfupi tumepeleka shilingi milioni 700 lakini najua Ofisi ya *DC* bado haijakamilika. Hii tunalichukua kuangalia jinsi gani tumefanya *allocation* ya *funds* niangalie kama Kaliua katika suala la jengo la Mkuu wa Wilaya hali ikoje halafu tutasukuma ili jengo liweze kukamilika. Ofisi hizi zilisimama muda mrefu na sasa hivi nimetoa *commitment* kubwa ya Serikali kupeleka kwa ajili ya umaziaji wa majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo usiwe na mashaka Dadangu tutajitahidi kwa kadri iwezekanavyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ndaki.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kuuliza swali ndogo tu la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jengo la Mkuu wa Wilaya ya Maswa limeshajengwa lakini limebakia umaliziaji. Mheshimiwa Naibu Waziri alishafika hapo na kuliona sasa anaweza kutuhakikishiaje kwamba mwaka unaoanza wa fedha, fedha kidogo kwa ajili ya umaliziaji zimetengwa ili Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Maswa aweze kuhamia kwenye jengo hilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. Ni lini *DC* atahamia kwenye jengo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge mwaka huu wa fedha unaokuja tutamaliza lile jengo la Mkuu wa Wilaya, tuna kila sababu kuhakikisha Wakuu wa Wilaya wetu majengo yao yote yanakamilika na tumejipanga katika hilo, Mheshimiwa Ndaki wala usihofu tutajitahidi kwa kadri iwezekanavyo ile kazi kubwa iliyobakia pale tuweze kuiimaliza ili Mkuu wetu wa Wilaya afanye kazi katika mazingira rafiki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante tunaendelea na Waheshimiwa Wabunge, swali namba 367 litaulizwa na Mheshimiwa Ally Seif Ungando, Mbunge wa Kibiti kwa niaba yake Mheshimiwa Ulega.

Na. 367

**Semina, Vyombo vya Uvuvi na Mikopo kwa Wavuvi**

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA (K.n.y MHE. ALLY S. UNGANDO)** aliuliza:-

Asilimia 90 ya wakazi wa Delta ya Mto Rufiji katika Kata ya Salale, Maparoni, Mbuchi na Kiangoroni ni wavuvi ambao hutumia mitumbwi isiyo na mashine na ndilo eneo pekee katika mwambao wa Bahari ya Hindi kunapatikana samaki aina ya kamba *(prawns)* kwa wingi; na kwa kuwa Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya mwaka 2015 imeazimu kuwapatia wavuvi wadogo wataalam, vifaa vya kisasa vya uvuvi ili wajiendeleze na kuongeza Pato la Taifa.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia wananchi wa maeneo hayo semina kuhusu uvuvi bora wa kisasa?

(b) Kwa kuwa mikopo hutolewa kwa vikundi

mbalimbali; je, Serikali itatoa mikopo kwa vikundi vya uvuvi vilivyopo kwenye maeneo hayo?

**MWENYEKIITI:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Olenasha.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ally Seif Ungando, Mbunge wa Kibiti lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imekuwa ikitoa mafunzo ya uvuvi endelevu kwa wavuvi kupitia semina, warsha, vipeperushi, makala, redio na luninga kwa kushirikiana na Halmashauri na wadau mbalimbali. Katika kusambaza teknolojia mbalimbali za uvuvi, katika mwaka 2016/2017, Wizara ilirusha hewani vipindi saba vya redio na kimoja cha luninga vilivyohusu Wakala wa Mafunzo *(FETA)*. Ukuzaji viumbe kwenye maji, uzalishaji bora wa samaki, mbinu za kutambua magonjwa ya samaki na uvuvi endelevu. Aidha, vipindi 19 vilirushwa hewani kwa lengo la kuwaelimisha vijana na kuwajengea uwezo wa kuingia katika uvuvi. Pia Wizara imechapisha nakala 1,000 za mwongozo wa ugani katika Sekta ya Uvuvi kwa lengo la kutoa elimu kwa wavuvi na wakuzaji viumbe kwenye maji.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza mpango wa kutoa ruzuku kwa wavuvi ambayo inalenga kuwasaidia wavuvi kupata zana bora na vifaa vya kuvulia zikiwepo injini za boti kwa utaratibu wa uchangiaji ambapo wavuvi watangaia asilimia 60 ya gharama na Serikali itatoa asilimia 40. Katika awamu ya kwanza jumla ya *engine* 73 zimenunuliwa na vikundi 27 kutoka Ukanda wa Pwani katika Halmashauri za Bagamoyo, Mafia, Lindi, Manispaa, Mtwara Mikindani, Temeke, Mkinga, Muheza na Tanga Jiji vimekidhi vigezo. Hivyo, napenda nitumie fursa hii kumuomba Mheshimiwa Mbunge ahimize wavuvi katika Halmashauri ya Kibiti kujiunga katika vyama vya Ushirika vya Msingi ili waweze

kutumia fursa hii kwa kuwa mpaka sasa hakuna kikundi kutoka Wilaya ya Kibiti au hata jirani Wilaya ya Rufiji kilijitokeza kuomba zana za uvuvi za ruzuku.

Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la *WWF* pamoja na Halmashauri ya Rufiji imewezesha wavuvi kuanzisha *VICOBA* 36 vyenye jumla ya wavuvi 829 na kupewa mafunzo ya ujasiriamali. Pia, Wizara kupitia Mradi wa Usimamaizi wa Uvuvi na Maendelea Shirikishi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (*SWIOFish)* inaandaa Mpango kazi utakaokuwa na program za vipindi mbalimbali kuhusu usimamizi endelevu wa rasilimali za uvuvi ambazo zitarushwa katika televisheni na radio mbalimbali. Wavuvi wa nchi nzima wakiwemo wa Kibiti watanufaika na elimu itakayotolewa kupitia mpango kazi huo.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ulega.

**MHE. ABDALLAH H. ULEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu haya ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu katika majibu ya msingi ameeleza kwamba Wilaya za Kibiti, Rufiji na Wilaya yangu ya Mkuranga ni miongoni mwa Wilaya ambazo wavuvi wake hajaomba mikopo. Inawezekana kabisa kutokuombwa kwa mikopo hii ni kutokana na ukosefu wa elimu ya kuweza kuwafahamisha na kuwawezesha waweze kuwa na uelewa wa kuomba hii mikopo.

Sasa swali langu, naomba Mheshimiwa Naibu Waziri aniambie moja kwa moja ni lini tunaweza tukashirikiana sisi na wao ili kwa haraka zaidi Watanzania hawa wa Kisiju, Kibiti Delta na Rufiji mpaka Bagamoyo waweze kutumia fursa hii ya mikopo inayotolewa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu majibu kwa kifupi tu maana jibu lako ni refu na lina majibu yote.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ulega siyo mgeni sana kwenye Ofisi ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, kwa hiyo, naendelea kumkaribisha amekuja mara nyingi sana kufuatilia changamoto za wananchi wake, aje ofisini hata akitaka leo mchana tuongee na tuangalie namna ya kufikisha elimu hii kwa ukubwa zaidi kwa sababu tayari Halmashauri zinatakiwa zitoe elimu kwa wavuvi na kuwafahamisha kwamba kuna fursa hiyo. Kama nilivyosema niko tayari kukaa naye tuweke mkakati wa kupeleka elimu zaidi.

**MWENYEKITI:** Mwisho Dkt. Semesi.

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wavuvi hata ho wa maeneo ya Rufiji na maeneo mengine wanaojishughulisha kwa mambo ya uvuvi wametengeneza *Beach Management Units* na hizi *BMUs* zina uongozi. Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa Wizara ya Kilimo pamoja na Halmshauri husika wakawa wanaviongezea nguvu hizi *Beach Managementi Units* kwa kuwasaidia kielimu hata na masuala ya kifedha?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama anavyosema vikundi vya usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika mwambao au tunaziita *Beach Management Units* ni kweli imekuwa ni fursa ambayo inaweza ikatumika katika kutoa elimu, lakini vilevile kutoa misaada mbalimbali ambayo inaweza ikawasaidia wavuvi kufanya shughuli za uvuvi katika utaratibu ambao ni endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wowote ambao Serikali imetoa elimu tumetumia sana *Beach Management Unit*, Serikali ndiyo imesaidia kuzianzisha lakini niendelee kumsihi Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote kujaribu kuhimiza Halmashauri zao ambao kimsingi wao

wanakaa kwenye Baraza la Madiwani kuendelea kutoa elimu kwa kupitia *Beach Management Units* lakini vilevile kuhakikisha kwamba tunatenga raslimali kwenye halmashauri zetu ili hiyo elimu iweze kutolewa kwa urahisi zaidi.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipa nafasi niweze kusema kuuliza swali moja la nyongeza.

Tunatambua kwamba katika kupambana na uvuvi haramu hawa *Beach Management Units* wamekuwa wakisaidia sana, lakini kwa bahati mbaya sana walikuwa hapati kipato cha moja kwa moja, kwa hiyo wakati mwingine wanageuka wao nao kushiriki katika uvuvi haramu.

Je, ni lini Serikali itaanzisha huu ufugaji wa samaki kwa njia ya *cage* ambao utakuwa unawapatia vile vikundi wa *Beach Management Units* kipato cha ziada ili waendelee kutunza maeneo yetu haya ya Uvuvi?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue kwanza nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mathayo kwa sababu amekuwa mmoja kati ya Wabunge ambao wamejitahidi sana kuhakikisha kwamba wavuvi wao wanaingia katika ufugaji wa samaki vilevile uvuvi ambao ni endelevu, tunatambua jithata hizo zimezaa matokeo mazuri sana kwani katika eneo analotoka uvuvi haramu umepungua sana. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba ufugaji wa samaki kwenye vizimba *(cage culture)* ni moja kati ya aina ufugaji wa sasa ambao Serikali imeamua kuhimiza wananchi wajihusishe nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inachofanya ni kutoa elimu pamoja na kuweka mazigira wezeshi ambayo wavuvi mbalimbali wanaweza wakajihusisha katika *cage culture* kwa hiyo katika *BMUs* lakini vilevile kwa wavuvi mmoja

mmoja kama kuna ambao wanataka kuingia katika ufugaji wa samaki katika vizimba Wizara yangu iko tayari kushirikiana na Halmashauri wanazotoka ili kutoa elimu ya njia sahihi ya kuweza kufanya ufugaji wa samaki kwenye vizimba.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sakala.

**MHE. SAUMU H. SAKALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali moja la nyongeza. Katika jibu la msingi la Mheshimiwa Waziri ametaja Wilaya ambazo zitapata fursa wavuvi hao Wilaya ya Pangani hakuitaja. Sasa ningependa kufahamu wana mpango gani na wavuvi wa Pangani hasa ukizingatia nao pia kuna uvuvi wa *prawns,* lakini pia wamesahaulika sana katika elimu, kitu ambacho wangeweza kupata elimu wangeweza kupata hiyo mikopo ambayo ingewasaidia katika suala zima la uvuvi. Ahsante *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ni lini Pangani?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, orodha ya Halmashauri au Wilaya ambazo nimetaja ni zile ambazo tayari zimeshanufaika na mpango huo wa wavuvi kupatiwa asilimia 40 ya fedha kwa ajili ya kununua vifaa vya uvuvi hasa injini za boti. Kwa hiyo, ninachosema mpango huu upo na unapatikana kwa Halmashauri zote ili mradi wenyewe wajipange na wakidhi vigezo halafu tutaoa asilimia 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Pangani, mimi nimefika Pangani na watu wa Pangani nawapenda sana, Mheshimiwa Aweso nilikutana naye kule. Kimsingi niliwaahidi kwamba wakijipanga kwenye vikundi, nipo tayari kuwasaidia waweze kupata asilimia hiyo 40. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwambia vilevile mheshimiwa Mbunge wapangeni wavuvi wenu katika vikundi, watafute fedha asilimia 60 halafu baada ya hapo

tutawasaidia kupata hiyo asilimia 40 waweze kununua injini na waweze kufanya uvuvi kwa njia ambayo ni rahisi zaidi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya Washeshimiwa Wabunge tunaendelea na swali linalofuata ambalo linaulizwa na Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Liwale.

Na. 368

**Adha ya Maji katika Mji wa Liwale**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA** aliuliza:-

Mji wa Liwale unakuwa kwa kasi lakini una chanzo kimoja cha maji ambacho kwa sasa hakiwezi kukidhi mahitaji hivyo kusababisha uhaba mkubwa wa maji.

(a) Je, ni lini Serikali itachukua hatua ya kuwaondolea wananchi adha ya upatikanaji wa maji?

(b) Je, mradi wa kumwagilia wa Ngongowele utakamilika lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Jimbo la Liwale, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha huduma ya maji ili kuwaondolea adha wananchi wa Mji wa Liwale, Serikali katika mpango wa muda mfupi imepanga kukarabati na kupanua mtandao wa majisafi, kununua na kufunga dira za maji kwa wateja, kukarabati chanzo cha maji na kukarabati matenki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi hizo zinatarajiwa kuanza mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kiasi

cha shilingi milioni 300 kimetengwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya kazi hizo.Taratibu za kumpata mkandarasi atakayetekeleza kazi hiyo zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mpango wa muda mrefu, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 3.5 katika bajeti wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na uandaaji wa vitabu vya zabuni katika Miji Mikuu ya Wilaya nchini ikiwemo na Mji wa Liwale. Taratibu za kumpata mtaalam mshauri atakayetekeleza kazi hizo zinaendelea. Kukamilika kwa upembuzi na usanifu wa kina kutatoa gharama halisi ya utekelezaji wa mradi mkubwa katika Mji wa Liwale pia idadi ya Kata zitakazonufaika na mradi huo wa maji zitajulikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, skimu ya umwagiliaji ya Ngongowele iliyopo Kata ya Ngongowele, Wilayani Liwale iliibuliwa mwaka 2008. Ujenzi wa skimu hii ulifanyika kwa awamu tatu kati ya mwaka 2009 na 2012 kwa kujenga banio, vigawa maji, kivusha maji, vivuko vya watembea kwa miguu, pamoja na kuchimba mifereji miwili yenye urefu wa jumla wa mita 4,800 ambapo mita 1,080 tayari zimesakafiwa. Aidha, kwa miaka miwili mfululizo 2010/2011 na 2011/2012 skimu hii ilikumbwa na mafuriko makubwa na kusababisha uharibifu wa baadhi ya miundombinu ambayo hata hivyo baadhi imefanyiwa marekebisho ili kudhibiti uharibifu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea na mapitio ya miradi yote ya umwagiliaji hapa nchini ili kubaini mahitaji na gharama za ukarabati ama kujengwa upya. *(Makofi)*

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa ninasikitika tu kwamba hili swali halijajibiwa; kwa sababu hapa nilizopewa ni *story* tu, nimeona hapa zimepatikana *story* tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tatizo letu Liwale ni kwamba Mji wa Liwale unategemea maji kutoka Mto Liwale na Mto Liwale sasa umekauka, kwa hiyo, shida

yetu ni kutafuta chanzo cha pili mbadala cha maji. Sasa hapa Mheshimiwa Waziri anasema kwamba hatua ya awali yaani kwa muda mfupi wanakarabati matenki, wanakarabati chanzo cha maji na wananunua dira. Sasa unakarabati chanzo cha maji, unakarabati vipi? Mto umekauka unaukarabati vipi? Matenki unayokarabati unataka uweke nini na mita unazokwenda kufunga unataka zitoe nini? Hapo naona swali bado halijajibiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, katika muda mrefu wanasema wametenga shilingi bilioni 3.5 lakini hizi shilingi bilioni 3.5 kuna Halmashauri 14 zimewekwa hapa. Kwa nini sasa Mheshimiwa Waziri hajatenganisha kujua kwamba Halmashauri fulani ina kiasi gani maana kuzifumba hapa ni nini?

**MWENYEKITI:** Swali Mheshimiwa…

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili ninalouliza mo wamba, *scheme* ya Umwagiliaji ya Ngongowele itakamilika nini? Nimepewa *story* tu. Sasa nataka nijue hatua gani imefikiwa ili tuweze kupata chanzo cha maji mbadala kwa Mji wa Liwale, hilo ndio swali ambalo naomba niulize. Vilvile naomba nirudie, tunaomba mradi wa Ngongowele ukamilike. Je, Mheshimiwa Waziri upo tayari kwenda na mimi kuangalia huo mradi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri. Waheshimiwa Wabunge msihutubie Bunge, uliza swali tu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utangulizi umesema majibu yote ni *story,* sio *story* ndiyo ukweli ulivyo. Mto Liwale ambao ndiyo chanzo cha maji cha Mji wa Liwale unakauka kiangazi na ndio maana tunaweka sasa upembuzi yakinifu. Lakini nikwambie maana ya ukarabati, ukarabati ni kuongeza uwezo ndani ya huo ukarabati basi tutabaini ni eneo gani sasa baada ya mto kukauka tunaweza tukapata maji ambayo yatahakikisha yanahudumia Mji wa Liwale bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye swali namba moja; hatua tunayoichukua ni kufanya upembuzi yakinifu, upembuzi yakinifu utabaini chanzo cha maji cha kudumu pamoja na huo Mto Liwale. Ikiwa siwezi kuanza kuzungumza utafiti utakaofanyika lakini baada ya kufanyika itabainisha ni wapi tutakuwa na maji ambayo yatakuwepo kwa miezi 12 ama kwa visima ama kwa kujenga bwawa ili yale maji yanapokuwa ni mengi kipindi cha kiangazi tuyapeleke kwenye bwawa tuyahifadhi ili tuweze kuhakikisha kwamba sasa Mji wa Liwale unakuwa na maji mwaka mzima. Ndio hatua tunayoichukua sasa hivi tunachukua hatua ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeuliza swali kuhusu mradi wa umwagiliaji utakamilika lini. Mradi ule ulikamilika, umepata madhara ya mafuriko. Sasa hivi tumepata fedha kutoka Serikali ya Japan, tunapitia miradi yote ambayo ilikuwa imekamilika lakini imepata matatizo mbalimbali yakiwemo ya kukosa maji, unakuta kwamba kilimo kinafanyika mara moja badala ya mara mbili. Kwa hiyo, tunafanya mapitio ya hiyo miradi ikiwemo mradi wako wa Ngongowele ili tuweze sasa kuhakikisha kwamba tunauimarisha ili wananchi waweze kunufaika na kile walichokitarajia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Naelewa ni maji, Mheshimiwa Kangi Lugola, Mheshimiwa Matembe na Mheshimiwa Lucia Mlowe, basi Waheshimiwa.

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na kilio cha muda mrefu cha kutokukamilika mradi wa maji wa Kibara, mradi wa maji wa Bulamba na mradi wa maji wa Nyabehu na hata Mheshimiwa Waziri Mkuu Pinda alifika maeneo yale na Mheshimiwa Maghembe. Sasa nataka kujua miradi hiyo mitatu kwasababu ni zaidi ya miaka nane itakamilika lini kwa sababu Mbunge wao amepiga kelele sasa mpaka hata mate yamenikauka? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ili mate yasikauke zaidi ya hapo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umesema kwamba mradi umechukua miaka nane ni ukweli. Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji tumeianza kwenye bajeti ya mwaka 2006/2007; kwa hiyo, umakta ijumlisha mpaka leo unakuta inakwenda kwenye hiyo miaka saba mpaka miaka nane. Ndani ya hiyo programu tulikuwa na miradi 1810, hadi leo tumeshakamilisha miradi 1333, bado 477. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndani ya hiyo ambayo imebaki ni pamoja na miradi yako Mheshimiwa Mbunge na tumeendelea kutenga fedha na mwaka wa fedha huu tulionao 2016/2017 tuliamua sasa kila Halmashauri kuiwekea bajeti, tukaweka maelekezo kwamba wakamilishe kwanza miradi inayoendelea kabla ya kuingia kwenye miradi mipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe Mheshimiwa Mbunge, kama kuna changamoto yoyote ile ambayo kama Wizara tunaweza kuingilia kitaalam basi naomba tuwasiliane ili tuweze kushughulikia hilo kuhakikisha kwamba miradi hiyo imekamilika.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Matembe.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wanawake wa Mkoa wa Singida wametaabika sana na kero kubwa ya ukosefu wa maji safi na salama kwa muda mrefu sasa. Je, Serikali haioni imefika wakati muafaka wa kuvuta maji kutoka Ziwa Victoria kupitia Igunga hadi Mkoa wa Singida ili kuwaondolea wananchi wa Mkoa wa Singida kero hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri tumetoka Liwale tunaelekea Singida sasa.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikupongeze wewe ni mama na unawapenda akina mama na unajua jinsi wanavyopata shida ya maji. Mkoa wa Singida ni miongoni mwa Mikoa ambayo haina vyanzo vya uhakika vya maji na mabwawa yaliyopo kama Kindai, *Lake Singidani* yote yana maji ya chumvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa mawazo mazuri na sisi tunawaza hilo. Kupitia mradi wa maji wa Ziwa Victoria sasa tunafikisha maji Igunga tunafikiria kwamba tufanyeje kuyatoa pale Igunga tupandishe Mlima Sekenke ili yaje mpaka Singida. Hayo ni mawazo namba moja ambayo na sisi tunayapokea, Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie kwamba tutayafanyia kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Lucia Mlowe swali la nyongeza.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona.

Kwa kuwa katika Mkoa wa Njombe na hasa katika Halmashauri ya Mji wa Njombe kumekuwa na tatizo kubwa sana la maji kwa muda mrefu, kuna mradi wa Hagafilo ambao wananchi wale waliahidiwa kwamba wataletewa mradi huo na kwamba fedha zingetoka huko India lakini hadi sasa hakuna chochote kinachoendelea.

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri ni lini mtatekeleza ahadi hiyo ya Serikali?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ni kweli Mji wa Njombe unapata huduma ya maji kutoka kwenye Mto unaopita pale Njombe na hiyo huduma haitoshelezi, lakini ni kweli kwamba Mji wa Njombe ni kati ya Miji 16 ambayo itafaidika na mkopo kutoka Serikali ya India.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ni kwamba kinachoendelea ni kwamba Kamati ya Madeni Hazina imeshakaa na kuridhia mkopo huo wa dola milioni 500. Kwa sasa Serikali kupitia Hazina wanakamilisha taratibu za kusaini ile *financial agreement,* pia Serikali kupitia Wizara ya Maji na Umwagiliaji sasa hivi inaandaa makandarasi watakaofanya usanifu wa haraka ili tuweze kuwaza tenda kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya huo mradi kukamilika nikuhakikishie Mheshimiwa Mlowe kwamba Mji wa Njombe sasa utakuwa na maji ya uhakika ambayo wananchi watapata maji safi na salama kwa wakati wote.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali namba 369 linaloulizwa na Mheshimwa Stanslaslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana.

Na. 369

**Mahitaji ya Maji Katika Jimbo la Nyamagana**

**MHE. STANSLAUS S. MABULA** aliuliza:-

Jimbo la Nyamagana lina ukubwa wa kilometa za mraba 256, kati ya hizo kilometa za mraba 71.56 ni eneo la maji ya Ziwa Victoria lakini bado wananchi wake hawapati maji ya uhakika ya bomba hasa kwa zile Kata zilizoko nje ya Mji.

Je, ni lini Serikali itahakikisha kuwa wananchi wa Nyamagana wanapata maji ya uhakika hasa ikizingatiwa kuwa wamezungukwa na Ziwa Victoria?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Jimbo la Nyamagana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya maji katika Wilaya ya Nyamagana, Jijini Mwanza inatolewa kwa asilimia 90 ya wakazi wote wa Wilaya hiyo. Hata hivyo baadhi ya wakazi ambao wanaishi sehemu za mwinuko pamoja na wanaoishi pembezoni mwa Jiji wanakosa huduma ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kutambua hilo imepata mkopo wa masharti nafuu kutoka *European Investment Bank (EIB)*kiasi cha Euro milioni 54 sawa na shilingi bilioni 110 ili kuboresha huduma ya maji katika Jiji la Mwanza kwa kuhusisha Wilaya za Nyamagana na Ilemela. Mkandarasi wa utekelezaji wa mradi huo amepatikana na ujenzi umeanza. Kazi zinazotekelezwa ni pamoja na kuboresha huduma ya majisafi katika maeneo ya milimani hususani yaliyo juu ya matenki ya maji ambayo hayapati huduma kwa sasa, kubadilisha mabomba ya zamani yaliyochakaa na kuongeza mtandao wa mabomba pamoja na upanuzi na kuboresha miundombinu ya majitaka na mabwawa ya kutibu majitaka. *(Makofi)*

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niishukuru tu Serikali kwa huu mradi wa *World Bank* wa Euro milioni 54 kwa niaba ya Jimbo la Nyamagana pamoja na Ilemela. Lakini niseme tu kwa hali ya kawaida kama wananchi wa Jimbo la Nyamagana wangekuwa wanapata maji kwa asilimia 90 sidhani kama Mbunge wao ningekuwa na sababu ya kusimama hapa na kuomba maji. Niseme tu ukweli ni kwamba inawezekana mtandao wa maji umesambazwa kwa kiasi kikubwa lakini upatikanaji wa maji sio sawa na takwimu zinavyosomwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la kwanza; zipo Kata za Buhongwa, Lwanima, Kishiri, Igoma na Nyegezi ni lini Serikali itakuwa tayari pamoja na huu mradi wa Euro milioni 54 kuangalia uwezekano wa kuongeza fedha zingine nyingi zaidi ili wananchi kwenye maeneo haya ya Buhongwa na maeneo ya Lwanima na Kata zingine nilizotaja waweze kupata maji kwa uhakika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, pale kwenye

Jimbo la Ilemela umekuwepo mradi wa Vijiji kumi toka mwaka 2010 mpaka hivi tunavyozungumza leo ni Kijiji kimoja peke yake cha Kayenze ndio kimepata maji.

Ni lini Serikali itahakikisha Vijiji vya Nyamadoke, Kahama, Kabangaja, Igogwe, Igombe, Kabusungu na Nyafula vinapata maji haya kwa wakati kama ambavyo ilikuwa imekusudiwa? Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu kwa kifupi, muda sio rafiki.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nichukue nafasi hii kumpokea Mheshimiwa Mbunge kwa sababu kila wakati anakuja ofisini kuhusu Mradi wa Maji wa Nyamagana, ndiyo maana Wizara ya Maji na Umwagiliaji pamoja na juhudi za wafanyakazi wote na Serikali tumehakikisha kwamba tumepata hizi Euro milioni 54 tukiwa pamoja na Mheshimiwa Mbunge. Maana yake kila wakati alikuwa anakuja kuzungumza kuhusu wananchi wake na amekuwa anasema inakuwa ni aibu kwa sababu Ziwa Victoria liko pale na watu hawana maji, ndiyo maana amesaidia katika kulisukuma hili ili tuweze kupata mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge amezungumzia baadhi ya Kata. Mradi huu utakapokuwa umekamilika zipo kata ambazo zitapata huduma ya maji, Kata hizi ni pamoja na Kishiri, Buhongwa, Bugarika, Nyegezi, Lwanima pamoja na Igoma. Aidha, vitongoji ambavyo vinazunguka katika hizo kata tutahakikisha kwamba zimepata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema kwamba tunakarabati miundombinu iliyopo, ikiwa ni pamoja na mabomba yaliyochakaa, yakichakaa maana yake kupeleka huduma ya maji kwa wananchi inakuwa kidogo kuna shida tutahakikisha sasa na vijiji vingine vyote vilivyobaki vinapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia amehoji kuhusu tamko la asilimia 90. Hesabu ya asilimia 90 tunaihesabu kwa kuchukua *population* ya watu waliopo katika lile eneo na kuangalia ni watu wangapi wanaopata maji, hatu-*cross over* kwenda kwenye vijiji vyote, hapana! Tunaangalia una watu wangapi katika Kata ya Nyamagana, je, ni wangapi ambao wanapata maji ndiyo tunapiga mahesabu kuhakikisha kwamba sasa hiyo asilimia tunaipata. Kwa hiyo, kunaweza kukawa na Kata lakini kwa sababu zina watu wachache ukakuta kwamba asilimia hii ni kubwa kumbe kuna Kata ambazo bado hazijapata maji. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo tumeendelea kushirikiana kufuatilia suala la wananchi wa Nyamagana kupata maji, tuendelee kuwasiliana ili kuona ili mradi utakapokamilika kusiwe na eneo litakalobaki bila kupata maji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nitachukua maswali mawili tu. Mheshimiwa Kiswaga.

**MHE. KISWAGA B. DESTERY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Kwanza naishukuru Serikali kwa kutupa mradi wa maji pale Magu Mjini, mkandarasi yuko *site;* lakini pia nipongeze Kampuni ya *Alliance Ginnery,* mwekezaji amechimba kisima kirefu pale salama na kinatoa lita 9,000 kwa saa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa suala hili la Nyamagana linafanana kabisa na Jimbo la Magu, kijiografia na kwa fursa zilizopo. Katika Tarafa ya Sanyo kwa maana ya Kisesa yote na vijiji vyake pamoja na Tarafa ya Ndagalu kuna hali mbaya sana ya maji katika Vijiji vya Ng'aya, Salama, Ndagalu, Nyabole, Kabila na Mahala...

**MWENYEKITI:** Swali sasa Mheshimiwa Destery.

**MHE. KISWAGA B. DESTERY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, kwa sababu Halmashauri tumeomba dharura, ni lini Serikali sasa itatupatia fedha kwa ajili ya kuchimba visima virefu ili tuweze kusaidia wananchi hao?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kweli kabisa kwamba tumesaini mradi mkubwa ili kupata maji Wilaya ya Magu Mjini, lakini nikiri kwamba kuna kata ambazo ziko pembezoni na huo Mji ambazo bado hazijapewa huduma ya maji, lakini nichukue ombi lako, tuhakikishe kwamba tunapeleka visima, nikuombe Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane. Sio wewe tu katika tarafa zako, zipo tarafa nyingi, wengine ni majirani zako, pale Kasoli hakuna maji. Kwa hiyo, niombe tuwasiliane ili tuweze kuangalia tufanyeje kupitia kwenye bajeti zako au maeneo mengine yoyote utakayoona yanawezekana tuhakikishe kwamba hayo maeneo yaliyobaki ya vijiji nayo pia yanapata walau dharura kwa kuchimbiwa visima kama maji yatakuwepo chini ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lengo la Wizara ya Maji na Umwagiliaji kuhakikisha kwamba wananchi wote wa Tanzania popote pale walipo, tunawapatia maji safi na salama. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Salma Mwassa.

**MHE. SALMA M. MWASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba wa maji katika Mkoa wa Dar es Salaam bado ni mkubwa sana, hasa kwenye maeneo ambayo hayana miundombinu ya maji. Miradi ile mikubwa ya maji imeainishwa kwamba itatekelezwa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini sasa Serikali itatekeleza miradi hiyo ya maji ipasavyo ili wananchi hao wa Mkoa wa Dar es Salaam waweze kupata maji kwa uhakika na umakini, hasa kwenye maeneo ya Makabe, Goba, Msigani na maeneo yote ya Gongo la Mboto? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kama tulivyotoa taarifa katika Bunge hili, tumekamilisha miradi miwili mikubwa, Ruvu Juu na Ruvu Chini. Ruvu Chini inatoa lita milioni 270 kwa siku, Ruvu Juu inatoa lita milioni 196 kwa siku, pia mwezi huu tunakamilisha vile visima 20 Mpera na Kimbiji ambavyo vitatoa lita milioni 260 kwa siku. Kwa hiyo huduma ya maji kwa Jiji la Dar es Salaam na sehemu ya Pwani itakuwa ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko changamoto ya kupeleka miundombinu, kwa sasa hivi tumesaini mkataba mmoja wa bilioni 32 ya kuweka mtandao wa maji pamoja na kuongeza matenki ya kuhifadhi maji kupeleka kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tumeshafanya mipango tayari, tunahitaji dola milioni 100 ili tuweze kuhakikisha kwamba tunakamilisha usambazaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam. Tunaendelea baada ya muda ambao siyo mrefu sana tutaona kwamba vijiji vyote, maeneo yote, mitaa yote ya Dar es Salaam inapata maji safi na salama, kwa sababu maji yapo kilichobaki ni kusambaza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Pamoja na Jimbo la Mbeya Vijijini kuzungukwa na milima inayotiririsha maji mwaka mzima, lakini wananchi katika vijiji vingi hawana maji salama.

Je, ni lini Serikali itajenga miundombinu kwa kuwapatia maji salama wananchi wa vijiji vya Mbeya Vijijini? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri ni lini mtajenga.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tunaendelea na usanifu na baadhi tumeshasaini mikataba kwenye Jimbo lake kuhakikisha kwamba wananchi wote wa Mbeya Vijijini, Jimbo la Mheshimiwa Mbunge wanapata maji safi na salama. Tulikuwa tumebuni miradi kwenye vijiji kadhaa lakini baadae tukagundua kwamba yale maji yatakwenda kwenye kijiji cha mwisho na kuacha vijiji vya katikati, tumechelewa kwa sababu ya kuhakikisha kwamba tunaainisha na vijiji vya katikati. Nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mwaka ujao wa fedha mapema kabisa tutasaini mikataba, na mimi Mheshimiwa Waziri ameshanipangia ratiba, katika ratiba Mikoa nitakayoizungukia ni pamoja na Mkoa wa Mbeya. Kwa hiyo ntahakikisha tunaambatana na wewe kwenda kwako ili tuweze kuona hivyo vijiji vyenye uhaba mkubwa wa maji.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda najua suala la maji ni tete, tunaendelea na swali namba 370 linaulizwa na Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa, Mbunge wa Kalenga.

Na. 370

**Kusimama kwa Miradi ya Maji Jimbo la Kalenga**

**MHE. GODFREY W. MGIMWA** aliuliza:-

Miradi mbalimbali ya maji katika Jimbo la Kalenga imesimama kutokana na wakandarasi kutolipwa licha ya wananchi kukabiliwa na tatizo la maji.

Je, ni lini Wakandarasi hao watalipwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa, Mbunge wa Jimbo la Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Iringa kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji imeendelea kutekeleza miradi mitano ya maji katika Vijiji vya Igangidung'u, Kikombwe, Weru, Mfyome, Magunga - Isupilo - Itengulinyi - Lumuli kuanzia mwezi Juni, 2012. Gharama ya miradi yote ni shilingi 4,060,691,054 ambapo hadi mwezi Machi, 2017 kiasi cha fedha zilizokuwa zimelipwa kwa wakandarasi waliofanya kazi ni shilingi 3,027,831,071 sawa na asilimia 74.56. Hadi sasa miradi minne ya Vijiji vya Igangidung'u, Weru, Mfyome na Kikombwe imekamilika na inatoa huduma ya maji. Miradi hii ilikuwa na gharama ya shilingi 1,862,549,397 na kiasi cha shilingi 1,716,002,352 kimelipwa na kilichobaki kitalipwa baada ya kipindi cha matazamio *(defects liability period)* kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Magunga - Isupilo – Itengulinyi – Lumuli wenye mkataba wa gharama ya shilingi 2,198,141,657 ulisimama mwezi Julai mwaka 2015 wakati mkandarasi akiwa amelipwa shilingi 1,311,828,719 na utekelezaji wa mradi ulikuwa umefikia asilimia 45. Kutokana na kuchelewa kwa malipo, mkandarasi alifungua kesi ya madai *(Adjudication* na *Arbitration NCC)* ya kulipwa riba kwa kucheleweshewa malipo ya *interest* pamoja na *standby cost* zinazofikia shilingi 939,276,170. Halmashauri haikukubaliana na madai hayo, hivyo, mkandarasi *(RJR Construction Co. Ltd)* akafungua shauri la madai *(arbitration NCC)* na shauri limeshasikilizwa tunasubiri uamuzi wa *arbitrator* ili tujue hatma ya madai hayo. Ni azma ya Serikali kuendelea na ujenzi wa mradi ili ukamilike na kuanza kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuleta fedha ili kuwalipa Wakandarasi kulingana na kazi zilizofanyika na kuhakikiwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mgimwa swali la nyongeza.

**MHE. GODFREY W. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza niishukuru Serikali kwa kupeleka fedha kwa ajili ya miradi hii ambayo imeorodheshwa, lakini kwa uhalisia ni kwamba miradi hii

haijakamilika kwa asilimia mia, miradi miwili mradi wa Mfyome na Mradi wa Magunga – Isupilo kuelekea Lumuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii kwa sababu imekaa kwa muda wa miaka miwili haijakamilika na Halmashauri imeshapelekwa Mahakamani kwa ajili ya kufanyiwa *arbitration,* napenda sasa kupata *commitment* ya Serikali ikiwa kama *arbitration* itaenda kinyume na matakwa ya Serikali, yaani Serikali ilipe fedha hizi kwa mkandarasi, itatumia mida gani kukamilisha malipo haya kwa wakandarasi ili wananchi wangu waweze kupata maji katika miradi yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika utaratibu wa kutafuta wakandarasi, Serikali inawaagiza wakandarasi kununua vifaa na hivyo katika ununuzi wa vifaa wakandarasi hawa wanatozwa kodi ya *VAT,* lakini wakati wa malipo baada ya kupeleka zile *certificates* Wizarani, Serikali hailipi zile fedha ambazo wakandarasi wameingia kwa maana ya *VAT* na hivyo basi miradi inaendelea kusimama...

**MWENYEKITI:** Swali.

**MHE. GODFREY W. MGIMWA:** ...miradi inaendelea kusimama kwa sababu ya kutofanyika kwa malipo haya. Napenda kujua, je, Serikali ina mtazamo gani sasa kuhakikisha kwamba *VAT* inalipwa kama fidia kwa hawa Wakandarasi ambao wako katika miradi hii? Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza linahusu shauri lililopo katika taasisi inayoitwa *Arbitration,* kwamba je, *ruling* ikishatokea Serikali italipa Mkandarasi kwa muda gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge, swali hili nilijibu tu kwamba shauri linaendelea na linazungumzwa

kwa mujibu wa sheria na taratibu za mikataba, kwa hiyo *ruling* itakapofikia pia tutalipa kutokana na taratibu zinazoendelea za kimkataba bila wasiwasi wowote. Labda niseme, nikuhakikishie kwamba Hazina, Serikali yako ya Awamu ya Tano kwa sasa hatuna mgogoro mkubwa; wakandarasi wakishaleta *certificate* wakati wowote tunalipa, hatuchukui muda mrefu. Kwa sasa nina shilingi bilioni saba, angeleta hata leo basi tusingechukua wiki moja tungekuwa tumeshamlipa tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili linahusu kodi, *VAT;* Mheshimiwa Mbunge, sisi tushughulikie utekelezaji wa miradi. Serikali imejigawa katika taasisi mbalimbali, suala hili lina wahusika na wahusika hao wameainishwa katika mikataba na Mkandarasi anajua inapofikia suala la *VAT* aende wapi. Kwa hiyo, tuliache suala hili litekelezwe na wahusika ambao ni watu wa *TRA.*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bobali na Mheshimiwa Getere.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Mchinga, katika vijiji vya Lihimilo na Kitowavi katika mwaka wa fedha 2016/2017 vilichimbwa visima ambavyo vinahitaji umaliziaji wa takribani kama shilingi milioni 142 kwa kisima kimoja na kingine shilingi milioni 132. Sasa kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba tayari wanazo pesa shilingi bilioni saba na anajua nimeshamsumbua sana juu ya suala hili, nihakikishie sasa ni lini hizi fedha, shilingi milioni 142 kwa Lihimilo na shilingi milioni 132 kwa Kitowavi mtazipeleka ili mkakamilishe vile visima?

**MWENYEKITI:**Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri yeye mwenyewe

ni Mjumbe, kwenye hii Kamati ya Maji na Umwagiliaji. Tumeweka utaratibu Mheshimiwa Mbunge, visima tumechimba, maji yamepatikana kilichobaki ni miundombinu. Utaratibu wetu tuliouweka, mwambie Mkurugenzi wako, wewe ni Diwani kwenye Halmashauri Mkurugenzi aingie mikataba na wakandarasi kwa ajili ya miradi ya kusambaza hayo maji kupeleka kwa wananchi, wakishasaini, wakitekeleza, *certificate* ikapatikana, Mheshimiwa Mbunge nakuomba uiwasilishe hata kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, ni kwamba hatupeleki hela bila kuwa na hati ya madai, tulifanya hivyo huko nyuma tukapata shida sasa hivi tumeboresha na niwaambie tu kwamba tumekwenda vizuri sana, hadi mwezi wa nne tarehe 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana na Hazina wanaendelea kuleta fedha, Wizara ya Maji kupitia Mfuko wa Maji tumeshapokea shilingi bilioni 118. Kwa hiyo, fedha tunayo, wakamilishe huo mradi walete tutalipa hiyo hela.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Bunda kuna miradi ya maji ya Nyamswa, Salama Kati, Mgeta, Nyang'alanga, Kiloleli, Nyabuzume, Kambugu na mradi wa umwagiliaji wa Maliwanda. Miradi yote hii ni ya muda mrefu sana. Nataka kujua tu Waziri kwamba hii miradi ambayo tayari mingi wameshaitolewa fedha na haijakamilika kwa muda mrefu, ni lini sasa hii miradi itakamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni mara kama ya nne kuuliza maswali haya kwenye Bunge hili.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kwani kuna migogoro na mkandarasi? Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nikiri, sio kwamba amekuja mara nyingi tu lakini ameandika barua zaidi ya mara tatu kulalamikia utekelezaji wa miradi katika Halmashauri yake ya Bunda, na kwamba fedha nyingi zimepelekwa, sio na Wizara ya Maji tu, zimepelekwa fedha na Wizara ya Maji, zimepelekwa fedha na *JICA* shilingi milioni 207 nakumbuka, lakini kuna *own source* pia ya Halmashauri imetoka miradi ile haijakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naona nitume watalaam wangu wa Wizara ya Maji waje kwako kuangalia hili baadae mimi pamoja na wewe tutakwenda kuangalia kuna tatizo gani, kama alivyosema Mwenyekiti pengine kuna shida ya makandarasi au kuna shida ya utekelezaji kwenye Halmashauri kama tulivyobaini katika maeneo mengine.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali namba 371 linaloulizwa na Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mheshimiwa Mbunge naona tufanye suala moja nitatuma wataalam wangu wa Wizara ya Maji waje kwako kuangalia hili baadaye mimi na wewe tutakwenda pamoja twende tukaangalie kuna tatizo gani kama alivyosema Mwenyekiti pengine kuna shida ya Wakandarasi au kuna shida ya watekelezaji wetu wa Halmashauri kama tulivyobaini katika maeneo mengine.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea swali namba 371 linaulizwa na Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Kaskazini.

Na. 371

**Ukosefu wa Mawasiliano ya Simu za Mkononi**

**MHE. PETER J. SERUKAMBA** aliuliza:-

Jimbo la Kigoma Kaskazini katika Kata ya Ziwani kuna tatizo kubwa la mawasiliano ya simu hasa katika vijiji vya Kalalangobo, Rubabara, Kigalye, Mtanga, Nyantole na Kazinga.

Je, ni lini wananchi watapatiwa mawasiliano hayo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mbunge wa Kigoma Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote umeviainisha vijiji vya Kata ya Ziwani vikiwemo vijiji vya Kalalangobo, Kigalye, Manga, Rubabara, Nyantole na Kazinga na kuviingiza katika miradi ya kufikisha huduma ya mawasiliano vijijini kwa kadri ya upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa miradi.

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa jibu lako fupi. Mheshimiwa Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, Mfuko wa Mawasiliano Vijijini haujapewa pesa za kutosha lakini Waziri anasema vijiji hivi vimeingia kwenye Mfuko wa Mawasiliano Vijijini. Je, nataka kujua kama kweli umeingia kazi hii inaaza lini?

Swali la pili, nilidhani Serikali ingekuja na jibu la kusema badala ya kutegemea bajeti ya Serikali, waongee na makampuni ya simu kama Halotel, Airtel, Vodacom na Tigo ili waweze kupeleka mawasiliano kwenye vijiji hivyo kwasababu mbele ya Kazinga kuna Mwamgongo ambayo Mwamgongo tayari kuna mawasiliano na huwezi kufika Mwamgongo lazima uanzie Kazinga. Kwa hiyo, nilitarajia Serikali badala ya kutegemea bajeti peke yake, nikuombe

uende ukaongee na makampuni ya simu ili yaweze kupeleka huduma hiyo kwenye vijiji hivyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kama nilivyoeleza katika jibu la swali la msingi kwamba ujenzi wa Miundombinu kwa ajili ya mawasiliano utafanyika mara baada ya fedha za mradi zitakapopatikana na vijiji hivi vyote tulivyovitaja tayari vimo katika mpango, vimeingia katika mpango vinasubiri upatikanaji wa fedha. Lini? Ni mara fedha zitakapopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ombi lake la pili, labda tu nimfahamishe kwamba, mfuko wa mawasiliano kwa wote unatekeleza miradi mbalimbali kupitia Kampuni hizo hizo za Halotel, Tigo, Airtel na Vodacom, wao hawatekelezi wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makampuni haya yanapata ugumu wa kupeleka mawasiliano katika vijiji kwa sababu wanasema havina faida na hivyo Serikali inatoa ruzuku kupitia mfuko huu wa mawasiliano kwa wote na fedha zinapopatikana tunatangaza *tender* na makampuni hayo ndiyo yanayoomba hizo zabuni kupeleka mawasiliano hayo katika maeneo hayo.

Kwa hiyo, nadhani ni kweli Halotel, Airtel, Voda hata kama tutakwenda kuwashawishi siyo rahisi wao kukubali kwasababu wanajua hakuna faida katika maeneo hayo na hivyo inahitajika ruzuku ya Serikali na ruzuku ya Serikali tunaitoa kupitia mfuko huu wa Mawasiliano kwa Wote.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea swali namba 372 linaulizwa na Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 372

**Serikali Kukarabati Chuo Kikuu cha Mzumbe**

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA** aliuliza:-

Baadhi ya majengo na mabweni katika *campus* ya Chuo Kikuu Mzumbe, Morogoro yana uchakavu mkubwa sana ikiwemo miundombinu ya maji vyooni.

Je, kuna utaratibu gani wa kuyafanyia ukarabati majengo haya na hasa kuwapunguzia shida wasichana wanaohitaji matumizi zaidi ya maji kuliko wengine?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu swali namba 22 tarehe 1 Februari, 2017 Serikali imeshaanza ukarabati wa Miundombinu na majengo katika *campus* kuu ya Chuo Kikuu Mzumbe kwa gharama ya shilingi bilioni mbili. Hadi kufikia terehe 31 Mei, 2017 jumla ya shilingi milioni 884,634,366 zilizotengwa zilikwishatolewa na Wizara yangu inaendelea kufuatilia fedha zilizobaki ili zitolewe kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa juhudi hizi za ukarabati unaoendelea kutekelezwa chuoni hapo ni dhahiri kwamba Serikali ina nia ya dhati ya kuinua hadhi ya chuo hiki na hivyo kuweka mazingira stahiki ya kufundishia na kujifunzia pamoja na kuwapunguzia shida wasichana wanaohitaji matumizi zaidi ya maji.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Asha Abdullah Juma.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa bado hali ya upatikanaji maji katika baadhi ya mabweni hasa vyooni haujarekebishwa pamoja na kutengewa hizo shilingi bilioni mbili na kupatikana hizo zilizopatikana. Je, ni lini Serikali itafanya zoezi la dharura kuhakikisha maji yanapatikana hasa hizi sehemu za vyooni wakati ukarabati mkubwa ukiendelea?

Swali la pili, nilitaka kufahamu katika ukarabati huo, je, Serikali ina huo mpango wa kuyabomoa kabisa yale majengo yaliyochoka na kuyaweka mengine yenye sifa na haiba ya Chuo hiki Kikuu cha Mzumbe na lini jambo hili litatekelezwa? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi tu, lini na kama mtayabomoa.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. la kwanza; katika kufanya marekebisho ya dharura tayari tumeshawaelekeza na hatua zinachukuliwa kuhakikisha kwa kutumia fedha zao za ndani Chuo cha Mzumbe kitaanza mara moja katika ukarabati wa miundombinu hiyo ya maji.

Lakini vilevile katika mpango wa kudumu kuhusiana pia na majengo ambayo yana hali mbaya, kwa mwaka huu wa fedha unaoanza Wizara yetu imejipanga vizuri sana na kwamba tuna fedha taslimu takribani shilingi bilioni 56 hizo tunazo mkononi kwa ajili ya kuboresha vyuo vyetu mbalimbali ikiwemo Mzumbe ambayo itapatiwa mabweni ya kutosha wanafunzi 3,000 pamoja na kumbi za mihadhara na majengo mengine ya utawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo vingine ni pamoja na Chuo Kikuu Huria ambacho kitapata jengo hapa Dodoma, Chuo cha Ushirika-Moshi lakini pia mabweni ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na pale *DUCE.*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ikupa Allex.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona.

Wakati Serikali inajibu swali mwezi Januari mwaka huu iliahidi kutenga fedha kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya ukarabati na kuvifufua vyuo vya watu wenye ulemevu; na kwa kuwa fedha hii haijatengwa, je, Serikali ina kauli gani kwa hili? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolijia majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wizara inazo fedha kwa ajili ya kufufua baadhi ya vyuo vya watu wenye ulemavu kupitia mradi wake wa *P4R.* Kwa hiyo naomba uwe na amani ni kwamba zoezi hilo litafanyika kama ambavyo tumeanza katika shule nyingine ikiwemo shule ya Luwila pale Songea, shule ya Kipera pale Iringa na nyinginezo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa swali la mwisho kwa siku ya leo linaulizwa na Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 373

**Uhalifu Unaofanywa na Baadhi ya Madereva wa Bodaboda na Bajaji**

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA** alijibu:-

Kumekuwa na wimbi kubwa la uhalifu unaofanywa na baadhi ya madereva wa bodaboda na bajaji katika maeneo mengi Jijini Dar es Salaam.

(a) Je, Serikali mpaka sasa imechukua hatua gani kudhibiti wimbi hili linalokuwa tishio kwa watumiaji wa vyombo vya usafiri?

(b) Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuhakiki na kutambua mmiliki, dereva na mahali zinapopaki bajaji na bodaboda?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kumekuwepo na ongezeko la uhalifu unaofanywa na waendesha bodaboda ama bajaji katika maeneo mengi Jijini Dar es salaam. Hata hivyo, Serikali kupitia Jeshi la Polisi imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kama kufanya doria za magari, doria za pikipiki na za watembea kwa miguu lakini pia kuanzisha na kushirikiana na vikosi vya ulinzi shirikishi ili kubaini na kuzuia uhalifu katika maeneo ya makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Serikali za Mitaa, Halmashauri na Jiji la Dar es Salaam imeendelea kuhakiki pikipiki hizo ikiwa ni pamoja na kuwapangia maeneo ya kuegesha (ku-*park)*. Aidha, kupitia usajili wa *TRA* na Serikali za Mitaa, Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam imeendelea kuhakiki pikipiki hizo ikiwa ni pamoja na kuanzisha utaratibu wa kuzisajili katika maeneo ya maegesho ili kupata kumbukumbu za mmiliki, dereva na eneo maalum wanaloegesha pikipiki hizo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa niseme kwamba majibu ya Waziri yanaonesha kana kwamba suala la bodaboda limeanza juzi ama jana.

Suala la bodaboda ni la muda mrefu na kero za watu wenye bodaboda zimekuwa ni kubwa kwa wananchi lakini bado Serikali inasema inajipanga kufanya haya na yale wakati bodaboda ni suala la muda mrefu. Ni dhahiri *traffic police*

wameelemewa na usimamizi wa kudhibiti uvunjifu wa Sheria Barabarani kwa waendesha bodaboda. Kwa mfano; bodaboda zina...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa uliza swali.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Ndiyo swali langu.

**MWENYEKITI:** Uliza swali sasa.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Si ndiyo swali langu naenda?

**MBUNGE FULANI:** Anasema uliza swali!

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Kwa mfano; Bodaboda zimekuwa zikipita kwenye *traffic lights* wakati wowote bila kufuata taa. Je, Serikali haioni ni wakati sasa wa kubadili ama kuboresha mikakati yake ili kuimarisha usalama barabarani hususani jinsi ya kusimamia hawa wenye bodaboda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, nchini Rwanda wenzetu wana utaratibu mzuri wa kusajili madereva wa bodaboda na kusajili vituo ambavyo wanafanyia kazi. Je, ni lini Serikali itasajili hawa vijana wenye bodaboda na maeneo wanayofanyia kazi ili kuweza kubaini watu wanaofanya uhalifu kwa kutumia bodaboda?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi majibu kwa kifupi tu maana majibu unayo hapo hapo

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali haya yaliyoulizwa nilishayajibu kwenye jibu la msingi. Ninachosema siyo kwamba Serikali inajipanga, ni Serikali imeshachukua hatua hizi na mambo haya yamefanyika kwa mfano, swali la msingi linauliza Dar es Salaam. Pale Dar es Salaam hatua kubwa sana imeshafanywa ya kusajili waendesha pikipiki na haikuishia

hivyo tu wamewapa mpaka jezi za kuwatofautisha na mtu mwingine ambaye hakupangiwa katika vituo hivyo. Lakini siyo hilo tu, ukisema tunajipanga ni kama vile pikipiki ni zile zile ambazo zilishasajiliwa. Kama tulishasajili wakija wapya inabidi pia tuendelee kuwasajili ndiyo maana utaona kwamba zoezi hilo linaendelea kuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hii ya waendesha bodaboda kupita kwenye taa, hilo ni jambo la tabia ambalo tumeendelea kuchukua hatua, lakini elimu imeshatolewa na utaratibu ambao wanatakiwa wafuate ulishatolewa, kwa hiyo, tunaendelea kuchukua hatua kwa wale wanaovunja sheria hizo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umevuka sana, tumevutana hivyo hivyo, nianze na matangazo.

Tangazo moja, Waheshimiwa Wabunge mnaona kwenye nafasi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kiti kiko wazi, lakini Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Waziri wa Maliasili na Utalii ndiyo anakaimu nafasi ya Kiongozi wa shughuli za Bunge humu Bungeni kwa siku ya leo. *(Makofi)*

Wageni tulionao waliopo kwenye Jukwaa la Spika ni wageni 34 wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni wanakwaya wa Kanisa la Moravian kutoka Mkoani Mbeya wakiongozwa na Mchungaji Steven Mwaipopo, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, ambao ni viongozi wa Chama cha Watu wenye Ualbino (ulemavu wa ngozi) chama chao cha *TAS.* Nao ni Ndugu Neema Temba, Mwenyekiti wa Chama cha Watu wenye Ualbino Tanzania, simama, karibu. Ndugu Mussa Kabimba, Katibu Mkuu wa Chama cha Watu wenye Ualbino Tanzania na Ndugu Jonas Lubago, Mtendaji Mkuu wa *Myright Project* ambao ni wadau wa chama hicho. Wameambata na watendaji wa Chama Rafiki cha Watu

wenye Ulemavu Tanzania *(SRF)* kutoka nchini Sweden ambao ni Ndugu Annika Omtedt, Hannes Lagrelius, Stellan Anderson na Therese Selen, karibuni sana. (Makofi)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 40 wa Mheshimiwa Hassan Masala, Mbunge wa Nachingwea ambao ni wanafunzi wa vyuo kutoka Nachingwea Mkoani Lindi, mko wapi wanafunzi kutoka Mkoani Lindi msimame? Kokote mliko ahsanteni sana.

Wageni waliokuja Bungeni leo kwa ajili ya maunzo; tunao wanafunzi 70 na walimu watano kutoka *Holy Trinity English Medium Primary School* ya Mkoani Dodoma, ahsanteni sana. Someni kwa bidii sana kwa faida yenu lakini pia kwa faida ya Taifa hili, karibuni sana. *(Makofi)*

Sasa Mheshimiwa Jenista Mhagama kama nilivyosema ambae ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu akishughulikia Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa kilele cha Maadhimisho ya 11 Kitaifa na ya Tatu Kimataifa ya uelewa juu ya Ualbino kitafanyika hapa Dodoma kuanzia tarehe 13 Juni, 2017 yaani kesho katika viwanja vya *Nyerere Square* - Dodoma. Kauli mbiu ya madhimisho haya ni Takwimu na Tafiti kwa Ustawi kwa Watu wenye Ualbino.

Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa katika sherehe za kuadhimisha siku hiyo hapo kesho muda wa saa saba mchana katika viwanja vya *Nyerere Square* - Dodoma. Shughuli yenyewe itaanza rasmi saa 2.00 asubuhi, kwa hiyo mnakaribishwa sana kwa tukio hilo muhimu sana.

Tunaendelea na matangazo, Mheshimiwa William Ngeleja, Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* anaomba niwatangazie matokeo ya michezo ya mpira wa pete *(netball)* uliochezwa siku ya Jumamosi tarehe 10 Juni, kwenye Uwanja wa Jamhuri kati ya *Bunge Queens* na Chuo cha Mipango cha hapa Dodoma nadhani. *Bunge Queens* walipata magoli 56 na Chuo cha Mipango kilipapata magoli manne. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, na nyota wa mchezo huo alikuwa si mwingine bali ni Mheshimiwa Yosepher Komba. Aidha mgeni rasmi alikuwa Mheshimiwa Ally Keissy na alisindikizwa na Mheshimiwa Mpakate, unaona mambo yalivyokuwa na utamu. *(Kicheko/Makofi)*

Lakini pia kuna wageni wa Mheshimiwa Grace Tendega, wako wapi, karibuni sana Waheshimiwa kwenye Bunge lenu, Bunge la Watanzania na ninyi muone mambo yanavyokwenda. *(Makofi)*

Pia nina tangazo la Mheshimiwa...

**MBUNGE FULANI:** BAWACHA.

**MWENYEKITI:** Hawa ni nani lakini?

**WABUNGE FULANI:** BAWACHA.

**MWENYEKITI:** Aah ni BAWACHA.

**WABUNGE FULANI:** Eeeh!

**MWENYEKITI:** Aah! Ndio maana mlikuwa mnaniletea hizi karatasi.

**WABUNGE FULANI:** Eeeh. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa nawashukuru sana, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, leo kwa sababu ya shughuli muhimu inayoanza, nimechukua uamuzi kwamba hapatakuwa na Mwongozo, kwa sababu angalieni muda. Lakini hapa hapo nitangaze, ni mazoea tuliyoyaanza huko nyuma tunaita ni *convention* (desturi) na ndio baadaye sasa zinakuwa kama sehemu ya kanuni zetu kupitia Kanuni ya 5.

Wakati wa Bunge la Bajeti kwa sababu siku ya Alhamisi tulianza asubuhi na Waziri wa Fedha akitoa taarifa

kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2016 alitoa kwa saa moja, ni hoja yenyewe pia, kwa hiyo saa kumi akaja akatoa sasa ile bajeti kuu ya Serikali. Na kwa maana hiyo, na hiyo alitoa kwa muda *open ended* hapangiwi muda huo lakini unaji-*manage* ndani ya muda ambao una shughuli. Sasa kutokana na hilo, taarifa ya Kamati ya Bajeti, na Kamati ya Kambi Rasmi ya Upinzani watasoma watakapowasilisha hapa kila mmoja saa moja. Huo ndio utaratibu ambao tumejiwekea kwa shughuli hii, kwa sababu ni tukio muhimu sana kwa Watanzania na Maendeleo ya Nchi yetu. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, Katibu!

**NDG. LAWRENCE MAKIGI- KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2016 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti awasilishe taarifa ya Kamati. Mheshimiwa Hawa Ghasia - Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MHE. HAWA A. GHASIA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni 105(8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2016, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2017/2018, Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/2017 pamoja na Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge ya Bajeti imetekeleza majukumu yake kwa mujibu wa kifungu cha

9(a)(i) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni ya 18 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 pamoja na kuzingatia misingi ya Sheria ya Bajeti Namba 11 ya mwaka 2015 pamoja na Kanuni zake. Aidha, Sera za Fedha na kodi ambazo zimeweka mfumo bora wa kisheria unaosimamia mchakato mzima wa Bajeti ya Serikali kuanzia uandaaji, uainishaji, utekelezaji, ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa kuhusu masuala ya Bajeti ya Serikali zilitumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilijielekeza zaidi katika kufuatilia mwenendo wa ukusanyaji mapato na kusimamia matumizi ya Serikali pamoja na kufanya uchambuzi wa masuala mbalimbali ya ukuaji wa uchumi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Taifa. Ni matarajio ya Kamati kuwa, kupitia taarifa hii Waheshimiwa Wabunge watapata fursa ya kuchangia masuala mbalimbali yanayohusu Bajeti na kutoa ushauri wao ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Kamati imegawanyika katika sehemu kuu nane. Sehemu ya kwanza ni Utangulizi; Sehemu ya Pili ni Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi wa Taifa; Sehemu ya Tatu ni Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2016/2017; Sehemu ya Nne ni Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Sehemu ya Tano ni Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Sehemu ya Sita ni Hoja zilizowasilishwa na Kamati za Kisekta wakati wa kujadili Bajeti za Wizara mbalimbali, Sehemu ya Saba ni maoni na mapendekezo ya Kamati na Sehemu ya Nane ni Hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshatoa maelezo ya kina juu ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2016 na kuelezea Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2017/2018 pamoja na Mapendekezo ya Bajeti kwa kipindi cha mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taswira ya Hali ya Uchumi wa nchi inaonyesha kuwa Pato la Taifa lilikuwa kwa wastani wa asilimia 7.0 kwa mwaka 2016 kama lilivyokua kwa mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa Pato la Taifa ni mojawapo ya kigezo vya kupima uwezo wa nchi kukua kiuchumi. Ukuaji huu wa uchumi umeleezwa kuwa umetokana na ufuaji wa umeme na kuongezeka kwa matumizi ya gesi asilia katika kufufua umeme; kuongezeka kwa uzalishaji viwandani pamoja na kuimarika kwa huduma ya usafirishaji. Aidha, ukuaji huu wa uchumi umechangiwa zaidi na ukuaji wa sekta mbalimbali hasa sekta ya ujenzi (asilimia 13.0); sekta ya habari na mawasiliano (asilimia 13.0); sekta ya usafirishaji na mizigo (asilimia 11.8) pamoja na uchimbaji wa madini na mawe (asilimia 11.5).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa shughuli za kiuchumi za kilimo umekuwa sio wa kuridhisha mathalani upande wa mazao, ufugaji, misitu na uvuvi. Sekta ya kilimo imekua kwa asilimia 2.1 ikilinganishwa na asilimia 3.4 kwa mwaka 2015. Pamoja na kuwa na kiwango kizuri cha ukuaji wa uchumi, kwa ujumla bado kuna changamoto kubwa ya kuhakikisha kuwa ukuaji huu unaenda sambamba na upunguzaji wa umaskini hasa kwa kuziwezesha sekta za kilimo, misitu, ufugaji na uvuvi zinazohusisha idadi kubwa ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016 mfumko wa bei ulipungua na kufikia asilimia 5.2 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.6 kwa mwaka 2015. Mfumuko wa bei umeendelea kupungua na kubaki katika kiwango cha tarakimu moja kwa muda wa miaka minne mfululizo. Kamati inaipongeza sana Serikali kwa hatua hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango Elekezi wa Miaka 15 (2011/12 - 2025) wa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Mwaka 2016/2017 ulikuwa ni mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Mpango wa Pili katika mfululizo wa miaka mitano mitano iliyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2016/2017 ulilenga kutekeleza miradi ya

maendeleo katika makundi yafuatayo; Miradi ya kielelezo; viwanda vya kukuza uchumi na ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda, kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu, uimarishaji wa mazingira wezeshi kwa uendeshaji wa biashara na uwezeshaji wa miradi mingine muhimu katika ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2016/2017 Serikali ilitenga shilingi trilioni 11.8 kwa ajili ya bajeti ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 8.7 zilikuwa za ndani na shilingi trilioni 3.1 za nje. Hata hivyo, hadi kufikia mwezi Aprili, 2017 fedha zilizotolewa ni shilingi trilioni 4.8 sawa na asilimia 38.5 ambapo fedha za ndani ni shilingi trilioni 4.6 sawa na asilimia 41.9 na fedha za nje shilingi bilioni 907.8 sawa na asilimia 29.1 ya fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na upatikanaji wa fedha kutokuwa wa kuridhisha; Serikali imejitahidi kupiga hatua ya utekelezaji katika miradi mbalimbali ikiwemo ile ya kielelezo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mradi wa Makaa ya Mawe na Chuma Liganga; Kamati inaunga mkono hatua ambazo Serikali imechukua katika kuanza kwa utekelezaji wa mradi huu husuani kutengewa kwa kiasi cha fedha cha dola za Kimarekani milioni kumi kwa ajili ya kulipa fidia na kutathmini baadhi ya maeneo ya kuwahamishia wananchi wanaopisha eneo la mradi huu. Kamati inashauri ulipaji wa fidia ufanyike mara moja ili kupisha uendeshaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia inaipongeza Serikali kwa hatua ilizochukua katika ijenzi wa reli ya kati ambapo tayari ujenzi wa reli ya kisasa kwa kiwango cha *standard gauge* kwa awanu ya kwanza kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro umeanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia inaipongeza Serikali kwa kufanikicha kutenga shilingi bilioni 500 kwa ajili ya kufufua Shirika la Ndege Tanzania na kuwezesha ununuzi

wa ndege mbili zenye uwezo wa kubeba abiria 76. Aidha, Serikali imekamilisha maandalizi ya kununua ndege nyingine nne kwa gharama ya dola za Kimarekani milioni 231.2 Kamati inapongeza Serikali kwa hatua hii ya maendeleo kwa kuwa itachochea ukuaji wa sekta ya usafirishaji pamoja na sekta ya utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia inaipongeza Serikali kwa kukamilisha kulipa fidia kwa kituo cha Kibishara cha Kurasini pamoja na kuanza kujenga gati nyingine katika Bandari ya Mtwara na hatua ambayo imefikia katika Ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza kutekeleza Mradi wa Shamba la Miwa na Kiwanda cha Sukari katika eneo la Mkulazi kwa kushirikisha kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya *NSSF* na *PPF* kupitia kampuni ya umiliki ya *Mkulazi Holding Company*. Mradi unategemewa kuwa na shamba la hekta 63,227 na kiwanda cha sukari kuzalisha tani za sukari 200,000. Kamati inapongeza Serikali kwa kufikia hatua hii ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia imetenga kiasi cha shilingi bilioni 50.5 kama malipo ya awali kwa ajili ya mradi wa ununuzi wa meli kwenye maziwa makuu (Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa). Ni matarajio ya Kamati kuwa kabla ya kufika mwaka 2020 mradi huu utakuwa umekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kukamilisha kujenga Kiwanda cha Viuadudu - TAMCO Kibaha ambacho ni Kiwanda pekee katika Bara la Afrika. Kamati inashauri Serikali kukitafutia kiwanda hiki masoko ya uhakika ya kuuzia viuadudu pamoja na kuipatia fedha za kutosha Wizara ya Afya ili iweze kununua na kuvigawa viuadudu hivi katika Halmashauri zetu ili kuihakikishia Tanzania ni nchi ambayo isiyokuwa na Malaria kama ambavyo Kauli Mbiu yetu inasema Tanzania bila Malaria inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hatua nzuri za utekelezaji wa miradi iliyoainishwa hapo juu, Kamati inaishauri Serikali kuondoa changamoto zilizojitokeza katika miradi mingine ya kielelezo kama ambavyo inaonekana katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/2017; Kamati inatambua jitihada za Serikali katika kuongeza makusanyo ya mapato yake kila mwaka. Takwimu zinaonyesha hadi Aprili, 2017 mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya Halmashauri yalifikia shilingi trilioni 13.6 sawa na asilimia 73.7 ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada nzuri za Serikali katika kuongeza makusanyo ya mapato, bado kiwango hiki cha makusanyo si cha kuridhisha ukilinganisha na mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Serikali na pamoja na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema Serikali ikafanya jitihada za kutafuta maeneo mengine ya vyanzo vya mapato *(potential areas)* ili iweze kugharamia bajeti yake iliyopangwa na hivyo kukidhi mahitaji halisi ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato ya kodi na yasiyo ya kodi; katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Aprili 2017 mapato ya kodi yalifikia shilingi trilioni 11.6 sawa na asilimia 77.1 ya lengo la kukusanya kiasi cha shilingi trilioni 15.1. Sababu kubwa za kutofikiwa kwa lengo la ukusanyaji wa kodi hizi ilielezwa kuwa ni pamoja na kushuka kwa mauzo ya bidhaa mbalimbali katika soko la ndani kama vile saruji, vinywaji baridi na bidhaa nyingine za jumla na rejareja, baadhi ya makampuni kupunguza wafanyakazi ili kuendana na hali halisi ya kibiashara pamoja na uzalishaji, kutokuongezeka kwa ajira kama ilivyotarajiwa na hivyo kuathiri kodi ya mapato, kushuka kwa uingizaji wa bidhaa nchini, pamoja na kutotumia kikamilifu mashine za kielekroniki *(EFDs).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mapato yasiyo ya kodi, hadi kufikia mwezi Aprili 2017, Serikali ilikuwa imekusanya kiasi cha shilingi trilioni 1.61 sawa na asilimia 59.8 ya lengo la mwaka. Aidha, mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yaliyokusanywa ni shilingi bilioni 399.3 sawa na asilimia 60 ya lengo la shilingi bilioni 665.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji katika maeneo ya mikopo ya masharti nafuu na masharti ya kibiashara ni kama inavyoonekana katika kitabu changu cha hotuba. Kuhusu suala la kutoza kodi ya *VAT* kwenye misaada ya wahisani inabidi liangaliwe upya kwa kuwa wahisani hawakubaliani na utaratibu huu kwa kuwa unapunguza kiwango halisi cha misaada unachopaswa kutolewa.

Mheshimiwa Mwenyekit, kwa upande wa matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni kama inavyoonekana katika kitabu changu cha hotuba ukurasa wa 14 hadi ukurasa wa 17. Pamoja na changamoto zilizojitokeza Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ilizochukua ya kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo. Hatua hii imeisaidia kuondoa matumizi yasiyo ya lazima na kuziba mianya ya uvujaji wa fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipitia na kujadili mashirika yafuatayo; *NARCO, TANAPA, COSTECH, NDC*, Shirika la Bandari Tanzania, *TPDC, EWURA,* Shirika la Umeme yaani *TANESCO* na kwa ujumla Kamati ilibaini yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Shirika la Bandari, Kamati ilibaini kuwa miongoni mwa sababu ya kushuka kwa ukuaji wa ufanisi wa bandari kutoka asilimia 10 hadi 6.7 kwa mwaka, zilikuwa ni pamoja na kuanzishwa kwa himaya moja ya forodha ya mizigo inayoenda DRC Congo, kodi ya ongezeko la thamani kwenye huduma zinazotolewa katika usafirishaji wa bidhaa za mizigo nje ya nchi jirani. Ongezeko la tozo ya Mkemia Mkuu wa Serikali kutoka dola za 100 kwa *bill of lading* hadi dola moja ya Marekani kwa tani katika kemikali kama vile mbolea na

*sulphur* na kuzolota kwa huduma za reli ya *TAZARA* na pamoja na *TRL* maeneo ya Dar es Salaam na ukanda wa shaba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali kufanya marekebisho ya Sheria ya Ongezeko la Thamani ikiwa ni pamoja na kufuta kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye huduma zinazotolewa katika usafirishaji wa bidhaa ya mizigo nje kwa lengo la kupunguza gharama za usafirishaji katika bandari zetu.

Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuangalia upya utaratibu wa *Single Custom Territory* kwa nchi za maziwa makuu kama vile Congo ambazo si mwanachama wa Jumuia ya Afrika Mashariki na pia kuangalia tozo ya Mkemia Mkuu wa Serikali katika bidhaa za kemikali pamoja na *sulpher* na mbolea kwa sababu inakimbiza baadhi ya wateja kutumia bandari yetu ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *NDC* kimsingi Kamati ya Bajeti inaona ipo haja ya Serikali kuangalia upya bajeti ya shirika hili ili kuhakikisha tunapata matokeo mazuri ya usimamizi wa utekelezaji wa miradi hii ambayo zaidi ya miaka 10 imekuwa ikizungumzwa na kutengwa fedha bila kukamilika. Kwa hiyo, Serikali inaiomba pia iongezee mtaji lakini pia majadiliano yawe yanachukua muda mfupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *TANAPA*; kamati imeona kwamba uwekezaji umekuwa sio wa kuridhisha sana hasa katika upande wa utangazaji wa vivutio vyetu vya utalii katika nchi na mfano mzuri tunauona kwamba wakati nchi ya Kenya imetenga kiasi cha dola za Kimarekani milioni saba sawa sawa na bilioni 16 na hawatozi kodi la ongezeko la thamani kwenye huduma za utalii. Tanzania imetenga kiasi cha shilingi bilioni saba tu na tunatoza Kodi Ongezeko la Thamani ya kiasi cha asilimia 18 kwenye huduma za utalii. Kwa hiyo, Kamati inapendekeza masuala hayo ambayo yanaleta changamoto katika Shirika letu la *TANAPA* yaangaliwe kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *TPDC;* Kamati inapendekeza kuwa ni vizuri Serikali iwekeze mtaji wa kutosha kupitia Shirika lake la *TPDC* kwenye suala la gesi ili kupunguza gharama za uzalishaji wa gesi na kutoa unafuu kwa wawekezaji wa viwanda kununua gesi kwa bei nafuu. Pia kuiwezesha kuwekeza katika *share* zake ambazo inamiliki katika miradi mbalimbali ambayo inaingiwa na baadhi ya wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *EWURA*; Kamati imeona tofauti na mashirika mengine ambayo yanatakiwa kuchangia asilimia 15 ya mapato yake *EWURA* haina gharama zozote za uzalishaji. Kwa hiyo, ni vizuri ikaandaa bajeti yake ya uendeshaji pamoja na taasisi ambazo zinachangiwa na *EWURA* na kiwango kinachobaki chote kipelekwe katika mfuko mkuu, ili kuiongezea Serikali kiwango cha mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *TANESCO* Kamati imebaini kwamba miongoni mwa changamoto kubwa inayoikabili shirika la *TANESCO* kwa sasa ni gharama za uendeshaji na uzalishaji wa umeme, mzigo wa madeni inayodai na kudaiwa na taasisi mbalimbali. Kwahiyo, Kamati inaishauri Serikali ilipe madeni inayodaiwa *TANESCO* na taasisi mbalimbali ili iweze kujiendesha na pia Serikali ilipe madeni ambayo *TANESCO* inadai taasisi za Serikali ili kuiwesha iweze kujiendesha. Na pia kasma za *utility* ya umeme ambazo zinapaswa kulipa *TANESCO* zilipwe moja kwa moja kutoka Hazina kwenda *TANESCO* badala ya kupitishia sekta husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri kwenye makampuni mengine ni kama inavyoonekana katika kitabu cha hotuba ukurasa wa 17 hadi ukurasa wa 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 98(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Bunge ya Bajeti imepewa jukumu la kuchambua mambo muhimu yaliyojitokeza kwenye Kamati za kisekta wakati wa kujadili utekelezaji wa bajeti za Wizara kwa

mwaka wa fedha 2016/2017 unaoishia tarehe 30 Juni na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017 unaoanza tarehe 01 Januari, 2017. Tarehe 5 Aprili, 2017 Kamati ya Bajeti ilikutana na Serikali pamoja na Kamati ya Uongozi kwa ajili ya kufanya mashauriano kuhusu hoja 42 zilizowasilishwa kwake. Hivyo, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa matokeo ya mashauriano hayo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja 21 zilizohusu nyongeza ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa mafungu mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali imetekeleza kama inavyoonekana katika kitabu cha hotuba ukurasa 25 hadi ukurasa wa 28.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa hoja mahususi tano ambazo zilipokelewa kwenye kamati ya bajeti taarifa yake naomba niitoe kama ifuatavyo-:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kulikuwa na hoja ya kuingozea *TTCL* mtaji. Serikali ilikubali kuanza kuiwezesha *TTCL* kwa kuipatia masafa kwa njia ambayo sio ya mnada kama kama masafa ya megawati 800 kwa njia ambayo sio ya masafa kama ambavyo mashirika mengine yatauziwa na pia Serikali iliahidi kwamba itaiwezesha *TTCL* ili iweze kujiendesha, naiomba Serikali iendelee kulifanyia kazi hilo na iweze kuiwezesha *TTCL* ili iweze kujiendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Tanga - Moshi - Arusha hadi Musoma. Kamati ilipendekeza kwamba fedha za mfuko wa reli zitumike kulipia gharama za upembuzi yakinifu na upembuzi wa kina wa reli yote kuanzia Tanga kupitia Arusha hadi Musoma na baadaye kuitangaza na ijengwe kwa njia ya ubia yaani wa Serikali na sekta binafsi yaani *PPP*. Bado tunasisitiza Serikali itekeleze kama kamati ilivyopendekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa hoja iliyowasilishwa iliyohusu kuwakilisha Mfuko wa Mazingira inawezeshwa kifedha; Kamati ya Bajeti imependekeza

ikatwe asilimia tano kutoka kwenye vyanzo takribani 11 vilivyohusu tozo mbalimbali za Wizara na taasisi zinazohusika. Serikali ilipendekeza kwamba suala hilo italipeleka katika Baraza la Mawaziri na maamuzi kutolewa katika kipindi cha nusu mwaka yaani Desemba, 2017. Pamoja na majibu ya Serikali Kamati inasisitiza Serikali ifanye mapitio ya mafungu yake na kuhakikisha kwamba inapata feha ili mfuko huu uanze kufanya kazi zake kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine iliyowasilishwa ni kuwa wakati wa mwaka wa fedha 2016/2017, wakati wa mashauriano Kamati ya Bajeti iliomba kupata tathimini ya gharama halisi ya ujenzi wa vituo vya afya na zahanati ili kutekeleza ujenzi na umaliziaji wa vituo vya afya na zahanati na ufanyike katika mwaka wa fedha wa 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mashauriano na Serikali Kamati inakubaliana na majibu ya Serikali hata hivyo imeshauri Serikali kuanza kutekeleza mradi huu kwa awamu, vile vile Serikali iwasilishe Bungeni mpango mkakati wa ujenzi wa maboma ya zahanati na vituo vya afya na unaonyesha gharama sahihi za ujenzi na ukarabati wa vituo husika pamoja na ramani itakayopendekezwa kujengwa kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kulikuwa na hoja ya kuongeza tozo ya Shilingi 50 ni kwa lita ya mafuta yaani petroli na dizeli kwenda katika mfuko wa maji. Hoja hii naomba niilezee pamoja na mapendekezo mengine ambayo yapo huko mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Serikali itachukua hatua mbalimbali kwa madhumuni ya kujiongezea mapato ya kodi, hatua hizo ni pamoja na kuongeza viwango vya kodi na tozo mbalimbali. Serikali imechukua hatua mbalimbali za kupunguza na kufuta kodi ili kujenga na kuimarisha uchumi wa viwanda utakaochochea ajira na ustawi endelevu wa jamii na hivyo kuingezea Serikali mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti ilipata fursa ya kupitia na kuchambua utekelezaji wa bajeti ya Serikali wa mwaka 2016/2017 pamoja na ulinganisho wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2017/2018. Kamati imefanya imefanya uchambuzi huu ilikupata hali halisi ya mwelekeo wa bajeti ya Serikali na kuona kwamba tunatekelezaje malengo ya bajeti tuliyojiwekea. Kuna tofauti kadhaa ya sula ya bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/2027 na hii ya mwaka 2017/2018, kumekuwepo na ongezeko au punguzo katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kamati imepitia na imeangalia sera za kodi na sera za matumizi katika bajeti ambazo zimepangwa kutekeleza katika bajeti ya mwaka 2017/2018. Pamoja na sera nzuri za mapato na matumizi ambazo zinaonekana katika kitabu chetu cha hotuba na kitabu cha Waziri wa Fedha. Pamoja pia na hatua nzuri ya kugharimia matumizi ya kawaida bado Deni la Taifa la shilingi trilioni 9.47 limekuwa mzigo kwa sababu linachukua shilingi trilioni 9.46 linachukua asilimia 30 ya bajeti ya Serikali na linachukua asilimia 48 ya matumizi ya kawaida. Aidha, mishahara shilingi trilioni 7.2 inachukua asilimia 36.5 ya matumizi ya kawaida na matumizi mengineyo yanachukua asilimia 15.5 ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaona kuwa Deni la Taifa ni mzigo mkubwa katika utekelezaji wa bajeti ya Serikali na hivyo kuathiri matumizi mengineyo ya mafungu mbalimbali ambayo yamepungua kwa asilimia mbili. Jitihada kubwa zinahitajika ili kuhakikisha ulipaji mkubwa wa Deni la Taifa unapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018; Serikali imetenga kiasi cha shilingi trilioni 11.99 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi trilioni 8.96 ni fedha za ndani na shilingi trilioni 3.02 ni fedha za nje ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2016/2017, fedha za maendeleo zimeongezeka kwa kiasi cha takribani shilingi bilioni 179.08 sawa na asilimia mbili Kamati inapongeza kwa hatua hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati; hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango imeanisha mapendekezo ya mabadiliko ya kodi na tozo mbalimbali ambayo pia yatakuwa ni sehemu ya pili ya mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali wakati wa kujadili muswada wa fedha yaani *Finance Bill 2017*. Hivyo Kamati itatoa maoni kuhusu eneo hili wakati wa kuwasilisha taarifa yake kwenye Muswada huu. Hata hivyo kamati inatoa pongezi kwa Serikali kwa kuchukua hatua za kodi, ada na tozo katika baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Kamati inapongeza Serikali kwa kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye bidhaa za mtaji yaani *capital goods* ili kupunguza gharama za ununuzi au uagizaji wa mashine na mitambo ya kuzalisha na hivyo kuvutia uwekezaji katika sekta ya viwanda. Hatua hii ya Serikali itasaidia kuharakisha maendeleo ya sekta ya viwanda katika viwanda vya mafuta ya kula, nguo, ngozi, dawa za binadamu na mifugo. Hata hivyo Kamati inapendekeza kuongeza neno na lisomeke *capital goods* na *processing chemicals,* badala ya kubaki *capital goods* peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia inapongeza Serikali kwa kuondoa kodi ya ongezeko la thamani kwenye huduma zinazotolewa kwenye usafirishaji wa bidhaa au mizigo nje ya nchi yaani *auxiliary transport service* hatua hii itasaidia kupunguza gharama za usafirishaji bidhaa nje pamoja na kusaidia kuongeza shehena za mizogo inayopitia katika bandari yetu kwenda nchi jirani zisizo na bandari, na hivyo kuongezea Serikali mapato. Ushauri huu ulikuwa wa Kamati kwa muda mrefu kwa hiyo kamati inapongeza kwa Serikali kutekeleza ushauri huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kamati inaipongeza Serikali kusamehe kodi katika maeneo yanayohusu ufugaji pamoja na vyakula vya mifugo hatua hii itahamasisha kuongeza ufugaji katika maeneo husika na hivyo kusaidia kuinua kipato cha mwananchi pamoja na Serikali. Kamati pia inaipongeza Serikali kwa pendekezo la kutoa ada asilimia

moja yaani *clearing fee* kwa thamani ya madini yanayosafirishwa nje ya nchi. Hatua hii itaongeza mapato stahiki ya Serikali pamoja na pendekezo hili kuitwa *clearing fee* inatafsiriwa kuwa ni kutoza mrahaba *loyalty* kamati inaona hatua hiyo inaongeza kiwango cha mrahaba kutoka asilimia nne hadi asilima tano. Kamati inaishauri Serikali kurekebisha kifungu cha 82 cha Sheria ya Madini ya mwaka 2010 kinachoruhusu ulipaji wa mrahaba ili kuondoa mkanganyiko uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoza kodi ya zuio ya asilimia tano ya bei ya kuuzia kwa wachimbaji wadogo ni hatua inayoongeza mapato ya Serikali, lakini inatafsiriwa kuwa wachimbaji wadogo watalipa mrabaha wa asilimia tisa na inaweza kusababisha wachimbaji wadogo kufanya biashara haramu. Kamati inaishauri Serikali itafute utaratibu tofauti wa kulipa kodi hii bila kuathiri sekta ndogo ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kuondoa *VAT* kwenye madini ya vito na bidhaa ya usonara *(Gems and Jewelry)* yanayouzwa ndani ya nchi ili kupunguza bei ya bidhaa hizo nchini kwani vito na bidhaa hizo za usonara zinaposafirishwa na kuuzwa nje zinakuwa hazina *VAT*. Hatua hii itasaidia biashara hii kukua ndani ya nchi na kuongeza ajira na bidhaa zetu nchini kuwa shindani ukilinganisha na bei za nje. Badala ya Serikali kutoza *VAT* itoze *Royalty* ya asilimia saba au nanekuongeza mapato kwenye madini ya vito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marekebisho ya ushuru wa bidhaa kwenye maeneo mbalimbali, kufutwa kwa ada ya mwaka kwenye leseni ya magari *(annual motor vehicle license)* Kamati inaopongeza sana Serikali kwa kuondoa ada hii kwa sababu imeondoa kero kubwa kwa wananchi na hivyo kurudisha imani kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*). Hatua hii itaiongezea mapato Serikali kuliko ilivyokuwa awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kutumia kiasi cha shilingi 40 kinachopendekezwa kutozwa katika kila lita moja ya petroli, dizeli na mafuta ya taa kupeleka kwenye Mfuko wa Maji kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji vijijini kwa asilimia 70 ya tozo na mijini asilimia 30 ya tozo. Pia Kamati inaishauri Serikali kuitumia Wakala wa Uchimbaji wa Visima na Mabwawa (*DDCA*) kikamilifu katika utekelezaji wa miradi ya maji mijini na vijijini kwa sababu Wakala huu imeonekana kufanya kazi kwa ufanisi zaidi kuliko Wakandarasi wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia inapendekeza Serikali iiwezeshe Wakala huu, ili iwe na uwezo wa kuweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Kamati pia inaishauri Serikali pia iangalie mgawanyo sawa wa mfuko huu wa maji, baina ya Mikoa hasa ile ya pembezoni na ambayo ina tatizo kubwa la maji kuliko ambavyo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zilizochukuliwa na Serikali ni nyingi na ni rafiki kwa mwananchi ambao wana nia ya kufanya biashara hata hivyo bado maeneo mengine ya kodi, ada na tozo ambayo Serikali iyachukue na kuangalia namna ya kuyafanyia kazi katika Sheria ya Fedha inayokuja. Maeneo hayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Iangalie upya utekelezaji wa kulipa asilimia 15 ya ushuru wa forodha kwa makampuni yanayoagiza sukari ya viwandani ambayo baadaye inatakiwa irudishwe kama *refund* kwa makampuni hayo. Changamoto kubwa iliyopo hapa ni kwamba, Serikali imekuwa hairudishi *refund* hizo kwa wakati na hata pendekezo la kuweka *Escrow Account* bado halijibu changamoto hii kwa kuwa mpaka sasa Serikali imeshikilia kiasi cha takribani shilingi bilioni 20 ambazo zinagharimu wenye viwanda kiasi cha shilingi milioni 400 kila mwezi kama riba kutoka kwenye mabenki. Madhara ya jambo hili ni pamoja na kuongeza gharama za uzalishaji, kupunguza uwezo wa kampuni kuwekeza, na pia katika mwaka huu wa fedha zaidi ya wafanya kazi 725 wamepunguzwa katika viwanda hivi. Aidha, Kamati inaamini kwamba mifumo ya Serikali ya usimamizi wa

uagizaji wa Sukari Viwandani kwa sasa imeimarishwa vya kutosha.

(ii) Ushuru wa bidhaa (*Excise Duty*) wa asilimia 17 kwenye *Electronic Communication Services;* Kamati inapendekeza irudi asilimia 14 badala ya 17 ilivyo sasa kwani nchi za jirani mfano Kenya inatoza asilimia 10, Uganda asilimia 12, Burundi inatoza sifuri na Rwanda asilimia 8. Lakini pia hii asilimia 17 ilikuwa ni tozo ya mpito tu kutoka ile asilimia 14.

(iii) Kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2016, makampuni ya simu yalitakiwa yawe yamejisajili katika soko la hisa la Dar es Salaam ifikapo tarehe 31 Desemba 2016. Mpaka sasa ni kampuni moja tu ambapo imefikisha hisa zake sokoni. Hali iliyojitokeza ni kutokana na elimu ndogo juu ya uwekezaji kwenye hisa, hali ya uchumi na mwitikio mdogo wa wananchi. Hata hivyo, Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi wa kuwapa Watanzania fursa ya kumiliki na kukuza uchumi kupitia soko la hisa na kuongeza uwazi katika uendeshaji wa Sekta ya Mawasiliano nchini. Pamoja na uamuzi huo mzuri, Kamati inashauri kwamba:-

(a) Sheria hiyo ifanyiwe marekebishon ili kiwango cha chini cha hisa kwa watanzania kianzie asilimia 15 hadi 25 na bila kuweka ukomo wa juu. Hii itatoa fursa kwa kampuni za simu kujitathmini na kuendelea kuhamasisha uuzaji wa hisa kadiri soko linavyoendelea kukua na hali ya uchumi unavyobadilika pamoja na uhitaji wa mitaji kwa sababu za uwekezaji wa Makampuni za simu;

(b) Serikali pia iruhusu kufungua soko kwa watu wa nje kununua na kuuza hisa ukizingatia kuwa zaidi ya asilimia 50 ya soko letu linahusisha wageni *foreigners;*

(c) Serikali pia ibadilishe tafsiri ya maneno *listed shares* katika kanuni za Sheria ya Soko la Mitaji la Dar es Salaam ya mwaka 2014. Sheria itambue hisa zote za kampuni zilizoandikishwa kwa mujibu wa Sheria ya mitaji na dhamana. Kwa mujibu wa kanuni *listed shares are those*

*shares listed and traded at stock exchange.* Inapendekezwa msingi wa tafsiri hii Kanuni uhamishiwe kwenye Sheria ya kodi ya mapato *(Income Tax Act)* na isomeke kwamba *listed shares are those shares of a listed company whose minimum requirement is listed at DSE.* Kamati inaona tafsiri hii itasaidia Serikali kudhibiti miamala *(transactions)* za mauziano ya hisa ambazo hazitatakiwa kupelekwa kwenye soko la hisa Kisheria. Mwenendo unaonyesha kuwa baadhi ya makampuni yamekuwa na tabia ya kuuziana hisa nje ya nchi bila mamlaka zetu za ndani kuwa na taarifa na hivyo kuikosesha Serikali mapato; *(Makofi)*

(d) Pia kuboresha tafsiri ya kipengele (e) cha Sheria ya Kodi ya Mapato *(Income Tax Act)* cha neno *investment assets* ili kuendana na tafsiri halisi ya neno *listed shares* ili isomeke *shares and securities of the listed company at DSE*; *(Makofi)*

(e) Kuhusu *Capital Gain Tax* kwenye soko la hisa inapendekezwa lifutwe na badala yake iwekwe *Security Transaction Tax* kama ilivyopitishwa na Bunge wakati wa Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2016.

(iv) Kodi ya Ongezeko la Thamani ya asilimia 15 kwenye huduma za kibenki Utekelezaji wa kodi hii umekuwa ukiumiza watumiaji wa mwisho (mwananchi) kinyume na maelezo ya Serikali. Pia gharama za uendeshaji kwenye mabenki zimeongezeka kiasi cha kwamba amana kwenye mabenki zimepungua na gharama za mikopo zimeongezeka na hivyo kuendelea kuathiri mtumiaji wa mwisho ambaye ni mwananchi.

(v) Kamati inapongeza pendekezo la Serikali la kufanya marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290 ili kupunguza ushuru wa mazao *(produce cess)* unaotozwa na Halmashauri za Wilaya nchini kutoka kiwango cha sasa cha asilimia tano ya thamani ya mauzo hadi asilimia tatu kwa mazao ya biashara na asilimia mbili kwa mazao ya chakula. Hata hivyo Kamati inaishauri Serikali kuweka kiwango kimoja cha ushuru huu kwa kiwango cha asilimia

tatu kwa mazao yote bila kutofautisha mazao ya biashara na mazao ya chakula kwa sababu ni vigumu kujua wakati gani maharage yanakuwa mazao ya biashara au mazao ya chakula, hivyo hivyo kwa mazao mengine. Hatua hii itampatia mkulima unafuu mkubwa na kuondoa mkanganyiko unaoweza kutokea kwa kutofautisha mazao ya biashara na mazao ya chakula. Aidha, Kamati inapendekeza kufutwa kwa ushuru kwenye mbegu zinazozalishwa nchini.

(vi) Kamati inapongeza pendekezo la Serikali la kupunguza kiwango cha Kodi ya Mapato ya Kampuni *(Corporate Income Tax).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni baadhi tu ya mapendekezo ya Kamati katika eneo la kodi, ada na tozo, mapendekezo mengine yatawasilishwa wakati wa kupitia na kuchambua Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hotuba yangu, iingie yote katika *Hansard* kama ilivyo.

Kamati inaishauri Serikali kushirikisha sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo hasa ya kielelezo ambayo inamtizamo wa kibiashara na pia kuiuanisha Sheria ya ubia na Sheria nyingine za uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilikuwa inaishauri Serikali kutekeleza mapendekezo ya taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2016. Kamati pia, ilikuwa inapendekeza kuunganishwa kwa baadhi ya taasisi za usimamizi yaani *regulatory bodies* badala ya kuwa kila moja kwa wakati wake inaenda kuwatembelea wawekezaji wetu basi Taasisi moja iwe inafanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuimarisha mifumo mbalimbali ya ukusanyaji wa mapato kwa njia za kieletroniki kama vile ya *Government e-payment Gateway System, Electronic Revenue Collection System* na mingineyo. Hatua hii itasaidia kudhibiti mianya ya

upotevu wa fedha pamoja na kupunguza urasimu katika ulipaji wa fedha yaani (kodi, ada na tozo). Kamati Pia, inasisitiza Serikali kuhakikisha matumizi ya *EFD* yanaimarishwa katika sekta za umma na binafsi ili kusaidia ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa Kamati ya Bajeti utasaidia Bunge lako tukufu kuelewa mchakato mzima wa Bajeti ya Serikali katika hatua zote za kibajeti yaani uandaaji, uidhinishaji, utekelezaji, ufuatiliaji pamoja na tathmini. Kamati inaikumbusha Serikali kuzingatia Sheria ya Bajeti katika kutekeleza majukumu yake ya kibajeti. Aidha, mabadiliko yote yanayotolewa na Serikali kuhusu marekebisho ya Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 ni vema yakapitishiwa kwenye Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia inaishauri Serikali kuangalia tozo mbalimbali zinazotozwa katika sekta ya utalii haswa *VAT* katika huduma za utalii kwenye masuala mazima ya uwindaji wa kitalii. Kwa sababu leseni inakatiwa *VAT*, faini inakatiwa *VAT*, kila kitu kinakatiwa *VAT. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kichocheo kimoja wapo cha kukuza sekta ya utalii ni usafirishaji wa anga. Serikali imefanya jitihada kubwa kuwekeza kwenye usafiri wa anga lakini tozo *(Railway Development Levy)* iliyowekwa kwenye Sheria ya Reli ya mwaka 2002 kwenye mafuta ya ndege *(JET A-1)* imekuwa ikiongeza gharama ya ununuzi wa mafuta ya ndege nchini kuliko nchi za jirani yaani Kenya na Uganda ambazo hazina tozo hii. Kamati inapendekeza Sheria hii ifanyiwe marekebisho ili kuondoa tozo hiyo kwenye mafuta ya ndege ya *JET A - 1. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo mengine ya Kamati, kwanza ni kuhusu kwenye suala zima la Deni la Taifa; pamoja na kuwa hadi kufikia Aprili, 2017 Deni la Taifa linalojumuisha deni la Serikali la ndani na deni la nje ya sekta binafsi lilifikia shilingi trilioni 50 ikilinganishwa na shilingi trilioni 39.27 Machi, 2016. Deni hili ni sawa na asilimia 41.3 ya Pato la Taifa ambalo ni shilingi trilioni 103.74. Kati ya kiasi hicho,

Deni la Serikali ni shilingi trilioni 42.9 na Deni la sekta binafsi ni shilingi trilioni 7.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa deni hili ni himilivu kwa vigezo vyote bado limekuwa ni mzigo mkubwa kwa Taifa letu na limeanza kuwa tishio kwa utengamavu wa uchumi jumla. Deni hili limeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na kuongezeka kwa mikopo isiyo na masharti nafuu kunakopelekea kuongezeka kwa gharama za kuhudumia deni. Mathalani, kiasi cha shilingi trilioni 5.2 kulipwa katika mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali iangalie fursa zilizopo za kuimarisha uhimilivu wa deni la Taifa ikiwa ni pamoja na kufanya majadiliano na wakopeshaji wa Kimataifa ambao ni pamoja na Benki ya Dunia kwa madhumuni ya kupata masharti nafuu kwa Deni la Taifa *(Debt Reprofiling)* kama walivyofanya wenzetu wa Kenya na Ghana. Serikali inaweza ikaongeza umri wa deni na pia kuangalia kujadiliana kuona uwezekano wa kupunguza kiwango cha riba. Serikali pia iharakishe kuifanyia nchi tathimini ya uwezo wa kukopa yaani *(sovereign credit rating)* na pia Serikali kuishirikisha sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo hasa yenye mtizamo ya kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali ihakikishe kwamba inapunguza Sekta isiyo Rasmi ili iweze kuchangia katika Pato la Taifa. Uchambuzi wa bajeti umeonyesha kwamba bajeti imejaribu kugusa maeneo ya msingi ya uwezeshaji wananchi kiuchumi pamoja na kutoa fursa kwa wafanyabiashara na wenye viwanda kuwekeza na kuzingatia fursa waliyopata kupitia kupunguzwa ama kufutwa kwa kodi na tozo mbalimbali zilizoidhinishwa. Nia ya Serikali ni kuhakikisha inapata mapato pasipo kuwepo na kero kutoka kwa wadau wa kodi.

Hata hivyo, kuna baadhi ya mapendekezo huenda yakaleta changamoto katika utekelezaji wake, hivyo ni vyema wananchi wakaelewa kwamba, nia ya Serikali ni kuboresha huduma kwa Umma na huduma hizi zina

gharama. Ni matarajio ya Kamati ya Bajeti kwamba gharama zinazolipwa kwa wananchi kwa njia ya kodi zinaenda kuboresha maisha ya wananchi kulingana na matarajio yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia napenda kumshukuru Waziri wa Fedha na Naibu wake pamoja na Katibu Mkuu. Napenda pia kumshukuru Makamu Mwenyekiti wangu Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, na wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah, pamoja na Sekretarieti ambayo ni Idara ya Bajeti ikiongozwa na Ndugu Lina Kitosi pamoja na Ndugu Michael Kadebe na wengine ambao wanaonekana katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti kwa taarifa yako na uwasilisho wako mzuri tunakushukuru sana.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU TAARIFA YA HALI YA UCHUMI WA TAIFA KWA MWAKA 2016, MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2017/18, TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2016/17 PAMOJA NA MAPENDEKEZO YA SERIKALI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18. – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni 105 (8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016 naomba

kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2016, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2017/18, Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/17 pamoja na Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/18.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bunge ya Bajeti imetekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Kifungu cha 9 (a-i) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016 pamoja na kuzingatia misingi ya Sheria ya Bajeti Namba 11 ya Mwaka 2015 pamoja na Kanuni zake. Aidha, Sera za fedha na kodi ambazo zimeweka mfumo bora wa kisheria unaosimamia mchakato mzima wa Bajeti ya Serikali kuanzia uandaaji, uidhinishaji, utekelezaji, ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa kuhusu masuala ya Bajeti ya Serikali zilitumika.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijielekeza zaidi katika kufuatilia mwenendo wa ukusanyaji mapato na kusimamia matumizi ya Serikali pamoja na kufanya uchambuzi wa masuala mbalimbali ya ukuaji wa uchumi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Taifa. Ni matarajio ya Kamati kuwa, kupitia taarifa hii Waheshimiwa Wabunge watapata fursa ya kuchangia masuala mbalimbali yanayohusu Bajeti na kutoa ushauri ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Kamati imegawanyika katika Sehemu Kuu Nane. Sehemu ya kwanza ni Utangulizi; Sehemu ya pili ni Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi wa Taifa; Sehemu ya tatu ni Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2016/17; Sehemu ya nne ni Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2016/17, Sehemu ya tano ni Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa fedha 2017/18, Sehemu ya sita ni Hoja zilizowasilishwa na Kamati za Kisekta wakati wa kujadili Bajeti za Wizara mbalimbali, Sehemu ya saba ni maoni na mapendekezo ya Kamati na sehemu nane Hitimisho.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 HALI YA UCHUMI WA TAIFA KWA MWAKA 2016

**Mheshimiwa *Spika***, Serikali imeshatoa maelezo ya kina juu ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2016 na kuelezea Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2017/18 pamoja na Mapendekezo ya Bajeti kwa kipindi cha mwaka 2017/18. Taswira ya Hali ya Uchumi wa nchi inaonyesha kuwa Pato la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 7.0 kwa mwaka 2016 kama lilivyokua kwa mwaka 2015.

**Mheshimiwa Spika,** ukuaji wa Pato la Taifa ni mojawapo ya vigezo vya kupima uwezo wa nchi kukua kiuchumi. Ukuaji huu wa uchumi umeleezwa kuwa umetokana na ufuaji wa umeme na kuongezeka kwa matumizi ya gesi asilia katika kufua umeme; kuongezeka kwa uzalishaji viwandani pamoja na kuimarika kwa huduma ya usafirishaji. Aidha, ukuaji huu wa uchumi umechangiwa zaidi na ukuaji wa sekta mbalimbali hasa sekta ya ujenzi (asilimia 13.0); Sekta ya habari na mawasiliano (asilimia 13.0); sekta ya usafirishaji na mizigo (asilimia 11.8) pamoja na uchimbaji wa madini na mawe (asilimia 11.5).

**Mheshimiwa Spika**, ukuaji wa shughuli za kiuchumi za kilimo umekuwa sio wa kuridhisha mathalani upande wa mazao, ufugaji, misitu na uvuvi. Sekta ya kilimo imekua kwa asilimia 2.1 ikilinganishwa na asilimia 3.4 kwa mwaka 2015. Pamoja na kuwa na kiwango kizuri cha ukuaji wa uchumi, kwa ujumla bado kuna changamoto kubwa ya kuhakikisha kuwa ukuaji huu unaenda sambamba na upunguzaji wa umaskini hasa kwa kuziwezesha sekta za kilimo, misitu, ufugaji na uvuvi zinazohusisha idadi kubwa ya wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Mwaka 2016 mfumuko wa bei ulipungua na kufikia asilimia 5.2 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.6 kwa mwaka 2015. Mfumuko wa bei umeendelea kupungua na kubaki katika kiwango cha tarakimu moja kwa muda wa miaka minne mfululizo. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0. UTEKELEZAJI NA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17

### 3.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango Elekezi wa Miaka 15 (2011/12 - 2025/26) wa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Mwaka 2016/17 ulikuwa ni mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Mpango wa Pili katika mfululizo wa miaka mitano mitano iliyopangwa.

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2016/17 ulilenga kutekeleza miradi ya maendeleo katika makundi yafuatayo; Miradi ya kielelezo; viwanda vya kukuza uchumi na ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda, kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu, uimarishaji wa mazingira wezeshi kwa uendeshaji wa biashara na uwekezaji na miradi mingine muhimu katika ukuaji wa uchumi.

Katika mwaka 2016/17, Serikali ilitenga shilingi trilioni 11.8 kwa ajili ya bajeti ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 8.7 zilikuwa za ndani na trilioni 3.1 za nje. Hata hivyo, hadi kufikia mwezi Aprili, 2017 fedha zilizotolewa ni shilingi trilioni 4.5 (asilimia 38.5) ambapo fedha za ndani ni shilingi trilioni 3.6 (asilimia 41.9) na fedha za nje shilingi bilioni 907.8 (asilimai 29.1) ya fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge.

### 3.2 Hatua zilizochukuliwa

**Mheshimiwa Spika**, mwenendo wa upatikanaji wa fedha usiokuwa wa kuridhisha umesababisha kasi ndogo ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo. Hata hivyo, Serikali imejitahidi kupiga hatua ya utekelezaji katika miradi mbalimbali ikiwemo ile ya kielelezo kama ifuatavyo:-

i) **Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma Liganga – Njombe**.

Kamati inaunga mkono hatua ambazo Serikali imechukua katika kuanza kwa utekelezaji wa mradi huu husuani kutengewa kwa fedha kiasi cha dola za Kimarekani Milioni 10 kwa ajili ya kulipa fidia pamoja na kuthaminisha baadhi ya maeneo ya kuwahamishia wananchi wanaopisha eneo la mradi. Kamati inashauri ulipaji wa fidia ufanyike mara moja ili kupisha uendelezaji wa mradi huu.

ii) **Ujenzi wa Reli ya Kati**.

Kamati inaunga mkono hatua ambazo Serikali imechukua katika kuanza kwa utekelezaji wa mradi huu kwa kutenga kiasi cha shilingi trilioni Moja kwa ajili ya ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha *standard gauge* kwa awanu ya kwanza kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro. Kamati inashauri Serikali kuharakisha kuanza ujenzi wa reli hiyo ya kisasa.

iii) **Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania**.

Serikali ilifanikiwa kutenga shilingi bilioni 500 kwa ajili ya kufufua shirika la Ndege Tanzania na kuwezesha ununuzi wa ndege mbili zenye uwezo wa kubeba abiria 76. Aidha Serikali imekamilisha maandalizi ya kununua ndege nyingine nne kwa gharama ya Dola za Kimarekani milioni 231.3 Kamati inapongeza Serikali kwa hatua hii ya maendeleo kwa kuwa itachochea ukuaji wa sekta ya usafirishaji pamoja na utalii.

iv) **Ujenzi wa mitambo ya kusindika Gesi ya kimiminika, Lindi.**

Serikali ilitenga kiasi cha shilingi milioni 800 kwa fedha za ndani ili uhakiki wa uthamini wa mali za wananchi watakaopisha mradi huu. Mradi huu unajumuisha ubia kati ya Shirika la Taifa la Petroli (TPDC) na Kampuni za BG/Shell, Statoil, Orphir, Pavilion na ExxonMobil. Kamati inashauri Serikali kuharakisha mchakato wa utekelezaji wa mradi huu.

v) **Uendelezaji wa Maeneo Maalum ya Kiuchumi.**

Serikali imeendelea na mikakati ya kuhakikisha maeneo maalum ya uwekezaji wa kiuchumi yaliyochukuliwa kutoka kwa wananchi yanaendelezwa kama yalivyokusudiwa.

Maeneo haya yanahusisha uwekezaji wa Kituo cha biashara cha kurasini, Ujenzi wa Bandari Bagamoyo na Ujenzi wa Bandari Mtwara.

vi) **Uanzishwaji wa shamba la miwa na kiwanda cha sukari Mkulazi.**

Serikali itatekeleza mradi huu kwa njia ya ubia kati ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya NSSF na PPF kupitia kampuni ya umiliki ya Mkulazi Holding Company. Mradi unategemewa kuwa na shamba la hekta 63,227 na kiwanda cha sukari kuzalisha tani za sukari 200,000. Kamati inapongeza Serikali kwa kufikia hatua hii ya maendeleo.

vii) **Ununuzi wa Meli kwenye Maziwa Makuu**.

Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 50.5 kama malipo ya awali kwa ajili ya mradi huu kwa Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa. Ni matarajio ya Kamati kuwa kabla ya kufika mwaka 2020 mradi huu utakuwa umekamilika.

viii) **Kiwanda cha Viuadudu-TAMCO Kibaha.**

Kamati inapongeza Serikali kwa kukamilisha ujenzi wa Kiwanda hiki ambacho ni kikubwa Barani Afrika. Kamati inashauri Serikali kukitafutia kiwanda hiki masoko ya kuuzia viuwadudu pamoja na kuipatia fedha ya kutosha Wizara ya Afya ili iweze kununua na kuvigawa kwa Halmashauri. Kwa kufanya hivi Serikali itakuwa imekipatia soko kiwanda hicho na pia kutokomeza ugonjwa wa malaria nchini na hivyo kuokoa fedha nyingi katika kutibia ugonjwa huo na hatimaye kuwa na nguvukazi ya kutosha kwenye ujenzi wa Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hatua nzuri za utekelezaji wa miradi iliyoainishwa pamoja na mingine, bado juhudi za Serikali zinahitajika katika kufufua, kujenga na kuviendeleza viwanda vya uzalishaji kama vile:-

i) Kiwanda cha kuzalisha Magadi Soda –Bonde la Engaruka , Arusha

ii) Kiwanda cha General Tyre – Arusha

iii) Uendelezaji wa Eneo la viwanda TAMCO-Kibaha

iv) Uendelezaji wa Maeneo ya Viwanda KMTC (Kilimanjaro) na Kange (Tanga)

### 3.3 Changamoto za Utekelezaji

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio haya. Kamati inaishauri Serikali kujielekeza katika kuondoa changamoto zifuatazo:-

a) Mwenendo wa utolewaji wa fedha usioridhisha kwenye miradi ya maendeleo. Kamatakwimu zinavyoonyesha hapo juu, hadi mwezi Aprili, 2017 miradi yamaendeleo ilipokea asilimia 38.5 tu ya bajeti iliyoidhinishiwa na Bunge. Fedha za ndani zilitolewa kwa asilimia 41.9 tu wakati fedha za nje zilizopokelewa niasilimia 29.1 tu ya bajeti ya maendelo iliyoidhinishwa.

b) Kutoshirikishwa ipasavyo kwa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kamati inaishauri Serikali kutekeleza miradi yake mingi kwa njia ya PPP badala ya ilivyo sasa. Takwimu zinaonesha kuwa Serikali inagharamia utekelezaji wa miradi mingi kwa wakati mmoja na asilimia kubwa ya miradi hiyo hutegemea kutekelezwa kwa mapato ya ndani ambayo hayatoshi kugharamia miradi yote.

c) Kutoimarishwa kwa mfumo wa uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya miradi. Serikali iliahidi kuimarisha Idara za ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo ili miradi iliyoanzishwa iweze kuleta tija kwa Taifa. Hata hivyo, katika mwaka 2016/17 Tume ya Mipango kwa kushirikiana na sekta husika ilifanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi 32 tu kati ya miradi iliyopo takribani 215.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2016/17

### 4.1 MWENENDO WA MAPATO

### 4.1.1 Mapato ya Ndani

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua jitihada za Serikali katika kuongeza makusanyo ya mapato yake kila mwaka. Takwimu zinaonesha kwamba, hadi kufikia Mwezi Aprili, 2017, mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya Halmashauri yalifikia shilingi trilioni 13.6 sawa na asilimia 73.7 ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 18.46.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na jitihada za Serikali katika kuongeza makusanyo ya mapato, bado kiwango hiki cha makusanyo si cha kuridhisha ukilinganisha na mahitaji makubwa na fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Serikali na pamoja na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ni vema Serikali ikafanya jitihada ya kutafuta maeneo mengine ya vyanzo vya mapato (potential areas) ili iweze kugharamia bajeti yake iliyopangwa na hivyo kukidhi mahitaji halisi ya wananchi. Kwa sasa zaidi ya asilimia 80 ya mapato ya ndani yanatumika zaidi katika kugharamia mishahara ya watumishi na kulipia Deni la Taifa.

### 4.1.2 Mapato ya Kodi na yasiyo ya Kodi

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Aprili 2017 mapato ya kodi yalifikia shilingi trilioni 11.6 sawa na asilimia 77.1 ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 15.1. Sababu kubwa za kutofikiwa kwa lengo la ukusanyaji wa kodi hizi ilielezwa kuwa ni pamoja na kushuka kwa mauzo ya bidhaa mbalimbali katika soko la ndani kama vile saruji, vinywaji baridi na bidhaa nyinginezo za jumla na rejareja, baadhi ya kampuni kupunguza wafanyakazi ili kuendana na hali halisi ya kibiashara pamoja na uzalishaji, kutoongezeka kwa ajira kama ilivyotarajiwa na hivyo kuathiri kodi ya mapato, kushuka kwa uingizaji wa bidhaa nchini, pamoja na kutotumia kikamilifu mashine za kielekroniki (EFD).

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa mapato yasiyo ya Kodi, hadi kufikia mwezi Aprili 2017, Serikali ilikuwa imekusanya kiasi cha shilingi trilioni 1.61 sawa na asilimia 59.8 ya lengo la mwaka la shilingi trilioni 2.69. Aidha, mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yalikusanywa bilioni 399.3 sawa na asilimia 60 ya lengo la shilingi bilioni 665.4.

### 4.1.3 Misaada na Mikopo yenye Masharti Nafuu na ya Kibiashara

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2016/17, Washirika wa maendeleo waliahidi kuchangia Bajeti ya Serikali kwa kiasi cha shilingi trilioni 3.6. Hata hivyo, hadi kufikia mwezi Aprili 2017, shilingi trilioni 2.3 tu ndizo zimepokelewa (sawa na asilimia 65). Hatua hii ya utekelezaji hafifu wa misaada na mikopo toka kwa wahisani kunadhoofisha utekelezaji wa Bajeti. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kukamilisha makubaliano na wahisani mapema ili iweze kupata fedha kwa ajili ya kugharamia bajeti hasa ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu suala la kutoza kodi ya VAT kwenye misaada ya wahisani inabidi liangaliwe upya kwa kuwa wahisani hawakubaliani na utaratibu huu kwa kuwa unapunguza kiwango halisi cha msaada unaopaswa kutolewa.

### 4.1.4 Mikopo ya ndani

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Aprili 2017 Serikali ilikuwa imekopa kiasi cha shilingi trilioni 4.7 sawa na asilimia 87.7 ya shilingi trilioni 5.37 zilizotarajiwa kukopwa kwa mwaka. Kamati inaona kuwa Serikali imeanza kuwa na utaratibu wa kukopa zaidi katika vyanzo vya ndani. Hali hii kiuchumi sio nzuri kwa kuwa taasisi za fedha zinakimbilia kuikopesha Serikali zaidi kuliko sekta binafsi na hivyo kudhoofisha maendeleo ya sekta binafsi.

## 4.2. MWENENDO WA MATUMIZI

### 4.2.1 Matumizi ya Serikali kwa ujumla

**Mheshimiwa Spika**, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/17 Bunge liliidhinisha Bajeti ya shilingi trilioni 29.539. Kati ya fedha hizo shilingi trilioni 6.602 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi trilioni 3.106 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi trilioni 11.820 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Aidha mchanganuo wa matumizi umeainishwa katika jedwali namba 1.

**Jedwali Namba 1: Ulinganisho wa Fedha zilizoidhinishwa na zile zilizotolewa mpaka Mwezi Aprili, 20**

| Na | AINA YA MATUMIZI | BAJETI ILIYOIDHINISHWA | KIASI KILICHOTOLEWA HADI APRILI 2017 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| | **MATUMIZI YA KAWAIDA** | | | |
| 1 | **Mishahara** | **6.60** | **5.32** | **80.65%** |
| 2 | Deni la Taifa | 8.05 | 7.70 | 97.2% |
| 3 | Matumizi Mengineyo | 5.11 | 2.38 | 46.57% |
| 4 | **Jumla Ndogo** | **17.72** | **15.48** | **87.4%** |
| | | | | |
| | **MATUMIZI YA MAENDELEO** | | | |
| 1 | Fedha za Ndani | 8.7 | 3.64 | 42% |
| 2 | Fedha za Nje | 3.11 | 0.907 | 29% |
| | **Jumla Ndogo** | **11.82** | **4.55** | **38%** |
| | **JUMLA KUU** | **29.53** | **20.03** | **67.8** |

**Mheshimiwa Spika,** takwimu zinaonesha kuwa bado tuna changamoto kubwa ya kutekeleza bajeti ya maendeleo (asilimia 38 tu) hasa katika upatikanaji wa fedha za ndani (asilimia 42 tu) na za nje (asilimia 29). Kamati inaipongeza Serikali katika kugharamia matumizi ya kawaida (asilimia 87.4); changamoto kubwa bado ipo katika upatikanaji wa fedha za matumizi mengineyo (asilimia 46.57) ukizingatia kiasi kikubwa cha matumizi ya kawaida kinaenda kulipia mishahara (asilimia 80.65) na Deni la Taifa (asilimia 97.2).

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na Kamati kuchambua utolewaji wa fedha kwa ujumla, bado kuna changamoto kubwa kwenye utolewaji wa fedha kwa baadhi ya mafungu.Kuna baadhi ya Mafungu yalipata fedha za matumizi ya kawaida kwa zaidi ya kiwango kilichoidhinishwa na bunge wakati mafungu mengine yalipata kiasi kidogo sana. Baadhi ya mafungu yaliyopokea zaidi ya kiasi cha bajeti kilichoidhinishwa na Bunge ni pamoja na Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (110.2%), Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Mipango (102.2%), Fungu 67 – Tume ya Ajira (114.5%), Fungu 96 – Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo (122.7%), Fungu 36 – Katavi (126%), Fungu 78 – Mbeya (117.6%). Aidha, Mafungu yaliyopokea fedha kidogo ni pamoja na Fungu 12 - Tume ya Mahakama (44.9%) na Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha (52.5%).

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua ilizochukua ya kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo. Hatua hii imesaidia kuondoa matumizi yasiyo ya lazima na kuziba mianya ya uvujaji wa fedha za umma.

### 4.3 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MASHIRIKA YA UMMA

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Msajili wa Hazina sura 370 kifungu 10(2) (c) vikisomwa pamoja na Sheria ya Bajeti Na 11 ya Mwaka 2015 kifungu cha 17 (a) kinampa majukumu Msajili wa Hazina kuchambua na kuidhinisha mipango na bajeti ya taasisi za umma. Kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Bajeti kifungu (7) (17) na (68); Kamati ya Bajeti ilipitia na kujadili utekelezaji wa bajeti za Mashirika ya Umma Nane (8) ya Umma kati ya Mashirika 271 kama sehemu ya mwanzo wa kutekeleza jukumu hili.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipitia na kujadili mashirika yafuatayo Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO); Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA); Kamisheni ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH); Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC);

Shirika la Bandari Tanzania (TPA); Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC); Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA); Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO). Kwa ujumla Kamati ilibaini yafuatayo:-

### 4.3.1 Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA)

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Shirika hili, Kamati ilibaini kuwa miongoni mwa sababu ya kushuka kwa ukuaji wa ufanisi wa bandari kutoka asilimia 10 hadi 6.7 kwa mwaka, zilikuwa ni pamoja na kuanzishwa kwa himaya moja ya forodha ya mizigo inayoenda DRC Congo; Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye huduma zinazotolewa katika usafirishaji wa bidhaa/mizigo nje ya nchi (*ancillary transport services*); ongezeko la tozo ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa kemikali (kama vile mbolea na sulphur) kutoka Dola za Marekani 100 kwa *bill of lading* hadi Dola moja ya Marekani kwa tani; na kuzorota kwa huduma za reli ya TAZARA na pamoja na TRL kwa maeneo ya Dar es Salaam na ukanda wa shaba (*copper belt*). Hivyo Kamati inaipongeza Serikali kwa kukubali kufanya marekebisho ya Sheria ya Ongezeko la Thamani ikiwa ni pamoja na kufuta kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye huduma zinazotolewa katika usafirishaji wa bidhaa/mizigo nje ya nchi (*ancillary transport services*) kwa lengo la kupunguza gharama za usafirishaji katika bandari zetu. Aidha, Serikali iangalie upya utaratibu wa single Custom Territory pamoja na kuangalia upya tozo ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

### 4.3.2 Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC).

**Mheshimiwa Spika,** Shirika hili lilianzishwa kwa ajili ya kubuni, kuendeleza na kusimamia utekelezaji wa miradi mipya ambayo inatoa mchango mkubwa katika maendeleo ya Taifa. Kamati imebaini kuwa shirika hili halina vyanzo vya mapato vya kuaminika hali ambayo inapelekea kushindwa kutekeleza majukumu yake. Kutokupatikana kwa fedha za kutosha kwa shirika hili kunapelekea kushindwa kusimamia utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati ya maendeleo kama vile Mradi wa Mchuchuma (makaa ya mawe) na

Liganga (chuma ghafi); Mradi wa makaa ya mawe wa Ngaka; Mradi wa kuzalisha Magadi katika bonde la Engaruka; Mradi wa Umeme wa Upepo Singida; kiwanda cha matairi Arusha na Mradi wa Kiwanda cha kuzalisha viuadudu-Kibaha.

**Mheshimiwa Spika**, kimsingi kamati ya bajeti inaona ipo haja ya Serikali kuangalia upya Bajeti ya Shirika hili, ili kuhakikisha tunapata matokeo mazuri ya usimamizi wa utekelezaji wa miradi hii ambayo ni zaidi ya miaka 10 imekuwa ikizungumziwa na kutengewa fedha bila kukamilika. Serikali ije na mkakati wa muda wa ukamilishaji wa miradi hii (time frame).

### 4.3.3 Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA)

**Mheshimiwa Spika,** sekta ya utalii ni eneo muhimu ambalo kama likisimamiwa vizuri litaiongezea mapato Serikali. Hata hivyo takwimu zinaonyesha kuwa Serikali haijaweza kuwekeza vya kutosha katika sekta hii ikilinganishwa na nchi jirani. Mfano mzuri tunauona kuwa wakati nchi ya Kenya imetenga kiasi cha Dola za Marekani Milioni 7 (shilingi bilioni 16) na hawatozi Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye huduma za utalii; Tanzania imetenga kiasi cha shilingi bilioni 7 na tunatoza kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ya kiasi cha asilimia 18 kwenye huduma za utalii pia kuna kodi na tozo. Kamati inaona bado jitihada zinahitajika katika kuongeza mtaji kwa sekta hii pia na kufanya marekebisho ya kodi na tozo mbalimbali zinazotozwa katika sekta hii ili kuongeza mapato ya Serikali. Aidha, bado juhudi za kutangaza vivutio vya utalii vipo chini na inahitaji nguvu ya ziada kufanya hivyo.

### 4.3.4. Shirika la Tume ya Taifa la Sayansi (COSTECH).

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Shirika hili Kamati ilibaini kuwa, limekuwa likipokea kiasi kidogo cha fedha kwa ajili ya shughuli za utafiti. Mfano hadi kufikia mwezi machi 2017 Tume imepokea kiasi cha shilingi bilioni 8.048 tu kati ya shilingi bilioni 23.88 ya fedha iliyoidhinishiwa na Bunge (sawa

na asilimia 34 tu). Kamati inaona kuwa mwenendo huu wa kutoa fedha pungufu kwa Tume kunaathiri majukumu ya msingi ikiwa pamoja na kushindwa kufanya utafiti zaidi pamoja na kushindwa kutoa matangazo mapya ya utafiti. Kamati inaona kuwa ni muhimu Serikali ikahakikisha kuwa inaiongezea fedha tume hii ili iweze kujiimarisha na hatimaye kusaidia katika kuendeleza masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu ambayo ni msingi mkuu wa uendelezaji wa uchumi wa viwanda. Aidha, ikumbukwe kuwa Tume hii ilianzishwa kwa makubaliano ya Azimio la Abuja, Hivyo Kamati inaishauri Serikali kuwa, utoaji wa ruzuku kwa Tume uzingatie utekelezaji wa makubaliano ya Abuja ya kutenga asilimia 1 ya Pato la Taifa kwa ajili ya shughuli za utafiti.

### 4.3.5 Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC),

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania lina jukumu la kusimamia na kuendeleza sekta ya Mafuta na gesi asilia kwa niaba ya Serikali. Katika kuhakikisha hili Sheria ya Petroli ya Mwaka 2015 inaipa Shirika jukumu la kujiendesha biashara katika Shughuli za mkondo wa juu mkondo wa kati na mkondo wa chini. Kwa kipindi cha nusu mwaka wa fedha 2016/17 shirika lilikusanya Shilingi bilioni 80.9 ikiwa ni asilimia 14 ya malengo ya Shilingi bilioni 560.3, kwa upande wa ruzuku, Shirika lilipokea shilingi bilioni 1.4 kwa ajili ya mishahara na OC sawa na asilimia 21 ya bajeti ya bilioni 23.2. Aidha, Kamati ilibaini pia kwa mwaka wa fedha 2016/17 shirika lilikutana na changamoto ya uhaba wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo, upatikanaji wa wateja wa gesi asilia pamoja na madeni ya mauzo ya gesi asilia ya kwa wateja wake, TANESCO, *PAN AFRICAN ENERGY* na Kilimanjaro Oil. Kamati inapendekeza kuwa ni vizuri Serikali iwekeze mtaji wa kutosha kupitia Shirika lake la *TPDC* kwenye suala la gesi ili kupunguza gharama za uzalishaji wa gesi na kutoa unafuu kwa wawekezaji wa viwanda kununua gesi kwa bei nafuu.

### 4.3.6. Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA)

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) ina jukumu la kusimamia Shughuli zote za

Kiuchumi na kiufundi katika Sekta ya Nishati na Maji ili kuhakikisha shughuli katika Sekta hizo zinafanyika bila kuathiri maslahi ya Taifa na wananchi kwa ujumla. Kamati inashauri EWURA iwe na bajeti yake na kiasi kinachokusanywa chote kiingie kwenye mfuko mkuu wa Serikali.

### 4.3.7 Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokuwa ikipitia bajeti ya Shirika hili ilibaini kuwa changamoto kubwa inayoikabili Shirika la Umeme (*TANESCO)* kwa sasa ni gharama za uendeshaji na uzalishaji umeme kuongezeka sana kiasi cha kushindwa kujiendesha kwa faida, pia Shirika lina changamoto ya madeni kiasi kisichopungua shilingi bilioni 800. Kamati inaishauri Serikali kuwekeza kwenye Shirika la TANESCO ili kupunguza gharama za uendeshaji na uzalishaji wa umeme, pia kulitazama upya deni la TANESCO kwa sababu deni hili linazalishwa na Serikali yenyewe kwa maana ya TANESCO linadaiwa na Taasisi za Serikali kama TPDC na Mashirika mengine. Aidha, Serikali ilipe madeni inayodaiwa na TANESCO ili kulisaidia Shirika kuendelea kujiendesha kibiashara kama Sheria inavyotaka. Kamati inapendekeza kuwa fedha zote za kasma ya umeme na maji kwenye bajeti ya Serikali (*Utility)* zilipwe moja kwa moja TANESCO badala ya kupitishia kwenye Wizara na Taasisi za Serikali.

### 4.3.8 Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO)

**Mheshimiwa Spika,** NARCO ni Taasisi ambayo ina rasilimali nyingi za ardhi na mifugo, hivyo ikiendeshwa vizuri itachangia kiasi kikubwa kwenye Pato la Taifa. Kampuni hii imekuwa ikijiendesha kwa ruzuku ya Serikali bila kuonyesha mpango wa uhakika wa kukuza ufanisi wa shughuli zake na hatimaye kushindwa kujitegemea kutokana na hali hiyo, Kamati inapendekeza kuwa NARCO isipewe mkopo wowote hadi itakapo tengeneza mpango mkakati wa kuonesha namna Kampuni hiyo itakavyo jikwamua kiuchumi na kuwa na uwezo wa kujiendesha kibiashara.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 HOJA ZILIZOJITOKEZA WAKATI WA KUCHAMBUA BAJETI YA SERIKALI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (4), ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Bunge ya Bajeti imepewa jukumu la kuchambua mambo muhimu yaliyojitokeza kwenye Kamati za Kisekta wakati wa kujadili utekelezaji wa Bajeti za Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/17 unaoishia tarehe 30 Juni, 2017 na makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha wa 2017/18 unaoanza tarehe 01 Julai, 2017. Tarehe 5 Aprili, 2017 Kamati ya Bajeti ilikutana na Serikali pamoja na Kamati ya uongozi kwa ajili ya kufanya mashauriano kuhusu **hoja 42** zilizowasilishwa kwake. Hivyo, napenda kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa matokeo ya mashauriano hayo ni kama ifuatavyo:

i) **Mheshimiwa Spika, Hoja 21** zilizohusu nyongeza ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mafungu mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2016/17 Serikali imetekeleza kama ifuatavyo:-

a) Fungu 96 – Wizara ya Habari Utamaduni, Sanaa na Michezo (Fedha kwa ajili ya TBC) **shilingi bilioni 1 (OC);** Serikali imetoa fedha yote kama ilivyoahidi.

b) Fungu 46-Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia **(Mlonganzila);** Serikali imetoa kiasi cha **shilingi bilioni 12.5 (Dev)** kati ya **shilingi bilioni 13** ilizoahidi.

c) Fungu 52-Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

- Ununuzi wa vifaa tiba kwa ajili ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili; **shilingi bilioni 1 (OC).** Serikali imeahidi kutoa fedha hizo kabla ya tarehe 30 Juni, 2017.

- Ununuzi wa mitambo na vifaa tiba katika taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI) **shilingi bilioni 3 (OC).** Serikali imeahidi kutoa fedha hizo kabla ya tarehe 30 Juni, 2017.

- Ununuzi wa vifaa tiba katika taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) **shilingi bilioni 2 (OC).** Serikali imeahidi kutoa fedha hizo kabla ya tarehe 30 Juni, 2017.

- Ununuzi wa mitambo ya maabara ya kuzalisha dawa asilia katika taasisi ya magonjwa ya binadamu (NIMR) **shilingi Milioni 800 (OC).** Serikali imeahidi kutoa fedha hizo kabla ya tarehe 30 Juni, 2017.

- Kuendeleza ujenzi wa Jengo la Taasisi ya Ustawi wa Jamii **shilingi Milioni 300.** Serikali imeahidi kutoa fedha hizo kabla ya tarehe 30 Juni, 2017.

d) Fungu 42 - Mfuko wa Bunge. Serikali ilikubali kutoa kiasi cha shilingi **bilioni 6.77** za Fedha za Maendeleo zilizobakia. Kati ya fedha hiyo Shilingi Bilioni 3.5 zimetolewa hadi sasa. Aidha, Serikali ilikubali deni la kiasi cha **shilingi bilioni 5** lilipwe na Hazina. Kati ya fedha hizo Serikali imeahidi kutoa kiasi cha shilingi milioni 897 kwa ajili ya kulipa madeni kiasi na kilichobakia kitalipwa na Hazina.

e) Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) kiasi cha **shilingi bilioni 5** kimetolewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kati ya **Shilingi bilioni 11.39** ilizoahidi.

f) Fungu 62 – Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Serikali imetoa kiasi cha **shilingi bilioni 79.986** kati ya **shilingi trilioni 1.7** hivyo hufanya fedha yote iliyotolewa hadi sasa kufikia shilingi bilioni 709.80.

g) **Fungu 40 -** Mfuko wa Mahakama. Serikali imetoa kiasi cha **shilingi bilioni 5** kati ya **shilingi bilioni 20** zilizoombwa.

h) **Fungu 31-OMR Mazingira**. katika mfuko wa Mazingira Serikali imetoa shilingi **Milioni 500** kati ya **shilingi bilioni 2** zilizoombwa.

ii) **Mheshimiwa Spika, Hoja 21** zilihusu nyongeza ya fedha kwa ajili ya makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2017/18 ambapo maombi yenye jumla ya kiasi cha **shilingi bilioni 86.22** kati ya fedha hizo shilingi **bilioni 46.64** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na **shilingi bilioni 39.58** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa maombi ya fedha za ziada kwa mwaka 2017/18 ni kwamba mpaka sasa Serikali haijatoa mrejesho wowote kwenye **maombi hayo**. Hata hivyo, Serikali inakubaliana na mapendekezo ya Kamati, na imeahidi kwamba itajadiliana na sekta husika ili kubaini vyanzo vya fedha kwa ajili ya kugharamia mahitaji ya mafungu husika. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kufanya *mid year review* kwenye mafungu haya ili kuona utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika,** aidha Kamati ya Bajeti ilipokea **Hoja Tano (5)** zilizojitokeza wakati wa kujadili utekelezaji wa Bajeti za Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/17 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha 2017/18. Hivyo, tarehe 7 Juni, 2017 Kamati ya Bajeti, Kamati ya Uongozi na Serikali walikutana kwa mujibu wa Kanuni ya 105 (1) kwa lengo la kufanya majumuisho kwa kuzingatia hoja hizo. Katika kikao hicho, Serikali ilitoa ufafanuzi kuhusu hoja husika kwa Kamati ya Bajeti na Kamati ya Uongozi. Hivyo basi, baada ya mashauriano hayo napenda kulijulisha Bunge kuwa matokeo ya mashauriano hayo ni kama ifuatavyo:

a) **Fungu 68 - Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano**:- Hoja ilihusu Kampuni ya Simu ya TTCL iongezewe mtaji ili iweze kuchangia Pato la Taifa. Kamati ilikubaliana na hoja hii na kupendekeza kwa kuanzia TTCL ipewe kiasi cha **shilingi bilioni 295.7** (USD 131,994,136) kama mtaji. Majibu ya Serikali hayaonyeshi ni mtaji wa kiasi gani utaipatia TTCL licha ya Serikali kubainisha kuwa itaipatia TTCL masafa ya 800MHz bila ya utaratibu wa mnada ambapo makampuni mengi

yatauziwa masafa hayo. Hata hivyo baada ya mashauriano kati ya Kamati ya Uongozi, Serikali na Kamati ya Bajeti Serikali imelichukua suala hili kwa ajili ya kulifanyia kazi zaidi.

b) **Fungu 68 - Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-** Hoja ilihusu kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga reli ya kisasa kutoka Dar es Salaam-Tanga-Moshi-Arusha –Musoma. Kamati ilipendekeza fedha za mfuko wa Reli zitumike kulipia gharama za upembuzi yakinifu na upembuzi wa kina kwa reli yote kuanzia Tanga kupitia Arusha hadi Musoma na baadaye kuitangaza ili ijengwe kwa njia ya ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi (PPP). Majibu ya Serikali yanaonyesha kuwa imetenga kiasi cha shilingi bilioni 1 kwa ajili ya kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali na ujenzi wa reli hiyo. Pia, Serikali imeelekeza Afisa Masuuli wa Fungu 62 kutumia fedha za Mfuko wa Reli kwa mujibu wa Sheria ya Reli Na 4 ya Mwaka 2002 na Mwongozo wa Uendeshaji wa Mfuko wa Reli wa Mwaka 2005. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali bado Kamati inasisitiza kuwa gharama za upembuzi yakinifu ulipiwe kwa fedha za Mfuko wa Reli.

c) **Fungu 31- Ofisi ya Makamu wa Raisi (Mazingira)** – Hoja iliyowasilishwa ilihusu kuhakikisha Mfuko wa Mazingira unawezeshwa kifedha. Aidha Kamati ya Bajeti ilipendekeza ikatwe asilimia 5 kutoka kwenye vyanzo takribani kumi na moja vinavyohusu tozo mbalimbali za Wizara na Taasisi zinazojihusisha na usimamizi na kulinda mazingira, ili mfuko huu uweze kupata kiasi cha fedha ili uanze kukamilisha majukumu yake (Rejea Bango kitita Kiambatisho Namba 2). Majibu ya Serikali yalionyesha kuwa kiasi cha shilingi bilioni 13.09 kinaweza kupatikana kutoka katika vyanzo husika, hata hivyo Serikali haikuwa tayari kuonyesha kiasi kitakachopelekwa kwenye fungu husika.

Aidha, Serikali imesema itapeleka mapendekezo haya kwenye Kikao cha Baraza la Mawaziri kwa maamuzi katika kipindi cha nusu Mwaka (Desemba, 2017). Pamoja na majibu mazuri ya Serikali Kamati inasisitiza Serikali ifanye mapitio ya mafungu yake na kuhakikisha inapata fedha ili Mfuko huu uanze kufanya kazi zake kwa mujibu wa majukumu yake.

d) **Fungu 52-Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii –** Hoja iliyowasilishwa ni kuwa katika mwaka wa fedha 2016/17 wakati wa mashauriano Kamati ya Bajeti iliomba kupata tathmini ya gharama halisi ya ujenzi wa vituo vya afya na zahanati ili utekelezaji na ujenzi na umaliziaji wa vituo vya afya na zahanati ufanyike katika mwaka wa fedha 2017/18. Mapendekezo ya Kamati yalihusu kupata gharama halisi za ujenzi wa kila kituo na zahanati pamoja na kujua katika mwaka wa fedha 2017/18 Serikali imetenga kiasi gani cha fedha katika kutekeleza jambo hili. Majibu ya Serikali ni kuwa imetenga kiasi cha shilingi bilioni 69 kwa ajili ya kuanza shughuli ya kukamilisha ujenzi wa maboma ya zahanati 1,538 na vituo vya afya 244. Baada ya mashauriano na Serikali, Kamati inakubaliana na majibu ya Serikali, hata hivyo imeshauri Serikali kuanza kutekeleza mradi huu kwa awamu. Vilevile, Serikali iwasilishe Bungeni mpango mkakati wa ujenzi wa maboma ya zahanati na vituo vya afya unaonyesha gharama sahihi za ujenzi na ukarabati wa vituo husika pamoja na ramani itakayopendekezwa kujengwa kwenye maeneo mbalimbali nchini.

e) **Fungu 49 - Wizara ya Maji na Umwagiliaji** – Hoja ilihusu kuongeza bajeti ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa kuongeza tozo ya TShs 50/= kwa Lita 1 zaidi kwenye bei ya Mafuta (Petroli na Dizeli) kwa ajili ya kuboresha zaidi Mfuko wa Maji. Mapendekezo ya kamati ni kuwa katika kiasi kitakachopatikana asilimia 70 ya makusanyo itumike kwa ajili ya kuboresha maji vijijini na asilimia 30 ya makusanyo itumike kwa ajili ya maji mjini. Majibu ya Serikali ni kuwa kuongeza kwa tozo ya shilingi 50 kwa kila lita ya mafuta kutasababisha kupanda kwa gharama za uzalishaji ambazo zitasababisha mfumuko wa bei hivyo kuongeza gharama za maisha ya wananchi. Hata hivyo Serikali imesema itahakikisha kiasi cha shilingi bilioni 408.617 kilichotengwa kwa mwaka 2017/18 kwa ajili ya miradi ya maji husan vijijini kitatolewa. Aidha, Serikali imesema imepata mkopo wa Dola za Kimarekani milioni 268 kwa ajili ya miradi ya maji Tabora, Nzega na Igunga na Dola za Kimarekani 500 kwa ajili ya miradi ya maji miji 16. Pamoja na kutolewa kwa majibu hayo kupitia kikao cha

mashauriano kilichofanyika tarehe 7 Juni, 2017, Serikali imeombwa kuangalia upya suala hili ili kuhakikisha kuwa Mfuko wa Maji unapata fedha za kutosha kutekeleza mradi wa maji vijijini.

## SEHEMU YA SITA

## 6.0 BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2017/18

### 6.1 Sura ya Bajeti

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Serikali itachukua hatua mbalimbali kwa madhumuni ya kujiongezea mapato ya kodi. Hatua hizo ni pamoja na kuongeza viwango vya kodi na tozo mbalimbali**.** Pia Serikali imechukua hatua mbalimbali za kupunguza na kufuta kodi ili **kujenga na kuimarisha uchumi wa viwanda utakao chochea ajira na ustawi endelevu wa jamii na hivyo kuiongezea Serikali mapato.** Kamati ya Bajeti ilipata fursa ya kupitia na kuchambua utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/17 pamoja na ulinganisho wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2017/18. Kamati imefanya uchambuzi huu ili kupata hali halisi ya mwelekeo wa Bajeti ya Serikali na kuona kwamba tunatekelezaje malengo ya bajeti tuliojiwekea. Kuna tofauti kadhaa kati ya sura ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/17 na hii ya mwaka 2017/18. Kumekuwepo na ongezeko au punguzo katika baadhi ya maeneo ya mapato na matumizi kwa asilimia kadhaa kama inavyoonyeshwa katika jedwali hapa chini.


**Jedwali Namba. Ulinganisho wa Sura Ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2016/17 na mwaka 2017/18 (Bilioni)**

**Mheshimiwa Spika,** Sura ya Bajeti 2017/18 inaonyesha kuwa kutakuwepo na ongezeko la kiasi cha shilingi trilioni 2.17 (sawa na asilimia 7) ya jumla ya bajeti yote. Serikali kupitia hotuba yake ya bajeti inapendekeza vyanzo mbalimbali vya kutekeleza malengo yale ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/18. Hata hivyo, kama ilivyokuwa kwa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/17; Kamati inasisitiza Serikali iongeze juhudi ya kupata fedha za ziada ukizingatia kuwa malengo ya

kupata fedha kwa bajeti ya 2016/17 kutoka katika vyanzo mbalimbali ilivyoainisha hayakufikiwa. Tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/17 inaonyesha kuwa hadi kufikia mwezi Aprili 2017 mapato kutoka katika vyanzo vyote yalifikia shilingi trilioni 20.71 sawa na asilimia 70.1 ya lengo la mwaka la shilingi trilioni 29.53 (Rejea ukurasa wa 26 wa hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona kuwa suala la msingi hapa ni namna gani Serikali itaongeza ufanisi katika kukusanya mapato hasa ya kodi na yasiyo ya kodi pamoja na kutafuta vyanzo vipya vya mapato ili kuziba nakisi ya bajeti.

**Kielelezo Na. 1: ULINGANISHO WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2016/17 NA 2017/18**



**Mheshimiwa Spika**, bajeti ya mwaka 2016/17 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2017/18, inaonesha kuwa kwa mwaka ujao wa fedha, Serikali itaongeza mapato ya ndani kwa asilimia 8; mapato ya mamlaka za Serikali za Mitaa yataongezeka kwa asilimia 3; Misaada na mikopo toka nje itaongezeka kwa asilimia 10; mikopo ya ndani itaongezeka

kwa asilimia 4; matumizi ya kawaida yataongezeka kwa asilimia 11 na matumizi ya maendeleo yataongezeka kwa asilimia 2.

### 6.2 Sera za Mapato

**Mheshimiwa Spika**, hotuba ya Bajeti 2017/18, imeainisha hatua mbalimbali zitakazochukuliwa na Serikali katika kuboresha ukusanyaji wa mapato yatakayofikia jumla ya kiasi cha shilingi trilioni 31.71. Kwa upande wa mapato ya ndani Serikali inalenga kukusanya kiasi cha trilioni 19.28; kati ya hizo Mapato ya kodi (TRA) ni shilingi trilioni 17.10 (sawa na ongezeko la asilimia 13); Mapato yasiyo ya kodi shilingi trilioni 2.18 (yamepungua kwa asilimia 19) na Mapato ya Halmashauri shilingi bilioni 687.30 (sawa na ongezeko la asilimia 3) . Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweza kuongeza mapato kwa ajili ya utekelezaji wa malengo yake ya kibajeti. Hata hivyo mwenendo unaonesha kuwa Serikali itategemea zaidi kupata mapato kutoka vyanzo vya ndani vya kodi na visivyo vya kodi. Ni matumaini ya Kamati kuwa ongezeko hili litafikiwa kwa kuongeza ufanisi katika kukusanya mapato toka katika vyanzo vilivyopo na sio kuongeza wingi na viwango vya kodi.


**Mheshimiwa Spika**, Sura ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2017/18 inaonesha kuwa Serikali inategemea kupata mikopo ya ndani kwa utaratibu wa kuuza dhamana na hatifungani za Serikali. Mikopo ya ndani inategemea kuwa kiasi cha shililingi trilioni 7.76 hii ikiwa ni ongezeko asilimia 4 ikilinganishwa na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/17. Kamati inaona kwamba ongezeko la mikopo linaweza kuwa halikwepeki, hata hivyo, ni muhimu kuzingatia athari zake katika kukua kwa Deni la Taifa. Aidha, ni vizuri Serikali ipunguze kutegemea mikopo ya ndani kwani ikizidi itathiri uwezo wa mabenki kukopesha sekta binafsi na hivyo kuathiri ukuaji wa uchumi.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali inategemea kupata kiasi cha shilingi trilioni 3.9 kutoka kwenye misaada na mikopo ya masharti nafuu. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 12.3 ya bajeti ya Serikali, pia ni kimeongezeka kwa asilimia 10 ikilinganishwa

na Bajeti ya Serikali ya mwaka 2016/17. Kamati inajiuliza namna gani Serikali imejipanga kupata fedha za ziada pindi malengo ya misaada na mikopo hayatafikiwa ukizingatia wahisani wamekuwa wakisuasua kutoa fedha zao na hivyo kuathiri utekelezaji wa bajeti mbalimbali zilizopita za mwaka 2015/16 na 2016/17. Mfano mzuri tunauona katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/17, hadi kufikia mwezi Aprili 2017 Serikali imepokea kiasi cha shilingi bilioni 907.8 kati ya shilingi trilioni 3.1 ya ahadi za wahisani kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimkiwa Spika**, Sura ya Bajeti haijaonyesha namna gani Mfuko wa Mapato ya Mafuta na Gesi utapata fedha kutoka katika sekta ya mafuta na Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Gesi ya Mwaka 2015 imeweka utaratibu wa matumizi ya mapato ya mafuta na gesi kwa kutumia masharti ya kibajeti *(fiscal rules)* yanayotoa mwongozo wa kuweka na kutoa fedha kwenye Mfuko kwenda katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kugharamia bajeti ya Serikali, kugharamia uwekezaji wa kampuni ya Mafuta ya Taifa; kuhakikisha utulivu wa kibajeti pamoja na akiba katika vizazi vijavyo.

**Kielelezo Na 2 : ULINGANISHO WA MAPATO YA SERIKALI KWA MWAKA 2016/17 NA 2017/18.**




| | Mapato ya Kodi | Mapato yasiyo na Kodi | Mapato ya Halmashauri | Mikopo ya Masharti Nafuu | Misaada na Mikopo ya Mir... | Misaada na Mikopo ya Kis... | Mikopo ya Masharti ya Kib... | Mikopo ya asilimia 1.5 ya... | Mikopo - Rollover |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2016/17 | 15,10 | 2,693 | 665,4 | 483,0 | 2,745 | 372,1 | 2,100 | 1,597 | 3,777 |
| 2017/18 | 17,10 | 2,183 | 687 | 941,2 | 2,473 | 556,0 | 1,594 | 1,220 | 4,948 |

**Chanzo**: Wizara ya Fedha

## 6.3 Sera za Matumizi


**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2017/18 Serikali imepanga kutumia kiasi cha shilingi trilioni 31.71 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Kati ya fedha hizi kiasi cha shilingi trilioni 19.71 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida (sawa na asilimia 62.17 ya bajeti yote) na shilingi trilioni 11.99 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo (sawa na asilimia 37.81).

**Mheshimkiwa Spika**, takwimu zinaonyesha kuwa matumizi ya kawaida yanazidi mapato ya ndani kwa kiasi cha shilingi bilioni 423 (sawa na asilimia 1.3) ya bajeti yote. Hii maana yake ni kwamba fedha zote tunazokusanya ndani ya nchi kwa kiasi kikubwa zitatosha kugharamia matumizi ya kawaida. Ni vema Serikali ikasimamia vizuri mapato ili kuhakikisha malengo ya matumizi ya kawaida yanafikiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Mfuko Mkuu wa Serikali utatumia kiasi cha shilingi trilioni 6 hii ikiwa ni ongezeko la kiasi cha trilioni 2 (sawa na asilimia 46.8) ukilinganisha na bajeti ya mwaka 2014/15. Mishahara imeongezeka kwa trilioni 1.15 (sawa na asilimia 21.6); Wizara zimeongezew**a** fedha kwa billioni 14.4 (sawa na asilimia 0.4); Mikoa imepunguziwa fedha kwa shilingi bilioni 46.5 (sawa na asilimia 54.8) na Serikali za Mitaa zimepunguziwa fedha kwa shilingi bilioni 34.6 (sawa na asilimia 6.1).

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na hatua hii nzuri ya kugharamia matumizi ya kawaida bado Deni la Taifa (trilioni 9.46) linachukua kiasi cha asilimia 30 ya bajeti yote ya Serikali na linachukua asilimia 48 ya matumizi ya kawaida. Aidha mishahara (trilioni 7.2) inachukua asilimia 36.5 ya matumizi ya kawaida na matumizi mengineyo (trilioni 3.04) yanachukua asilimia 15.5 ya matumizi ya kawaida. Kamati inaona kuwa Deni la Taifa ni mzigo mkubwa katika utekelezaji wa Bajeti ya Serikali na hivyo kuathiri matumizi mengineyo (OC) ya mafungu mbalimbali ambayo yamepungua kwa asilimia 2. Jitihada kubwa zinahitaji ili kuhakikisha ulipaji huu mkubwa wa Deni la Taifa unapungua.

**Kielelezo Na 3: ULINGANISHO WA BAJETI ZA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA 2016/17 NA 2017/2018 (TSh.Bilioni)**




**Chanzo**: Wizara ya Fedha

## 6.4 Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2015/16

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18; Serikali imetenga kiasi cha shilingi trilioni 11.99 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizi kiasi cha shilingi trilioni 8.96 ni fedha za ndani na shilingi trilioni 3.02 ni fedha za nje. Ikilinganishwa na Mwaka wa fedha 2016/17, fedha za maendeleo zimeongezeka kwa kiasi cha takribani shilingi bilioni 179.08 (sawa na asilimia 2).

## SEHEMU YA SABA

## 7.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 7.1 Utekelezaji wa hatua za kodi, ada, tozo na hatua nyingine

**Mheshimiwa Spika**, hotuba ya waziri wa Fedha na Mipango imeanisha mapendekezo ya mabadiliko ya kodi na tozo mbalimbali ambayo pia yatakuwa ni sehemu ya pili ya mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali wakati wa

kujadili Muswada wa Fedha (Finance Bill, 2017). Hivyo, Kamati itatoa maoni kuhusu eneo hili wakati wa kuwasilisha taarifa yake kwenye Muswada huu. Hata hivyo, Kamati inatoa pongezi kwa Serikali kwa kuchukua hatua za kodi, ada, tozo katika baadhi ya maeneo yafuatayo:-

- Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye bidhaa za mtaji (Capital goods) ili kupunguza gharama za ununuzi/uagizaji wa mashine na mitambo ya kuzalishia na hivyo kuvutia uwekezaji katika sekta ya viwanda. Hatua hii ya Serikali itasaidia kuharakisha maendeleo ya sekta ya viwanda hasa katika viwanda vya mafuta ya kula, nguo, ngozi, madawa ya binadamu na mifugo. Hata hivyo kamati inapendekeza kuongeza neno na lisomeke *capital goods and processing chemicals* badala ya kubaki *capital goods* pekee yake.

- Kuondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye huduma zinazotolewa kwenye usafirishaji wa bidhaa/mizigo nje ya nchi (ancillary transport services). Hatua hii itasaidia kupunguza gharama ya usafirishaji bidhaa/mizigo nje pamoja na kusaidia kuongeza shehena za mizigo inayopitia bandari ya Dar es Salaam kwenda nchi za jirani zisizo na bandari na hivyo kuiongezea Serikali mapato. Huu ndio ulikuwa ushauri wa Kamati kwa muda mrefu, kamati inapongeza hatua hii;

- Kusamehe kodi katika maeneo yanayohusu ufugaji pamoja na vyakula vya mifugo, hatua hii itahamasisha kuongezeka ufugaji katika eneo husika na hivyo kusaidia kuinua kipato cha mwananchi na mapato ya Serikali;,

- Kamati inaipongeza Serikali kwa pendekezo la kutoa ada ya asilimia moja (clearing fee) kwa thamani ya madini yanayosafirishwa nje ya nchi, hatua hii itaongeza mapato stahiki ya Serikali. Pamoja na pendekezo hilo kuitwa *clearing fee* linatafsiriwa kuwa ni kutoza mrabaha *(Royalty).* Kamati inaona hatua hiyo inaongeza kiwango cha mrabaha (Royalty) kutoka asilimia 4 hadi asilimia 5. Kamati inashauri Serikali kurekebisha kifungu cha 86 cha Sheria ya Madini ya

Mwaka 2010 kinachohusu ulipaji wa mrabaha ili kuondoa mkanganyiko uliopo;

- Kutoza kodi ya zuio ya asilimia 5 ya bei ya kuuzia kwa wachimbaji wadogo ni hatua inayoongeza mapato stahiki ya Serikali, lakini inatafsiriwa kuwa wachimbaji wadogo watalipa mrabaha wa asilimia 9 na inaweza kusababisha wachimbaji wadogo kufanya biashara haramu. Kamati inashauri Serikali itafute utaratibu tofauti wa kulipa kodi hii bila kuathiri sekta ndogo ya wachimbaji wadogo;

- Kamati inashauri Serikali kuondoa VAT kwenye madini ya vito na bidhaa za usonara (Gems and Jewellery) yanayouzwa ndani ya nchi ili kupunguza bei ya bidhaa hizo nchini kwani vito na bidhaa hizo za usonara zinaposafirishwa na kuuzwa nje zinakuwa hazina VAT. Hatua hii itasaidia biashara hii kukua ndani ya nchi na kuongeza ajira na bidhaa zetu nchini kuwa shindani ukilinganisha na bei za nje. Badala ya Serikali kutoza VAT itoze Royalty ya asilimia 7 au 8 ili kuongeza mapato kwenye madini ya vito;

- Marekebisho ya ushuru wa bidhaa kwenye maeneo mbalimbali ya sekta ya kilimo yatasaidia kuhamasisha uzalishaji na kulinda viwanda vya ndani pamoja na kuhamasisha kilimo cha matunda kama malighafi kwa viwanda vya ndani; na

- Kufutwa kwa ada ya mwaka ya leseni ya magari (annual motor vehiscle licence) imeondoa kero kubwa kwa wananchi na hivyo kurudisha imani kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Hatua hii itaiongezea mapato Serikali kuliko ilivyokuwa awali. Kamati inashauri Serikali kutumia kiasi cha shilingi 40 kinachopendekezwa kutozwa katika kila lita moja ya petroli , Dizeli na Mafuta ya Taa kipelekwe kwenye Mfuko wa Maji kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji vijijini kwa asilimia 70 ya tozo na mijini asilimia 30 ya tozo. Pia Kamati inaishauri Serikali kuitumia Wakala wa Uchimbaji Visima na Mabwawa (DDCA) kikamilifu katika utekelezaji wa miradi ya maji mijini na vijijini ikiwa ni pamoja na kuiwezesha Wakala hii ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, hatua zilizochukuliwa na Serikali ni nyingi na ni rafiki kwa mwananchi ambaye ana nia ya kufanya biashara hata hivyo bado kuna maeneo mengine ya kodi, ada na tozo ambayo Serikali iyachukue na kuangalia namna ya kuyafanyia kazi katika Sheria ya Fedha inayokuja. Maeneo hayo ni haya yafuatayo:-

**i)** Iangalie upya utekelezaji wa kulipa asilimia 15 ya ushuru wa forodha kwa makampuni yanayoagiza sukari ya viwandani ambayo baadae inatakiwa irudishwe kama *refund* kwa makampuni hayo. Changamoto kubwa iliyopo hapa Serikali imekuwa hairudishi *refund* hizo kwa wakati na hata pendekezo la kuweka Escrow Account bado halijibu changamoto hii kwa kuwa mapaka sasa Serikali imeshikilia kiasi cha takribani bilioni 20 ambazo zinawagharimu wenye viwanda kiasi cha shilingi milioni 400 kila mwezi kama riba kutoka kwenye mabenki. Madhara ya jambo hili ni pamoja na kuongezeka gharama za uzalishaji, inapunguza uwezo wa kampuni kuwekeza na kwa mwaka huu mmoja imesababisha kupunguza zaidi ya ajira 700. Aidha, Kamati inaamini kwamba mifumo ya Serikali ya usimamizi wa uagizaji wa Sukari ya Viwandani kwa sasa imeimarishwa vya kutosha.

**ii)** Ushuru wa bidhaa (Excise Duty) wa asilimia 17 kwenye *'Electronic Communication Services';* Kamati inapendekeza irudi asilimia 14 badala ya 17 ilivyo sasa kwani nchi za jirani mfano Kenya inatoza asilimia 10, Uganda inatoza asilimia 12, Burundi inatoza asilimia 0 na Rwanda inatoza asilimia 8.

**iii)** Kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2016, makampuni ya simu yalitakiwa yawe yamejisajili katika soko la hisa la Dar es Salaam ifikapo tarehe 31 Desemba 2016. Mpaka sasa ni kampuni moja tu ambayo imefikisha hisa zake sokoni. Hali iliyojitokeza ni kutokana na elimu ndogo juu ya uwekezaji kwenye hisa, hali ya uchumi na mwitikio mdogo wa wananchi. Hata hivyo, Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi wa kuwapa watanzania fursa ya kumiliki na kukuza uchumi kupitia soko la hisa na kuongeza uwazi katika

uendeshaji wa Sekta ya Mawasiliano nchini. Pamoja na uamuzi huo mzuri, Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

(f) Sheria hiyo ifanyiwe marekebishon ili kiwango cha chini cha hisa kwa watanzania kianzie asilimia 15 badala ya 25 na bila ya kuweka ukomo wa juu. hii itatoa fursa kwa kampuni za simu kujitathmini na kuendelea kuhamasisha ununuzi wa hisa kadiri soko linavyoendelea kukua na hali ya uchumi inavyobadilika pamoja na uhitaji wa mitaji kwa shughuli za uwekezaji wa kampuni za simu;

(g) Serikali ifikirie kuruhusu kufungua soko kwa watu wa nje kununua na kuuza hisa ukizingatia kuwa zaidi ya asilimia 50 ya soko letu linahusisha wageni *'foreigners';*

(h) Serikali ibadilishe tafsiri ya maneno ***'listed shares'*** katika kanuni za Sheria ya Soko la Mitaji la Dar es Salaam (DSE) ya Mwaka 2014. Sheria itambue hisa zote za kampuni zilizoandikishwa kwa mujibu wa Sheria ya mitaji na dhamana. Kwa mujibu wa kanuni ***'listed shares are those shares listed and traded at stock exchange'***. Inapendekezwa msingi wa tafsiri hii Kanuni uhamishiwe kwenye Sheria ya kodi ya mapato (Income Tax Act) na isomeke kwamba ***'listed shares are those shares of a listed company whose minimum requirement is listed at DSE'***. Kamati inaona tafsiri hii itasaidia Serikali kudhibiti miamala (transactions) za mauziano ya hisa ambazo hazitatakiwa kupelekwa kwenye soko la hisa kisheria. Mwenendo unaonyesha kuwa baadhi ya makampuni yamekuwa na tabia ya kuuziana hisa nje ya nchi bila mamlaka zetu za ndani kuwa na taarifa na hivyo kuikosesha Serikali mapato;

(i) Kuboresha tafsiri ya kipengele (e) cha Sheria ya Kodi ya Mapato (Income Tax act) cha neno *Investment assets* ili kuendana natafsiri halisi ya neno listed shares ili isomeke ***'Shares and Securities of the Listed Company at DSE'***;

(j) Kuhusu *Capital Gain Tax* (CGT) kwenye soko la hisa (DSE) linapendekezwa lifutwe na badala yake iwekwe *Security*

*Transaction Tax* (STT) kama ilivyopitishwa na Bunge wakati wa Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2016.

**iv)** Kodi ya Ongezeko la Thamani ya asilimia 18 kwenye huduma za kibenki (VAT). Utekelezaji wa kodi hii umekuwa ukimuumiza mtumiaji wa mwisho (Mwananchi) kinyume na maelezo ya Serikali. Pia gharama za uendeshaji kwenye mabenki zimeongezeka kiasi cha kwamba amana kwenye mabenki zimepungua na gharama za mikopo zimeongezeka na hivyo kuendelea kumuathiri mtumiaji wa mwisho ambaye ni mwananchi.

**v)** Kamati inapongeza pendekezo la Serikali la kufanya marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, SURA 290 ili kupunguza ushuru wa mazao (produce cess) unaotozwa na Halmashauri za wilaya nchini kutoka kiwango cha sasa cha asilimia 5 ya thamani ya mauzo hadi asilimia 3 kwa mazao ya biashara na asilimia 2 kwa mazao ya chakula. Hata hivyo Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuweka kiwango kimoja cha ushuru huu kwa kiwango cha asilimia 3 kwa mazao yote bila kutofautisha mazao ya biashara na mazao ya chakula. Hatua hii itampatia mkulima unafuu mkubwa na kuondoa mkanganyiko unaoweza kutokea kwa kutofautisha mazao ya biashara na ya chakula. Aidha, kamati inapendekezakufutwa kwa ushuru kwenye mbegu zinazozalishwa nchini.

**vi)** Kamati inapongeza pendekezo la Serikali la kupunguza kiwango cha Kodi ya Mapato ya Kampuni (Corporate Income Tax)

**vii)** Kuhusu miradi inayochelewa kutekelezwa mfano Mradi wa Mchuchuma na Liganga ambayo imekwama kutekelezwa kutokana na kutopata muafaka wa vivutio vinavyoombwa na mwekezaji katika mradi huu. Hali hii inasababishwa na maamuzi ya Serikali ya kumuuondolea Waziri wa Fedha na Mipango uwezo wa kutoa msamaha wa Kodi katika Sheria mbalimbali. Kamati inaishauri Serikalikufanya marekebisho kwenye Sheria husika ili kurejesha mamlaka ya Waziri kama taasisi kutoa misamaha ya kodi

kwa miradi yenye tija kwa Taifa na hivyo kurahisisha utekelezaji wa miradi husika.

**Mheshimiwa Spika**, haya ni baadhi tu ya mapendekezo ya Kamati katika eneo la kodi, ada na tozo, mapendekezo mengine yatawasilishwa wakati wa kupitia na kuchamua Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2017.

### 7.3. Mfuko wa Mapato ya Mafuta na Gesi (Oil and Gas Fund)

**Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi ya Mwaka 2015 imetoa masharti ya kibajeti yatakayowezesha Mfuko wa Mapato na Gesi kupata mapato ambayo yatachukuliwa kama sehemu ya kugharamia nakisi ya bajeti (asilimia 3 ya Pato la Taifa), kugharamia miradi ya maendeleo inayohusiana na uwekezaji wa mafuta na gesi pamoja na kutunza kiasi cha mapato hayo kwa ajili ya kizazi kijacho. Hata hivyo, mpaka sasa Serikali haijawa na maelezo ya kuridhisha kuhusu uwepo wa mfuko huu na kiasi cha fedha kilichopo. Kamati inaona kuwa ni vema Serikali ikalichukulia jambo hili kwa umuhimu mkubwa ili kuweza kusaidia maendeleo ya nchi yetu kuwa endelevu.

### 7.4. Mapitio ya Sheria za Ubia na Uwekezaji

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuhaulisha Sheria zote zinazohusiana na masuala ya Uwekezaji pamoja na ubia nchini. Mfano Tanzania Investment Act 1997, Export Processing Zone Act 2006, Mining Act 2010, Public Private Partnership Act, 2010 na Public Procurement Act, 2011. Kuhaulishwa kwa Sheria hizi kutahamasisha sekta binafsi kutoka ndani na nje ya nchi kushiriki katika utekelezaji wa Miradi mbalimbali ya maendeleo kwa sababu taratibu za uwekezaji na ubia katika Sekta mbalimbali zitakuwa chini ya mwavuli mmoja. Kupitia Sheria hizi Sekta ya Umma kushirikiana na Sekta Binafsi zitapata fursa za kujenga, kuendesha na kuwekeza katika miradi muhimu ambayo itasaidia kutoa huduma za kijamii na kiuchumi na kuwawezesha wananchi kupata ajira na kuongeza kipato kupitia miradi hiyo ya uwekezaji na ubia.

### 7.5. Ugharamiaji wa miradi ya maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini mwenendo usioridhisha wa utoaji wa fedha kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Tathmini inaonesha katika Bajeti iliopita, pamoja na kuwa Serikali iliainisha vyanzo vya fedha katika kugharamia miradi mbalimbali ikiwemo ile ya kitaifa ya kimkakati, bado fedha hizo hazikupatikana kwa wakati uliopangwa au kutofika kabisa na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi husika. Takwimu zinaonyesha hadi kufikia mwezi Aprili 2017 kiasi cha shilingi trilioni 4.5 kilikuwa kimetolewa sawa na asilimia 38.5 ya bajeti ya maendeleo (trilioni 11.8) ukijumuisha fedha zilizokuwa zimetolewa na halmashauri. Kamati inashauri kuwa Serikali kubadili mtazamo wake kuhusu kutekeleza miradi ya maendeleo kwa fedha zake yenyewe badala ya kutegemea fedha za wahisani kwa kiwango kikubwa. Ni vema Serikali ikatekeleza miradi michache ya kimkakati ambayo sekta binafsi imeshindwa kuitekeleza. Miradi mingine yote Serikali ishirikishe Sekta Binafsi kwa njia ya Ubia au kwa kuweka mazingira bora kuiwezesha Sekta binafsi kuitekeleza yenyewe.

### 7.6. Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya mdhibiti na Mkaguzi mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2016 inayozungumzia taarifa za fedha zinazohusu Taasisi za Serikali kuu na Ukaguzi wa Mashirika ya Umma imeainisha mapungufu mbalimbali yanayoonekana katika eneo la manunuzi na mikataba, madeni, matumizi yasiyokuwa na nyaraka na vithibitisho pamoja na makadirio ya kodi ambayo hayajakusanywa. Kamati inashauri Serikali kuzingatia ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika maeneo yote yaliyoanishwa na Serikali ichukulie hatua inayostahili.

### 7.7. Taasisi za zinazohusika na shughuli za udhibiti

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali iangalie uwezekano wa kuunganisha taasisi zinazojihusisha na

shughuli za udhibiti kama vile TBS, TFDA, OSHA, TOSCI, WAKALA WA VIPIMO na nyinginezo zinazotoa huduma hizo na kutoza tozo na ada mbalimbali na hivyo kuwa na utitiri wa tozo na kuleta usumbufu wa kurudia kazi zinazofanana. Kuunganishwa kwa taasisi hizi chini ya mwamvuli mmoja kutaondoa ukiritimba na usumbufu kwa wafanyabiashara na hivyo kuokoa muda na kuongeza uzalishaji

### 7.8. Ukusanyaji wa Kodi katika vyanzo mbalimbali vilivyoainishwa

**Mheshimiwa Spika**, hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango imeanisha maeneo mbalimbali yatakayosaidia kupatikana kwa mapato ya Serikali. Kamati inashauri Serikali kufanya tathmini ya vyanzo husika ili kuona kama vitatimiza malengo ya mapato yaliyokusudiwa kwa kuwa vyanzo vingine vimekuwa havikidhi haja. Aidha, Serikali iongeze juhudi za kuongeza mapato kwa kufanyia kazi mapendekezo ya vyanzo vipya vya mapato ambavyo vimekuwa vikipendekezwa mara nyingi na Kamati ya Bunge ya Bajeti na wabunge kwa ujumla. Hatua hii itasaidia kupunguza utegemezi kutoka kwa wafadhili kughamia bajeti ya Serikali.

### 7.9 Uimarishaji wa mifumo ya ukusanyaji wa mapato

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuimarisha mifumo mbalimbali ya ukusanyaji wa mapato kwa njia za kieletroniki kama ile ya *Government e-payment gateway system, electronic revenue collection system (e-RCS)* na mingine. Hatua hii itasaidia kudhibiti mianya ya upotevu wa fedha pamoja na kupunguza urasimu katika ulipaji wa fedha (Kodi, ada na tozo). Pia, Kamati inasisitiza Serikali kuhakikisha matumizi ya EFD's yanaimarishwa katika sekta za umma na binafsi ili kusaidia ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

### 7.10. Hoja za kibajeti zilizowasilishwa na Kamati za kisekta

**Mheshimiwa Spika,** hoja hizi za Kamati za Kisekta zilizowasilishwa ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu. Ni

vema Serikali ikatambua kuwa kutokutekeleza hoja hizi ambazo kimsingi zimo ndani ya Bajeti ya Serikali ni kulirudisha nyuma Taifa katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kamati bado inatoa wito Serikali kuhakikisha inatekeleza ahadi zake za kutoa fedha bila kuathiri kuathiri Sura ya Bajeti inayopendekezwa. Hii inamaanisha kwamba ukomo *(ceiling)* wa Bajeti ya Serikali kwa baadhi ya mafungu uangaliwe upya ili kukidhi mahitaji hayo ya ziada

### 7.11. Uzingatiaji wa Majukumu ya Kamati ya Bajeti na Sheria ya Bajeti

**Mheshimiwa Spika,** uwepo wa Kamati ya Bajeti unasaidia Bunge lako tukufu kuelewa mchakato mzima wa Bajeti ya Serikali katika hatua zote za kibajeti yaani uandaaji, uidhinishaji, utekelezaji, ufuatiliaji pamoja na tathmini. Kamati inaikumbusha Serikali kuzingatia Sheria ya Bajeti katika kutekeleza majukumu ya kibajeti. Aidha mabadiliko yoyote yanayoletwa na Serikali kuhusu marekebisho ya Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015 yapitishwe kwenye Kamati ya Bajeti.

### 7.12. Utalii

**Mheshimiwa Spika,** Kamati baada ya kupitia taarifa ya Hali ya Uchumi na Taifa kwa Mwaka 2016 na Mapendekezo ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2017/18 haijaona sekta ya utalii ikipewa uzito unaostahili. Sekta hii kwa mwaka wa fedha 2014/15 ilichangia asilimia 17.5 ya Mapato ya Nje na Mwaka 2015/16 ilichangia asilimia 14. Hii ni taswira ya sekta hii kuendelea kushuka katika uchangiaji wa Pato la Taifa.Sekta hii pia inakabiriwa na changamoto za kisheria na kimkakati. Kamati inashauri yafuatayo:-

- VAT kwenye huduma za kitalii ziondolewe. Tozo hii inaongeza gharama kwenye huduma za kitalii

- Mapato yatokanayo na uwindaji wa kitalii yanachangia asilimia 25 ya Mapato yanayotokana na utalii. Serikali iangalie uwezekana wa kuondoa tozo na kodi zinazotozwa kwa wawindaji na kampuni za uwindaji ili nchi

yetu iweze kushindana na kuwa kivutio kwenye biashara hiyo.Sheria ya Uwindaji iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2009/ 10 ambayo inataka asilimia 85 ya maeneo ya uwindaji wapewe wazalendo ibadilishwe ili kuruhusu wawekezaji wa nje kushirikiana na wawekezaji wa ndani katika kufanya biashara hiyo.

- Kichocheo kimoja wapo cha kukuza sekta ya utalii ni usafiri wa anga. Serikali imefanya jitihada kubwa kuwekeza kwenye usafiri wa anga lakini tozo (Railway Development Levy) iliyowekwa kwenye Sheria ya Reli ya Mwaka 2002 kwenye mafuta ya ndege (JET A-1) imekuwa ikiongeza gharama ya ununuzi wa mafuta ya ndege nchini kuliko nchi za jirani za Kenya na Uganda ambazo hazina tozo hii. Kamati inapendekeza Sheria hii ifanyiwe marekebisho ili kuondoa tozo hiyo kwenye mafuta ya ndege ya JET A - 1.

### 7.13 Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye huduma za meli za mizigo zinazoingia Nchini

**Mheshimiwa Spika,** meli zinazoleta mizigo kutoka nje ya nchi zimekuwa zikitozwa VAT kwa huduma zinzofanywa kupitia wakala wa meli hizo, wakati huduma ya aina hii kwa nchi za ukanda wa bahari ya hindi hazitozwi VAT na hivyo kusabisha meli nyingi kukwepa kupitisha mizigo yao katika bandari ya Dar es Salaam hali inayosababisha kupungua kwa mizigo inayohudumiwa kupitia bandari hii. Kamati inashauri serikali kuondoa kodi hiyo ili kuongeza matumizi ya bandari yetu na kuimarisha ushindani na nchi jirani.

### 7.14 Deni la Taifa:

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia 2017 Deni la Taifa linalojumuisha deni la Serikali na deni la nje la sekta binafsi lilifikia shilingi trilioni 50 ikilinganishwa na trilioni 39.27 Machi 2016. Deni hili ni sawa na asilimia 41.3 ya Pato la Taifa ambalo ni shilingi trilioni 103.74. Kati ya kiasi hicho, Deni la Serikali ni shilingi trilioni 42.9 na Deni la Sekta Binafsi ni shilingi trilioni 7.9.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwa deni hili ni himilivu kwa vigezo vyote bado limekuwa ni mzigo mkubwa kwa Taifa letu na limeanza kuwa tishio kwa utengamavu wa uchumi jumla. Deni hili limeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na kuongezeka kwa mikopo isiyo na masharti nafuu kunakopelekea kuongezeka kwa gharama za kuhudumia deni.

Mathalani, kiasi cha shilingi trilioni 5.2 kililipwa katika mwaka 2015/16 kama gharama za kuhudumia Deni la Taifa kikiwa kinajumuisha marejesho ya mkopo, riba na malipo mengine yanayohusu Deni hilo. Malipo haya ni makubwa ikilinganishwa na fedha inayobaki kugharamia huduma za kijamii na miradi ya maendeleo. Kamati inashauri kuwa;

- Serikali iangalie fursa zilizopo za kuimarisha uhimilivu wa deni la Taifa ikiwa ni pamoja na kufanya majadiliano na wakopeshaji wa Kimataifa ambao ni pamoja na Benki ya Dunia kwa madhumuni ya kupata masharti nafuu kwa Deni la Taifa (Debt Reprofiling) kama walivyofanya wenzetu wa Kenya na Ghana.

- Serikali kuishirikisha Sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo yenye mtizamo wa kibiashara.

- Kuifanyia nchi tathmini ya uwezo wa kukopa (Sovereign Credit Rating)

### 7.15 Sekta isiyo Rasmi

**Mheshimiwa Spika,** mchango wa Sekta isiyo rasmi kwenye ukusanyaji wa mapato sio wa kuridhisha kutokana na kutokuwepo kwa takwimu sahihi na kubainshwa kwa walipa kodi kupitia sekta hiyo. Hivyo, kamati inashauri Serikali kubuni mbinu mathubuti pamoja na kuweka mifumo

itakayowezesha Serikali kupata mapato kutoka kwenye Sekta isiyo rasmi.

## SEHEMU YA NANE

## 8.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa bajeti umeonesha kwamba bajeti imejaribu kugusa maeneo ya msingi ya uwezeshaji wananchi kiuchumi pamoja na kutoa fursa kwa wafanyabiashra na wenye viwanda kuwekeza kwa kuzingatia fursa waliyopata kupitia kupunguzwa ama kufutwa kwa kodi na tozo mbalimbali zilizoainishwa. Nia ya Serikali ni kuhakikisha inapata mapato pasipo kuwepo na kero kutoka kwa wadau wa kodi.

Hata hivyo kuna baadhi mapendekezo huenda yakaleta changamoto katika utekelezaji wake. Hivyo ni vyema wananchi wakaelewa kwamba nia ya Serikali ni kuboresha huduma kwa umma na huduma hizi zina gharama. Ni matarajio ya Kamati ya Bajeti kwamba gharama zinazolipwa na wananchi kwa njia ya kodi, zinaenda kuboresha maisha ya wananchi kulingana na matarajio yao.

## SEHEMU YA TISA

## 9.0 SHUKRANI

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa mara nyingine kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Napenda nimshukuru Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dk. Philip I. Mpango; Naibu Waziri wake Mhe. Dkt. Ashatu K. Kijaji na wataalam wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao walioutoa kwa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Mheshimiwa Josephat S. kandege; Makamu Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao katika kujadili na kutoa mapendekezo mbalimbali

yaliyohusu uchambuzi wa Bajeti ya Serikali. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo;

1) Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, Mb – Mwenyekiti
2) Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb - M/ Mwenyekiti
3) Mhe. Hamida Mohamedi Abdallah, Mb
4) Mhe. David Ernest Silinde, Mb
5) Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
6) Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
7) Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb
8) Mhe. Susan Peter Maselle, Mb
9) Mhe. Agustino Manyanda Masele, Mb
10) Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
11) Mhe. Flatei Gregory Massay, Mb
12) Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
13) Mhe. Janet Zebedayo Mbene, Mb
14) Mhe. Cecil David Mwambe, Mb
15) Mhe. Susana Chogisasi Mgonukulima, Mb
16) Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb
17) Mhe. Juma Hamad Omar, Mb
18) Mhe. Ali Hassan Omari, Mb
19) Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
20) Mhe. Jerome D. Bwanausi, Mb
21) Mhe. Jitu Vrajlal Soni, Mb
22) Mhe. Abdallah M. Bulembo, Mb
23) Mhe. Andrew John Chenge, Mb
24) Mhe. Mussa A. Zungu, Mb
25) Mhe. Japhet Ngalilonga Hasunga, Mb
26) Mhe. Dalali Peter Kafumu, Mb
27) Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb
28) Mhe. Joseph Roman Selasini, Mb

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kuchukua fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Dr. Thomas Kashililah na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kuishukuru Idara ya Bajeti ikiongozwa na Ndg. Lina Kitosi

Mkurugenzi; Ndugu Michael Kadebe Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Uchambuzi wa Bajeti; Ndugu Mathew Kileo Mkurugenzi Msaidizi sehemu ya Vyanzo vipya vya Mapato; na Sekretarieti ya Kamati ikiongozwa na Makatibu wa Kamati Ndugu Godwin Godfrey, Maombi Kakozi na Lilian Masabala kwa utaalamu wao wa uchambuzi na kuihudumia vema Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha.

**Hawa Abdulrahman Ghasia (Mb)**
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**
**12/06/2017**

**MWENYEKITI:** Sasa namuita Msemaji wa Kambi Rasmi Bungeni awasilishe. Ngoja kidogo Mheshimiwa Silinde kaa kwanza.

Waheshimiwa Wabunge nadhani mmepokea taarifa hizi, taarifa ya Kamati ya Bajeti mnayo.

**WABUNGE FULANI:** Hatuna.

**MWENYEKITI:** Bado, lakini kwa *record* za *Hansard* imewasilishwa rasmi, hii hapa na ndiyo Kanuni, Kanuni zimetekelezwa.

La pili kwa upande wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na wenyewe wametekeleza hii hapa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa vile hamna hiyo nakala; lakini zitakuja; kuna maelekezo ya Mheshimiwa Spika baada ya kuipitia...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Tulieni! Baada ya maelekezo ya Mheshimiwa Spika, hotuba ni nzuri tu wala hamna matatizo. Ila kwenye ukurasa wa 18(vii), ukiwa na hii ni *paragraph* ya tatu, maelekezo ni kwamba hiyo sentensi ya mwisho kwenye *paragraph* ya tatu (vii) Mheshimiwa Silinde i-*note* hapo, imeshaondolewa. Siyo lazima uijue wewe. *(Kicheko)*

Tunaenda *paragraph* ya 10 ambayo kwenye hii itakuwa ukurasa wa 70, *paragraph* 10.1 Ibara yote ya 10.1 imeondolewa kwa maelekezo ya Mheshimiwa Spika. Kwa hiyo, utaanza na Ibara ya 10.2.

Kwenye Ibara ya 10.6 katika aya ya mwisho sentensi yote ya hiyo ibara ambayo inaanza na maneno: *"ni wazi kwamba...."* inaendelea na kuhitimisha *"...na hii ndiyo changamoto kwake."* yameondolewa.

Waheshimiwa Wabunge, mwisho kwenye eneo la taarifa hii kwenye Ibara ya 10.10 ambayo inahusu Utawala bora, sentensi ya mwisho ya Ibara ya pili ya taarifa inayoanzia na maneno: *"Mheshimiwa Spika, kibaya zaidi..."* inaendelea na kumalizia: *"...kuhusu uwezo wake wa kukopa."* Hayo maneno kwa *paragraph* hiyo na yenyewe yameondolewa kwa mujibu wa kanuni zetu za Bunge.

Baada ya kusema hayo Mheshimiwa David Silinde, sasa nakutaka sasa uwasilishe hoja yako kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani. *(Makofi)*

**MHE. DAVID E. SILINDE - NAIBU MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza kuwasilisha hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani nimepata hayo maelekezo na nilitumiwa hii *memo* hapa, wameondoa

maeneo mengi, lakini lengo la hotuba yetu ilikuwa ni kuisaidia Serikali. Hotuba yetu ina kurasa 201 na tunawasilisha kurasa 201 ili Serikali isome na kwa sababu kuna mlundiko wa matatizo kwenye hili Taifa tutaendelea kujaza ili mambo yaendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Halima James Mdee, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa, Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatoa maoni hayo, napenda kutumia fursa hii kipekee kutoa pole nyingi kwa *CHADEMA Family* na UKAWA, kwa kuondokewa na mmoja wa waasisi wa CHADEMA, Mzee Philemon Ndesamburo aliyefariki dunia tarehe 31 Mei, 2017 huko Moshi, Kilimanjaro na hatimaye kupumzishwa katika nyumba yake ya milele tarehe 6 Juni, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa limepoteza mwanamageuzi wa karne, aliyekuwa tayari kupoteza maisha yake kwa ajili ya mabadiliko ya kweli ya kisiasa, kiuchumi na kijamii katika Taifa letu. Kama chama tutamkubuka kwa kuyaenzi yale yote aliyoyaasisi kwa mustakabali mwema wa chama chetu na Taifa kwa jumla. Hakika ni vigumu kuziba pengo aliloliacha, Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema, peponi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya salamu hizo za rambirambi, naomba nitambue mchango uliotukuka wa Mheshimiwa Halima James Mdee, ambaye ndiye Waziri Kivuli mwenye dhamana ya kuisimamia Serikali katika masuala ya Fedha na Mipango, kwa kufanya kazi usiku na mchana, kufanya tafiti na uchambuzi wa nyaraka mbalimbali na kupata takwimu ambazo zimejenga msingi wa hotuba hii kwa zaidi ya asilimia 90. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti na nchi zinazoendelea ambapo watu wenye upeo na weledi wa kufanya kazi namna hii huenziwa na kujengewa mazingira mazuri ya kuwa bora zaidi. Katika nchi zinazoendelea watu wa aina hii hukumbana na madhila mengi ikiwa ni pamoja na kuwekwa vizuizini kwa sababu tu ya ujasiri wao wa kuisimamia na kuikosoa Serikali tena katika misingi ya kikatiba na kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutofautiana kifikra ni afya ya akili na ili uvumbuzi utokee lazima uwe na fikra mbadala *(alternative thinking).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilidhani kuwa Serikali na Chama cha Mapinduzi wangetambua kuwepo wa watu wenye fikra mbadala katika Taifa hili, ni tunu na zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu, lakini badala yake Serikali wameona kuwa uwepo wa watu hao ni kama mwiba na kikwazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kunukuu maneno ya kitabu cha mwasisi wa Taifa la Afrika ya Kusini Hayati Nelson Mandela *"No Easy Walk To Freedom"* kama maneno ya faraja kwa Wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni waliopatwa na madhila mbalimbali kwa nyakati tofauti ikiwa pamoja na kufungiwa kuhudhuria vikao vya Bunge au kuadhibiwa kwa namna moja ama nyingine wakati wakitekeleza majukumu yao ya kibunge, kwamba wasifadhaike kwa kuwa imewapasa kupitia njia hiyo, ili kufikia lengo lililo kubwa zaidi la kutwaa madaraka ya dola kwa njia ya kidemokrasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, sasa naomba nitangulize *bashraff* ya Bajeti ya Serikali iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kupata idhini ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge ambao kwa umoja wao walisema

kuwa bajeti hii haijawahi kutokea katika historia ya hivi karibuni ya bajeti za Serikali. Kambi Rasmi ya Upinzani inakiri kwamba ni kweli haijawahi kutokea bajeti ya namna hii na kwamba bajeti hii imevunja rekodi kwa sababu zifuatazo:- *(Makofi)*

Moja, Bajeti hii ni bajeti ambayo takwimu za vitabu vyake vyote vya matumizi *Volume I, II, III* na *IV* zinatofautiana sana. Pia sura ya Bajeti iliyosomwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango inatofautiana pia na vitabu hivyo. Wakati kitabu cha Mapato ya Serikali kinaonesha kuwa Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018 itakusanya jumla ya shilingi trilioni 23.9, kitabu cha Matumizi ya Serikali kinaonesha kuwa Serikali inakusudia kutumia jumla ya shilingi trilioni 26.9 ikiwa ni ongezeko la matumizi ya shilingi trilioni tatu ambayo vyanzo vyake havijaonyeshwa kwenye kitabu cha mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo, sura ya bajeti iliyosomwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango inaonesha kuwa bajeti ya Serikali kwa maana ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni kiasi cha shilingi trilioni 31.7, kiasi ambacho hakionekani popote katika vitabu vya mapato na matumizi ya Serikali. Hali kadhalika kwa mujibu wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano tarakimu hii ya shilingi trilioni 31.5 inaonekana kwamba ni makisio ya bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Hivyo, sasa hivi tunaekeleza mapendekezo ya mpango kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na siyo 2017/2018. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inakiri kabisa kwamba hii haijawahi kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, hii ni bajeti ambayo imedhamiria kuua kabisa dhana ya ugatuaji madaraka kwa Serikali za Mitaa *(D by D),* kwa kuziondolea Serikali za Mitaa madaraka yake yote ya kisheria ya kukusanya kodi ya majengo, kodi ya mabango, ushuru wa huduma za mijini kwa malengo ya kujiendesha na kurudisha mamlaka hayo ya ukusanyaji wa kodi hizo Serikali Kuu kupitia *TRA*. Hii inadhihirisha kwamba yote yaliyofanywa na Serikali za CCM zilizopita na gharama zote zilizotumika kuimarisha madaraka kwenye

Serikali za Mitaa yalikuwa hayana maana yoyote. Kambi Rasmi ya Upinzani inakiri kwamba haijapata kutokea bajeti ya Serikali yenye lengo la kuua Serikali za Mitaa kwa kuzipunguzia madaraka na kuziondolea vyanzo vyake vya mapato. Kwa lugha nyepesi, Serikali ina tamaa ya vyanzo vya Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, hii ni bajeti ambayo kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania inawalipisha Watanzania maskini wasio na uwezo wa kumiliki magari kodi ya ada ya mwaka ya leseni za magari yaani *annual motor vehicle licence fee* kwa kuhamishia kodi hiyo kwenye ushuru wa bidhaa za mafuta. Ieleweke kupanda kwa bei ya mafuta kutasababisha kupanda kwa nauli katika sekta ya usafirishaji, jambo litakalosababisha kupanda kwa bei za vyakula, kupanda kwa bei za kusaga na kukoboa nafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanda bei kwa pembejeo za kilimo, kushindwa kupata nishati ya mwanga vijijini kutatokana na kupanda kwa bei za mafuta hususan mafuta ya taa. Kwa maneno mengine bajeti hii imelenga kuwabebesha wananchi masikini mzigo wa kodi kwa matumizi ya anasa ya watu wa tabaka la kati na juu wenye uwezo mkubwa kifedha kwa kuweza kumiliki magari na vitu vingine vya thamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, Kambi Rasmi ya Upinzani inakiri kabisa kwamba haijawahi kutokea bajeti ya namna hii ya kuwanyonya maskini na kuwaneemesha matajiri. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani haijawahi kuona chombo chochote cha moto cha usafiri wa barabarani kinachotumia mafuta ya taa, inashangaza sana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni bajeti ambayo kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania itatoza kodi ya shilingi 10,000 kwa nyumba zote katika Halmashauri zote nchini ambazo hazijafanyiwa uthamini zikiwemo nyumba za tembe na tope kwa wananchi maskini waishio vijijini. Hii iko katika ukurasa wa 48 kipengele cha tatu cha hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri 2017/2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala ya Serikali kupunguza kodi kwenye vifaa vya ujenzi ili wananchi wa vijijini waweze kuwa na nyumba bora na zenye staha na badala ya Serikali kufanya uthamini wa ardhi na nyumba za wananchi masikini waishio vijijini ili waweze kupata hatimiliki itakayoongeza thamani ya ardhi na nyumba zao, ili waweze kutumia hati hizo kupata mikopo itakayoboresha maisha yao, bado Serikali imeendelea kuwabamiza kodi katika ufukara na uduni wao. Haya ni mastaajabu. Nina hakika Kambi Rasmi ya Upinzani inakiri kabisa haijawahi kuona bajeti ya namna hii ya kumnyonya maskini. *(Makofi)*

Tano, hii ni bajeti ambayo imeendelea kupandisha kodi kwenye bidhaa ambazo uzalishaji wake hutumia malighafi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Silinde, subiri kidogo.

Waheshimiwa Wabunge,...

**MHE. DAVID E. SILINDE - NAIBU MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilindie muda wangu.

**MWENYEKITI:** Muda wako tunaulinda. Nataka tu niwaongoze kitu kimoja. Kwa mujibu wa kanuni, unaruhusiwa kupiga makofi na makofi yanayofahamika ni hivi...*(Makofi/ Kicheko)*

Unapiga hivi. Nasema hivi...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio na kupiga makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaruhusiwa kabisa, lakini tumia mikono yako hivi, kupiga makofi. Eeh! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Endelea Mheshimiwa.

**MHE. DAVID E. SILINDE - NAIBU MSEMAJI MKUU WA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni bajeti ambayo imejinasibu kama bajeti ya uchumi wa viwanda wakati haijaonesha popote mkakati wa kuongeza uzalishaji wa nishati ya umeme ambayo ndiyo msingi wa uzalishaji katika viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni bajeti ambayo haijataja popote itaongeza ajira kiasi gani kwa Watanzania na wala haijasema itapunguza umaskini kwa kiwango gani, kwa mwaka wa fedha 2017/2018? Aidha, ni bajeti ambayo haikuzungumzia mahali popote utekelezaji wa ahadi ya Serikali ya CCM ya kugawa shilingi milioni 50 kila kijiji. Ni uwongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wahenga walisema; ukistaajabu ya Musa utayaona ya firauni. Maajabu ya bajeti hii ni mengi, lakini itoshe kusema tu kwamba ukiwa muongo basi uwe pia na kumbukumbu nzuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge na hata wananchi wanaweza kusahau mengine, lakini hili la ahadi ya shilingi milioni 50 kwa kila kijiji ni mapema mno kuweza kusahau. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutolea maelezo ahadi hii ya shilingi milioni 50 kwa kila kijiji ili wananchi wajue kama wamekopwa au wamedhulumiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, waliosema kwamba bajeti hii haijawahi kutokea walikuwa sahihi na Kambi Rasmi ya Upinzani inawaunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti na bajeti mbadala za Kambi Rasmi ya Upinzani zilizopita ambazo ziliweka msisitizo katika ukuaji wa uchumi *(rural growth),* safari hii bajeti mbadala ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imebeba kauli mbiu ya ukuaji shirikishi *(inclusive economic growth)* ambapo watu wote watatakiwa kushiriki katika kujenga uchumi,

katika mazingira yao na pia ukuaji wa uchumi unatakiwa uwaguse watu wote katika matabaka yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa uchumi unakuwa shirikishi unapotokea kwenye sekta ambazo watu maskini wanafanya kazi kama vile kilimo, unatokea katika maeneo ambayo watu maskini wanaishi kwa mfano maeneo ambayo hayajaendelea na yasiyo na rasilimali, unatumia nyenzo za uzalishaji ambazo watu maskini wanazo kwa mfano nguvu kazi isiyo ya kitaalamu na unapunguza bei za bidhaa ambazo watu maskini wanatumia kwa mfano chakula, mafuta na nguo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo, ukipima hali ya Tanzania utaona kwamba uchumi wetu siyo shirikishi kwa kuwa ukuaji wake hautokei katika sekta ambazo watu maskini wanafanya kazi au maeneo ambayo watu maskini wanaishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ukuaji wa uchumi wetu hautumii nyenzo za uzalishaji ambazo watu maskini wanazo, na pia ukuaji huo haujapunguza bei za bidhaa ambazo watu maskini wanatumia. Kimsingi bajeti hii ambayo imeshabikiwa kwamba haijawahi kutokea, iko kinyume kabisa na mahitaji hayo ya ukuaji shirikishi wa uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya uchumi wa Taifa kupitia Taarifa ya Benki Kuu *(BOT)* ya Aprili, 2017, kwa mujibu wa Taarifa ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwezi Aprili, hali ya uchumi wa Taifa ilikuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumuko wa bei katika mwezi Machi, 2017 ulipanda kwa wastani wa 6.4% ukilinganisha na mwaka 2016 ambapo mfumuko huo ulikua kwa 5.2%. Ongezeko husika limesababishwa na ongezeko la bei ya chakula kama vile unga, mahindi, mihogo, ndizi, mboga mboga na sukari. Aidha, akiba ya chakula kwenye ghala la Taifa *(National Food reserve Agency – NFRA)* kulikuwa na akiba ya chakula cha tani 86,000. Hii haijumuishi maghala ya watu binafsi. Mzunguko wa fedha na upatikanaji wake

*(money supply)* ulikua kwa 4.5% mwaka 2017 ukilinganisha na mwaka 2015 ulikua kwa 15.5%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyongeza ya upatikanaji wa fedha katika sekta binafsi kutoka kwenye taasisi za fedha ilikua kwa kiwango cha 3.7% kwa mwaka 2017. Ukuaji ulikuwa kwa kiwango cha chini ukilinganisha na mwaka uliopita 2016 ambapo ongezeko lilikuwa la 23.6%. Hali hii ni kiashiria kwa kusuasua kwa sekta ya fedha nchini na mzunguko ama upatikanaji wa fedha kwa wafanyabishara, ikiwa ni ongezeko la 7.1%. kwa Serikali za Mitaa na kwingineko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauzo ya nje yalianzia kwa dola za Kimarekani milioni 8,921 mwaka 2017 ikiwa ni pungufu kwa 3% ikilinganishwa na mwezi Machi, 2016. Kwa takwimu hizo za hali ya uchumi, wala haihitaji kuwa na shahada ya uchumi kujua kama hali ya uchumi wa nchi yetu siyo nzuri. Kwa mwenendo huu, ni dhahiri kuwa uchumi wetu unaporomoka na Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili juu ya mikakati iliyopanga kunusuru hali ya uchumi wetu ambayo kwa vigezo vyote inaporomoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Benki ya Dunia tarehe 11 Aprili, 2017 ilitoa ripoti yake juu ya uchumi wa Tanzania na haya yalikuwa yamezungumzwa. Kukua kwa uchumi wa Tanzania kumepungua kutokana na upatikanaji wa fedha kuwa hafifu na kutokutabirika ama kutokueleweka kwa Sera ya Serikali ya Awamu ya Tano. Kubadilika badilika kwa Sera za Serikali na ukuaji wa kasi ndogo kwenye sekta binafsi ilipunguza ukuaji wa pato la ndani toka 7.2% mwaka 2015 mpaka 6.9%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji wana wasiwasi, wana mashaka na sera zisizotabirika kutokana na Serikali ya sasa. Kuporomoka ama kushuka kwa kasi ya mzunguko wa fedha na kuongezeka kwa mikopo isiyolipika kumeiathiri sana sekta binafsi. Kubadilika badilika kwa sera kunapotokea mara kwa mara kunasababisha sintofahamu kwa sekta binafsi na

sintofahamu zinazohusu athari katika maamuzi ya wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabenki ya Tanzania yanajilinda ama yanajiwekea wigo mkubwa dhidi ya hasara inayopatikana kwa mikopo isiyolipwa kutokana na hali mbaya ya kibiashara tokea Awamu ya Tano iingie madarakani kwa kutoza riba kubwa kwa mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la saba, baadhi ya wawekezaji wa kigeni wameamua ama wametaka kupunguza shughuli zao za uzalishaji au kusitisha mipango ya kupanua shughuli za uwekezaji kwa sababu ya masharti mapya, magumu na utozwaji wa kodi mkubwa. Tanzania inatajwa kuwa nchi ambayo siyo rahisi kufanya biashara ikiwa inaongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya malipo *(the highest number of payments)* katika ukanda wa Afrika Mashariki. Kuna malipo tofauti tofauti zaidi ya 48 ya kikodi. Ni nchi ya pili kwa kuwa na kiwango kikubwa cha kodi, yaani asilimia 44.9% katika ukanda wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo taswira ya hali ya mwenendo wa uchumi wetu kutokana na uchambuzi uliofanywa na wataalam wa fedha na uchumi Kitaifa na Kimataifa. Pamoja na yote hayo, tunaambiwa kila kitu kinakwenda vyema. Uongo huu na upotoshwaji unaofanya na Serikali kupitia Wizara ya Fedha, lazima ufike mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya uzalishaji, baada ya hotuba za Wizara mbalimbali kukamilika, tumegundua yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali imeweza kutekeleza 30% tu ya miradi ya maendeleo. Kilimo kinachoajiri asilimia 75 ya Watanzania kimedorora, ukuaji umeporomoka mpaka asilimia 1.7 toka asilimia sita iliyotarajiwa. Viwanda vingi vilivyosajiliwa *TIC* ni viwanda ambavyo havina uhusiano wa moja kwa moja na shughuli pana za kiuchumi za nchi yetu. Viwanda vya

usindikaji wa bidhaa zitokanazo na kilimo, mifugo na uvuvi siyo kipaumbele cha Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya sekta ya kilimo, sekta ya viwanda na nishati. Viwanda haviwezi kuwa imara bila kuwa na malighafi za kutosha kutoka kwa wazalishaji na umeme wa kuweza kuviendesha. Hakuna dhamira ya Serikali kufufua kilimo. Kijiografia Tanzania ilipaswa kuwa kapu la nafaka la Afrika ya Mashariki na Kati, yenye uwezo wa kuzalisha chakula kitakachojitosheleza mahitaji ya ndani na ya ziada kwa nchi za jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri Mkuu, ukurasa wa 19 iliainisha kwamba katika kuhakikisha Watanzania wanashiriki kikamilifu kwenye uchumi wa viwanda, Serikali inahamasisha zaidi sekta binafsi ya hapa Tanzania pamoja na mashirika mengine ya umma ijenge viwanda na kwamba jitihada hizo zimewezesha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa maana ya *NSSF, LAPF, GEPF, PSPF* na *NHIF* kuanza kufufua, kuendeleza na kujenga viwanda vipya vipatavyo 27 katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma *(PIC)* kwa kipindi cha Januari, 2016 hadi Januari, 2017 ikizungumzia madeni makubwa ambayo Serikali inadaiwa na mashirika na Taasisi zake, inaainisha kwamba Kamati ilipokea taarifa ya Msajili wa Hazina kuhusu utendaji wa taasisi mbalimbali za umma na kubaini madeni makubwa ambayo Serikali inadaiwa na taasisi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Kamati inasema, kwa ujumla uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Serikali imekuwa na tabia ya kutumia huduma au kukopa kutoka katika taasisi zake za ndani bila kufanya malipo. Serikali imekuwa ikikiri kudaiwa fedha nyingi na madeni hayo yamekuwa yakilimbikizwa mwaka hadi mwaka. Hali hii inadidimiza ukuaji wa taasisi hizo na kusababisha hasara kubwa katika utendaji wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfuko ambao unaonekana kuathirika zaidi ni Mfuko wa *PSPF* ambao unaidai Serikali zaidi ya shilingi trilioni 3.3 ambayo yanajumuisha madeni yanayotokana na dhima ya mafao ya watumishi wa Serikali ambao waliathiriwa na Mfuko wa *PSPF* kipindi unaanzishwa mwaka 1999. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi la pili linatokana na madeni ya uwekezaji. Kumekuwa na kukinzana baina ya Serikali na Mfuko wa *PSPF*. Wakati Serikali inadai deni inalodaiwa ni shilingi bilioni 290, Mfuko wa *PSPF* unadai deni halisi ni shilingi bilioni 533. Pamoja na mkanganyiko huo, Serikali imeshindwa kutekeleza ahadi yake ya kutoa hati fungani zenye thamani ya shilingi bilioni 290 kwa ajili ya kulipa deni hilo. Deni la tatu ni madeni ya malimbikizo ya mchango wa mwajiri kwa maana ya asilimia 15 ya Serikali kila mwezi, deni linalotokana na malimbikizo ya shilingi bilioni 253.78 ambalo ni la kipindi cha kuanzia Julai, 2015 hadi Februari, 2016. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani haiwezi kuruhusu wizi wa namna hii kuendelea kufanywa na Serikali dhidi ya fedha za wavuja jasho. Ikumbukwe kwamba hizi siyo fedha za Serikali, ni fedha za wanachama wanazochanga ili waweze kulipwa mafao yao punde wanapostaafu. Serikali inalazimisha mifuko kujenga viwanda wakati fedha za mifuko zilizotumika katika uwekezaji kwenye maeneo mbalimbali hususan sekta ya nyumba zikiwa hazina uhakika wa kurejeshwa kutokana na maamuzi mabovu ya uwekezaji yaliyofanywa na mashirika husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana hapa ikaeleweka kwamba hatupingi Mifuko ya Hifadhi kushirikiana na Serikali katika uwekezaji, lakini ni jambo lisilokubalika tukiendelea kuiruhusu Serikali kuifanya mifuko hii mirija ya kuchota fedha pasipo kulipa. Tunamtaka Waziri wa Fedha na Mipango aliambie Bunge lako Tukufu katika Bajeti ya mwaka 2017/2018 wametenga kiasi gani maalum kwa ajili ya kulipa madeni ya Mifuko ya Hifadhi za Jamii?

Pili, utaratibu wa utekelezaji wa malipo ukoje tofauti na makubaliano yaliyopita ambayo Serikali haikuyatekeleza? *(Makofi)*

Tatu, viwanda 27 vinavyotarajiwa kujengwa na fedha za mfuko, kila mfuko utachangia kiasi gani na kwa utaratibu gani wa marejesho wa fedha za wanachama? *(Makofi)*

Nne, viwanda husika vitajengwa wapi? Vigezo gani vimetumika katika kuchagua ama uchaguzi wa maeneo ya kujenga viwanda hivyo? *(Makofi)*

Tano, kama mradi wa viwanda tajwa unalipa, ni kwa nini sekta binafsi haijengi, badala yake zinatumika fedha za watumishi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, deni la taifa linasimamiwa na Sheria ya Madeni, Dhamama na Misaada ya Serikali ya mwaka 1974. Kulingana na vifungu namba 3 na 6 vya Sheria ya Madeni, Dhamana na Misaada ya Serikali, 1974. Waziri wa Fedha ndiye mwenye dhamana ya kukopa na kutoa dhamana kwa niaba ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, deni la taifa limeendelea kuwa changamoto kubwa kwa uchumi wetu. Kukua kwa deni la Taifa kunasababisha bajeti ya Serikali kuendelea kuwa tegemezi na hivyo kushindwa kutatua kero za kiuchumi kwa wananchi. Kwa bahati mbaya wananchi wengi hawaelewi hili na hawaelewi undani wa deni la taifa na athari zake katika maisha yao ya kawaida. Jambo la kusikitisha ni kwamba Serikali imekuwa ikitumia mwanya wa wananchi kutokufahamu kwa undani athari za deni la taifa, kuendelea kukopa mikopo mikubwa yenye masharti ya kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendelea kukopa kwa namna hiyo, kunaendelea kuwabebesha walipa kodi wa Tanzania mzigo mkubwa wa madeni ambayo yanazidi kufanya hali halisi ya maisha kwa wananchi iendelee kuwa ngumu kwa kuwa Serikali inatumia fedha nyingi kulipa madeni

badala ya kutumia fedha hizo kugharamikia miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Benki Kuu ya mwezi wa nne, 2017 na hotuba ya Bajeti 2017/2018 inaonesha kwamba deni la Taifa limefikia shilingi trilioni 50.8. Ikumbukwe mpaka Juni 2016 deni la Taifa lilikuwa shilingi trilioni 41; deni la ndani likiwa shilingi trilioni 10.978 na deni la nje likiwa shilingi trilioni 39.3. Kwa kipindi cha mwaka mmoja deni la Taifa limeongezeka kwa dola za Kimarekani milioni 884.8, sawa na shilingi trilioni mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kati ya shilingi trilioni 8.67 zilizotengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo, kwa maana ya Wizara ya Fedha, shilingi trilioni nane zilikuwa kwa ajili ya kulipia deni la taifa. Fedha zilizotumika kulipa deni ni nyingi kuliko fedha zinazotumika kugharamikia miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa deni la nje, Serikali kuu peke yake inadaiwa dola za Kimarekani milioni 13,792.9 sawasawa na shilingi trilioni 30.8. Kwa mwaka mmoja pekee nyongeza ya mkopo, yaani deni la nje ilikuwa dola za Marekani milioni 455.4 sawasawa na shilingi trilioni 1.018 (rejea Jedwali la *External Debt Stock Borrowers* katika Ripoti ya *BOT* ya Aprili). Kwa upande wa deni la ndani, mpaka mwezi Machi, 2017 deni la ndani lilifika shilingi bilioni 10.976.8. Ongezeko la mwezi la shilingi bilioni 327 na ongezeko la mwaka kwa shilingi trilioni 1.53.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa deni la ndani, wakopeshaji wakuu ni benki za biashara asilimia 41% ambao wanaidai Serikali shilingi trilioni 4.578, wakifuatiwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii asilimia 27%, ambayo mpaka mwezi Machi, 2017 wanaidai Serikali shlingi trilioni 2.995.3, nyongeza ya shilingi trilioni 1.482 ukilinganisha na mwezi Machi, 2016 (Rejea Jedwali Na. 5.4 la Ripoti ya *BOT* mwezi Aprili, 2017).

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa ni kauli za Serikali kwamba deni la Taifa ni himilivu. Kambi Rasmi ya Upinzani tumekuwa tukitoa tahadhari ya mara kwa mara kutokana na ukweli kwamba Serikali imekuwa ikihamisha goli *(change of goal post)* kila mara ili kujitafutia uhalali wa kuendelea kukopa huku Taifa likiingizwa kwenye matatizo makubwa. Katika hotuba yetu ya Mpango wa Taifa wa mwaka 2017/2018 tulihoji hali hili pasipo kupatiwa majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza ni kwamba kauli za uhimilivu zimeanza kutajwa tangu mwaka 2008 wakati deni la Taifa likiwa trilioni 7.8 mpaka 2017 yaani kwa maana ya miaka tisa sasa, deni limefikia shilingi trilioni 50.8. Kwa lugha nyepesi ni kwamba kila Mtanzania anadaiwa shilingi milioni moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hoja za Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni za kipindi kirefu, yaani kuanzia mwaka 2010/2011 mpaka 2016/2017 hatimaye tahadhari juu ya uhimilivu wa deni la Taifa imetolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Katika taarifa yake ya mwaka iliyotolewa mwezi Machi, 2017 Mkaguzi Mkuu alikuwa na haya ya kusema:-

Moja, deni la taifa lilianza kukua kwa kasi tangu mwaka 2007/2008 wakati nchi ilipopata misamaha wa madeni.

Pili, deni la taifa limeongezeka kwa asilimia 149 kwa miaka mitano iliyopita bila kuhusisha madeni yaliyoachwa nje ya mseto. *(Makofi)*

Tatu, mikopo isiyo ya masharti nafuu imeongezeka kwa asilimia 17 kutoka shilingi trilioni 7.8 mwaka 2014/2015 mpaka shilingi trilioni 9.15 mwaka 2015/2016 na mikopo yenye masharti nafuu kupungua. Mwaka 2012 mikopo ya masharti nafuu ilikuwa asilimia 89 ya deni la nje ikilinganishwa na asilimia 69 kwa mwaka 2015/2016. Hii ni kusema kwamba mikopo isiyo ya masharti nafuu kwa maana ya mikopo ya

kibiashara ilikua kwa asilimia 31 ya deni la nje mnamo mwezi Juni, 2016 ikilinganishwa na asilimia 11 miaka mitano iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, ongezeko la madeni ya nje yenye masharti ya kibiashara unaongeza gharama za kuhudumia deni kadiri mikopo inavyoiva. Hii ni kutokana na vipindi vifupi vilivyotolewa katika kulipa deni (mara nyingi ni miaka mitatu), riba kubwa na muda mfupi wa deni kuiva.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, taarifa ya uhimilivu wa deni la taifa inaonesha kwamba kwa kuangalia gharama za kuhudumia deni la taifa, ikilinganishwa na mapato ya ndani, gharama hizo ziko juu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za kuhudumia deni zikichanganywa na gharama nyingine kama vile mishahara ya wafanyakazi ni gharama ambazo zinaiacha Serikali na kiasi kidogo sana cha fedha za kugharamia miradi ya maendeleo na huduma nyingine za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na rasilimali kutelekezwa katika kulipa madeni, ni kiashiria kuwa Serikali itaendelea kutegemea mikopo ili kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Matokeo ya utegemezi huu ni kukua kwa madeni ya ndani na nje ambayo sio ya masharti nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, mikopo husika pia inaendelea kuongeza gharama za kuhudumia deni. Ongezeko la mikopo isiyo ya masharti nafuu na mikopo ya ndani imesababisha gharama za kukopa kuwa juu. *CAG* anatoa wito kwa watunga sera kuchukua tahadhari (sisi Wabunge). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba, Serikali kukopa ndani kwa wingi kunasababisha msongamano wa sekta binafsi katika fedha chache zilizokuwa zimebaki katika mabenki. Kwa lugha nyingine *CAG* anasema kukopa kwa wingi kwa Serikali katika mabenki ya ndani kunaua uwezo wa wafanyabiashara wa ndani kukopa. Hata wakifanikiwa kukopa, masharti yanakuwa magumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niongelee muundo na usimamizi wa deni la taifa kupitwa na wakati. Mkakati wa Taifa wa Madeni *(NDS)* wa mwaka 2002 uliandaliwa kwa mazingira ya Sheria ya Mikopo ya Serikali, Dhamana na Misaada ya mwaka 1974 yaani miaka 43 iliyopita. Hali ya uchumi na mazingira ya kuanzishwa kwa sheria na mkakati wa *NDS* yamebadilika kutokana na mabadiliko ya kiuchumi ambayo yametokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kupanuka kwa wigo wa deni la Taifa katika suala la vipengele na mikopo mikubwa ambayo imefanyika, Sheria na Miongozo inayosimamia deni la Taifa haiko sambamba na maendeleo hayo na vyombo vinavyotumika vimepitwa na wakati na kwa sababu kufanya hivyo kunasababisha usimamizi wa deni la taifa kuwa changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anabainisha katika ripoti yake aliyoitoa hivi karibuni kwamba wakati wa mahojiano na idara mbalimbali zinazosimamia deni la taifa chini ya Wizara ya Fedha yaani Idara ya Uchambuzi wa Sera, Mhasibu Mkuu wa Serikali, Idara ya Fedha za Nje na Msajili wa Hazina, Tume ya Mipango na Benki Kuu ya Tanzania, amebainisha kwamba mfumo uliopo sasa unaongeza uzembe katika uendeshaji, uratibu duni na kutokuwa na taarifa za kutosha katika vitengo na taarifa sahihi kupitia taasisi na kusababisha kuwa na rekodi zisizosahihi na zisizojitosheleza kuhusiana na deni. Hayo ni maneno ya *CAG.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchumi unaokua kwa wastani wa 6.5% mpaka 7% kwa mwaka, ni vigumu sana kuweza kulipa deni la taifa linalokua kwa asilimia 14 kwa miaka mitano. Bila kuwa na vyanzo vipya vya mapato au kusamehewa deni hili, itakuwa vigumu sana kuweza kulipa deni hilo kikamilifu. Hii ni kwa sababu uwiano wa ukuaji wa uchumi hauendani na kasi ya ukuaji wa deni hata kidogo. Pamoja na upungufu wote huo, Serikali imeendelea kujitapa kuwa inakopesheka, hivyo kuashiria kutokuwepo kwa hofu yoyote ya kukopa huko holela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachosikitisha zaidi ni kuwa sehemu kubwa ya mikopo hii inakopwa katika soko la ndani. Hali hii imekuwa ikileta ushindani mkubwa kwa wananchi na wajasiriamali wanaotaka kukopa ili kukuza mitaji. Hali hii hufanya riba za mabenki kushindwa kushuka na hivyo kuwaathiri wakopaji na uchumi wa nchi kwa ujumla. Kwa maneno mengine, Serikali imekuwa inazuia wajasiriamali wasikope kwa riba za bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya uchambuzi wa uhimilivu wa deni la taifa uliofanyika mwaka 2015 na 2016 na inaonesha kuwa uwiano wa gharama za kuhudumia deni na mapato ya nchi (vyanzo vya ndani ya mapato) unakua kwa kasi sana. Hii inajidhihirisha katika bajeti ya mwaka 2016/2017 ambapo Serikali kupitia vyanzo vyake vya ndani vya mapato ya kodi, yasiyo na kodi na mapato ya Serikali ya Mitaa, imefanikiwa kukusanya shilingi trilioni 13.5. Fedha zilizotengwa kuhudumia deni la taifa ni shilingi trilioni nane tu na fedha zilizotengwa kwa ajili ya mishahara ni shilingi trilioni 7.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchanganuo hapo juu unaonesha kwamba kwa mishahara na deni la taifa peke yake fedha zinazotumika ni shilingi trilioni 15.2 huku makusanyo ya nchi yakiwa ni shilingi trilioni 13.5 kwa tafsiri nyingine, Serikali ina uwezo wa kulipa mishahara na kuhudumia deni la taifa tu, huku ikiwa ina upungufu wa shilingi trilioni 1.7. Bila mikopo Serikali isingekuwa na ubavu wa kufanya shughuli zozote zile za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kama hii inatarajiwa kujitokeza katika bajeti ya mwaka 2017/2018 kwani kati ya shilingi trilioni 19 zinazotarajiwa kukusanywa kutokana na mapato ya ndani, shilingi trilioni 16.6 zinatarajiwa kulipa misharaha na kuhudumia deni la taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inaweza kuwa mbaya zaidi mwaka huu, kwa sababu Serikali imejiwekea maoteo makubwa ya makusanyo ambayo hayana uhalisia. Kama mwaka 2016/2017 Serikali ilipanga kukusanya shilingi

trilioni 29.5, ikaambulia kukusanya shilingi trilioni 20.7 pungufu ya shilingi trilioni tisa, ni miujiza gani itakayoiwezesha Serikali kukusanya shilingi trilioni 31.7 kwa mwaka wa fedha 2017/ 2018? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inakopa kwa masharti ya biashara kulipa mikopo. Hayo ndiyo maajabu yenyewe. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, inaonyesha kwamba Serikali inatarajia kukopa shilingi trilioni 7.763 kutoka soko la ndani na nje kwa masharti ya kibiashara; mikopo ya ndani ikiwa shilingi trilioni 6.168, ambapo shilingi trilioni 4.9 ni kwa ajili ya kulipia dhamana za Serikali zinazoiva.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa aina hii unachangia kwa kiasi kikubwa kuongeza mzigo wa deni kwa nchi. Serikali imeshindwa kulipa madeni kwa kutumia vyanzo vyake vya mapato. Tabia hii inazidi kuota mizizi, kwani katika mwaka 2014/2015 kati shilingi trilioni 1.8 zilizokopwa katika soko la ndani, zaidi ya shilingi trilioni 1.1 zilitumika kulipa madeni ya hati fungani wakati shilingi trilioni 0.69 ziliwekwa kwenye miradi ya maendeleo. Hiki ni kiashiria cha karibu sana cha Serikali kufilisika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukopa mikopo ya kibiashara yenye riba kubwa ili kulipa mikopo yenye riba ndogo au kwa uendeshaji wa kawaida wa Serikali au Taasisi zake ni kiashiria cha kutosha kuainisha maamuzi yasiyo na uelewa wa kawaida sana wa utawala na usimamizi wa fedha. Mikopo ya kibiashara hutafutwa kwa matumizi ya uwekezaji wenye malengo la uzalishaji siyo kama inavyofanyika sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imani ya Taasisi za Fedha za Kimataifa kwa Tanzania imepungua. Imefikia hatua hata kupata mikopo ya biashara imekuwa shida. Katika bajeti ya mwaka uliopita 2016/2017 Serikali ilipanga kukopa kutoka kwenye vyanzo vya kibiashara vya nje yaani shilingi trilioni 2.1 ili kugharamia miradi ya maendeleo. Fedha hizo hazikupatikana kwa maelezo kwamba Soko la Fedha za Kimataifa kutokuwa na hali nzuri. Sababu inayotolewa na

Serikali haina ukweli. Ni kwamba Taasisi za Fedha za Kimataifa zinakwepa kuikopesha Serikali kwa sababu haina uhakika juu ya uwezo wa Serikali wa kulipa mikopo pamoja riba kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu imekuwa ikikwepa kufanyiwa tathmini/uhakiki wa uwezo wa kukopesheka *(credit rating)* kwa kipindi kirefu sasa; inashindwa hata na Rwanda, sijui kuna siri gani inafichwa? Matokeo yake wanatarajia kupewa mikopo kwa huruma na hisani jambo ambalo halifanyiki katika ulimwengu wa uchumi wa kisasa na biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kutanzua kitendawili na utata wa deni hili:-

(i) Ni rai ya kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kurudia ushauri tulioutoa miaka minne na kulitaka Bunge liridhie na kumwelekeza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi maalum *(special audit)* katika kitengo cha deni la Taifa ili kujua mikopo inayochukuliwa kila wakati inatumika kufanyia nini; na miradi iliyotekelezwa kama ni miradi ya kipaumbele kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa.

(ii) Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaendelea kuitaka Serikali, kama ambavyo tumesema miaka mitano iliyopita, kuitaka Bunge litunge sheria ili liweze kudhibiti ukopaji na matumizi ya mikopo ya Serikali. Vilevile tunapendekeza katika sheria hiyo iwe ni lazima kwa Serikali kupata kibali kutoka katika Bunge kabla ya kuweza kukopa. Hii inafanyika katika nchi nyingi duniani kama vile Marekani na Uingereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali wakati wa majadiliano ya mikataba ya mikopo, kutumia utaratibu wa *interest rate swap* kutokana na ukweli kwamba sababu mojawapo inayosababisha deni kukua kwa kasi kunatokana ni kuporomoka kwa thamani ya shilingi yetu na kuwa na riba ambazo zinabadilika mara kwa mara. *Interest swapping* maana yake ni kukubaliana kuweka

kiwango cha riba kulingana na thamani ya shilingi ambayo inasaidia kuwa ni kiwango kile kile cha riba bila kujali kama thamani ya shilingi itapungua ama itaongezeka. Hii inasaidia kufanya deni lisiongezeke kwa kasi kutokana na kupungua kwa thamani ya shilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukirejea uchambuzi tulioufanya hapo juu kuhusiana na deni la taifa na tishio lake katika mustakabali wa nchi hii, ni mtu asiye na uelewa peke yake pekee ama mabashite ndio ambao hawataona hatari kubwa sana iliyo mbele yetu. Ni lazima sasa Bunge lako Tukufu lichukue nafasi yake kuisimamia Serikali kiukamilifu kama matakwa ya kikatiba yanavyolitaka. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukipitia hotuba yetu tumeonesha sasa hivi kuna vyanzo vipya vya mbadala wa mapata, tumeviandika pale ambapo Serikali mnaweza mkavichukua na vilevile tumeainisha sura ya bajeti mbadala kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na mambo muhimu ya kujifunza. Serikali yetu mbadala tutakapochukua madaraka itafanya *credit rating* ili iweze kuaminika Kimataifa kwa minajili ya kukopesheka kwenye riba nafuu na pia kupata mikopo ya kibishara toka nje. Mapato ya mikopo ya kibiashara kutoka nje yataongezeka kufikia shilingi trilioni 3.79 toka hii trilioni 1.5 ya Serikali ya sasa kwa sababu Serikali yetu mbadala itatoa *euro bond* ama *International bond* zenye thamani ya dola bilioni moja Kimataifa ili kupata fedha za kugharamikia bajeti. *(Makofi)*

Tatu, kutokana na kuaminika kwa Serikali mbadala (ya kwetu hiyo) tutapata mikopo nafuu kutoka nje yenye thamani ya shilingi trilioni 5.071, mapato ya Halmshauri tutayashusha yatafikia kiwango cha shilingi bilioni 387 kutoka Serikali ya sasa ambayo inanyang'anya kila kitu ya shilingi bilioni 687 ili kuziwezesha Halmashauri kufanya miradi yake ya maelekezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wahenga wetu walishasema kwamba sikio la kufa halisikii dawa. Nimeanza na methali hiyo kwa kuwa kwa miaka yote ya uhai wa Bunge

la Kumi na mpaka Bunge hili la Kumi na Moja, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiishauri Serikali kubana matumizi kwa kupunguza bajeti ya matumizi ya kawaida na yasio ya lazima na kuelekeza fedha hizo kwenye miradi ya maendeleo, lakini kinyume chake Serikali hii, imeendelea kuongeza bajeti ya matumizi ya kawaida na hata matumizi yasiyo ya lazima na kupunguza bajeti ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuthibitisha jambo hili, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imefanya tathmini ndogo ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa maana ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo kwa miaka mitatu mfululizo iliyopita na kubaini kwamba utekelezaji wa bajeti ya Serikali umeweka matumizi ya kawaida kama kipaumbele kuliko bajeti ya maendeleo ambayo ndiyo imekuwa dira ya ujenzi wa uchumi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mwaka 2014/2015 utekelezaji wa bajeti ya maendeleo ulikuwa asilimia 40, mwaka 2015/2016 asilimia 31.24, mwaka 2016/2017 asilimia 35. Ukitafuta wastani wa uwekezaji wa bajeti ya maendeleo kwa kutumia takwimu hizi kwa miaka tajwa utakuta utelezaji wa bajeti kwa miaka hiyo haujazidi asilimia 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa utekelezaji wa bajeti ya maendeleo uko chini ya wastani, utekelezaji wa bajeti ya matumizi ya kawaida yakiwemo matumizi yasiyo ya lazima umebaki kuwa juu kwa mfano mwaka wa fedha 2014/2015 matumizi ya kawaida yalikuwa ni asilimia 91; mwaka 2015/2016 matumizi ya kawaida asilimia 81; na mwaka huu ambao haujaisha mpaka sasa matumizi ya kawaida yapo zaidi asilimia 70. Ukitafuta wastani wa kutumia takwimu hizi kwa miaka tajwa, utakuta bajeti ya matumizi ya kawaida imekuwa ikitekelezwa kwa takriban asilimia 80.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuweka *record* sawa; utekelezaji wa zaidi ya asilimia 70 wa bajeti ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2016/2017 haumaanishi kwamba Serikali imebana

matumizi, bali imegoma kutoa fedha ambazo zilikuwa zimepangwa kutumia, kwa maana hiyo fedha zimebaki kuwa ni deni la Serikali. Kwa maneno mengine, matumizi ya kawaida bado yapo juu ukilinganisha na matumizi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo huu wa kutumia mapato yetu kwa matumizi ya kawaida kwa takriban asilimia 80 na kutoa fedha kiduchu kwa miradi ya maendeleo ambazo nazo zimekuwa hazitolewi kwa wakati, kunaifanya nchi yetu kuwa na uchumi wa mchumia tumbo *(hand to mouth economy).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 31mwaka 2017 wakati nawasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu bajeti ya Wizara ya Fedha nilieleza kwa kirefu jinsi ambavyo Serikali ya CCM imekuwa ikipuuza utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo ndiyo msingi wa uchumi wa wananchi kwa kutotoa fedha za utekelezaji wa miradi hiyo. Katika maelezo yangu nilitaja Wizara kumi za mfano, kuonesha utofauti wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge na fedha halisi zilizotolewa na Serikali kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa bado Serikali haijatoa sababu za msingi za utekelezaji duni wa namna hii ya bajeti ya maendeleo, nitarudia sehemu hiyo ili kwa mara nyingine kuipa Serikali nafasi ya kuwaeleza wananchi wa Tanzania ina lengo gani hasa kwa kutokuteleza bajeti ya maendeleo kwa takriban asilimia 70? Nilizotolea mfano na kutokupatiwa fedha za maendeleo kwa ukamilifu wake katika mwaka wa fedha 2017 ilikuwa ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira; nilieleza kuwa kati ya shilingi bilioni 10.9 za miradi ya maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge lako ni shilingi bilioni 1.2 tu sawa na asilimia 11.3 ya fedha hizo ndizo zilizotolewa na Hazina. Nilitoa angalizo kwamba fedha hizo ndizo hutumika kupambana na uharibifu wa mazingira yetu ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ambayo

yamekuwa na athari kubwa sana kwa wananchi wake kama vile ukame, mafuriko, magonjwa ya milipuko, njaa na kadhalika na kwamba kitendo cha Serikali kutokutoa fedha hizo maana yake ni kubariki athari mbaya zinazotokana na uharibufu wa mazingira ziendelee kuwaangamiza wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Tume ya Kudhibiti UKIMWI; kati ya shilingi bilioni 10.1 za miradi ya maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge ni shilingi bilioni 2.7 tu sawa na asilimia 27 ya bajeti ndizo zimetolewa. Nilieleza kwamba tafsiri ya kutotekeleza bajeti hiyo maana yake ni kwamba vita dhidi ya maambukizi ya UKIMWI hapa nchini siyo kipaumbele tena ya Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ni Wizara ya Sayansi, Elimu, Teknolojia na Ufundi; nilieleza pia kwamba kati ya shilingi bilioni 897 zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ni shilingi bilioni 500 tu sawa na asilimia 55 ndizo ambazo zilikuwa zimetolewa hadi kufikia Machi. Hata hivyo, mchanganuo wa fedha hizi ni kwamba shilingi bilioni 427 sawa na asilimia 48 zilikuwa ni kwa ajili ya mikopo ya Elimu ya Juu na shilingi bilioini 470 sawa na asilimia 52 zilikuwa ni kwa ajili ya kughalamikia miradi halisi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za maendeleo katika Sekta ya Elimu zinaonekana kuwa nyingi kwa kuwa zimechanganywa pamoja na fedha za mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri kwamba ni muhimu tukatenganisha kati ya miradi halisi ya maendeleo na mikopo ya wanafunzi ili kuweza kupata picha halisi ya nini hasa kinakwenda kutumika kutatua changamoto za uboreshaji, upanuzi, ujenzi wa miundombinu na shughuli za utafiti katika sekta hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija kwenye miradi halisi ya maendeleo, kati ya miradi 16 iliyotengwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 Kamati ya Bunge ya maendeleo ya huduma za jamii ilifanya ukaguzi wa miradi mitano ambayo sawa na asilimia 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote yataingia kama yalivyo, msiwe na wasiwasi namaliza, yote yataingia kama yalivyo maana *page* ni 200, namalizia hotuba yetu. Katika bajeti mbadala za mwaka 2011/2012 na mwaka 2012/2013 Kambi Rasmi ya Upinzani ilipendekeza masuala kadhaa ili kusaidia kuongeza mapato ya Serikali kwa upande mmoja na kwa upande wa pili kutasaidia kupunguza umaskini wa kipato kwa wananchi wa kawaida.

(i) Ilikuwa ni kupunguza misamaha ya kodi kufikia asilimia moja ya pato la taifa kama wenzetu wa Uganda na Kenya.

(ii) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alitakiwa kufanya ukaguzi maalum *(special audit)* ili kujua mikopo inayochukuliwa kila wakati inatumika kufanya nini; na miradi inayotekelezwa kama miradi ya kipaumbele kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako. Bado ukaguzi maalum haujafanyika hadi sasa.

(iii) Kuongeza kima cha chini cha mshahara kwa wafanyakazi wa Umma hadi shilingi 315,000 kwa mwezi. Inashangaza kuwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imeshindwa hata kutangaza nyongeza ya mishahara licha ukweli kwamba hali ya maisha imekuwa ngumu. *(Makofi)*

(iv) Kufanya marekebisho katika Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 kwa kufuta sehemu ya kodi ya mapato inayotoa fursa kwa Kampuni za Madini kutumia Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 1973 iliyofutwa, pendekezo letu lilikuwa na lengo la kutaka kuweka mfumo wa *straight line method of depreciation* ya asilimia 20 badala ya sasa ambako kampuni ya madini hufanya *100 percent depreciation* kwa mitambo yao mwaka wa kwanza na hivyo kucheleweza kulipa *corporate tax.* Pendekezo hili ambalo lingeipatia Serikali mapato mengi na hasa kwa sasa bado halijatekelezwa na Kampuni za Madini zenye mikataba.

(v) Kuanzisha *Real Estate Regoratory Authority* kama tunavyofanya kwa mwaka uliopita na kwamba kila

mwenyumba ya kupangisha lazima atambuliwe na kulipa kodi stahiki kutokana na biashara ya kupangisha nyumba. Serikali bado haijatekeleza pendekezo hilo.

(vi) Kushushwa kwa tozo ya kuendeleza stadi *(Skills Development Levy)* kutoka 6% ya sasa mpaka 4%, katika pendekezo hilo tunashauri kuwa waajiri wote walipe kodi ikiwemo Serikali na Mashirika ya Umma.

(vii) Kuwepo na utaratibu kuweka *sticker* maalumu ya kazi za sanaa zinazotolewa na mamlaka za Serikali kuonesha uhalali wa muuzaji wa kazi hizo ili wasanii wanaozitengeneza wanufaike na kazi zao. Pendekezo hili lilikubaliwa na Serikali na hivi sasa *TRA* na *COSOTA* wameanza kulifanyia kazi ili kuhakikisha wasanii wetu wanafaidika na jasho lao.

(viii) Kuzuia kabisa kusafirisha ngozi ghafi kwenda nje ya nchi na badala yake kuwe na mpango wa kuziongezea thamani na kuzitumia ngozi ghafi hapa nchini ili kuleta tija katika uchumi wa Taifa na kutengeneza ajira na kuongeza thamani ya mauzo ya nje.

(ix) Kuongeza mazingira ya ukuaji wa uchumi vijijini *(rural of growth)* kuboresha miundombinu ya umeme, barabara, maji na umwagiliaji sambamba na kuundwa kwa Mamlaka ya Maendeleo Vijijini *(Rural Development Authority)* chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

(x) Kujenga uwezo wa viwanda vya ndani ili kuviwezesha kuzalisha na kuuza nje bidhaa za kilimo na mifugo zitakazoongezwa thamani.

(xi) Kuboresha elimu na afya hasa kwa Shule, Zahanati na Vituo vya Afya vilivyopo katika maeneo ya vijijini kwa kutoa Motisha kwa wafanyakazi wa sekta hizo.

(xii) Kuanzisha pensheni ya wazee wote nchini wenye umri zaidi ya miaka 60. Serikali ipo kimya kuhusu suala hili muhimu kwa wazee wetu.

(xiii) Tulipendekeza kwamba utaratibu wa Vitambulisho vya Taifa uainishwe na mfumo wa kutoa namba ya vitambulisho kwa mlipa kodi *(TIN Number)* ili kila mwananchi awajibike kujaza fomu za taarifa za kodi, *tax returns* bila kujali kipato chake. Suala hili lingewezesha kupanua wigo wa kodi kwa kuongeza idadi ya walipa kodi nchi na kupunguza mianya ya ukwepaji kodi. Pendekezo hili bado halijatekelezwa. *(Makofi)*

(xiv) Tulipendekeza kwamba misamaha ya kodi yote iwekwe wazi na ikaguliwe na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, suala hili bado halijafanyiwa kazi.

(xv) Kuanzishwe Chuo Kikuu cha Mtwara *(Mtwara University for Petrolium Studies)* ili kufundisha wataalamu wa kutosha wa Sekta ya Mafuta na Gesi na kuliandaa Taifa kuwa na wasomi mahiri wa maeneo hayo na hivyo kunufaika na utajiri huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kuwambusha Watanzania kuwa Serikali hii ya CCM inayoongoza na Mwenyekiti wa sasa wa CCM imekuwepo madarakani miaka mingi tangu Taifa letu lipate uhuru. Hivyo, matatizo tuliyonayo kama Taifa yana unasaba ya moja kwa moja na Serikali hii. Aidha, niwakumbushe pia kuwa Rais aliyepo sasa madarakani, aliyopo Serikalini kwa sasa, alikuwepo Serikalini kwa zaidi ya miaka 20 iliyopita. Kwa hiyo, masuala ya ufisadi, sheria mbovu na uwekezaji wa Sheria za Madini zinazoharibu matumizi ya rasilimali zilitungwa akiwa sehemu ya Serikali. Kwa hiyo, kuwaambia Watanzania kuwa anajenga Tanzania mpya ni propaganda tu, kwani bajeti ya Serikali iliyopita imetekelezwa kwa asilimia 34 tu ya miradi ya maendeleo. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania mpya tuionayo ni Tanzania ambayo Serikali inaziba wananchi midomo kwa kutumia Sheria ya Makosa ya Kimtandao; Tanzania ambayo wananchi wake hawana haki ya kuona *Bunge live* ili kuona Wawakilishi wao wanatekeleza majukumu yao; Tanzania ambayo Vyama vya Siasa haviruhusiwi kufanya mikutano ya

hadhara kueneza sera zao kwa wananchi tofauti na utaratibu tuliuojijengea kwa miaka takribani 25; Tanzania ambayo Katiba ya nchi inakanyagwa kwa kauli na matendo ya baadhi ya viongozi wa Serikali; Tanzania ambayo wafanyakazi katika mwaka wa pili wa bajeti...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. *(Makofi/Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MHE. DAVID E. SILINDE - NAIBU MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hayo, naomba hotuba yetu ya kurasa 201 iingie kama ilivyo katika *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi/Vigelegele)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge Waliimba UKAWA kweli; kweli kweli kweli UKAWA)*

**MWENYEKITI:** Haya. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Silinde tunakushukuru kwa wasilisho lako kwa niaba ya Kambi ya Upinzani.

Waheshimiwa Wabunge, naendelea kuwakumbusha kwamba kanuni za Bunge ni Kanuni za Bunge. Kwa hiyo, hapa nina orodha ya Waheshimiwa Wabunge ambao wameendelea kutumia kitabu kupiga makofi. Ninayo orodha hii na mara ngapi wamerudia. Sasa kama itaendelea mchana, na mimi nipo hapa mchana. Kama itaendelea mchana, nitakutaja na ukiendelea nakutoa nje. *Period!* Mimi natenda haki kwa wote, sitajali kama anatoka huku.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO, MHESHIMIWA HALIMA JAMES MDEE (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU HALI YA UCHUMI WA TAIFA, MPANGO WAMAENDELEO WA TAIFA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FDHA 2017/18 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Halima James Mdee (Mb), naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa, Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/18.

**Mheshimiwa Spika,** kabla sijatoa maoni hayo, napenda kutumia fursa hii, kipekee kutoa pole nyingi kwa CHADEMA FAMILY, kwa kuondokewa na mmoja wa waasisi wa CHADEMA, Mzee Philemo Ndesamburo, aliyefariki dunia tarehe 31 Mei, 2017 huko Moshi, Kilimanjaro na hatimaye kupumzishwa katika nyumba yake ya milele tarehe 6 Juni, 2017. Marehemu Mzee Philemon Ndesamburo licha ya kuwa mwasisi wa CHADEMA, lakini pia alijitoa kwa hali na mali kukifadhili na kukilea Chama cha Demokrasia na Maendeleo na kukifikisha hapa kilipo leo. Mafanikio tuliyo na yo leo kama chama, na kama wabunge wa CHADEMA na viongozi wa chama kwa ngazi mbali mbali, na mafanikio tuliyo nayo leo, katika siasa za vyama vingi hapa nchini, kwa sehemu fulani yanatokana na juhudi za Mzee wetu huyu.

**Mheshimiwa Spika,** Taifa limempoteza mwanamageuzi wa karne, aliyekuwa tayari kupoteza maisha yake, kwa ajili ya mabadiliko ya kweli ya kisiasa, kiuchumi na kijamii katika Taifa letu. Kama chama, tutamkubuka kwa kuyaenzi yale yote aliyoyaasisi kwa mustakabali mwema wa chama chetu na Taifa kwa jumla. Hakika ni vigumu kuziba pengo aliloliacha.

Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi, AMINA.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya salama hizo za rambi rambi, naomba nitambue mchango uliotukuka wa Mhe. Halima James Mdee (Mb) ambaye ndiye Waziri Kivuli mwenye dhamana ya kuisimamia Serikali katika masuala ya Fedha na Mipango, kwa kufanya kazi usiku na mchana kufanya tafiti na uchambuzi wa nyaraka mbalimbali na kupata takwimu ambazo zimejenga msingi wa hotuba hii kwa zaidi ya asilimia 90.

**Mheshimiwa Spika,** tofauti na nchi zilizoendelea ambapo watu wenye upeo na weledi wa kufanya kazi namna hii huenziwa na kujengewa mazingira mazuri ya kuwa bora zaidi, katika nchi zinazoendelea watu wa aina hii hukumbana na madhila mengi ikiwa ni pamoja na kuwekwa kizuizini kwa sababu tu ya ujasiri wao wa kuisimamia na kuikosoa Serikali tena katika misingi ya kikatiba na kisheria.

**Mheshimiwa Spika,** wakati Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Mbowe (Mb) anahitimisha hotuba yake kuhusu Bajeti ya Serikali hapa Bungeni tarehe 6 Aprili, 2017 alisema kwamba: ***"… ili maendeleo ya kiuchumi yaweze kumfikia kila mwananchi ni lazima uchumi huo uwe shirikishi. Uchumi huo hauwezi kuwa shirikishi ikiwa tunabaguana kwa misingi ya tofauti za kisiasa au tofauti nyinginezo. Uchumi wa nchi yetu hauwezi kujengwa na kundi moja la jamii na kulibagua linguine. Hali kadhalika uchumi wa nchi yetu hautajengwa na chama kimoja cha siasa kwa kukibagua kingine au kuchochea migogoro ndani ya vyama vingine. Mshikamano wa kitaifa ni muhimu sana katika kujenga uchumi ulio imara. Ndoto ya kufikia uchumi wa viwanda haiwezi kufikiwa tukiwa na msigano wa namna hii***". Aidha, aliongeza pia kwamba: ***"kutofautiana kifikra ni afya ya akili, na ili uvumbuzi utokee lazima kuwe na fikra mbadala – 'alternative thinking' Nilidhani kuwa Serikali na Chama cha Mapinduzi wangetambua kuwa uwepo wa watu wenye fikra mbadala katika taifa hili ni tuna na zawadi kutoka kwa***

***Mwenyezi Mungu; lakini badala yake Serikali wameona kuwa uwepo wa watu hao ni kama mwiba na kikwazo."***

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kunukuu maneno ya Kitabu cha mwasisi wa Taifa la Afrika ya Kusini Hayati Nelson Mandela ***"No Easy Walk To Freedom"*** kama maneno ya faraja kwa Wabunge wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni waliopatwa na madhila mbalimbali kwa nyakati tofauti ikiwa ni pamoja na kufungiwa kuhudhuria vikao vya bunge au kuadhibiwa kwa namna nyingine yoyote ile, wakati wakitekeleza majukumu yao ya kibunge, kwamba wasifadhaike; kwa kuwa imewapasa kupitia njia hiyo, ili kufikia lengo lililo kubwa zaidi la kutwaa madaraka ya dola kwa njia ya kidemokrasia.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya utangulizi huo, sasa naomba nitoe Bashraff ya Bajeti ya Serikali iliyowasilisha mbele ya Bunge lako kwa ajili ya kupata idhini ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima kubwa, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuungana na waheshimiwa Wabunge ambao kwa umoja wao walisema kuwa bajeti hii haijawahi kutokea katika historia ya hivi karibuni ya bajeti za Serikali. Kambi Rasmi ya Upinzani inakiri kwamba ni kweli haijawaji kutokea bajeti ya namna hii na kwamba bajeti hii imevunja rekodi kwa sababu zifuatazo:-

1. Bajeti hii ni bajeti ambayo takwimu za vitabu vyake vya mapato na matumizi (Volume I, II, III &IV) zinatofautiana sana, na pia sura ya bajeti iliyosomwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango inatofautiana pia na vitabu hivyo. Wakati kitabu cha Mapato ya Serikali kinaonyesha kuwa Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/18 itakusanya jumla ya shilingi trilioni 23.9; kitabu cha Matumizi ya Serikali kinaonyesha kuwa Serikali inakusudia kutumia jumla ya shilingi trilioni 26.9 ikiwa ni ongezeko la matumizi ya shilingi trilioni 3 ambayo vyanzo vyake havijaonyeshwa kwenye kitabu cha mapato. Wakati huo huo, sura ya bajeti iliyosomwa na Waziri wa Fedha na Mipango inaonyesha kuwa bajeti ya Serikali kwa maana ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/18 ni

kiasi cha shilingi trilioni 31.7 – kiasi ambacho hakionekani popote katika vitabu vya mapato na matumizi ya Serikali. Hali kadhalika kwa mujibu wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Mikaka Mitano tarakimu hii ya shilingi trilioni 31.7 inaonekana kwamba ni makisio ya bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/19. Hivyo, sasa hivi tunatekeleza mapendekezo ya Mpango kwa mwaka wa fedha 2018/19 na sio 2017/18. ***Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inakiri kabisa kwamba haijawahi kutokea!!!***

2. Hii ni bajeti ambayo imedhamiria kuuwa kabisa dhana ya ugatuaji madaraka kwa Serikali za Mitaa (D by D) kwa kuziondolea Serikali za Mitaa madaraka yake ya kisheria ya kukusanya kodi ya Majengo, Kodi ya Mabango na Ushuru wa huduma mijini (City Service Levy) kwa malengo ya kujiendesha, na kurudisha madaraka hayo ya ukusanyaji kodi hizo Serikali Kuu kupitia TRA. Hii inadhihirisha kwamba yote yaliyofanywa na Serikali za CCM zilizopita na gharama zote zilizotumika kuimarisha madaraka kwenye Serikali za mitaa yailikuwa hayana maana yoyote. ***Kambi Rasmi ya Upinzani inakiri kwamba haijapata kutokea bajeti ya Serikali yenye lengo la kuuwa Serikali za Mitaa kwa kuzipunguzia madaraka na kuziondolea vyanzo vyake vya mapato.***

3. Hii ni bajeti ambayo kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania inawalipisha watanzania maskini wasio na uwezo wa kumiliki magari kodi ya ada ya mwaka ya leseni za magari (Annual Motor Vehicle Licence Fee) kwa kuihamishia kodi hiyo kwenye ushuru wa bidhaa za mafuta ya petrol, dizeli na mafuta ya taa ambapo athari zake ni kupanda kwa gharama za maisha kwa wananchi masikini. Ieleweke kupanda kwa bei ya mafuta kutasababisha kupanda kwa nauli katika sekta ya usafirishaji jambo litakalosababisha kupanda kwa bei za vyakula, kupanda kwa bei za kusaga na kukoboa nafaka kwa kutumia mashine zinazotumia petrol au dizeli kwa wananchi waishio vijijini, kupanda bei kwa pembe jeo za kilimo, kushindwa kupata nishaati ya mwanga kwa wananchi waishi vijijini kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta ya taa nk. Kwa maneno mengine bajeti hii imelenga kuwabebesha wananchi masikini

mzigo wa kodi kwa matumizi ya anasa ya watu wa tabaka la kati na juu wenye uwezo mkubwa kifedha wa kuweza kumiliki magari na vitu vingine vya thamani kubwa. ***Katika hili, Kambi Rasmi ya Upinzani inakiri kabisa kwamba haijawahi kutokea bajeti ya namna hiyo ya kuwanyonya masikini na kuwaneemesha matajiri. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani haijawahi kuona chombo chochote cha moto cha usafiri wa barabarani kinachotumia mafuta ya taa.***

4. Hii ni bajeti ambayo kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania Serikali itatoza kodi ya shilingi elfu kumi (10,000/=) kwa **nyumba *zote katika halmashauri zote nchini*** ambazo hazijafanyiwa uthamini zikiwemo nyumba za tembe na tope kwa wananchi masikini waishio vijijini. (Hii iko katika ukurasa wa 48 kipengele cha iii cha hotuba ya Bajeti 2017/18) Badala ya Serikali kupunguza kodi kwenye vifaa vya ujenzi ili wananchi wa vijijini waweza kuwa na nyumba bora zenye staha, na badala ya Serikali kufanya uthamini wa ardhi na nyumba za wananchi masikini waishio vijijini ili waweze kupata hati miliki itakayoongeza thamani ya ardhi na nyumba zao ili waweze kutumia hati hizo kupata mikopo itakayoboresha maisha yao; bado Serikali imeendelea kuwabamiza kodi katika ufukara na uduni wao.

***Haya ni mastaajabu!!!, na hakika Kambi Rasmi ya Upinzani haijawahi kuona bajeti ya namna hii.***

5. Hii ni bajeti ambayo imeendelea kupandisha kodi kwenye bidhaa ambazo uzalishaji wake hutumia malighafi inayozalishwa ndani ya nchi kama vile shayiri, zabibu, tumbaku n.k, jambo ambalo ni dhahiri litapunguza bei za mazao hayo, na hivyo kupunguza kipato cha wakulima wa mazao hayo. Kwa maneno mengine, bajeti hii haimjali mwananchi masikini ambaye ndiye mzalishaji wa malighafi hizo.

6. Hii ni bajeti ambayo imejinasibu kama bajeti ya uchumi wa viwanda wakati haijaonyesha popote mkakati wa kuongeza uzalishaji wa nishati ya umeme ambayo ndiyo msingi wa uzalishaji viwandani.

7. Hii ni bajeti ambayo haijataja popote itaongeza ajira kiasi gani kwa watanzania na wala haijasema itapunguza umasikni wa watanzania wa kiwango gani kwa mwaka wa fedha 2017/18. Aidha, ni bajeti ambayo haikuzungumzia popote utekelezaji wa ahadi ya Serikali ya kutoa shilingi milioni 50 kwa kila kijiji.

**Mheshimiwa Spika,** wahenga walisema,"ukistaajabu ya Musa, utaona ya Firauni. Maajabu ya bajeti hii ni mengi lakini itoshe kusema tu kwamba ***"ukiwa mwongo, basi uwe pia na kumbukumbu nzuri"*** Waheshimiwa wabunge na hata wananchi wanaweza kusahau mengine, lakini hili la ahadi ya shilingi milioni 50 kwa kila kijiji ni mapema mno kuweza kulisahau. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutolea maelezo ahadi hii ya shilingi milioni 50 kwa kila kijiji ili wananchi wajue kama wamekopwa fedha hii au wamedhulumiwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa hayo machache, ***waliosema kwamba bajeti hii haijawahi kutokea walikuwa sahihi, na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawaunga mkono.***

**Mheshimiwa Spika,** tofauti na bajeti mbadala za Kambi Rasmi ya Upinzani zilizopita ambazo ziliweka msisitizo katika Ukuaji wa Uchumi Vijijini (Rural Growth) safari hii bajeti mbadala ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imebeba kauli mbiu ya Ukuaji Shirikishi wa Uchumi (Inclusive Economic Growth) ambapo watu wote wanatakiwa kushiriki katika kujenga uchumi katika mazingira yao na pia ukuaji wa uchumi unatakiwa uwaguse watu wote katika tabaka zote.

**Mheshimiwa Spika,** wakati Kiongozi wa Upinzani Bungeni akiwasilisha hotuba yake kuhusu bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu hapa Bungeni tarehe 6 Aprili, 2017, alisema kwamba: "tangu Serikali hii ya awamu ya tano iingie madarakani imekuwa ikijigamba kuwa uchumi wa nchi unakuwa kwa kasi ikilinganishwa na serikali za awamu zilizotangulia, lakini kumekuwa na kilio kikuu kwa upande wa wananchi kuhusu hali ya maisha kuendelea kuwa ngumu kuliko wakati wowote katika historia ya nchi yetu". Aidha, alisema

kwamba: "kilio hiki cha wananchi kinamaanisha kwamba ukuaji wa uchumi unaohubiriwa na Serikali haujawafikia wananchi ambao ndio wadau wakubwa wa nchi hii".

**Mheshimiwa Spika,** Kiongozi wa Upinzani alinukuu maneno ya Wanazuoni wa uchumi wanaosema kwamba ***"Growth is inclusive when it takes place in the sectors in which the poor work (e.g. agriculture); occurs in places where the poor live (e.g. undeveloped areas with few resources); uses the factors of production that the poor possess (e.g. unskilled labour); and reduces the prices of consumption items that the poor consume (e.g. food, fuel and clothing)."***

**Mheshimiwa Spika,** kwa tafsiri isiyo rasmi ni kwamba ukuaji wa uchumi unakuwa shirikishi unapotokea kwenye sekta ambazo watu maskini wanafanya kazi kama vile kilimo; unatokea katika maeneo ambayo watu masikini wanaishi kwa mfano maeneo ambayo hayajaendelea na yasiyo na rasilimali; unatumia nyenzo za uzalishaji ambazo watu masikini wanazo kwa mfano nguvukazi isiyo ya kitaalamu; na unapunguza bei za bidhaa ambazo watu masikini wanatumia kwa mfano chakula, mafuta na nguo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa muktadha huo, ukipima hali ya Tanzania utaona kwamba uchumi wetu sio shirikishi kwa kuwa ukuaji wake hautokei katika sekta ambazo watu masikini wanafanya kazi au maeneo ambayo watu masikini wanaishi. Aidha, ukuaji wa uchumi wetu hautumii nyenzo za uzalishaji ambazo watu masikini wanazo na pia ukuaji huo haujapunguza bei za bidhaa ambazo watu masikini wanatumia. Kimsingi bajeti hii ambayo imeshabikiwa kwamba haijawahi kutokea, iko kinyume kabisa na mahitaji hayo ya ukuaji shirikishi wa uchumi.

## 2. MWENENDO WA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MIAKA MTATU ILIYOPITA 2014/15 – 2016/17

**Mheshimiwa Spika,** wahenga wetu walishasema kwamba ***"Sikio la kufa halisikii dawa"*** Nimeanza na methali hiyo, kwa kuwa, kwa miaka yote ya uhai wa Bunge la Kumi na mpaka bunge hili la kumi na moja, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni

imekuwa ikiishauri Serikali kubana matumizi kwa kupunguza bajeti ya matumizi kawaida yasiyo ya lazima na kuelekeza fedha hizo kwenye miradi ya maendeleo, lakini kinyume chake Serikali hii ya CCM imeendelea kuongeza bajeti matumizi ya kawaida hata kwa matumizi yasiyo ya lazima na kupunguza bajeti ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuthibitisha jambo hili, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imefanya tathmini ndogo ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa maana ya matumizi ya kawadia na matumizi ya maendeleo kwa miaka mitatu mfululizo iliyopita na kubaini kwamba utekelezaji wa bajeti ya Serikali umeweka matumizi ya kawaida kama kipaumbele kuliko bajeti ya maendeleo ambayo ndiyo dira ya ujenzi wa uchumi katika nchi yetu. Kwa mfano mwaka 2014/15 utekelezaji wa bajeti ya maendeleo ulikuwa ni asilimia 40, mwaka 2015/16 asilimia 31.24 na mwaka 2016/17 asilimia 35.26. Ukitafuta wastani wa utekelezaji wa bajeti ya maendeleo kwa kutumia takwimu hizi kwa miaka tajwa utakuta kwamba utekelezaji wa bajeti ya maendeleo kwa miaka hiyo haujawahi kuzidi asilimia 40.

**Mheshimiwa Spika,** wakati utekelezaji wa bajeti ya maendeleo uko chini ya wastani, utekelezaji wa bajeti ya matumizi ya kawaida yakiwemo matumizi yasiyo ya lazima umebaki kuwa juu. Kwa mfano kwa mwaka wa fedha 2014/15 matumizi ya kawaida yaikuwa ni asilimia 91, mwaka 2015/16 asilimia 81 na mwaka 2016/17 asilimia 68.7. Ukitafuta wastani kwa kutumia takwimu hizi kwa miaka tajwa utakuta bajeti ya matumizi ya kawaida imekuwa ikitekelezwa kwa kwa takriban asilimia 80.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuweka rekodi sawa kwamba; utekelezaji wa asilimia 68.7 wa bajeti ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2016/17, haumaanishi kwamba Serikali imebana matumizi bali imegoma kutoa fedha ambazo zilikuwa zimepangwa kutumiwa na kwa maana hiyo, fedha hizo zinabaki kuwa ni deni la Serikali. Kwa maneno mengine matumizi ya kawaida bado yako juu ukilinganisha na matumizi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** mwenendo huu wa kutumia mapato yetu kwa matumizi ya kawaida kwa takriban asilimia 80 na kutoa fedha kiduchu kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambazo nazo hazitolewi kwa wakati, kunaifanya nchi yetu kuwa na uchumi wa 'mchumia tumbo' – yaani ***hand to mouth economy.***

## 3. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 31 Mei, 2017 wakati nawasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu bajeti ya Wizara ya Fedha, nilieleza kwa kirefu jinsi ambavyo Serikali hii ya CCM imekuwa ikipuuza utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo ndiyo msingi wa uchumi wa wananchi kwa kutotoa fedha za utekelezaji wa miradi hiyo. Katika maelezo yangu nilitaja Wizara 10 za mfano kuonyesha tofauti ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge na fedha halisi zilizotolewa na Serikali kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa bado Serikali haijatoa sababu za msingi za utekelezaji duni namna hii wa bajeti ya maendeleo, nitarudia sehemu hiyo, ili kwa mara nyingine kuipa Serikali nafasi ya kuwaeleza wananchi ina lengo gani hasa kwa kutotekeleza bajeti ya maendeleo kwa takriba asilimia 70.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara nilizozitolea mfano kwa kutopatiwa fedha za maendeleo kwa ukamilifu wake katika mwaka wa fedha 2016/17 ilikuwa ni kama ifuatavyo:

### i. Ofisi ya Makamu wa Rais ( Mazingira)

**Mheshimiwa Spika,** nilieleza kuwa, kati ya **shilingi bilioni 10.9** za miradi ya Maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge katika ofisi hii, ni shilingi **bilioni 1.2** tu sawa na asilimia **11.3** ya fedha ya fedha hizo zilizotolewa na hazina kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo. Kwa maneno mengine bajeti ya Maendeleo ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira haikutekelezwa **kwa asilimia 88.7.**

**Mheshimiwa Spika,** nilitoa angalizo kwamba, fedha hizi ndizo hutumika kupambana na uharibifu wa mazingira yetu ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi ambayo yamekuwa na athari kubwa sana kwa wananchi kama vile ukame, mafuriko, magonjwa ya mlipuko, njaa nk na kwamba kitendo cha Serikali kutotoa fedha hizo maana yake ni kubariki athari mbaya zinazotokana na uharibifu wa mazingira ziendelee kuwaangamiza wananchi.

**ii. Tume ya Kudhibiti Ukimwi :**

**Mheshimiwa Spika,** Kati ya shilingi bilioni 10.1 za miradi ya maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge, ni shilingi bilioni 2.7 tu sawa na asilimia **27** ya bajeti ndio zimetolewa. Nilieleza kwamba tafsiri ya kutotekeleza bajeti hiyo kwa asilimaia 73, maana yake ni kwamba; vita dhidi ya maambukizi ya UKIMWI hapa nchini si kipaumbele tena cha Serikali hii ya awamu ya tano.

**iii. Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi:**

**Mheshimiwa Spika,** nilieleza pia kwamba, kati ya shilingi bilioni 897.6 zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ni shilingi bilioni 500.4 sawa na asilimia 55 ndizo ambazo zilikuwa zimetolewa hadi kufikia Machi, 2017. Hata hivyo, mchanganuo wa fedha hizo ni kwamba, shilingi bilioni 427 (asilimia 48) zilikuwa ni kwa ajili ya mikopo ya elimu ya juu na shilingi bilioni 470 (asilimia52) zilikuwa ni kwa ajili ya kugharamia miradi halisi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** fedha za maendeleo katika sekta ya elimu zinaonekana kuwa nyingi kwa kuwa zimechanganywa pamoja na fedha za mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri kwmba; ni muhimu tukatenganisha kati ya miradi 'halisi ya maendeleo' na ' Mikopo ya wanafunzi' ili kuweza kupata picha halisi ya nini hasa kinakwenda kutumika kutatua changamoto za uboreshaji/ upanuzi/ujenzi wa miundombinu na shughuliza utafiti katika sekta hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, tukija kwenye miradi halisi ya maendeleo, kati ya miradi 16 ambayo ilitengewa fedha katika mwaka wa fedha 2016/17 Kamati ya Bunge ya Maendelelo na Huduma za Jamii ilifanya ukaguzi wa miradi 5 tu sawa na na 12% ya miradi yote. Kati ya miradi hiyo mitano , ni miwili tu iliyopatiwa fedha! Tena kwa kiwango kidogo sana. Ifuatayo ni Hali halisi ya miradi mitano iliyokaguliwa :

- Mradi wa upanuzi wa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA) – Mradi namba 6361. Bunge liliidhinisha **shilingi bilioni 4, hakuna fedha yoyote iliyopelekwa**

- Mradi wa ukarabati wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam (Mradi namba 6350). **Bunge iliidhinisha shilingi bilioni 9.4, hakuna fedha yoote iliyopelekwa**

- Mradi wa Hospitali ya Mloganzila (Namba ya Mradi 6364).Chuo kiliomba shilingi 14,549,727,933 (BN. 14.5) hakuna fedha iliyopelekwa mpaka 13/Mei /2017 wakati wa hotuba ya bajeti ya wizara ya elimu inasomwa.

- Mradi wa Mfuko wa Utafiti na Maendeleo wa COSTECH (Namba ya Mradi 6345. Katika Malengo ambayo nchi nchi imejiwekea , ni kutenga 1% ya Pato la Taifa. Hata hivyo, mfuko huu ulitengewa kiasi cha **shilingi bilioni 12.8 tu sawa na 0.012% ya pato la Taifa** . Pamoja na udogo huo , kiasi kilichotolewa ni shilingi bilioni 4.07 tu (sawa na 31.7%). Kati ya hizo fedha M**fuko mkuu wa hazina uliotakiwa kutoa bilioni 8 ilitoa shilingi bilioni 1.5 tu** na TCRA iliyotakiwa kutoa shilingi bilioni 4.8 ilitoa shilingi bilioni 2.57 tu.

- Mradi wa ujenzi wa DIT teaching Tower (Namba ya Mradi 4384). Mradi huu una umri wa miaka 11 (2006-2017)...bado unasuasua, hakuna pesa na Matokeo yake gharama za mradi zimeongezeka toka bilioni 5 mpaka bilioni 9.

**iv. Wizara ya Maji**

- **Tume ya Taifa ya umwagiliaji- Fungu 05:**

**Mheshimiwa Spika, katika sekta ya Maji,** kati ya **shilingi bilioni 35.3** za miradi ya maendeleo zilizodhinishwa na Bunge, ni **shilingi bilioni 2.9 tu** sawa na **asilimia 8.4** zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo. Kwa upande wa **usambazaji wa maji ,mijini na vijijini** kati ya shilingi bilioni 915.1 zilizotengwa, zilizotolewa ni shilingi bilioni 181.2 **sawa na 19.8%** ya fedha zote za miradi ya Maendeleo ndizo zilizotolewa.

**Mheshimiwa Spika,** nilisema na narudia tena kusema kwamba; utekelezaji duni namna hii wa bajeti ya maendeleo katika sekta ya maji ni matusi kwa watanzania ambao uhaba wa maji umewafanya waishi kama wanyama; na kwamba; ule usemi wa Serikali wa kumtua mama ndoo ya maji, kwa mazingira haya ni dhihaka na ni ulaghai kwa akina mama wote wa nchi hii ambao wanaendelea kusota na kukumbana na kila aina ya kadhia katika kutafuta maji. Aidha, niliitahadharisha Serikali Ikumbuke kwamba, hawa kina mama inaowafanyia mzaha kaatika suala la maji ndio mtaji mkubwa wa kura waliyoipa ushindi, na sasa imeshindwa kutumiza ahadi yake ya kuwatuma ndoo za maji kichwani, kwa kushindwa kutekeleza bajeti ya maendeleo iliyodhinishwa na Bunge.

**v. Wizara ya Viwanda na Biashara**:

**Mheshimiwa Spika,** Kati ya shilingi **bilioni 42.1** zilizotengwa, wizara ilipokea shilingi **bilioni 7.6 tu sawa na 18.6%.** Nileeleza wazi na ninarudia tena kwamba; kwa utekelezaji huo wa bajeti, ni aibu kwa Serikali kutumia Kauli mbiu ya ***'Tanzania ya Viwanda'*** kama kampeni ya kuchochea ukuaji wa uchumi kupitia viwanda.

**vi. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:**

**Mheshimiwa Spika,** nilieleza pia kwamba, pamoja na unyeti wa Wizara hii, bado ilikumbwa na janga hili la kutopewa

fedha za maendeleo. Moja ya mradi muhimu sana katika wizara hii ni mradi wa Defence Scheme ( mradi namba 6103) ambao unatekelezwa chini ya Kifungu namba 2002- Military Research and Development Fungu 57. Mradi huu, ulitengewa jumla ya shilingi bilioni 151.1. lakini Mpaka mwezi Machi,2017 wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni 30 tu sawa na 20% tu! Mbali na mradi tajwa hapo juu kwa mujibu wa Taarifa ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama [1] fedha za miradi ya maendeleo ziliwasilishwa ni 14.5% tu, yaani Bunge liliidhinisha shilingi bilioni 230, pesa zilizotolewa hadi Machi 2017 ni shilingi bilioni 33.9. Halafu tunaitangazia dunia kwamba tuna lengo la kuwa na jeshi dogo la kisasa lenye weledi, wakati Serikali haitoi fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo kupitia miradi hiyo ndiyo tunaweza kuwekeza katika teknolojia ya kisasa na hivyo kuwa na jeshi la kikisasa.

### vii. Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi:

**Mheshimiwa Spika,** Kilimo kiliidhinishiwa shilingi 101,527,497,000 (bilioni 101). Kiasi kilichotolewa ni shilingi 3,369,416,66 (bilioni. 3.369) **sawa na 3.31%**. Kwa upande wa mifugo na uvuvi, kiasi cha shilingi 15,873,215,000 (bilioni 15.8) kiasi kilichotolewa ni bilioni 1.2. **Sawa na 8% .** Kwa maneno mengine, Kilimo ambacho tunasema kwamba ndio uti wa mngongo wa uchumi wa Tanzania, bajeti yake ya maendeleo haikutekelezwa kwa takriban asilimia 97. Serikali inahubiri Uchumi wa Viwanda ikijua fika kwamba viwanda hivyo haviwezi kuendelea bila ukuaji katika sekta ya kilimo, lakini haitoi fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo katika sekta ya Kilimo.

**[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA SPIKA]**

viii. Wizara ya Maliasili na Utalii , fedha za ndani za miradi ya maendeleo zilizotengwa ni shilingi bilioni 2. Fedha zilizotolewa ni shilingi milioni 156,688,000 sawa na **8%**

[1] Iliyowasilishwa tarehe 16/5/2017

ix. Wizara ya Ardhi, Nyumba na maendeleo ya makazi, fedha za miradi ya maendeleo zilizotengwa ni shilingi bilioni **25.30** . Fedha zilizotolewa mpaka sasa ni shilingi bilioni **7.63 tu.**

**x. Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:**

**Mheshimiwa Spika,** wizara hii ilitengewa fedha za Maendeleo kwa mchanganuo ufuatao:

- Ujenzi iliidhinishiwa shilingi trilioni 2.17 zilizotolewa ni shilingi trilioni 1.07 sawa na asiliia 58.7

- Uchukuzi iliidhinishiwa shilingi trilioni 2.49 zilizotolewa ni shilingi bilioni 761.5 sawa na asilimia 30.5

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi uliofanywa hapo juu unaonyesha wazi kwamba, ufanisi wa Serikali ya awamu ya tano katika utekelezaji bajeti ya Miradi ya maendeleo na mpango wa kuwaondolea umasikini watanzania ni kwa wastani wa 0%- 20%. Wizara pekee iliyoweza kuvuka 50% ni Wizara ya Ujenzi na inafahamika kwamba yapo ***'maslahi mapana'*** yanayohitaji kulindwa katika wizara hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** wakati Serikali hii ya awamu ya tano inashindwa kutekeleza bajeti ya maendeleo kwa takriban asilimia 70, ni Serikali hii hii ambayo kwa nyakati tofauti imekuwa ikijigamba kwamba imefanikiwa kukusanya mapato kwa kiwango cha hali ya juu kuzidi makisio iliyoyaweka kila mwezi.

**Mheshimiwa Spika,** Swali la msingi la kujiuliza hapa ni kwamba; hizo fedha amabazo Serikali inajisifu kukusanya kwa wingi zinakwenda wapi?? Au zinatumika vibaya – kwa maana ya matumizi ambayo hayajaidhinishwa na bunge? Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili, ni kwa nini haikutoa fedha za kutosha kutekeleza miradi ya maendeleo kwa takriban wizara zote, kwa kisingizio kwamba kulikuwa na upungufu wa fedha lakini wakati huo huo

inautangazia umma kwamba imekusanya mapato mengi kuzidi lengo la makusanyo.

**Mheshimiwa Spika,** Ni Serikali hii hii ambayo kupitia Ilani ya chama chake, na kupitia dira ya taifa ya maendeleo ya 2025 na 2020 kwa upande wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imekuwa ikituambia kwamba suluhisho la kuondokana na hali duni ya uchumi na utegemezi ni kuendesha modernization ya uchumi. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali iliahidi kufanya mambo yafuatayo:

i) Kutilia Mkazo katika matumizi ya maarifa ya kisasa (Sayansi na Teknolojia)

ii) Kuandaa rasilimali watu katika maarifa na mwelekeo

iii) Kufanya mapinduzi ya kilimo, ufugaji na uvuvi

iv) Kufanya mapinduzi ya viwanda ambavyo ndivyo kiongozi wa uchumi wa kisasa

v) Mapinduzi katika nishati na miundombinu ya kisasa

**Mheshimiwa Spika,** Suala la Msingi ambalo wabunge wa pande zote mbili tunapaswa kutafakari na kujiuliza, kutokana na uchambuzi uliofanywa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni hapo juu, hivi kweli itakapofika 2020 na 2025 malengo (i-v) yatatimia? Na kama nafsi zetu zinatuambia kwamba hayatatimia, tunajipanga vipi kutumia kipindi hiki cha bajeti KUJISAHIHISHA ili mwaka ujao wa fedha TUSIJIULIZE maswali hayahaya?!

## 4. HOJA ZA NYUMA ZA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU BAJETI YA SERIKALI

**Mheshimiwa Spika,** katika Bajeti Mbadala za mwaka 2011/12 na 2012/13 Kambi Rasmi ya Upinzani ilipendekeza masuala kadhaa ili kusaidia kuongeza mapato ya Serikali kwa upande mmoja na kwa upande wa pili kusaidia kupunguza umasikini wa kipato kwa wananchi wa kawaida na hivyo kuboresha maisha yao. Masuala tuliyoyapendekeza ni pamoja na:

1. Kupunguza misamaha ya kodi hadi kufikia asilimia moja (1%) ya pato la Taifa kama wenzetu wa Uganda na Kenya.

2. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alitakiwa kufanya ukaguzi maalum (special audit) katika kitengo cha Deni la Taifa (fungu 22) ili kujua mikopo inayochukuliwa kila wakati inatumika kufanyia nini, na miradi iliyotekelezwa kama ni miradi ya kipaumbele kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Bado ukaguzi maalum haujafanyika hadi sasa.

3. Kuongeza Kima cha chini cha mshahara kwa wafanyakazi wa umma hadi Tsh 315,000 kwa Mwezi. Inashangaza kuwa katika mwaka wa fedha 2017/18 Serikali imeshindwa hata kutangaza nyongeza ya Mishahara licha ya ukweli kwamba hali ya maisha imezidi kuwa ngumu.

4. Kuifanyia marekebisho sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 kwa kufuta sehemu ya Kodi ya Mapato inayotoa fursa kwa kampuni za madini kutumia sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 1973 iliyofutwa (grandfathering). Pendekezo letu lilikuwa na lengo la kutaka kuweka mfumo wa ***'straightline method of depreciation'*** ya asilimia 20 badala ya sasa ambapo Kampuni za Madini hufanya ***'100 percent depreciation'*** kwenye mitambo yao mwaka wa kwanza na hivyo kuchelewesha kulipa ***'Corporate Tax'***. Pendekezo hili ambalo lingeipatia Serikali mapato mengi na kwa sasa bado halijatekelezwa kwa Kampuni za madini zenye mikataba.

5. Kuanzisha **Real Estate Regulatory Authority** kama tulivyofanya kwa mwaka uliopita na kwamba kila mwenye nyumba ya kupangisha lazima atambuliwe na kulipa kodi inavyostahili kutokana na biashara ya kupangisha nyumba/vyumba. Serikali bado haijatekeleza pendekezo hili, hakuna sera ya nyumba na hivyo Serikali hupoteza mapato mengi sana kwenye sekta ya nyumba, kodi za nyumba kuwa juu sana na kuumiza vijana wanaoanza maisha na kutozwa kwa mwaka mzima.

6. Kushushwa kwa tozo ya kuendeleza stadi (*Skills Development Levy – SDL)* kutoka asilimia sita (6) ya sasa mpaka asilimia nne (4). Katika pendekezo hilo tulishauri kuwa waajiri wote walipe kodi hii ikiwemo Serikali na Mashirika ya Umma. Serikali imechukua pendekezo hili kwenye mapendekezo ya Bajeti ya mwaka 2013/14 lakini bila kuhusisha mwajiri Mkuu, Serikali. Ni vema kodi hii ilipwe na waajiri wote nchini na ishuke kuwa asilimia 4.

7. Kuwepo na utaratibu wa kuweka *stiker* maalumu kwa kazi za sanaa zinazotolewa na mamlaka za serikali kuonyesha uhalali wa muuzaji wa kazi hizo ili wasanii wanaozitengeneza wanufaike na kazi zao. Pendekezo hili lilikubaliwa na Serikali na hivi sasa TRA na COSOTA wameanza kufanya kazi hii ili kuhakikisha wasanii wetu wanafaidi jasho lao.(ufanisi wake ukoje?)

8. Kuzuia kabisa kusafirisha ngozi ghafi kwenda nje ya nchi na badala yake kuwe na mpango wa kuziongezea thamani na kuzitumia ngozi ghafi hapa nchini ili kuleta tija katika uchumi wa taifa kwa kutengeneza ajira na kuongeza thamani ya mauzo nje. Serikali iliamua kupandisha ushuru. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Bungeni inaamini kuwa kuna haja kubwa ya kuzuia kuuza mazao ghafi nje ili kukuza ajira za ndani na kuongeza thamani ya mauzo yetu nje.

9. Kujenga Mazingira ya ukuaji wa uchumi vijijini (Rural Growth) kwa kuboresha miundombinu ya umeme, barabara, maji na Umwagiliaji. Sambamba na kuundwa kwa Mamlaka ya Maendeleo Vijijini (Rural Development Authority) chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.Lengo likiwa kuwe na fedha mahsusi, kutoka chanzo mahsusi zinazotengwa na kuwekewa uwigo (ringfenced ) wa kutotumika kwa shughuli nyingine yoyote zaidi ya kufanya maendeleo vijijini. Pendekezo hili Serikali imelidharau na madhara yake ni kuwa maendeleo ya vijijini hayana uratibu mzuri na hivyo kusahaulika kabisa.

10. Kukarabati Reli ya Kati na matawi yake.

11. Kujenga uwezo wa viwanda vya ndani ili kuviwezesha kuzalisha na kuuza nje bidhaa za kilimo na mifugo zilizoongezewa thamani. Tuliitaka serikali kupiga marufuku uuzaji nje wa korosho ghafi kama ilivyovyo kwa ngozi ghafi kwa kuanzia. Serikali haijaweka mkakati wowote wa kuhakikisha korosho yote nchini inabanguliwa kabla ya kuuzwa nje.

12. Kuboresha elimu na afya hasa kwa shule na zahanati/ Vituo vya Afya vilivyo katika maeneo ya vijijini kwa kutoa motisha kwa wafanyakazi wa sekta hizi walio kwenye Halmashauri za Wilaya. Tulipendekeza pia kuanzishwa kwa posho za mazingira magumu. Serikali haijatekeleza pendekezo hili.

13. Kuanzisha pensheni ya uzeeni kwa wazee wote nchini wenye umri wa zaidi ya miaka 60. Serikali ipo kimya kuhusu suala hili muhimu sana kwa wazee nchini.

14. Tulipendekeza kwamba utaratibu wa vitambulisho vya Taifa uoanishwe na mfumo wa kutoa namba ya utambulisho kwa mlipa kodi (TIN Number) ili kila mwananchi awajibike kujaza fomu za taarifa za kodi ‘tax returns’ bila kujali kipato chake. Suala hili lingewezesha kupanua wigo wa kodi kwa kuongeza idadi ya walipa kodi nchini na kupunguza mianya ya ukwepaji kodi. Pendekezo hili bado halijatekelezwa na serikali.

15. Ilipendekezwa kwamba misamaha yote ya kodi iwekwe wazi na ikaguliwe na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Bajeti ya mwaka 2014/2015 imeridhia pendekezo hili na kuahidi kuwa misamaha ya kodi itawekwa wazi. Utekelezaji wake bado unasuasua!

16. Kuanzisha Chuo Kikuu cha Mtwara (Mtwara University for Petroleum Studies) ili kufundisha wataalamu wa kutosha wa sekta ya Mafuta na Gesi na kuliandaa Taifa kuwa na wasomi mahiri wa maeneo hayo na hivyo kufaidika na utajiri wa Mafuta na Gesi uliopo nchini kwetu. Serikali ipo kimya

kuhusu pendekezo hili kama ambavyo imekuwa kimya KABISA kwenye suala la Mafuta na Gesi katika hotuba za wizara ya Nishati na Madini na Hotuba ya Bajeti. Wakati miaka michache iliyopita ilikuwa inalipigia upatu kwa mbwembwe nyingi sana.

**5. HALI YA UCHUMI WA TAIFA - TAARIFA YA BENKI KUU YA TANZANIA YA MWEZI - APRIL 2017**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa taarifa ya Benki Kuu ya Tanzania ya Mwezi Aprili, 2017, hali ya uchumi wa Taifa ilikuwa kama ifuatavyo:

i. **Mfumuko wa Bei:** katika Mwezi Machi, 2017 mfumuko wa bei ulikuwa kwa wastan wa 6.4% ukilinganisha na mwaka 2016 ambapo mfumuko ulikuwa kwa 5.4%. Ongezeko husika limesababishwa na ongezeko la bei ya chakula kama vile unga, mahindi, mihogo, ndizi, mbogamboga, sukari n.k

ii. **Akiba ya chakula:** kwenye ghala la Taifa (National Food reserve Agency NFRA) kulikuwa na akiba ya chakula ya tani 86,444. Hii haijumuishi maghala ya watu binafsi.

iii. **Mzunguko wa fedha:** Mzunguko wa fedha na upatikanaji wa fedha (Money Supply and Credit ), ulikuwa kwa 4.1% (22,539) mwaka 2017 ikilinganisha na 15.5% mwaka 2016 ( 21,648.5)

iv. **Upatikanaji wa fedha katika sekta binafsi**: Nyongeza ya upatikanaji wa fedha wa sekta binafsi kutoka kwenye taasisi za fedha ilikuwa kwa kiwango cha **3.7%** kwa mwaka 2017 . Ukuaji ulikuwa wa kiwango cha chini ikilinganishwa na ongezeko la **23.6**% mwezi Machi 2016. Hali hii ni kiashiria cha kusua sua kwa sekta ya fedha nchini na mzunguko / upatikanaji wa fedha kwa wafanyabishara.

v. **Mwenendo wa kibajeti:** Makusanyo ya mwezi Machi, 2017 yalifikia shilingi trilioni 1.45 ikilinganishwa na shilingi Trillion 1.325 mwaka 2016. Mapato yaliyotokana na kodi ni shilingi trilioni 1.3 ikiwa ni ongezeko la 7.1%. Serikali za mitaa toka vyanzo vya ndani shilingi bilioni 45.3.

**vi. Usafirishaji wa Bidhaa Nje** : Mauzo ya nje yaliinza dola za kimarekani milioni 8,921 mwaka 2017 ikiwa ni pungufu kwa 3% ikilinganishwa na mwezi Machi, 2016.

**Mheshimiwa Spika,** kwa takwimu hizo za hali ya uchumi, wala haihitaji kuwa na shahada ya uchumi kujua kama hali ya uchumi wa nchi yetu sio nzuri. Kwa mwenendo huo, ni dhahiri kuwa uchumi wetu unaporomoka na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza bunge hili juu ya mikakati iliyopanga ili kunusuru hali ya uchumi wetu ambayo kwa vigezo vyote inaporomoka.

## 5.1. HALI YA UCHUMI WA TAIFA – TAARIFA YA BENKI YA DUNIA

**Mheshimiwa Spika,** Tarehe 11 Aprili, 2017 - Benki ya Dunia ilitoa Ripoti yake juu ya uchumi wa Tanzania na ilikuwa na haya ya kusema :

i. Kukua kwa uchumi kumepungua kutokana na upatikanaji wa fedha kuwa hafifu na kutotabirika/ kutokueleweka kwa Rais Magufuli.

ii. Kuubadilika badilika kwa sera za serikali na ukuaji kwa kasi ndogo kwa sekta binafsi ilipunguza ukuaji wa pato la ndani toka 7.2% ( 2015) mpaka 6.9% (2016)

iii. Wawekezaji wana wasiwasi/ mashaka na sera zisizotabirika kutoka za serikali ya Rais Magufuli.

iv. Kuporomoka /kushuka kwa kasi kwa mzunguko wa fedha na kuongezeka kwa Mikopo isiyolipwa kumeiathiri sana sekta binafsi.

v. Kubadilika badilika kwa sera kunapotokea mara kwa mara kunasababisha sintofahamu kwa sekta binafsi na sintofahamu husika zina athari katika maamuzi ya wawekezaji.

vi. Mabenki ya Tanzania yanajilinda /yanajiwekea wigo Mkubwa (LARGE BUFFER) dhidi ya hasara inayopatikana kwa

Mikopo isiyolipwa (kutokana na hali mbaya ya kibiashara tokea awamu ya tano iingie madarakani) kwa kutoza riba kubwa katika Mikopo.

vii. Baadhi ya wawekezaji wa kigeni wameamua/ wanataka kupunguza shughuli zao za uzalishaji au kusitisha mipango ya kupanua shughuli za uwekezaji kwa sababu ya masharti mapya magumu na kutozwa kodi kubwa. Tanzania inatajwa kuwa nchi ambayo sio rahisi kufanya biashara ikiwa inaongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya malipo (the highest number of payments) katika ukanda wa Afrika Mashariki.[2] Kuna malipo tofauti tofauti zaidi 48 ya kikodi.Na ni nchi ya pili kwa kuwa na kiwango kikubwa cha kodi (44.9%) katika ukanda wa Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika,** Hii ndio taswira ya hali ya mwenendo wa uchumi wetu kutokana na uchambuzi uliofanywa na wataalam wa fedha na uchumi kitaifa na kimataifa. Pamoja na yote hayo tunaambiwa kila kitu kinakwenda vyema!! Uongo huu na upotoshwaji unaofanya na serikali hii kupitia wizara ya fedha lazima ufike mwisho!!

## 6. MAENDELEO YA KISEKTA – SEKTA YA UZALISHAJI – VIWANDA

**Mheshimiwa Spika,** baada ya hotuba za wizara mbalimbali kukamilika tumegundua yafuatayo:

i. Kwamba, kwa mwaka wa fedha 16/17 serikali imeweza kutekeleza 30% tu ya miradi ya Maendeleo

ii. Kilimo Kinachoajiri 75% ya watanzania kimezidi kudorora.. ukuaji umeporomoka mpaka 1.7 % toka 6% iliyotarajiwa

iii. Viwanda vingi vilivyosajiliwa TIC ni viwanda ambavyo havina uhusiano wa moja kwa moja na shughuli pana za kiuchumi za nchi yetu.

---

[2] Price waters Coopers ,Comparative world studies of Tax Regimes 2014

iv. Viwanda vya usindikaji wa bidhaa zitokanazo na kilimo, Mifugo na uvuvi sio kipaumbele cha serikali

v. Hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya sekta ya kilimo , sekta ya viwanda na nishati. Viwanda haviwezi kuwa imara bila kuwa ma malighafi za kutosha kutoka kwa wazalishaji na Umeme wa kuweza kuviendesha.

vi. Hakuna dhamira ya serikali kufufua kilimo. Kijiografia Tanzania ilipaswa kuwa kapu la nafaka la Afrika ya Mashariki na Kati , yenye uwezo wa kuzalisha chakula kitakachotosheleza mahitaji ya ndani na zida kwa ajili ya nchi Jirani

**Mheshimiwa Spika,** Hotuba ya waziri mkuu, ukurasa wa 19 iliainisha kwamba katika kuhakikisha watanzania wanashiriki kikamilifu kwenye uchumi wa viwanda , serikali inahamasisha zaidi sekta binafsi ya hapa nchini Pamoja na Mashirika ya umma inajenga viwanda. Na kwamba jitihada hizo zimewezesha Mifuko ya hifadhi ya jamii ya NSSF, LAPF,LAPF,GEPF ,PSPF na NHIF kuanza kufufua, kuendeleza na kujenga viwanda vipya vipatavyo 27 katika maeneo mbalimbali nchini!

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya mwaka ya shughuli za Kamati nya kudumu ya Bunge ya uwekezaji wa mitaji ya umma (PIC ) kwa kipindi cha Januari ,2016 hadi Januari 2017 ikizungumzia madeni makubwa ambayo serikali inadaiwa na Mashirika na Taasisi zake inaainisha kwamba Kamati ilipokea taarifa ya msajili wa hazina kuhusu utendaji wa taasisi mbalimbali za umma na kubaini madeni makubwa ambayo serikali inadaiwa na Taaasisi hizo. Taarifa ya Kamati inasema.... ***Kwa ujumla uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa serikali imekuwa na tabia ya kutumia huduma au kukopa kutoka katika taasisi zake bila kufanya malipo.*** Serikali imekuwa ikidaiwa fedha nyingi na madeni hayo yamekuwa yakilimbikizwa mwaka hadi mwaka . Hali hii inadidimiza ukuaji wa Taasisi hizo na kusababisha hasara kuwa katika utendaji wao.

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko ambao unaonekana kuathirika zaidi ni Mfuko wa PSPF ambao unaidai serikali zaidi ya shilingi Trillion 3.3. ambayo yanajumuisha Madeni yanayotokana na dhima ya mafao ya watumishi wa serikali ambao walirithiwa na mfuko wa PSPF kipindi iliyoanzishwa mwaka 1999 (pre 1999).

**Mheshimiwa Spika,** Mpaka kufikia Juni 2015, serikali ilikuwa inadaiwa shilingi trillion 1.97. Kiasi kilicholipwa na PSPF kwa wastaafu kimezaa riba ya shilingi bilioni 698 **na kusababisha deni la shilingi trillion 2.67.** Kwa mujibu wa taarifa zilizowasilishwa na **Mfuko, uwezo wa mfuko kulipa kulipa mafao kwa wanachama wake unategemeana na namna serikali itakavyolipa michango** yake kwa wakati pamoja na kulipa deni la wanachama kipindi cha utumishi kabla ya julai 1999.

**Mheshimiwa Spika,** Kundi la pili linatokana na madeni ya uwekezaji. **Kumekuwa na kukinzana baina ya serikali na mfuko wa PSPF.** wakati serikali inadai deni inalodaiwa ni bilioni 290 , mfuko wa PSPF unadai deni halisi ni shilingi bilioni 533. Pamoja na mkanganyiko huo , **serikali imeshindwa kutekeleza ahadi yake ya kutoa hati fungani zenye thamani ya shilingi bilioni 290** kwa ajili ya kulipa deni hilo. Na deni la tatu ni madeni ya malimbikizo ya mchango wa mwajiri (15% ya serikali kila mwezi) Deni linalotokana na malimbikizo ya shilingi bilioni 253.78 ambalo ni la kipindi cha kuanzia Julai 2015 hadi Februari 2016.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali pia inadaiwa madeni makubwa katika Mifuko mingine, miongoni mwao ni NSSF,LAPF , NHIF ,PPF n.k kama ambavyo taarifa za Kamati za Bunge na Taarifa za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Serikali zinazotolewa kila mwaka zinavyoaainisha.. Kambi rasmi ya upinzani inashangazwa na kushtushwa na pendekezo hili jipya la kutumia Mifuko hii hii kujenga viwanda vipya 27, wakati serikali hailipi madeni inayokopa.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani haiwezi kuruhusu wizi wa namna hii kuendelea kufanywa na Serikali dhidi ya

fedha za wavuja jasho wa nchi hii! Ikumbukwe kwamba, hizi sio fedha za serikali, ni fedha za wanachama wanazochanga ili waweze kulipwa mafao punde wanapostaafu. Serikali inalazimisha mifuko kujenga viwanda wakati bado fedha za mifuko zilizotumika katika uwekezaji kwenye maeneo mbalimbali (hususan sekta ya nyumba) zikiwa hazina uhakika wa kurejeshwa kutokana na maamuzi mabovu ya uwekezaji yaliyofanywa na Mashirika husika.[3]

**Mheshimiwa Spika,** Ni muhimu sana hapa ikaeleweka kwamba , hatupingi Mifuko ya hifadhi kushirikiana na serikali katika uwekezaji,lakini ni uwendawazimu tukiendelea kuiruhusu serikali kuifanya Mifuko hii ni mirija ya kuchota fedha pasipo kulipa! Tunamtaka waziri wa fedha aliambie Bunge hili tukufu:

i) Katika Bajeti ya mwaka 2017/18 wametenga kiasi gani maalum kwa ajili ya kulipa madeni ya Mifuko ya Hifadhi za Jamii?

ii) Utaratibu wa utekelezaji wa malipo ukoje tofauti na makubaliano yaliyopita ambayo serikali haikuyatekeleza?

iii) Viwanda 27 vinavyotarajiwa kujengwa na fedha za mfuko kila mfuko utachangia kiasi gani na kwa utaratibu gani wa mrejesho wa fedha za wanachama?

iv) Viwanda husika vitajengwa wapi? Na vigezo gani vimetumika katika uchaguzi wa maeneo ya kujenga viwanda husika?

v) Kama mradi wa viwanda tajwa unalipa, ni kwa nini sekta binafsi haijengi? badala yake zinatumika fedha za wanachama?

---

[3] Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani ya Wizara ya Fedha na Mipango, fungu la msajili wa hazina imefanya uchambuzi wa uwekezaji wa kizembe usiofuata kanuni na miongozo ya Mifuko husika kulikopelekea hasara kubwa kwa baadhi ya mifuko.

## 7. DENI LA TAIFA (Fungu 22)

**Mheshimiwa Spika,** Deni la Taifa linasimamiwa na Sheria ya Madeni , Dhamama na Misaaada ya Serikali ya Mwaka 1974 ((iliyorekebishwa 2004) na **kulingana na vifungu namba 3 na 6 vya sheria ya madeni , dhamana na misaaada ya serikali ,1974. Waziri wa Fedha ndiye mwenye dhamana ya kukopa na kutoa dhamana kwa niaba ya serikali.**

**Mheshimiwa Spika,** Deni la Taifa limeendelea kuwa changamoto kubwa kwa uchumi wetu. Kukua kwa **Deni la Taifa kunasababisha bajeti ya Serikali kuendelea kuwa tegemezi na hivyo kushindwa kutatua kero za kiuchumi za wananchi**. Kwa bahati mbaya wananchi wengi hawaelewi undani wa deni la taifa na athari zake katika maisha yao ya kawaida. Jambo la kusikitisha ni kwamba Serikali imekuwa ikitumia mwanya wa wananchi kutokufahamu kwa undani athari za deni la taifa **kuendelea kukopa mikopo mikubwa yenye masharti ya kibiashara**.

**Mheshimiwa Spika,** Kuendelea kukopa Kwa namna hiyo kunaendelea kuwabebesha walipa kodi wa Tanzania mzigo mkubwa wa madeni ambayo yanazidi kufanya hali ya maisha kwa wananchi iendelee kuwa ngumu **kwa kuwa Serikali inatumia fedha nyingi kulipa madeni badala ya kuzitumia fedha hizo kugharamia miradi ya maendeleo**.

### 7.1. Mseto wa Deni la Taifa na Madhara yake Kibajeti

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Benki Kuu ya mwezi April, 2017 na Hotuba ya Bajeti 2017/18 inaonyesha kwamba Deni la Taifa limefikia **shilingi trillion 50.8** (Ikumbukwe mpaka mwaka jana Juni 2016 deni la Taifa lilikuwa shilingi Trillion 41) .Deni la ndani likiwa shilingi trillion 10.978. na deni la nje likiwa shilingi trillion 39.3 ( USD 17,578). Kwa kipindi cha mwaka mmoja deni la Taifa limeongezeka kwa Dola za Kimarekani milioni 884.8 ( sawa na shilingi trilioni 2).

**Mheshimiwa Spika,** Ikumbukwe kwamba kwa mwaka wa fedha 2016/17 kati ya shilingi 8,671,038,922,510(Trillion 8.67)

zilizotengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo (Wizara ya Fedha) shilingi 8,009,341,187,000 (Trilion 8) zilikuwa ni kwa ajili ya kulipia deni la Taifa.[4] Fedha zilizotumika kulipa deni,ni fedha nyingi kuliko fedha zilizotumika kwa miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa **deni la nje Serikali kuu peke yake** inadaiwa Dola za Kimarekani 13,792.9 **(Tshs Trillion 30.8).** Kwa mwaka mmoja pekee nyongeza ya mkopo (deni la nje) ilikuwa Dola za Kimarekani milioni 455.4 **( Tshs Trillion 1. 018)** Rejea Jedwali : External Debt Stock Borrowers katika Ripoti ya BOT ya Aprili, 2017. Kwa upande wa **Deni la Ndani:** Mpaka mwezi Mach, 2017 deni la ndani lilifika shilingi **10.976.8** bilioni. Ongezeko la mwezi la shilingi **bilioni 327** na ongezeko la mwaka kwa shilingi **Trillion 1.53**

**Rejea Jedwali 5.1 : Deni la Serikali (Government Domestic Debt Stock) 2007-2017 (Ripoti ya BOT mwezi April 2017)**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa deni la ndani wakopeshaji wakuu ni **Benki za biashara (41%)** ,mpaka mwezi Machi, 2017 wanaidai serikali shilingi 4,578.8 bilioni (Trillion 4.578), wakifuatiwa na **mifuko ya hifadhi ya jamii, (27%)**, ambayo mpaka Mwezi March 2017 wanaidai serikali shilingi Trillion 2.995.3 , nyongeza ya shilingi Trillion 1.482 ukilinganisha na mwezi Machi, 2016.

**Rejea Jedwali namba 5.4** (Ripoti ya BOT mwezi April 2017): Linaloonyesha mchanganuo wa deni la ndani la serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Imekuwa ni kauli za serikali kwamba deni la Taifa ni himilivu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni tumekuwa tukitoa tahadhari ya mara kwa mara kutokana na ukweli kwamba serikali imekuwa ikihamisha goli (Change of Goal Post) kila mara ili kujitafutia uhalali wa kuendelea kukopa huku Taifa likiingizwa kwenye matatizo makubwa.

---

[4] Hotuba ya waziri wa fedha na Mipango, Mhe. Dr. Philip I Mpango (MB), akiwasilisha Bungeni makadirio ya mapato na matumizi yam waka 2017/18, pg,12

Katika hotuba yetu ya mpango wa Taifa wa mwaka 2017/18 tulilihoji hili pasipo kupatiwa majibu.Cha kushangaza ni kwamba kauli za uhimilivu zimeanza kutajwa toka 2008 wakati deni likiwa shilingi Trilion 7.8 mpaka 2017 deni likiwa limefika shilingi Trillion 50.8

**Mheshimiwa Spika, Baada ya hoja za Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni za kipindi kirefu (2010/11; 2011/12; 2012/13, 2013/14, 2014/15; 2015/16 na 2016/17) hatimaye tahadhari juu ya uhimilivu wa deni la Taifa imetolewa na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za serikali. Katika Taarifa yake ya mwaka iliyotolewa mwezi Machi, 2017 Mkaguzi Mkuu alikuwa na haya ya kusema :**

**1.** Deni la Taifa lilianza kukua kwa kasi tangu mwaka 2007/08 wakati nchi ilipopata msamaha wa madeni

**2.** Deni ya Taifa limeongezeka kwa 149% kwa miaka mitano iliyopita bila kuhusisha madeni yaliyoachwa nje ya mseto

**3.** Mikopo **isiyo ya masharti nafuu yanaongezeka kwa 17%** . Kutoka shilingi bilioni 7,835 mwaka 2014/15 mpaka shilingi bilioni 9.155 mwishoni mwa mwaka 2015/16 . **Na mikopo yenye masharti nafuu kupungua** . Mwaka 2012 mikopo ya masharti nafuu ilikuwa 89% ya deni la nje ikilinganishwa na 69% mwishoni mwa mwaka 2015/16. **Hii ni kusema kwamba mikopo isiyo ya masharti nafuu (Mikopo ya Kibiashara) ilikuwa 31% ya deni la nje mnamo mwezi Juni 2016 ikilinganishwa na 11% miaka mitano iliyopita.**

**4.** Ongezeko la madeni ya nje yenye masharti ya kibiashara unaongeza gharama za kuhudumia deni kadiri mikopo inavyoiva . Hii ni kutokana na vipindi vifupi vinavyotolewa katika kulipa deni ( mara nyingi miaka mitatu), riba kubwa na muda mfupi wa deni kuiva!

**5.** **Taarifa ya uhimilivu wa deni la Taifa** inaonyesha kwamba kwa kuangalia gharama za kuhudumia deni la Taifa ,ikilinganishwa na mapato ya ndani ,gharama hizo ziko juu sana .Gharama za kuhudumia deni zikichanganywa

na gharama nyingine kama vile mishahara ya wafanyakazi ni gharama ambazo zinaiacha serikali na kiasi kidogo sana cha fedha za kugharamia miradi ya maendeleo na huduma nyingine za kijamii.

**6.** Kutokana na rasilimali kuelekezwa katika kulipa madeni , ni kiashiria kuwa serikali itaendelea kutegemea mikopo ili kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Matokeo ya utegemezi huu ni kukua kwa madeni ya ndani na nje ambayo siyo ya masharti nafuu. Mikopo husika pia inaendelea kuongeza gharama za kuhudumia deni.[5] ' ongezeko la mikopo isiyo ya masharti nafuu na mikopo ya ndani imesababisha gharama za kukopa kuwa juu, CAG anatoa wito kwa watunga sera kuchukua tahadhari.

**7.** Serikali kukopa ndani kwa wingi kunasababisha 'msongamano' wa sekta binafsi katika fedha chache zitakazokuwa zimebaki katika mabenki. Kwa lugha nyingine CAG anasema kukopa kwa wingi kwa serikali katika mabenki ya ndani **kunaua uwezo wa wafanyabiashara wa ndani kukopa**! hata wakifanikiwa kukopa masharti yanakuwa magumu sana.

### 7.2. Muundo na Usimamizi wa Deni la Taifa Kupitwa na Wakati

**Mheshimiwa spika,** Mkakati wa Taifa wa Madeni (NDS) wa mwaka 2002 uliandaliwa kwa mazingira ya sheria ya Mikopo ya serikali , Dhamana na Misaada ya mwaka 1974 (Miaka 43 iliyopita). Hali ya uchumi na mazingira ya kuanzishwa kwa sheria na mkakati wa NDS yamebadilika mno kutokana na mabadiliko ya kiuchumi ambayo yametokea.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na kupanuka kwa wigo wa deni la Taifa katika suala la vipengele na mikopo mikubwa ambayo imefanyika, sheria na miongozo inayosimamia deni la Taifa haiko sambamba na maendeleo hayo na vyombo vinavyotumika vimepitwa na wakati na kwa sababu hiyo kufanya usimamizi wa deni la taifa kuwa changamoto**.**

---

[5] Tanzania economic Update Report , May 2016

**Mheshimiwa Spika,** Mkaguzi Mkuu wa hesabu za serikali anabainisha [6] katika ripoti yake aliyoitoa hivi karibuni kwamba wakati wa mahojiano na idara mbalimbali zinazosimamia deni la Taifa chini ya wizara ya fedha ( idara ya uchambuzi wa sera (PAD), Mhasibu Mkuu wa Serikali (ACGEN), Idara ya fedha za Nje(EFD), Msajili wa Hazina, Tume ya Mipango na Benki Kuu ya Tanzania amebainisha kwamba **mfumo uliopo sasa unaongeza uzembe katika uendeshaji,uratibu duni na kutokuwa na taarifa za kutosha katika vitengo na taarifa sahihi kupitia taasisi na kusababisha kuwa na rekodi zisizosahihi** na zisizojitosheleza kuhusiana na deni !!haya ni maneno ya CAG !!!

**Mheshimiwa Spika,** katika uchumi unaokuwa kwa wastani wa asilimia kati 6.5 na 7 kwa mwaka, ni vigumu sana kuweza kulipa deni la Taifa linalokua kwa 149% kwa miaka 5. Bila kuwa na vyanzo vipya vya mapato au kusamehewa deni hili itakuwa vigumu sana kuweza kulipa deni hilo kikamilifu. Hii ni kwa sababu uwiano wa ukuaji wa uchumi hauendani na kasi ya ukuaji wa deni hata kidogo. Pamoja na upungufu wote huu, Serikali imeendelea kujitapa kuwa inakopesheka, na hivyo kuashiria kutokuwepo na hofu yeyote ya kukopa huku holela.

**Mheshimiwa Spika,** kinachosikitisha zaidi ni kuwa sehemu kubwa ya mikopo hii inakopwa katika soko la ndani. Hali hii imekuwa ikileta ushindani mkubwa kwa wananchi na wajasiriamali wanaotaka kukopa ili kukuza mitaji. Hali hii hufanya riba za mabenki kushindwa kushuka na hivyo kuwaathiri wakopaji na uchumi wa nchi kwa ujumla. Kwa maneno mengine, serikali imekuwa inazuia wajasiriamali wasikope kwa riba za bei nafuu, hivyo kufanya baadhi ya wanaokopa kwa riba zilizopo, ambazo ni kubwa kufilisiwa. Hali hii hurudisha biashara nyuma na inainyima serikali fursa ya kukuza uchumi na kukusanya mapato zaidi.

---

[6] Ripoti kuu yam waka ya mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za serikali, kuhusu taarifa za fedha za Taasisi za Serikali Kuu kwa mwaka unaoishia Tarehe 30Juni ,2016. Machi 2017, uk.76

### 7.3. Mzigo Mkubwa wa Deni kwa Taifa (Debt Stress)

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya uchambuzi wa uhimilivu wa deni la Taifa uliofanyika mwaka 2015 na 2016 inaonyesha kuwa **uwiano wa gharama za kuhudumia deni na mapato ya nchi** (vyanzo vya ndani ya mapato) **unakua kwa kasi sana** [7]. Hili limejidhihirisha katika bajeti ya mwaka 2016/17 ambapo serikali kupitia vyanzo vyake vya ndani (**mapato ya kodi, mapato yasiyo na kodi na mapato ya serikali ya mtaa)** ilifanikiwa kukusanya shilingi **trillion 13.5**.[8] Fedha zilizotengwa kuhudumia deni la Taifa zikiwa shilingi 8,009,341,187,000 (Trilion 8). Na fedha zilizotengwa kwa ajili ya mishahara ni Trillion 7.2.

Mheshimiwa Spika,Mchanganuo hapo juu unatuonyesha kwamba Kwa mishahara na deni la Taifa peke yake fedha zilizotumika shilingi Trillion 15.2 huku makusanyo ya nchi yakiwa ni shilingi 13.5 Kwa tafsiri nyingine werikali ina uwezo wa kulipa mishahara na kuhudumia deni la Taifa tu! Huku ikiwa na upungufu wa shilingi Trillion 1.7. Bila mikopo serikali isingekuwa na ubavu wa kufanya shughuli yoyote ile!! Hii ni hatari

**Mheshimiwa Spika,** Hali kama hii inatarajiwa kujitokeza katika bajeti ya mwaka 2017/18 kwani kati ya shilingi Trillion 19 zinazotarajiwa kukusanywa kutokana na mapato ya Ndani , Shilingi trillion 16.6 zinatarajia kulipa misharaha na kuhudumia deni la Taifa.[9]

**Mheshimiwa Spika,** hali inaweza kuwa mbaya zaidi mwaka huu sababu serikali imejiwekea maoteo makubwa ma makusanyo ambayo hayana uhalisia. Kama mwaka 2016/17 ilipanga kukusanya shilingi Trillion 29.53 ikaambulia kukusanya shilingi Trillion 20.7 (Pungufu ya Trillion 9) Ni miujiza gani itakayoiwezesha serikali kukusanya Trillion 31.7 kwa mwaka wa fedha 2017/18?!!

---

[7] Ofisi ya Taifa ya UKAGUZI, Ripoti kuu ya mwaka ya mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Machi 2017

[8] Hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. DKT Philip I. Mpango,Mapendekezo ya serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha mwaka 2017/18, 8 Juni 2017, Uk 26 & 27

[9] Trillion 7.2 zinalipa mshahara na trillion 9.461 zikihudumia deni la Taifa.

### 7.4. Serikali Inakopa kwa Masharti ya Kibiashara Kulipa Mikopo: Maajabu!!!!!

**Mheshimiwa Spika,** Hotuba ya Waziri,[10] inaonyesha kwamba serikali inatarajia kukopa shilingi Trillion 7.763 kutoka soko la **ndani** na **nje** kwa masharti ya Kiabiashara. Mikopo ya ndani ikiwa shilingi Trillion 6.168, ambapo shilingi bilioni 4.948.2 ni kwa **ajili ya kulipia dhamana za serikali zinazoiva**.

**Mheshimiwa Spika,** utaratibu wa aina hii unachangia kwa kiasi kikubwa kuongeza mzigo wa deni kwa nchi! Serikali imeshindwa kulipa madeni kwa kutumiavyanzo vyake vya mapato!

Tabia hii inazidi kuota mizizi, kwani katika mwaka 2014/15 kati shilingi trilioni 1.8 zilizokopwa katika soko la ndani, zaidi ya shilingi trilioni 1.1 zilitumika kulipa madeni ya hati fungani wakati shilingi trilioni 0.69 tu ziliwekwa kwenye miradi ya maendeleo. Hiki ni kiashiria cha karibu sana kwa serikali kufilisika.

**Mheshimiwa Spika,** Kukopa mikopo ya kibiashara yenye riba kubwa ili kulipa mikopo yenye riba ndogo au kwa uendeshaji wa kawaida wa serikali au taasisi zake ni kiashiria cha kutosha kuainisha maamuzi yasiyo na uelewa wa kawaida sana wa utawala na usimamizi wa fedha. **(basic business and economic sense).** Mikopo ya kibiashara hutafutwa kwa matumizi ya uwekezaji wenye lengo la uzalishaji.

### 7.5. Imani ya Taasisi za Fedha za Kimataifa kwa Tanzania Imepungua

**Mheshimiwa Spika,** Imefikia hatua hata kupata 'hiyo mikopo ya biashara' imekuwa shida. Katika bajeti ya mwaka 2016/17 serikali ilipanga kukopa kutoka kwenye vyanzo vya kibiashara shilingi trillion 2.1 ili kugharamia miradi ya maendeleo. Fedha hizo hazikupatikana kwa maelezo kwamba soko la fedha za kimataifa kutokuwa na hali nzuri.

---

[10] Uk. 79

**Mheshimiwa Spika,** sababu inayotolewa na serikali haina ukweli. Ukweli ni kwamba taasisi za fedha za kimataifa zinakwepa kuikopesha serikali kwa sababu haina uhakika juu ya uwezo wa serikali wa kulipa mkopo pamoja riba kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali yetu imekuwa ikikwepa kufanyiwa tathmini/uhakiki wa uwezo[11] wa kukopesheka (Credit Rating)[12] kwa kipindi kirefu sasa,inashindwa hata na Rwanda!! sijui kuna siri gani inafichwa. Matokeo yake wanatarajia kupewa mikopo kwa huruma na hisani jambo ambalo halifanyika katika ulimwengu wa Biashara!

**Mheshimiwa Spika,** Ili kuweza kutanzua kutendawili na utata wa deni hili;

i) Ni rai ya kambi rasmi ya upinzani bungeni kurudia ushauri tulioutoa miaka minne na kulitaka Bunge liridhie na kumwelekeza Mkaguzi Mkuu wa hesabu za serikali kufanya ukaguzi maalum (special audit) katika kitengo cha Deni la Taifa (fungu 22) ili kujua mikopo inayochukuliwa kila wakati inatumika kufanyia nini, na miradi iliyotekelezwa kama ni miradi ya kipaumbele kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

ii) Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaendelea kuitaka serikali kama ambavyo tumesema miaka mitano iliyopita kulitaka Bunge litunge sheria ili liweze kudhibiti ukopaji na matumizi ya mikopo ya serikali. Vile vile tunapendekeza katika sheria hiyo iwe lazima kwa serikali kupata kibali kutoka katika Bunge kabla ya kuweza kukopa. Hii inafanyika katika nchi nyingi duniani kama vile Marekani na Uingereza.

---

[11] Kiwango/thamani

[12] Credit Rating is an assessment of creditworthiness of a borrower in general terms or with respect to a particular debt or financial obligation. Credit ratings determines the likelihood that the borrower will pay back a loan within the confined time of the loan agreement without defaulting.

iii) Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali wakati wa majadiliano ya mikataba ya mikopo, kutumia utaratibu wa 'Interest rate swap[13]'kutokana na ukweli kwamba sababu mojawapo inayosababisha deni kukua kwa kasi kunatokana ni kuporomoka kwa thamani ya shilingi yetu na kuwa na riba ambazo zinabadilika mara kwa mara. Interest swapping maana yake ni kukubaliana kuweka kiwango cha riba kulingana na thamani ya shilingi ambayo inasaidia kuwa ni kiwango kilekile cha riba bila kujali kama thamani ya shilingi itapungua au itaongezeka. Hii inasaidia kufanya deni lisiongezeke kwa kasi kutokana na kupungua kwa thamani ya shilingi.

**Mheshimiwa Spika,** Ukirejea uchambuzi tulioufanya hapo juu kuhusiana na deni la Taifa na tishio lake katika mustakabali wa nchi hii, ni mwendawazimu pekee ambaye hataona hatari kubwa sana iliyo mbele yetu. Ni lazima sasa Bunge lako tukufu lichukue nafasi yake kuisimamia serikali kiukamilifu kama matakwa ya katiba yanavyolitaka ili kulinusuru Taifa.

## 8. UPOTEVU WA MAPATO KATIKA SEKTA YA MADINI NA HADITHI ZA 'MCHANGA' ZA SERIKALI YA CCM

**Mheshimiwa Spika,** Hivi karibuni kumeibuka mjadala mpana juu ya rasilimali za nchi yetu baada ya sakata la Makinikia ama "Mchanga wa Dhahabu'.Katika hali ya kushangaza kuna upotoshwaji wa makusudi unaotaka kufanywa wenye dhamira ya kuonyesha kwamba ETI LEO kambi Rasmi ya upinzani Bungeni inapinga MAMBO ambayo kwa miaka mingi huko nyuma tumekuwa tukiyapambania dhamira ikiwa utajiri wa nchi hii uwanufaishe watanzania .

**Mheshimiwa Spika,**Nirejee hotuba yetu ya miaka ya karibuni iliyosomwa na aliyekuwa waziri kivuli wa fedha na Uchumi Ndugu James Fransis Mbatia wakati akiwasilisha HOTUBA MBADALA ya Bajeti mwaka 2014/15 akiielezea serikali ya CCM juu ya upotevu wa MAPATO katika sekta ya Madini. Naomba nirejee maelezo yake kama ifuatavyo:

---

[13] Interest rate Swap is a contractual agreement between two parties to exchange interest payments

i) Taarifa za shirika la fedha Duniana (International Monetary Fund - IMF) zinabainisha kuwa kati ya mwaka (2008 – 2011) mapato ghafi ya dhahabu yaliongezeka toka Dola za Marekani millioni 500 hadi bilioni 1.5 kwa sababu ya kuongezeka kwa uzalishaji na bei ya dhahabu kuongezeka dhamani, lakini mapato kwa serikali yalibaki kuwa Dola za Marekani milioni 100 kwa mwaka kwa wastani.Hali hii imesababishwa kwa kiasi kikubwa kwa msamaha wa kodi kwa makampuni (Corporate income tax holidays). Hakuna kampuni hata moja liliyolipa kodi hii hadi 2012. Taarifa ya IMF inaonesha pia kwa kuzingatia hali hii, hakuna mategemeo kuwa kipato kutokana na madini kitaongezeka hivi karibuni.

ii) **Mheshimiwa Spika,** pamoja na kupitishwa sheria mpya ya madini ya mwaka 2010, migodi iliyopo bado inaendelea kulindwa na mikataba iliyoingiwa kwa kutumia sheria iliyofutwa. Makubaliano ya kati ya Serikali na makapuni hayo inaonesha kuwa Tanzania inapoteza fedha nyingi sana, kwa mifano:

iii) Taarifa ya Tume ya Bomani ilikadiria serikali ilipoteza sh. bilioni **39.8 mwaka 2006/7** na sh. bilioni **59 mwaka 2007/8** kutokana na msamaha wa kodi ya mafuta tu (**fuel levy exemptions) kwa makampuni sita tu**. **Kufikia mwishoni mwa mwaka 2011, makampuni ya uchimbaji madini yalikuwa yanadai takribani Dola za Marekani miioni 274 kurejeshewa kutokana na msamaha wa kodi hiyo toka 2002.**

iv) Makampuni yamepewa haki ya kumiliki madini yake, ikiwemo haki ya kuuza hisa na mitaji yake bila kulipa kodi ya mapato (capital gains tax).

v) Mikataba na sheria inawapa makampuni ruksa ya kutumia hasara wanazopata kufidia kulipa kodi.

vi) Mwaka 2010, Tanzania Minerals Audit Agency (TMAA) ilikagua makampuni 12 na kugundua mapungufu/ udanganyifu wa matumizi ya makampuni wa Dola za Marekani milioni 705.8, ambapo serikali ilikosa mapato ya Dola za Marekani 176 milioni. Hii ilikuwa mara ya kwanza

TMAA kufanya ukaguzi, je, kwa miaka 10 kabla ya hapo serikali ilipoteza kiasi gani cha mapato?

vii) **Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa taarifa ya Kamati ya Viongozi wa Kidini juu ya Haki za kiuchumi na Umoja (A report commissioned by the Interfaith Standing Committee on Economic Justice and the Integrity of Creation) iliyoitwa The *One Billion Dollar Question* iliyotokana na utafiti wa kutafuta mianya na kiasi cha upotevu wa mapato kwa nchi katika sekta ya madini, upotevu wa mapato ulikadiriwa kufikia Dola za Marekani bilioni 1.07 kwa mwaka 2009/10 kwa njia ya **misamaha ya kodi, ukwepaji kodi, uhamilishaji mitaji na vivutio vya kodi kwa uwekezaji**.

viii) **Mheshimiwa Spika,** upotevu huo wa Dola za Marekani bilioni 1.07 (takribani sh trilioni 1.7) ilikuwa ni takribani asilimia 17 ya bajeti yote ya serikali kwa mwaka 2009/10. Hoja hizo zote za kambi zilijibiwa kwa kejeli kubwa sana na wabunge walio wengi wa CCM zikiongezewa mbwembwe na mtoa hoja (WAZIRI mwenye dhamana ya Fedha) , Rais Magufuli akiwa sehemu yao!

**Mheshimiwa Spika,** Tukiwa mwaka wa pili wa utekelezaji wa bajeti ya serikali ya awamu ya tano ya CCM , bajeti ambayo imevunja rekodi kwa kuwa utekelezaji mbovu kuliko uliowahi kutokea kwa upande wa miradi ya maendeleo (0-30%),Huku Halmashauri zetu zikiwa HOI BIN TAABAN kwa kunyang'anywa mapato, imeibuka hoja ya MCHANGA WA DHAHABU. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haihitaji Bunge lako tukufu kutumia misuli mingi kujadili 'mchanga' ambao kwa mikataba yetu NI MALI YA MWEKEZAJI. Mchanga ambao hata kama wote ungegeuka dhahabu leo ,stahili yetu kama nchi ni mrabaha wa asilimia nne tu!! Tunataka Bunge lijadili kuhusu DHAHABU yetu na madini yetu mengine yanayoibiwa kila uchwao NA SIO MCHANGA!

**Mheshimiwa Spika,** Tunataka Bunge hili lirejee makosa yaliyofanywa na wana CCM wenzao mwaka 1997(KUJISAHIHISHA na kuwaomba Radhi watanzania) walipoleta sheria ya marekebisho ya sheria mbalimbali za

fedha ( Financial Laws Miscellaneous Amendments Act 1997) ambayo ilifanya marekebisho makubwa katika sheria mbalimbali za kodi , tozo na ushuru mbalimbali kwa makampuni ya madini. Matokeo yaliyoisababishia nchi kukosa mapato ya kutosha katika madini, matokeo yake nchi inashindwa kujitosheleza kibajeti ,inajiendesha kwa kukopa huko huko kwa wanufaika wa MADINI yetu na sasa deni la TAIFA limefikia shilingi Trillion 50.8

**Mheshimiwa Spika,** Tukifika hapo, TUTAMPOGEZA RAIS, lakini si kwa maigizo yanayofanyika sasa.

## 9. WANANCHI WANATAKA BAJETI INAYOZINGATIA UKUAJI SHIRIKISHI – INCLUSIVE GROWTH

**Mheshimiwa Spika,** Hakuna ubishi kwamba mipango mbali mbali ya serikali imekuwa ikigonga mwamba kwa sababu mipango inakuwa mingi, fedha kidogo na hakuna mwendelezo (consistency). Jambo likipangwa kutekelezwa kwa miaka mitano , lisipofanikiwa tunarukia jambo lingine hata kama hatukufanya uwekezaji wakutosha, Matokeo yake hakuna kinachofanikiwa!

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaendelea kusisitiza kwamba huwezi kuondoa umasikini bila kuigusa sekta inayoajiri watanzania walio wengi! TUNARUDIA Kama Kilimo hakitaendelezwa, ina maana kwamba, itakuwa ni ndoto kuondoa 75% ya Wananchi wetu katika lindi la umasikini. Sekta ya Kilimo imedumaa si kwa sababu nyingine yeyote zaidi ya Ukweli kwamba hakuna uwekezaji wa maana unaofanyika!

**Mheshimiwa Spika,** Ripoti zinaonyesha kwamba Shughuli za kiuchumi za kilimo zilikuwa kwa kasi ndogo ya **asilimia 3.5 mwaka 2014/15** ikilinganishwa na asilimia **2.3 mwaka 2025/16** .Mwaka 2017 kimezidi kudidimia kufikia **1.7%**...tusishangae mwaka 2018 tukiambiwa ukuaji wa sekta hii imefikia 0.5%!! ni wazi kwamba hakuna miugiza inayoweza fanyika kama serikali inatenga **shilingi bilioni 3.3** kuhudumia **watanzania milioni 30** , wakati huo huo **shilingi Trillion 1** zimelipwa

'CASH' kununua ndege ambazo zinahudumia **watanzania 10,000**[14].

**Mheshimiwa Spika,** Licha ya kupuuzwa, bado sekta hii imeendelea kuongoza kwa kuwa na mchango mkubwa katika pato la Taifa kwa kuchangia kwa asilimia 29.0 ya pato la Taifa ikifuatiwa na shughuli za ujenzi (13%), biashara na matengenezo (10.7%) na ulinzi na utawala 6.4%.

**Mheshimiwa Spika,** hata hotuba wa waziri [15]I naonyesha ni kwa namna gani serikali ya CCM haina mpango kabisa na wakulima wan chi hii (75% ya watanzania) kwa miradi inayopewa msukumo wa KIPEKEE kwa mwaka 2016/17-2020/21 kati ya vipaumbele 8, suala la KILIMO limezungumziwa katika kamradi kamoja ka uanzishwaji wa shamba la miwa nakiwanda cha sukari,na pesa zilizotengwa ni shilingi bilioni mbili tu!! HII NI ZAIDI YA MZAHA!

**Mheshimiwa Spika,ILI Kilimo kiweze kupiga hatua:-**

1. Lazima tufanye utambuzi wa maeneo ya kipaumbele kwa Taifa

2. Utambuzi wa aina ya mazao ambayo ni kipaumbele kwa Taifa baada ya kufanya utafiti [16]wa kina wa kujua **mahitaji ya soko; soko la ndani, kwenye ukanda wa Africa Mashariki, Afrika na Dunia** ambayo yakifanyiwa uwekezaji maalum na ya kimkakati wa serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi na wakulima wadogo tutataweza ongeza pato la Taifa na kupunguza umasikini lakini kubwa zaidi kusaidia ukuaji wa sekta nyingine!

3. Lazima kuwe na mkakati maalum wa kuongeza thamani ya mazao ya kimkakati ( Maendeleo ya viwanda vidogo na vya kati)

---

[14] Rejea Hotuba ya Kambi Rasmi ya upinzani Bungeni, wizara ya fedha 2017/18. Ofisi ya Msajili ya Hazina juu ya hali ya Kampuni ya Ndege.

[15] Hotuba ya waziri wa fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango (MB), Taarifa ya Hali ya uchumi 2016 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa mwaka 2017/18

[16] Hoja ya kutenga 1% ya GDP kwa shughuli za utafiti ililenga kupatia ufumbuzi maswali kama haya.

4. Miundombinu bora ya kuunganisha maeneo ya kimkakati na soko

5. Ujenzi na Upanuzi wa mabwawa ya umwagiliaji (irrigation schemes) kwenye maeneo ya mkakati

6. Hakikisha kuna pembembejeo za kilimo za kutosha sambamba na mbolea na mbegu kwa wakulima

**Mheshimiwa Spika,** Uchumi imara wa Brazil leo,unategemea KILIMO NA VIWANDA[17] Pamoja na mambo mengine ulianzia katika uwekezaji wa zao la KAHAWA .Brazil ilitambulika Duniani kwa zao husika, hata mtikisiko wa uchumi ulipotokea miaka ya 1930 serikali ilihakikisha inafanya uwekezaji kupitia program maalum kuhakikisha zao husika haliteteteki. Kilimo kilikwenda sambamba ya viwanda vidogo na vya kati vya kuongezea thamani . Hii ilikwenda sambamba na ujenzi wa miundombinu ya Barabara na reli kwa ajili ya kuunganisha maeneo ya uzalishaji (yaliyotambulika kimkakati) na masoko.

**Mheshimiwa Spika,** Kukosekana kwa umakini kunaonekana kwenye hotuba wa waziri wa fedha na mipango juu ya jukumu la Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB)[18]. Waziri anasema katika mwaka 2017/18 Benki ya Maendeleo ya Kilimo itaboresha huduma za kibenki kwa kuanzisha mazao maalum kwa wakulima wadogowadogo kulingana na mnyororo husika wa thamani kulingana na vipaumbele vya Mikoa husika.. Na kwamba Benki imepanga kufanya maandalizi ya kutoa Mikopo ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika maeneo yaliyoainishwa na Tume ya Taifa ya umwagiliaji.. vilevile benki imepanga kuwa jengea uwezo wakulima wadogowadogo, Wafanyakazi wa Benki, benki nyingine na Wadau mbalimbali wa kilimo nk.

---

[17] How can Tanzania move, From poverty to prosperity? Edited by L.A. Msambichaka- J.K .Mduma – O .selejio- O.J Mashindano, pg 173

[18] Benki hii ilianzishwa kwa lengo la kuiwezesha Tanzania kufikia mapinduzi ya Kilimo . Uanzishwaji wa benki hii ilikuwa moja ya maazimio kumi ya KILIMO KWANZA yaliyofikiwa mwaka 2009.

**Mheshimiwa Spika,** mbali na kwamba haijulikani hivyo vipaumbele vya mikoa vina uhusiano gani na Malengo Mapana ya Taifa ili kuelekeza Mikopo kwenye maeneo husika ni Ukweli usiopingika kuwa benki hii ni MFU.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa wasiofahamu uanzishwaji wa benki hii mwaka 2009 , Benki hii ilikuwa shughuli ya pili kwa umuhimu (Baada ya shughuli ya 1 ya "kuongeza bajeti ya Serikali kwa ajili ya Kilimo kwanza ")Kati ya shughuli 15 za nguzo ya pili ya Kilimo Kwanza. Ilidhamiriwa TADP ianzishwe ikiwa na mtaji wa dola za kimarekani milioni 500 (kipindi kile shilling bilioni 800, sasa hivi Trilion 1.1)….Fedha hizo zingepatikana iwapo serikali ingetenda bilioni 100 kila mwaka …. Lengo likiwa ni kukopesha wakulima wadogo wadogo kwa masharti na riba nafuu!! Benki hii muhimu iliishia kuambulia shilingi bilioni 60 tu mwezi April 2015.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa nini tunaogopa kufanya utambuzi wa KITAALAM , kuwekeza, hatimaye kurekebisha pale ambapo tunakosea pasipo kuchoka mpaka pale azma ya NCHI ikakapotimia?

**Mheshimiwa Spika,** Kwa hili, tuna la kujifunza kutoka India. Mapinduzi ya viwanda India ni Matokeo ya mkakati/mpango maalum wa miaka mitano mitano wa toka mwaka 1951 unaoendelea mpaka sasa, huku Mkakati mahsusi wa Maendeleo ya viwanda ukianza mwaka 1970. Iliwachukua zaidi ya muongo mmoja kwa India kugundua kwamba walikosea 'kutaka kuanzisha viwanda vikubwa' wakati rasilimali watu(ndani ya nchi) ya kuviendesha viwanda hivyo haipo. Kuziba mwanya huo wenzetu walianzisha mkakati maalum wa kutumia DIASPORA ambao wamekuja kuwa na mchango chanya sana katika mapinduzi ya Uchumi na viwanda![19]

**Mheshimiwa Spika,** Natambua kwamba kila nchi ina mazingira tofauti na fursa tofauti. Sisi kama Taifa tunajipambanua vipi? Kambi rasmi ya upinzani Bungeni

[19] India ina diaspora wanaokadiriwa kufikia milioni 20 wanaoishi katika mataifa mbalimbali 70 duniani.

inasisitiza ,UKUAJI SHIRIKISHI wa uchumi hauwezi kuacha Maendeleo ya KILIMO .Mkurugenzi Mwendeshaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) akitoa utangulizi katika semina ya waheshimiwa wabunge kuhusu kuanzishwa kwa TADB alisema: *"ili Tanzania ifanikiwe katika kupunguza umasikini na kujenga uchumi wa viwanda , ni lazima ifanye mapinduzi kwenye sekta ya Kilimo.*

**Mheshimiwa Spika,** Ni ukweli unaouma kwamba, viwanda haviwezi kuwepo bila malighafi. Lakini vilevile viwanda (kama vitajengwa ) havitakuwa na msaada katika kupunguza tatizo la AJIRA nchini kama hatuna rasilimali watu ya ndani ya kutosha kuweza kuviendesha..Korea ya Kusini ilikuwa na POTENTIAL toka miaka ya 1970 ya kuanzisha viwanda vya magari (automotive industries),lakini iliwachukua miongo miwili kabla ya nchi kuibuka kama moja ya wazalishaji wa magari toka bara la Asia. Waliwekeza katika rasilimali watu mahsusi kwa ajili ya viwanda husika kwa zaidi ya miaka 20. Walipoibuka walipenya kiurahisi kabisa na kuwa washindani wakubwa katika uzalishaji wa magari!

**Mheshimiwa Spika,** Somo la Korea ya Kusini na India linatuambia kwamba BAJETI inayozingatia UKUAJI SHIRIKISHI wa uchumi unatutaka tuwekeze katika ELIMU na mafunzo kwa VITENDO. Na sio elimu kiujumla wake, bali mkazo uwekwe (toka ngazi ya msingi) kwenye maeneo ya kimkakati ambayo TAFITI zinaonyesha kwamba tukiwekeza ,tutapenya kwenye SOKO! Hivi Tanzania ya viwanda ambayo ndio Wimbo wa TAIFA wa kila mmoja wetu tumeihuisha vipi katika mipango yetu mbalimbali ya nchi ? Hivi nikiiuliza serikali leo, kiwanda cha chuma cha liganga na mchuchuma kinatarajiwa kuendeshwa na nani?? Kwa manufaa ya nani?? Na kwa maandalizi gani?? Au ndio yale ya dhahabu, zinavunwa na wageni sisi tunaishia kugombana sababu ya MCHANGA

**Mheshimiwa Spika,** Maendeleo ya sekta moja inategemea ukuaji wa sekta nyingine. Viwanda sio mbadala (Substitutive ) wa Kilimo , bali ni sekta mbili zinazotegemeana. Viwanda

/Kilimo haviwezi kukua bila kukuza / kuboresha sekta hizi mbili kwa pamoja . Kama Kilimo kitachukuiwa kuwa ni ‘ moyo’ wan chi, basi viwanda itakuwa ni ‘ubongo’.

## 10. UCHAMBUZI WA KINA WA HALI YA UCHUMI WA TAIFA, MPANGO WA TAIFA WA MAENDELEO NA BAJETI YA SERIAKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18

### 10.1. [MANENO YA KIFUNGU HIKI YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA SPIKA]

### 10.2. Uchambuzi wa Bajeti na Hali ya Uchumi

- **Ukuaji wa Uchumi Usiopunguza Umasikini**

**Mheshimiwa Spika,** Ni jambo lisilobishaniwa tena kuhusu kuongezeka kwa ukali wa maisha kwa kila mtanzania. Kwa muda mrefu, Serikali ya CCM imekua ikitumia kigezo cha ukuaji uchumi kupotosha kuhusu hali halisi ya uchumi wa taifa letu. Serikali ya awamu ya tano inatumia dhana ya ukuaji uchumi kwa asilimia 7% kama hoja ya kukaririsha watanzania waamini kwamba hali ya uchumi ni shwari na kwamba kiwango chetu cha ukuaji uchumi ni kikubwa ukilinganisha na nchi washindani wetu hususani Kenya ambayo uchumi wake unakua kwa asilimia 6%.

**Mheshimiwa Spika,** Kwanza, nivema tukafafanua kwamba uchumi wa Kenya ni zaidi ya dola 65 billion, hivyo unapokua kwa asilimia6% ni sawa na ongezeko la dola 4bn , wakati uchumi wa Tanzania wa dola 45billion, unapokua kwa asilimia 7% ni sawa na ongezeko la dola 3bn Hii ni tafsiri muhimu sana kujulikana kwa watanzania kwamba kwa mwaka uchumi wa Kenya unaongezeka kwa kiasi kikubwa kuliko uchumi wetu badala ya kuwadanganya na takwimu za asilimia bila kuzingatia ukubwa wa uchumi wa kila nchi.

**Mheshimiwa Spika,** ni vema ikaeleweka pia kwamba ukuaji huu wa uchumi kwa asilimia 7% haukuanza leo baada ya Serikali ya awamu ya tano kuingia madarakani, ukuaji huu umekuwepo kwa zaidi ya muongo mmoja sasa, kwa maana

tangu awamu ya tatu(rejea hotuba ya bajeti ya 2005/06), chini ya Benjamini Mkapa, uchumi ulikua kwa kiwango hicho cha asilimia7%, na ifahamike tu kwamba mwaka 2011, Ukuaji huo ulifikia asilimia 7.9.

**Mheshimiwa Spika,** Nivema ikafahamika kwamba changamoto tuliyonayo kama taifa kuhusu uchumi sio ukuaji tena, bali namna ya kufanya ukuaji huo utafsiri maisha ya watanzania. Ilitegemewa tangu kuingia awamu ya nne na sasa ya tano, kazi kubwa ingekuwa kuhakikisha ukuaji wa uchumi unapunguza umasikini, badala yake imekua kinyume chake kwani awamu ya nne imeshindwa kupunguza idadi ya masikini, na mbaya zaidi awamu hii inafanya vibaya zaidi kuliko awamu ya nne katika mkakati wa kupunguza umasikini kama inavyojipambanua kwenye ripoti mbalimbali za kiuchumi za kimataifa na kitaifa sanjari na hali halisi wanayopitia wananchi kwasasa.

**Mheshimiwa Spika,** Bado Uchumi wetu kwa kiasi kikubwa unakuzwa na sekta zilezile, za Utalii, Madini, Huduma ya fedha,Mawasiliano, ambazo kwa hakika zinabeba watu wachache na ndio sababu ya uchumi kuendelea kukua bila kupuguza umasikini.Kwa zaidi ya muongo mmoja, Taasisi maarufu nchini inayohusika na tafiti za kiuchumi ijulikanayo kama Research on Poverty Alleviation(REPOA) imebainisha wazi kwamba ili kupunguza umasikini ni sharti kukuza sekta ya kilimo katika dhana pana(mazao, uvuvi na ufugaji) kwa asilimia 8% mpaka 10%, na kwamba tukikuza Kilimo kwa kiasi hicho kwa miaka mitatu3 mfululizo tutakata umasikini kwa asilimia 50%.

**Mheshimiwa Spika,** Ni bahati mbaya kwamba tangu awamu ya tatu mpaka awamu ya nne kilimo kiliendelea kukua chini ya asilimia 4% na mbaya zaidi, katika mwaka wa kwanza wa serikali ya wamu ya tano inayojinasibu kama serikali ya masikini, kilimo kimekua kwa asilimia 1.7%, kiwango ambacho ni hafifu kupata kutokea tangu Utawala wa Mkapa na Kikwete.

**Mheshimiwa Spika,** Ndio sababu Kambi rasmi ya upinzani bungeni tunapenda watanzania watambue kuwa Rais John Pombe Magufuli ni adui wa wakulima wa nchi hii, bajeti hii tunayomaliza ya 2016/17 ruzuku ya mbolea ilitengewa billioni10 na katika Bajeti hii ya pili 2017/18 Ilipanga kutumia billioni15 kama ruzuku ya pembejeo ukilinganisha na billion 78 ya mwaka wa mwisho wa Kikwete 2015/16. Ni vema ikaeleweka kwamba moja ya tatizo kubwa katika sekta ya kilimo Tanzania ni matumizi duni ya mbolea kwani imesisitizwa kwenye ripoti mbalimbali za tafiti za uchumi na kilimo.Kwa mujibu wa Ripoti ya Umasikini na Maendeleo ya Binadamu 2014(Poverty and Human Development 2014), Matumizi ya Mbolea Tanzania ilikuwa ni 9kg kwa ekari1 wakati nchi zenye chumi ndogo kama Malawi, wakulima wameweezeshwa kiasi cha kutumia 29kg kwa ekari1 na nchi zilizpiga hatua zaidi kwa kilimo kama China, ekari 1 wanatumianzaidi ya 260kg.

Kama tathimini hii ya matumizi ya 9kg kwa ekari1 Tanzania ni utafiti wakati ambapo serikali ya awamu ya nne walau ilikuwa ikitenga fedha kiasi cha kuonekana kwenye ruzuku ya mbolea, watanzania na hususan wakulima wanapaswa kujiuliza leo, ambapo Serikli inatenga 10billioni kutoka 78billioni hali itakuwaje?.

**Mheshimiwa Spika,** Ni vigumu kwa Serikali ya Tanzania kufanya mapinduzi makubwa kiuchumi yenye kupunguza umasikini bila kukuza kilimo katika dhana pana(mazao,ufugaji na uvuvi). Kwa mujibu wa Ripoti ya USAID ya 2014, asilimia 70% ya watanzania wanategemea Kilimo, na kati yao asilimia 75% ni wanawake. Hivyo masikini wakubwa Tanzania ni wanawake ambao ni asilimia 75% ya watu wote wanaotegemea kilimo, hiyo mwenendo wa sasa ambapo Bajeti ya Miradi ya kilimo katika mwaka huu wa fedha inatekelezwa kwa asilimia 2.2%, rekodi ambayo haijapata kutokea tangu Uhai wa Taifa hili ni ishara tosha kwamba Serikali hii haina mpango na masikini watanzania, na tabia ya Mhe Rais kujinasibu kuwa ni Rais wa masikini ni sawa na dhihaka kwa masikini wa Tanzania.

**10.3. Mkwamo wa Uchumi na Ongezeko la Ukata Nchini**

**Mheshimiwa Spika,** imekuwa changamoto kubwa hata miongoni mwa wachumi kuhusu hali ya uchumi nchini hasa inapoonekana biashara nyingi zinafungwa, walipa kodi wakubwa kama TBL , Benki za biashara , Kampuni za simu zote zinatangaza hasara. Manunuzi ya nje(imports) kuzidi kushuka, sekta ya nyumba(real estate) inazidi kuporomoka, kampuni zinazidi kupunguza wafanyakazi, soko la mitaji(stock market) linazidi kufanya vibaya, ukata kwenye uchumi (decline in liquidity) unazidi kuongezeka, lakini bado serikali inatangaza uchumi kuwa ni imara na kwamba mwaka 2016 inakadiriwa kukua kwa asilimia 7% na kwamba utaendelea kukua kwa asilimia 7.2% mwaka 2017.

**Mheshimiwa Spika,** Ipo haja ya kuchunguza uhalisia wa takwimu zetu kuepuka kujenga uchumi hewa kwa takwimu za kupika , ndio sababu IMF hivi karibuni wametahadharisha kuwa mwenendo mbovu wa sera za kibajeti na kutokutabirika kwa utawala huu kutasababisha kuzorota kwa uchumi katika mwaka huu wa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza hilo kwani hata ripoti za tathimini ya Uchumi ya robo mwaka inayotolewana Benki kuu(Quartely Economic review) inaonesha kuwa sekta zote kiuchumi zina hali mbaya, Rejea ripoti ya robo ya kwanza, robo ya pili na hata robo ya tatu .

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya fedha ni kichocheo kikubwa kwa sekta binafsi ambayo duniani kote ndio injini ya uchumi, kwa kigezo cha ulinganisho wa mikopo kati ya 2015/16 na 2016/17, takwimu za ripoti ya mwisho ya BoT ya Disemba 2016, iliyopo tovuti ya Bank Kuu inaonesha kwa mfano; Mikopo kwa sekta ya usafiri na Mawasiliano; mwaka 2015/16 ilikua kwa asilimia 33.1% ukilinganisha na ukuaji wa asilimia -0.1% kwa mwaka 2016/17, mikopo sekta ya uzalishaji viwandani mwaka 2015/16 ilikua kwa asilimia 22.3% ukilinganisha na asilimia 8.8% mwaka 2016/17. Mikopo ya Biashara ilikua kwa asilimia 16% mwaka 2015/16 ukilinganisha na asilimia -4.1% mwaka 2016/17. Mikopo kwa sekta ya ujenzi ilikuwa kwa asilimia 12.3% mwaka 2015/16 ukilinganisha na ukuaji wa

asilimia -4.15%. Ripoti zote za Bank Kuu kuhusu tathimini ya uchumi katika mwenendo wa mikopo kwa sekta mbalimbali inaashiria kuparanganyika kwa uchumi baada ya kuingia kwa awamu ya tano.

**Mheshimiwa Spika,** Ripoti ya robo ya pili ya tathimini ya kiuchumi inayotolewa na Bank Kuu BoT(Quartely Economic Reviews) ambayo ni ripoti ya robo ya pili ya utekelezaji wa bajeti hii ya 2016/17 inayoanza katika robo ya tatu ya tathimini ya uchumi ya BoT iliyoanzia Oktoba mpaka Disemba , 2016, inaonesha kuwa ujazo wa fedha kwenye uchumi(M3) uliongezeka kwa kiasi cha billion 645.1billions ukilinganisha na kiasi cha 3501.2 billions katika kipindi kama hicho mwaka 2015/16 sawa na upungufu wa ujazo wa fedha kwa asilimia 540%.

**Mheshimiwa Spika,** takwimu hizi zinaonesha wazi kwamba nchi ina hali mbaya isiyovumilika na inayohitaji mpango wa maalumu kuokoa uchumi huu kwa maana ya Stimulus package kama tulivyofanya mwaka 2008 kufuatia mtikisiko wa uchumi duniani kwani hali ya sasa ni mbaya kuliko 2008, Kwani Ripoti hizo za Benki Kuu zinaonesha wazi kwamba kushuka huko kwa ujazo wa fedha kwenye uchumi kunatokana na kushuka kwa kiwango cha mikopo kutoka Benki za biashara kwa sekta binafsi, na hivyo kuyumba kwa sekta bbinafsi ambayo kimsingi ndio injini ya uchumi.Na ndio sababu Benk Kuu ya Tanzania, kama msimamizi wa sera ya fedha, ikachukua hatua mbili kama namna ya kutafuta ufumbuzi wa ukata wa fedha kwenye uchumi(liquidity tightness). Hatua ya kwanza ni ile ya tangazo la kupunguza riba(credit discount) kwa mikopo ya Bank kuu kwenda bank za biashara kutoka riba ya asilimia 16% mpaka riba ya silimia 12%. Ikafuatiwa na tangazo la Bank Kuu la kupunguza dhamana za Bank za biashara zinazowekwa bank kuu kutoka asilimia 10% mpaka asilimia 8%

**Mheshimiwa Spika,** Hatua zote hizo zilichukuliwa kwa lengo la kukabili ukata kwenye uchumi kwa kuhakikisha sekta binafsi zinapata mikopo na kuchangamsha biashara kwenye uchumi na hivyo kukabili ukata mkali unaokabili uchumi

kwasasa.Hata hivyo, pamoja na juhudi zote hizo za Bank Kuu kwa kutumia sera ya fedha(Monetary Policy), bado ukata umebaki kuwa tatizo kwenye uchumi ikiwa ni kielelezo kwamba mzizi wa tatizo la uchumi kwa sasa chimbuko lake sio sera ya fedha( monetary policy)bali sera ya bajeti na mazingira ya biashara kwa ujumla(fiscal policy&Business environment).

**Mheshimiwa Spika,** Tatizo la uchumi kwasasa sio benki kukosa fedha kukopesha sekta binafsi, tatizo ni Serikali imeshindwa kujenga mazingira rafiki kwa biashara na wawekezaji kwa ujumla.wafanyabiashara na wawekezaji wa ndani na nje kwa ujumla wanakabiliwa na mazingira magumu kibiashara ndio sababu kiwango cha mikopo isiyolipika(Non Performing loans-NPL) kimezidi kuongezeka kwa kiasi ambacho hakijawahi kutokea kwa zaidi ya miongo miwili.Kwa mujibu wa ripoti ya BoT, kiwango cha mikopo isiyolipika kimefikia zaidi ya asilimia 10 ambapo wastani ni asilimia 5.

**Mheshimiwa Spika,** Hii ni ishara mbaya sana kwa sekta binafsi ambayo ndio inapaswa kuwa injini ya uchumi katika uchumi wa soko.Sio kwamba wafanya biashara hawa wanapenda kushindwa kulipa mikopo hiyo bali mazingira ya biashara ni mabovu na hivyo kusababisha wafanyabiashara kuogopa kukopa kwajili ya biashara na pia mabenki kuongeza urasimu wa kutoa mikopo kwa hofu ya mikopo isiyolipika kutokana na mazingira mabovu ya kibiashara ambayo msingi wake ni sera duni za kodi na utawala unaoendesha nchi kwa amri zaidi ya sheria. Na ndio maana hata ripoti ya mwaka 2017 kuhusu urahisi wa kufanya biashara(EASY OF DOING BUINESS) inayotolewa na Bank ya Dunia, Tanzania bado iko nyuma ya Kenya, Uganda na Rwanda ambao ndio washindani wetu kibiashara.

### 10.4. Wafanyabiashara Washirikishwe Kutatua Mgogoro wa Kiuchumi

**Mheshimiwa Spika,** Tangu awamu ya tatu chini ya Benjamini Mkapa kiliundwa chombo kinaitwa Tanzania National

Business Council-TNBC, Chombo hiki ni jukwaa muhimu kati ya Serikali na wafanyabiashara nchini, na kimuundo kinaongozwa na Rais kama Mwenyekiti.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na umuhimu wa chombo hiki kwajili ya kukutanisha na kugonganisha fikra kuhusu majibu ya uchumi na biashara nchini, Mhe Rais hakuwahi kuitisha chombo hiki kwa zaidi ya mwaka mmoja, na hata baada ya kuitisha baada ya shinikizo kubwa, bado maoni ya wawekezaji na wafanyabiashara yameendelea kupuuzwa. Ni wito wa Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni kumtaka Mheshimiwa Rais na wataalamu wake atumie jukwaa hili kusaka majawabu ya hali mbovu ya kibiashara inayoendelea nchini kwa kuchanga mawazo ya bongo za pande zote, wafanyabiashara na wataalamu wake. badala ya kusikia upande mmoja wa watendaji wake ambao wengi ni wanataaluma kutoka vyuo vikuu ambao kwa kiasi kikubwa hawajawahi kuwa practioners.

**10.5. Uamuzi wa Kuondoa Fixed Deposits za Serikali kwenye Benki za Biashara .**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inapaswa kuachana na Sera na Mipango ya kubahatisha au majaribio kwenye Uchumi. Itambukwa mwaka 2016 mwanzoni Serikali ilifanya uamuzi wa kuondoa fedha zake zote zilizokuwa zikiwekwa kwenye benki za biashara na kuzipeleka benki kuu BoT kwa hoja kwamba benki za biashara zinafaidi fedha hizo za serikali kwa kuzifanyia biashara.

**Mheshimiwa Spika,** Baadaye mwaka huu, Serikali hiyohiyo imehamasisha benki za biashara zikakope fedha benki kuu kwa riba punguzo kutoka asilimia 16% mpaka asilimia 12%. Kambi rasmi ya upinzani tunajiuliza, hivi ni akili gani iliyoamua kuondoa fedha za serikali kwenye benki za biashara ambako zilikuwa zinazalisha riba ya mpaka asilimia 15% na kuzipeleka benki Kuu ambako hazizalishi chochote? Kama awali Serikali ilikuwa inaweka fedha zake benki za biashara kwa riba ya asilimia 15% ni sawa na kusema serikali ilikuwa inazikopesha benki za biashara fedha yake kwa riba ya asilimia 15% lakini

sasa imeamua kuzikopesha kwa mlango mwingine benki hizo hizo kwa riba ya asilimia 12%. Kwa utaratibu wa uliofutwa ni serikali ilikuwa inapata riba ya asilimia 15 na sasa umeletwa utaratibu unaoitwa bora ambapo sasa serikali itapata riba ya asilimia 12%. Akili iko wapi katika jambo hili?

### 10.6. Ni wajibu wa Serikali Kutekeleza Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge

**Mheshimiwa Spika,** Jukumu la kujadili na kuamua kuhusu Bajeti ni moja ya majukumu muhimu kabisa ya Bunge hili tukufu ambalo tumepewa kikatiba. Jukumu la Serikali katika Bajeti ni utekelezaji tu. Na ndio maana mwaka 2015, Bunge hili lilipitisha Sheria ya Bajeti kwa lengo la kuhakikisha nidhamu na ufanisi katika kupanga, kutekeleza na kusimamia utekelezaji wa Bajeti.

**Mheshimiwa Spika,** Ni bahati mbaya sana, kama nilivyoeleza awali kwamba Utawala huu unaongoza kwa kutokuheshimu sheria na Katiba, makosa hayo yanajidhihirisha pia katika utekelezaji wa bajeti hii ya kwanza katika utawala wa awamu ya tano.Serikali kwa agizo la Mhe Rais imetumia fedha za bajeti hii kutekeleza baadhi ya mambo ikiwemo kuhamishia Serikali Dodoma,mambo ambayo hayakupitishwa naBunge kwenye Mpango wa Bajeti wa 2016/ 17.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi rasmi ya Upinzani haina tatizo na dhamira njema ya Serikali kuhamia Dodoma au utekelezaji wa mpango wowote kwajili ya huduma kwa wananchi. Tunachosisitiza ni kwamba uendeshaji wa Serikali lazma ufuate sheria na taratibu. Uendeshaji wa Serikali usiofuata Sheria na taratibu ni utawala wa fujo.Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015( The Budget Act 2015, Sect 34), inasisitiza wazi kwamba Serikali haitaruhusiwa kutekeleza mradi wowote ambao hakupitishwa na Bunge kwenye Mpango wa bajeti.Maamuzi ya namna hii yanapora mamlaka ya Bunge letu, na ni utovu wa nidhimu wa hali ya juu wa Serikali hii kwa Muhimili wa Bunge ambao kikatiba ndio Muhimili Mkuu wa dola (Supreme organ of the State).

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kwa msisitizo, nitumie maneno yaliyotumiwa na Jaji Maghimbi wa Mahakama Kuu Kanda ya arusha aliyetoa dhamana kwa Mhe Godbless lema , akionekana kukemea tatizo la Mahakama kuingiliwa, alisema ***"Ni lazma Mahakama zionee wivu mamlaka yake".***

**Mheshimiwa Spika,** Hilo ndilo neno ningependa Bunge pia tulitumie kama sote tunajitambua bila kujali tofauti zetu: ***Kwamba ni lazma Bunge lionee wivu Mamlaka yake*** . Na lisikubali Mamlaka yake yapokonywe na Serikali au Mamlaka nyingine ya dola. Ni lazma tuhakikishe Serikali inatekeleza majukumu yake ndani ya ukomo wa mamlaka yake na sio vingineyo kwani kuacha Serikali ifanye maamuzi ya Bunge, itafanya pia ya Mahakama na kuingiza taifa hili kwenye kile waingereza wanaita ***'Kangaroo Governance". Kwa maana ya Utawala usio na utaratibu***.

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Bajeti ndio kipimo cha uwezo wa uongozi kutimiza wajibu wake kwani ni bajeti inayotafsiri ahadi za Ilani ya Chama kilichopo Madarakani katika kufikia Dira ya Taifa, sanjari na ahadiMgombea Urais. Mafanikio ya Rais yeyote yanapimwa katika namna anavyomudu kutekeleza bajeti na sio idadi ya purukushani au ziara za kushtukiza na matamko yasiyo na ukomo kila kukicha na yasiyo ya kimkakati kuweza kutolewa na Ofisi kuu ya Nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti 2016/17, inaonesha wazi kwamba miradi ya maendeleo iliyotekelezwa ni asilimia 38% ya makadirio ya Bajeti. Kwamba, wakati makadirio ya matumizi kwa miradi ya maendeleo yalikuwa billion 11,820,503, Serikali imefanikiwa kutekeleza kwa kutoa billion 3,647.7 na fedha za nje billion 907.

**[MANENO YAMEFUTWA KWA MAELEKEZO YA SPIKA]**

### 10.7. Uwezo wa Kujitegemea Kiuchumi na Kibajeti

**Mhe shimiwa Spika,** Uchambuzi wa Bajeti hii unaonesha wazi kwamba chini ya CCM Taifa hili litasafiri zaidi ya karne bila kufikia uwezo wa kujitegemea. Kwa mfano, katika Bajeti ya

2016/17 , Makusanyo ya Kodi yalikuwa trilioni 11.6 dhidi ya makisio ya trilioni 15, na makusanyo yasiyo ya kodi yalikuwa trilioni 1.6 dhidi ya makisio ya trilioni 2.69 na makusanyo toka serikali za mitaa yalikuwa billion 399 dhidi ya makisio ya billion 665.

**Mheshimiwa Spika,** Wakati uwezo wa Serikali yetu yenye umri zaidi ya nusu karne ukiwa kiasi hicho, kiasi cha deni lililoiva mwaka 2016/17 ilikuwa trilioni 8 wakati msahahara peke yake ikiwa trilioni trilioni7?. Hii maana yake katika mwaka uliokwisha, makusanyo yetu jumla ya ndani trilioni 13.5 wakati hitaji la mshahara na deni peke yake likifika trilioni 15. Ni mazingira haya Rais Uhuru wa Kenya ataendelea kutukujeli kuwa Tanzania bado tuna serikali ambayo sio tu inakopa kugharimia miradi yote ya maendeleo bali inakopa kujiendesha kwa matumizi ya kawaida na hata mishahara ya walimu na watumishi haijimudu bila kukopa.

**Mheshimiwa Spika,** Hali ni hiyo pia katika Bajeti ya 2017/18, kwani Bajeti hii imekosa ubunifu wa vyanzo vya mapato, na hivyo itaendeleza aibu ya kushindwa kujimudu hata kugharamia mishahara ya watumishi kwani hakuna ubunifu wowote katika vyanzo vya mapato. ***Ni Bajeti iliyojaa rhetorics.*** Imekosa ubunifu katika vyanzo vya mapato, imekosa mkakati wa kuchochea sekta binafsi iweze kuchochoa uchumi, haisemi kwa utekelezaji wa bajeti hii itatengeneza ajira ngapi wala haisemi bajeti hii itapunguza umasikini kwa kiasi gani ili iweze kupimika mwisho wa siku.Kifupi ni bajeti ya mazoea, iliyojielekeza kwenye vyanzo vya mapato kwa mazoea na hivyo kukosa nyongeza ya ubunifu.

**Mheshimiwa Spika,** Nasisitiza kuwa Bajeti hii ni ya mazoea kwasababu maeneo yaliyongezwa kodi ni yaleyale ya miaka yote. Bajeti hii haisemi lolote kuhusu mkakati wa kumwinua wakulima ambao ni70% ya watanzania hasa katika mazingira ya sasa ambapo kilimo kimeporomoka kufikia ukuaji wa 1.7%, zaidi kwenye kilimo imebaki na msimamo wa kupunguza kiasi cha ruzuku kutoka 78bn ya mwaka 2015 mpaka 15bn ya mwaka 2017/18.Haina chochote kuhusu bank

ya wakulima, iliyoanzishwa mwaka 2015 kwa kusudio la mtaji wa 1trilioni na kukopesha wakulima 200,000 kwa mwaka lakini sasa imeishia kukopesha wakulima 3700 na mtaji wa billion 60 tu kwa miaka 3.

**Mheshimiwa Spika** Bajeti hii haisemi lolote kuhusu kujenga na kuimarisha wajasiliamali wadogo na wakati ambao ni asilimia 40% ya ajira zote.

### 10.8. Kukwama kwa Mikopo toka nje na Utekelezaji wa Miradi ya Kibajeti

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Tanzania imekuwa kinara wa kupata misaada na mikopo nafuu toka nje kuliko Serikali zote ukanda huu wa kusini na Mashariki ya afrika. Hii ni kwa mujibu wa ripoti ya Official Development Aid (ODA) ya mwaka 2013. Kwa mujibu wa Ripoti hii, Tanzania tunayokaririshwa kuwa nchi ya Amani na Utulivu imekuwa ikipata misaada (Grants) kuliko nchi zilizo vitani au zisizo na usalama kabisa duniani kama Kongo DRC na Sudan. Hii ni moja ya aibu kubwa kwa Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mwenendo huo wa miongo kadhaa ya Taifa hili kupata upenedelo huo wa misada zaidi ya kiwango cha nchi zilizo vitani, bado misaada hiyo haijaweza kuleta tija ya maana kiuchumi zaidi ya kujenga Serikali yenye akili tegemezi badala ya kujitegemea.

Serikali hii ya awamu ya tano, kuanzia kwenye hotuba ya Rais bungeni pamoja na hotuba ya wizara ya Bajeti 2016/17 lisisitiza kwa kiasi kikubwa dhana ya kutotegemea nje ingawa bajeti yake ni tegemezi kuliko ile ya awamu ya nne. Kwa mfano, Katika Bajeti ya mwisho ya awamu ya nne, kiwango cha misaada na mikopo nafuu toka nje ilikuwa trilioni 2.6, wakati bajeti ya kwanza ya Rais John Pombe Magufuli anayejitangza kutotegemea nje, misaada na mikopo nafuu ilikuwa 3.6trilioni. Huu ni ushahidi wazi kwamba serikali hii inategemea nje kuliko Serikali iliyopita.

### 10.9. Vita dhidi ya Rushwa na Ufisadi

**Mheshimiwa Spika,** Ripoti ya Transparency Inernational kwa mwaka 2016 kuhusu tathimini ya hali rushwa na ufisadi

duniani,Tanzania ni miongoni mwa nchi tano katika Afrika ambazo ziliguswa mahususi katika Ripoti hiyo, Kwa kifupi, ushauri wa jumla kuhusu nchi hizo za Kenya, Nigeria, South Africa, Ghana kuhusu mapambano dhidi ya ufisadi, ripoti hiyo inasema kwamba: ***"African Leaders that come to Office on an anti corruption ticket, will need to live up their pledges to deliver corruption free services to their citizen, they must implement their commitments to their principles of governance, democracy and human rights. This includes strengthening the insitutions that hold government accountable as well as electoral systems that allow citizens to either re elect them or freely chose an alternative.***

**Mheshimiwa Spika,** Kwa tafsiri isiyo rasmi, Ripoti hiyo inasema kwamba " Viongozi wa Afrika walioingia madarakani kwa tiketi ya vita dhidi ya ufisadi wanapaswa kuishi ahadi zao kuhakikisha rai wanapata huduma bila rushwa,na ili kufikia hatua hiyo ni lazma Viongozi hao wahakikishe wanatimiza wajibu huo kwa misingi ya utawala bora, demokrasia na haki za binadamu. Hii ni pamoja na kuhakikisha Taasisi zinazosimamia uwajibikaji wa serikali zinaimarishwa pamoja na mifumo ya uchaguzi inaimarishwa kuhakikisha wananchi wanaweza kuirudisha serikali hiyo madarakani au kuchagua serikali mbadala kwa hiari yao"

**Mheshimiwa Spika,** Hii ni ripoti Muhimu sana kwa utawala huu na ni vema Serikali hii ijenge tabia ya kusikiliza taasisi za kitaalamu zinasema nini kuhusu utawala wake. Kambi rasmi ya Upinzani inaunga mkono ripoti hii kwamba ili vita dhidi ya ufisadi iwe endelevu na yenye mafanikio ni lazma kama nchi tujenge taasisi imara za kuisimamia Serikali likiwemo Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Hali ya sasa ambapo Serikali inadhoofisha bunge kwa kuliweka gizani na kwa miongozo isiyokwisha toka Ikulu, Hali ya sasa ambapo Ofisi ya CAG inabanwa kibajeti ishindwe kutimiza majukumu yake ya ukaguzi ili kulisaidia Bunge kuisimamia Serikali, Hali ya sasa ambapo vyombo vya habari vinabanwa kuhakikisha vinaandika habari tamu kwa serikali, Ni mfano mbaya kabisa na ni

kielelezo tosha kwamba serikali haipo serious katika vita dhidi ya Ufisadi nchini kwani kinachoendelea ni serikali inaharibu yenyewe na inataka ijikosoe yenyewe na kujisimamia yenyewe.

### 10.10. UTAWALA BORA UNAVYOCHOCHEA UKUAJI WA UCHUMI

**Mheshimiwa Spika,** Ni aibu kwamba ingawa Washirika wa Maendeleo toka nje wamendelea kupunguza kwa kasi kiasi chao cha mikopo na misaada, bado bajeti za Serikali ya CCM zimendelea kuongeza kiasi cha utegemezi wa mikopo na misada toka huko bila kutatua msingi wa tatizo la kukwama huko. Tangu mwaka 2014/15 Nchi za Ulaya zimekuwa kwenye mahusiano mabovu na taifa letu kutokana na Serikali kushindwa kusimamia misingi ya utawala bora na Demokrasia kama sharti lao muhimu katika ushirikiano. Ni katika msingi huo Tanzania imekosa fedha toka Millenium Challenge Accounts (MCC II) zaidi ya 1trilion, ambapo nchi kama Ghana wamendelea kupata.

**Mheshimiwa Spika,** Kwasababu ya kuharibu uchaguzi mkuu zanzibara, Sheria mbovu ya makosa ya mitandao, kuliweka bunge gizani, Kuzuia mikutano ya kisiasa kwa vyama kinyume cha Katiba, yote hii imesababisha mahusiano mabovu kati ya Tanzania na nchi washirika wa maendeleo na ndio sababu ya kukwama kwa mikopo nafuu kutoka mataifa hayo pamoja na taasisi za fedha.

**[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA SPIKA]**

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania tangu zama za Mhe Mkulo kama waziri wa fedha mpaka Mgimwa na baadae Saada Mkuya na sasa Dr Mpango inapiga stori za kufanyiwa uhakiki wa uwezo wake kukopesheka(CREDIT RATING).Huu ni mfano wa namna tulivyo na Serikali isiyo na akili ya kibiashara. Duniani kote kuna Agency tatu zinazofanya kazi hii, ambazo ni Moodys, Standard&Poor na Fitch, kwa muda mrefu kumekuwa na mazungumzo yasiyokwisha kuhusu kampuni ya Moodys kufanyia uhakiki uchumi wetu lakini hakuna kinachoendelea. Ni vema Serikali ikakamilisha mazungumzo

hayo yasiyokwisha kwani uwezekano wa Tanzania kuendelea kupata mikopo ya kawaida toka nje umezidi kufifia.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi rasmi ya Upinzani inasisitiza hili kwani hata ripoti ya IMF ya Januari 9,2017, kuhusu mwenendo wa uchumi wetu imesisitiza hili, kwamba ni lazma Serikali ihakikishe inapata mikopo toka nje ili kutekeleza miradi mikubwa ya kibajeti kwakuwa ukosefu wa fedha hizo kwenye miradi hiyo ni moja ya sababu za ukata kwenye uchumi kwani imepunguza mzunguko wa fedha kwa kiasi kiubwa nchini.

### 10.11. Miradi ya Kimkakati katika Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ni nchi iliyobarikiwa kiasi kikubwa cha rasilimali lakini kwasababu ya ukosefu wa uongozi wenye maono bado rasilimali hizo hazijaweza kuliondoa taifa kwenye lindi na umasikini. Idadi ya watanzania masikini imezidi kuongezeka mwaka hadi mwaka badala ya kupungua.

**Mheshimiwa Spika,** Ripoti ya Poverty &human Development, inaonesha kwamba tangu kama taifa tuanze marekebishoya Uchumi (economic restructuring) katika miaka ya 1990, umaskini Tanzania ulikuwa asilimia 39% wakati idadi ya watu ilikuwa milioni 25, sawa na masikini milioni 9.750,000 na sasa kiasi cha umasikini ni asilimia 28, wakati idadi ya watu imefikia milioni 48, sawa na masikini milioni13.44.

**Mheshimiwa Spika,** Sababu kubwa ya kuendelea kuongezeka kwa masikini ni sera mbovu mtazamo finyu wa CCM katika kujua mahitaji ya Taifa na namna ya kuweka vipaumbele ili kufikia malengo. Badala yake imebaki chama kilekile kinabadilisha majina ya awamu na watawala bila kubadili mbinu zenye kuleta majawabu ya matatizo ya umasikini wetu watanzania. Moja ya Agenda kwa Afrika kwenye mwaka huu kwenye World Economic Forum, ilikua ni "AFRICA FORGET ABOUT NATURAL RESOURCES BUT TECHNOLOGY".

**Mheshimiwa Spika,** Naamini kama Mhe Rais angeshiriki mkutano huu wa kimkakati angeweza kupata mawazo zaidi ya dunia imefikia wapi na inahitaji nini kwasasa. Dunia kwasasa inahitaji tuwekeze zaidi kwenye kujenga rasilimali watu zaidi ya vitu. Ni utawala wa ajabu unaweza kuacha kuboresha elimu ya vijana wake ikatumia fedha hizo kununua ndege au kujenga barabara. Ndio maana sisi kama CHADEMA/UKAWA tulisistiza na tunaendelea kusisitiza kuwa Mradi pekee wa kimkakati kukwamua Taifa hili hapa ni kusuka mfumo wa elimu na kuhakikisha vijana wanapata elimu bora itakayowawezesha kushiriki dunia ya ushindani kama wadau sio watazamaji. Tunapaswa kujenga Taifa la watu ambao wanaweza kukabili maisha hata nchi hii ikigeuka kuwa jangwa lisilo na rasilimali yoyote kama ilivyo Israel. Inasikitisha kwamba huduma ya elimu nchini kuanzia shule za msingi mpaka Chuo Kikuu imebaki vurugu tupu. India ambayo miaka ya 1970tulikuwa nayo sawa kiuchumi, sasa inauza wataalamu wake nchi za Ulaya na marekani, wakati sisi bado tunauza mchanga, tumbaku na ngozi.

### 10.12. Mradi wa Chuma na Makaa ya Mawe

**Mheshimiwa Spika,** eneo la Liganga linakadiriwa kuwa na makaa ya mawe zaidi ya tani milioni 428 kiwango ambachi kinaweza kutumika kwa takribani miaka 500 (Kwa mujibu wa utafiti wa NDC),na chuma tani milioni 126.

**Mheshimiwa Spika,** Tangu awamu ya tatu mpaka ya nne kumekuwa za masimulizi yasiokwisha kuhusu namna kuvuna utajiri huu wa makaa ya mawe na chuma.Lakini kwasababu ya mtazamo finyu kibiashara, awamu zote zimekuja na kuondoka na kuacha masimulizi hayo. Awamu ya tano, kwenye bajeti 2016/17, iliahidi kufanyia kazi suala hili, lakini ni bahati mbaya sana, maelezo kwenye kitabu cha utekelezaji wa bajeti, yanatoa picha kwamba hakuna jipya zaidi ya mwendelezo wa masimulizi.

**Mheshimiwa Spika,** Akiba hiyo ya chuma na makaa ya mawe ni biashara kubwa na kama Serikali ingeweka mkazo kukamilisha utaratibu wa kukamilisha miradi hiyo miwili kwa pamoja Tanzania ingeweza kufikia kiwago cha kuuza nje sio

chini ya tani milioni 2 za chuma na makaa ya mawe, na kuvuna dola za kutosha kuendesha nchi hii. Ilikuvuna chuma, inahitajika umeme zaidi ya 250MW, wakati mradi uliokwama wa kuzalisha makaa ya mawe Liganga unaweza kuzalisha kwa kuanzia zaidi ya 600MW, kiasi ambacho kingetosha kuendesha mtambo wa kufua chuma na kubaki na ziada ya umeme ya 350MW.

**Mheshimiwa Spika,** Laiti kama tungekuwa na Uongozi makini, miradi hii miwili ilipaswa kuwa ya kwanza na yenye kupewa kipaumbele kabla hata ya kujielekeza kwenye ujenzi wa reli. Hii inatokana na ukweli kwamba ujenzi wa reli ya kati yenye urefu wa zaidi ya 2,400km itakayogharimu zaidi ya dola million 7,000, utahitaji mamilion ya tani za chuma, kiasi ambacho kama tungekuwa tumekamilisha mradi huo wa chuma tungeweza kupunguza gharama hizo kwa kiasi kikubwa na mradi huo ungekuwa soko kubwa kwa mradi wa chuma, kuliko sasa ambavyo Serikali itakapoanza ujenzi wa reli na kuhitaji kutumia fedha za kigeni kuagiza chuma nje na kwa bei ambayo ni kubwa ukilinganisha na kama ingenunua chuma nchini.Hivyo ni ushauri wa Kambi rasmi ya upinzani kwamba serikali ikamilishe miradi hii ya Liganga na Mchuchuma ili kupunguza gharama kubwa za ujenzi wa reli ya kati.

### 10.13. Mradi wa Liquified Natural Gas(LNG)

**Mheshimiwa Spika,** Tangu miaka ya 2011, Serikali ya CCM ilitangaza kwa matangazo makubwa kuhusu ujenzi wa uchumi wa gesi baada ya kuvumbuliwa kiasi kikubwa cha gesi nchini kinachozidi futi za ujazo trilioni 55. Mategemea makubwa katika biashara hii ya gesi yalitegemea sana uwekezaji mkubwa katika mradi huu ambao unakadiriwa kufikia dola billion 30, uwekezaji ambao kama ungeanza mwaka huu inakadiriwa ungesababisha uchumi kukua kwa asilimia 7.2 kwa mujibu wa Gavana wa Benki Kuu.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu wenye uwekezaji wa dola 30billion ni mradi wa kihistoria katika ukanda huu wa Afrika Mashariki, na kwakweli katika historia ya Tanzania kwani dola billion 30 ni karibu asilimia 75% ya uchumi wa Tanzania ambao

kwasasa ni takribani dola billion 45. Uwekezaji wa dola billion 30 ni zaidi ya theluthi moja ya uchumi wa Kenya, Dola billion 30, ni karibu sawa na uchumi wote wan chi ya Uganda unaokadiriwa kuwa dola billion 30.

**Mheshimiwa Spika,** Ni uchungu kusema kwamba ingawa taarifa ya utekelezaji wa bajeti serikali inasema mradi huu utaanza mwaka 2019/20 ,Ukweli ni kwamba wawekezaji katika mradi huu ambao ni kampuni za State Oil, BG/Shell, Exxon Mobile na Orphir , wamekwishamua kuahirisha uwekezaji huu. Kwa mujibu wa Jarida la Reuters, la Novemba16, Meneja wa kampuni ya Sate amekaririwa akisema kwamba kutokana na kutoeleweka kwa Serikali ya Tanzaia, wao wameamua watafanya uamuzi kuhusu uwekezaji huo miaka mitano 5 kutoka 2016, yaani 20 kusisitiza kwamba ikiwa hivyo, wataingiza mtaji miaka mitano5 kutoka mwaka huo 2021, ikimaanisha kwamba ratiba ya kampuni hizi kuleta mtaji ni mwaka 2026.

**Mheshimiwa spika,** Huu ndio ukweli ambao Serikali haiusemi na badala yake inatoa maelezo yaliyojaa simulizi kwa suala muhimu na la kimkakati kama hili. Kifupi ni kwamba Serikali ya awamu tano haiaminiki, haitabiriki kwa wafanyabiashara wa ndani nanje kama IMF iliyosisitiza hivi karibuni. Na kwakuwa mitaji inatafutwa duniani, wawekezaji hawahawa ambao wameahirisha mradi huu hapa kwetu wanaendlea kuwekeza nchini Mozambique, na watakapomaliza, ni wazi Mozambique yenye gesi kuliko Tanzania, ikiwa na LNG Plant, itatawala soko lote la gesi kusini na mashariki ya Afrika, wakati Tanzania ikiendelea na utawala wake wa purukushani sio na maono wala mkakati.

## 11. HALI YA SIASA NCHINI NA UCHUMI WA TAIFA

**Mheshimiwa Spika,** uchumi wa nchi yoyote unategemea hali ya utulivu wa kisiasa pamoja na uzingatiwaji wa misingi ya kidemokrasia na haki za binadamu. Ni dhahri kuwa mambo hayo yakikosekana kutakuwa na athari za moja kwa moja za kiuchumi katika taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza kuhusu uchumi shirikishi ambao unalenga kuhakikisha kuwa ukuaji wa uchumi unaendana na kuboresha maisha ya wananchi. Malengo haya hayawezi kufikiwa kama bado hali ya nchi kisiasa sio nzuri kutokana na baadhi ya makundi kuminywa kupaza sauti yao na kutoa maoni juu ya masuala yanayoendelea katika taifa.

**Mheshimiwa Spika**, katika hali hiyo ningependa kugusia masuala yafauatayo ambayo yanahitaji majibu na hatua za Serikali;

**(a) Daftari la Wapigakura (PVR)**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inalo jukumu la kuilinda Katiba ya nchi kwa kutekeleza matakwa ya kikatiba juu ya haki ya wananchi kushiriki katika uchaguzi kwa kupiga kura. Aidha Serikali inalo jukumu la kuhakikisha kuwa matakwa ya kisheria kuhusu masuala ya uendeshaji wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi yanazingatiwa ikiwemo maandalizi ya daftari la kudumu la wapiga kura.

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 5(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema kwamba: "*Kila raia wa Tanzania aliyetimiza umri wa miaka kumi na minane anayo haki ya kupiga kura katika uchaguzi unaofanywa Tanzania na wananchi. Na haki hii itatumiwa kwa kufuata masharti ya ibara ndogo ya (2) pamoja na masharti mengineyo ya Katiba hii na ya Sheria inayotumika nchini Tanzania kuhusu mambo ya uchaguzi.*

**Mheshimiwa Spika**, Ili kuhakikisha kuwa haki ya wananchi ya kupiga kura inalindwa, Ibara ya 5(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 imelipa Bunge mamlaka ya kutunga sheria ya uchaguzi na kuweka masharti ya kuanzisha daftari la kudumu la wapiga kura na kuweka utaratibu wa kuboresha daftari hilo.

**Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi sura namba 343 toleo la mwaka 2015 kifungu cha 15(5) inaelekeza

Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuboresha daftari la kudumu mara mbili ikiwa na maana ya mara tu baada ya uchaguzi na kabla ya uchaguzi mkuu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni toka Bunge la kumi imekuwa ikiitaka Serikali kutekeleza takwa hilo la kisheria lakini Serikali imekuwa ikiziba masikio.

**Mheshimiwa Spika**, huu ni mwaka wa pili toka uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 ulipofanyika lakini hakuna dalili yoyote inayoonesha kuwa daftari la kudumu la wapiga kura litaboresha kama ambavyo sheria inataka. Ukisoma kwa makini Fungu 61 Tume ya Taifa ya Uchaguzi haina kifungu ambacho kimetengewa fedha kwa ajili ya kuboresha daftari la kudumu la wapiga kura.

**Mheshimiwa Spika**, Hii maana yake ni kuwa tunaelekea mwaka wa tatu bila kuboresha daftari la wapiga kura. Huu ni ukiukwaji wa taratibu za kisheria ambazo kama taifa tumejiwekea. Ikumbukwe kuwa lengo la kuboresha daftari ni muhimu kwa sababu kumekuwa na chaguzi ndogo za Udiwani na Ubunge ambazo zote zimefanyika kwa kutumia daftari la wapiga kura lililoboreshwa mwaka 2015.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ili kuepuka malalamiko ya wadau wa siasa nchini kwa kuboresha daftari la wapiga kura ili kukidhi matakwa kikatiba na kisheria kama ambavyo tumeeleza.

**Mheshimiwa Spika**, kuboreshwa kwa daftari la wapiga kura haiondoi hoja ya hitaji la kuwa na Tume huru ya uchaguzi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa na madai ya muda mrefu ya kuwa na Tume huru ya uchaguzi. Majibu ya Serikali kwenye hoja hii yamejikita kusubiri mchakato wa Katiba mpya kukamilika.

**Mheshimiwa Spika**, Watanzania wote wanajua kuwa mchakato wa Katiba mpya umekwama na Rais ameshasema hadharani kuwa wakati wa kampeni hakutamka popote kuhusu Katiba mpya na hivyo inaonekana si kipaumbele chake. Hii maana yake ni kuwa majibu ya hoja ya kuwa na

Tume huru ya uchaguzi itasubiri Katiba mpya hayatakuwa na mantiki baada kauli ya Rais.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuwe na mwelekeo mzuri wa huko tunakoelekea Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kuwe na mabadiliko ya Katiba iliyopo ili kukidhi masuala ya kidemokrasia nchini na kuondoa malalamiko ya wadau wa siasa nchini. Ikumbukwe kuwa kabla ya uchaguzi wa mwaka 2015 kulikuwa na majadiliano ambayo hayakufikia mwisho yaliyokuwa yanasimamiwa na Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD) ambayo yalipendekeza kuwe na marekebisho ya mpito ya Katiba iliyopo ya mwaka 1977 kwa ajili ya kuepuka mambo ambayo yanaweza kuharibu uchaguzi mkuu wa mwaka huo.

**Mheshimiwa Spika**, Ili kuwa Taifa linaloheshimu misingi ya kidemokrasia nchini Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kurudia baadhi ya mapendekezo ya Kamati ya Kituo cha Demokrasia Tanzania ili kuwe na marekebisho ya Katiba ya mpito katika masuala yafuatayo yanayohusu Tume ya Uchaguzi;

- Uteuzi wa Mwenyekiti na Mkurugenzi wa Tume uthibitishwe na Bunge na sio kuteuliwa na Rais pekee.

- Tume ya Taifa ya Uchanguzi kuhakikisha kuwa inakuwa na ofisi kwa kila Jimbo la Uchaguzi na ofisi za Uratibu za Mikoa na sio kuwatumia Wakurugenzi wa Halmashauri na ofisi ambazo zipo chini ya TAMISEMI

- Tume ya Taifa ya Uchaguzi iweke utaratibu wa kuboresha daftari la kudumu la wapiga kura kuwa wa kudumu. Hii ni kwa sababu kila mwaka kunakuwa na wapiga kura wapya ambao hufikia umri wa miaka 18.

- Kuhakikisha kuwa Tume ya Taifa ya uchaguzi baada ya marekebisho inasimamia pia uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

- Katiba iruhusu baada ya matokeo ya uchaguzi mkuu, matokeo ya Urais yapingwe Mahakamani.

**Mheshimiwa Spika**, demokrasia ikishamiri vizuri katika nchi uchumi utakua na kufanya nchi yetu kuendelea. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha inalichukulia kwa uzito jambo hili kwa ajili ya mustakabali mwema wa yetu.

### (b) Hali ya Siasa Zanzibar

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 28 Machi, 2016 Shirika la MCC lilifikia uamuzi wa kusitisha misaada yake kwa Tanzania[20]. Sababu za kusitishwa kwa misaada hiyo pamoja na mambo mengine ni kutokana na kufutwa kwa uchaguzi halali wa Zanzibar wa tarehe 25 Oktoba, 2015 pamoja na Serikali kutumia sheria ya makosa ya kimtandao kuzuia uhuru wa kutoa maoni.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kusisitiza kuwa kurudiwa kwa uchaguzi feki wa Zanzibar wa tarehe 20 Machi, 2016 hakujawa dawa ya kutatua mkwamo wa kisiasa Zanzibar. Wananchi wa Zanzibar walifanya maamuzi yao tarehe 25 Oktoba, 2015 kwa kumchagua Maalim Seif Sharif Hamad lakini sauti yao haikusikika kwa sababu kuna kikundi cha watu ambao hawaheshimu misingi ya demokrasia nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha tunasisitiza kuwa marudio ya uchaguzi Zanzibar hayajawa dawa kwa wanachama wa Chama cha Wananchi CUF walioteswa na kupigwa na Mazombi huku vyombo vya dola vikishuhudia kama ambavyo ambavyo tulieleza kwa kirefu kwenye hotuba ya Kambi ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano.

**Mheshimiwa Spika**, marudio ya uchaguzi wa Zanzibar hayajafanyika kwa mujibu wa Katiba wala Sheria bali kwa matakwa ya mtu mmoja ambaye aliamua kufuta uchaguzi huo bila kuwa na mamlaka ya kisheria wala Katiba.

---

[20]https://www.mcc.gov/news-and-events/release/stmt-032816-tanzania-partnership-suspended

**Mheshimiwa Spika**, thamani ya fedha zilizozuiliwa na MCC ni takribani 1.5 Trilioni[21], Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haishangai kuona miradi ya REA ikisuasua kutokana na ukosefu wa fedha. Hata bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Nishati na Madini imeshuka (kutoka 1,056,354,669,000 hadi 938,632,006,000) tofauti na mwaka wa fedha uliopita. Ikumbukwe kuwa wakati Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji suala hili Serikali ilijinasibu kuwa itagharamia miradi ya REA kwa fedha za ndani.

**Mheshimiwa Spika**, ukweli ni kwamba fedha za MCC zilikuwa muhimu kwa nchi lakini kutokana na kukiukwa kwa misingi ya demokrasia na kuwaziba wananchi midomo kunakofanywa na Serikali ya CCM fedha hizo zikazuiwa.

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 01 Juni, 2017 Balozi Msaidizi wa Marekani hapa nchini, alitoa taarifa yake kwa waandishi wa habari kuhusu mambo mbalimbali yanayoendelea nchini[22]. ***"At this same crossroads, however, is another path. One which leads to a Tanzania where people are afraid to use their voice, and where development stagnates. Down this road, entrepreneurs hang back from starting new business due to stifling or inconsistently applied regulations. Government institutions remain susceptible to corruption and inefficiencies. Schools and medical centers do not have the resources they need. And are unable to serve those who need them. The security forces are feared and operate outside the rule of law. People distrust their neighbors and wonder where their loyalties lie. Citizens are afraid to offer their views – limiting the debate that is so often needed to come up with the best way forward. In this direction, the efforts of millions of hard-working, talented Tanzanians – especially young Tanzanians – will see a less certain future".***

**Mheshimiwa Spika,** kwa tafsiri isiyo rasmi maoni haya yanaweza kujengwa katika dhana zifuatazo;

---

[21] http://www.mwananchi.co.tz/Marekani-yaipoka-Tanzania-Sh-1-4-trilioni/-/1596774/3139372/-/ewa7s1z/-/index.html

[22] https://tz.usembassy.gov/tanzania-at-the-crossroads/

(i) Watanzani wamekuwa waoga kutoa maoni yao
(ii) Maendeleo ya nchi yetu yanarudi nyuma
(iii) Wajasiriamali wanaogopa kufanya biashara zao kutokana na vikwazo vya kikanuni
(iv) Jitihada za kupambana na rushwa hazina ufanisi
(v) Shule na hospitali hazina rasilimali za kutosha
(vi) Vyombo vya dola vinafanya kazi kinyume na utawala wa sheria
(vii) Serikali inazuia mijadala- kama ilivyozuia kuzinduliwa kwa Kitabu cha Ndugu Alphoce Lusako ambaye alikuwa Mwanafunzi aliyefukuzwa masomo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mara mbili.

(viii) Hakuna mustakabali mwema kwa vijana ambao ni wachapakazi na wenye vipaji

**Mheshimiwa Spika,** Hii ndiyo hali ya siasa katika nchi yetu kwa jicho la kimataifa. Huu ndio ukweli ambao Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iliuweka wazi katika hotuba zake kwa Wizara mbalimbali. Japo mengine yalifutwa na kutoingia ndani ya Bunge lakini ukweli utabaki palepale kuwa hali sio nzuri ndani ya nchi yetu kwa sasa kwa sababu imejengwa hofu kubwa miongoni mwa Watanzania.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kwamba Rais anapenda kusisitiza kuwa msema kweli ni mpenzi wa Mungu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inachelea kuhoji kuwa ni ukweli upi ambao Serikali yake inapenda kuusikia? Hii ni kutokana na juhudi za kila namna ya kuzuia mawazo mbadala kusikika kwa wananchi. Ukweli upi ambao Rais anapenda kuusikia wakati amezuia kinyume na sheria mikutano ya vyama vya siasa? Ukweli ni upi anaopenda kuusikia wakati wananchi hawawezi kusikia na kuona moja kwa moja mijadala ya wawakilishi wao ndani ya Bunge?

### (c) Sheria ya Makosa ya Kimtandao na Uhuru wa Kujieleza

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Makosa ya Kimtandao (Cyber Crime Act) imekuwa mwiba wa uhuru wa kujieleza nchini.

Hii inatokana na vyombo vya dola kujizolea sifa ya kuendelea kuwakamata vijana mbalimbali na kuwafungulia mashitaka ya uchochezi au makosa ya kimtandao kutokana na kuamua kutumia uhuru wao wa kikatiba kutoa maoni na kujieleza.

**Mheshimiwa Spika**, wapo vijana wengi ambao wamekuwa wakikamatwa na kuteswa hasa kwenye Kituo Kikuu cha Polisi na Kituo cha Polisi cha Oysterbay Jijini Dar Es Salaam, kutokana na kuandika na kutoa maoni yao mtandaoni ambayo huonekana ikikosoa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Hivi karibuni alikamatwa kijana kutoka Wilaya ya Mbozi Mkoa wa Songwe Mdude Nyagali pamoja na Nicas David, ambapo baada ya Mdude kukamatwa huko Mbozi aliteswa bila kupelekwa hospitali na baadae kusafirishwa kwenda Dar es Salaam ambapo pia alipata mateso akiwa Kituo cha Polisi cha Oysterbay bila ya kupelekwa Mahakamani.

**Mheshimiwa Spika**, ni baada ya Wakili na Rais wa Chama cha Wanasheria wa Tanganyika Mhe. Tundu Lissu (Mb) kuwaeleza Polisi kuwa angepeleka maombi Mahakama Kuu ya **Habeas Corpus** ndipo aliporudishwa tena Mbozi na kufunguliwa mashtaka ya uchochezi ambapo mwezi wa Aprili mwaka 2017 Mahakama imemkuta bila hatia yoyote.

**Mheshimiwa Spika**, mwendelezo wa Serikali kutumia Sheria ya Makosa ya Kimtandao "Cyber Crime Act" ya mwaka 2015 umekuwa mwiba mchungu kwa watu kutoa maoni yao ndani ya nchi. Ni ishara kuwa Serikali haipendi matumizi ya mitandao ya kijamii na ndiyo maana Mkuu wa nchi wakati anapokea ndege za Bombadier Jijini Dar es Salaam alisema kuwa anatamani malaika washuke kuizima mitandao hiyo na kusahau kuwa wakati wa uchaguzi mkuu 2015 alitumia mitandao hiyo hiyo kujinadi na kutafuta kura.

**Mheshimiwa Spika**, ni wazi kuwa Sheria hiyo inatumika kama malaika kuzuia uhuru wa kutoa maoni kwenye mitandao ya kijamii. Mamlaka makubwa waliyopewa Polisi kukamata

computer au simu za mikononi tuliyaeleza kwa kirefu wakati sheria hiyo ilipokuwa inapitishwa Bungeni kwenye Bunge la kumi.

**Mheshimiwa Spika**, Ndiyo maana mpaka sasa nchi washirika wa maendeleo na Jumuiya ya Kimataifa ikiwemo Umoja wa Ulaya na Shirika la Millenium Challenge Corporations (MCC), wameikosoa sheria hiyo kuwa inakiuka misingi ya demokrasia na utawala bora kwa sababu inazuia uhuru wa raia wa kujieleza; na kwa sababu hizo Shirika la MCC iliamua kuinyima Tanzania fedha za misaada katika miradi ya umeme kutokana na Serikali kutumia sheria hiyo kuzuia uhuru wa kujieleza.

**Mheshimiwa Spika**, kuna orodha ndefu ya vijana wa Kitanzania ambao tayari walishapandishwa kizimbani kutokana na Sheria hii ya Makosa ya Kimtandao kwa kuikosoa Serikali ya awamu ya Tano na hususani Mkuu wa Nchi, orodha hiyo ya vijana ni kubwa kuliko matumizi ya vifungu vingine vya Sheria hii, jambo linaloifanya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni iamini kuwa uwepo wa Sheria hii ulilenga kuzuia uhuru wa kujieleza ili Serikali hii iendelee na vitendo vya ukandamizaji wa haki nyigine na ikose kabisa watu wa kuikosoa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kuwa Sheria ya Makosa ya Kimtandao ni ya kibaguzi. Hii ni kutokana na ukweli kwamba wapo makada wa Chama cha Mapinduzi wanaotoa matusi mpaka ya nguoni kwa viongozi wa Vyama vya Upinzani lakini sheria hiyo haitumiki kuwachulia hatua. Kutokana na hali hiyo, mtu yeyote anaweza kujenga hoja kuwa sheria hiyo wametungiwa wapinzani pekee na si upande mwingine. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuleta marekebisho ya sheria hiyo ili kuondoa vifungu kandamizi ambavyo vinalalamikiwa na wadau na wananchi kwa ujumla.

## 12. UCHUMI NDANI YA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

**Mheshimiwa Spika**, ili nchi yetu iendelee ni lazima kwa namna moja ama nyingine kuhakikisha kuwa inatumia kwa ukamilifu

fursa zilizopo katika nchi jirani na hasa nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Kwa takwimu za hivi karibuni zinaonyesha kuwa biashara inayofanyika ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki pekee ni ya thamani ya dola za kimarekani **milioni 5,632.9.**

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania haijatumia vizuri fursa zilizopo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki hasa kwenye nchi za Uganda, Rwanda na Burundi. Izingatiwe kuwa Taifa changa la Sudani ya Kusini tayari limeshajiunga katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na kufanya soko la ndani ya Jumuiya kupanuka kwa kiasi kikubwa. Takwimu zinaonesha kuwa Tanzania inafanya sana biashara na Kenya kuliko Taifa lolote ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa mwaka 2015 Tanzania iliuza bidhaa Kenya kwa thamani ya dola za kimarekani **milioni 852.7** ikilinganishwa na dola za kimarekani **milioni 448.1** mwaka 2014. Aidha, kwa kipindi hicho hicho Tanzania iliuza bidhaa Uganda zenye thamani ya dola za kimarekani **milioni 56.4** kwa mwaka 2015 na dola **milioni 73.7** kwa mwaka 2014[23].

**Mheshimiwa Spika**, kwa nchi za Rwanda na Burundi Tanzania iliuza bidhaa zenye thamani ya dola milioni 41.9 na 41.3 kwa mwaka 2015 pekee. Ikumbukwe kuwa tayari Sudani ya Kusini imejiunga rasmi na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na pia Tanzania inajinasibu na uchumi wa viwanda, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hatua ambazo inachukua kuhakikisha kunakuwa na mkakati wa kupanua soko la bidhaa za Tanzani kwenda nchi za Uganda, Rwanda na Burundi katika hatua za awali.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza Bunge lako tukufu kama kuna mkakati wowote wa kuhakikisha kuwa inawezesha wafanyabiashara na wawekezaji wa ndani kuhakikisha wanatumia vizuri fursa mpya ya soko la nchi ya Sudani ya Kusini ambayo ni nchi mshirika mpya ndani ya Jumuiya.

---

[23] EAC Facts and Figures 2016 Report.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali inaweza kuja na majibu ya idadi ya watu na ukubwa wa soko katika nchi za Burundi na Rwanda, majibu kama hayo hayatakuwa na mantiki kwa sababu nchi ya Kenya pekee iliuza bidhaa zenye thamani ya dola milioni 250 kwa mwaka 2015 pekee. Huku Tanzania kwa hizo mbili ikiwa imeuza bidhaa zenye thamani ya dola milioni 83.2 tu kiwango ambacho ni cha chini mara tatu kuliko kile cha wenzetu wa Kenya.

**Mheshimiwa Spika**, kwa takwimu hizi ni ishara kwamba hatujatumia vizuri fursa za soko lililopo ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ieleweke kuwa nchi yetu iko kimkakati ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo inapakana na nchi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki isipokuwa Sudani ya Kusini. Ni dhahiri kuwa, Serikali ikitumia vizuri fursa zilizopo nchi yetu inaweza kupata soko kubwa la bidhaa kuliko nchi zingine za Jumuiya.

**Mheshimiwa Spika**, ni lazima kuwe pia na mkakati wa kuhakikisha kuwa uchumi wa maeneo ya mpakani na nchi washirika wa Afrika Mashariki unawanufaisha wananchi wanaoishi maeneo hayo kuanzia baadhi ya maeneo ya Kigoma, Kagera, Mwanza, Mara, Kilimanjaro, Arusha na Tanga. Badala ya maeneo hayo kukumbwa na kadhia za wahamiaji haramu au wakimbizi wa vita, migogoro ya mipaka na ujambazi ni lazima yanufaike kiuchumi na kuwafanya kuona umuhimu wa Jumuiya kuliko ilivyo sasa.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Benki ya mwaka 2016 iliyochambua mazingira ya biashara ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (Doing Business 2016-Measuring Regulatory Quality and Efficiency), imeipa Tanzania kiwango cha chini cha mazingira bora ya kufanya biashara ndani ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

**Mheshimiwa Spika**, Katika viasharia vyote na vipengele vyake, Tanzania ilikuwa na kiwango cha chini kabisa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki katika viashiria 21 wakiongozwa na Burundi ambayo katika imekuwa na viwango 26 vya chini kabisa (lowest regional performance). Wakati huohuo nchi

ya Rwanda ikiwa na alama 29 katika viashiria vya kuwa nchi yenye mazingira bora ya kufanya biashara.

**Mheshimiwa Spika**, takwimu hizi si ishara nzuri kwa nchi yetu kama moja ya nchi kongwe ndani ya Jumuiya Mashariki. Moja ya kiashiria ambacho Tanzania imefanya vizuri kuliko nchi zingine ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (Best Regional Performance) ni kusimamia na kuheshimu mikataba. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina wasiwasi kama mwaka huu 2017 bado Tanzania itaongoza katika kiashiria hiki baada ya mgogoro unaoendelea kati ya Serikali na kampuni ya madini ya Acacia.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kupitia kwa Waziri wa Fedha akishirikiana na Waziri wa Viwanda na Biashara kuhakikisha kuwa inaboresha mazingira ya biashara na kuiondoa nchi yetu kwenye aibu ya kuwa na mazingira karibu sawa na nchi kama Burudni ambayo mara kadhaa imekumbwa na machafuko ya kisiasa ya ndani.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuifanyia kazi taarifa ya Benki ya Dunia na kubadili mfumo ili kuweka mazingira bora ya biashara kuliko kuwaona wafanyabiashara na wawekezaji ambao wamewekeza ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na hasa nchini mwetu kama maadui na si marafiki katika ukuaji wa uchumi.

## 13. UTEKELEZAJI WA MIRADI MIKUBWA YA KIMKAKATI

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa kumekuwa na ugumu wa kupata mikopo ya riba nafuu kutoka nje kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo hapa nchi kama vile miradi mikubwa ya uzalishaji wa umeme wa maji –Stigler's Gorge, uzalishaji wa Chuma-Liganga, ujenzi wa Reli ya Kati na matawi yake kwa ***Standard Gauge***, ujenzi wa kiwanda kikubwa na cha kisasa cha nguo mikoa ya Magharibi au Ziwa na ujenzi wa Kiwanda cha ku- liquify Gas (LNG) na kuiweka kwenye mitungi tayari kwa usambazaji nchi nzima na nje ya nchi; basi Kambi Rasmi ya Upinzani

inapendekeza kufanyia utaratibu wa kupata mikopo ya ndani kwa mfumo wa **“Organized Local Loans Syndications**”.

**Mheshimiwa Spika,** mfumo huu ni kwa Mabenki ya ndani pamoja na mifuko ya hifadhi ya jamii kushirikiana kutoa mkopo ili kufanikisha utekelezaji wa mradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na utaratibu huo tuliopendekeza hapo juu, Serikali inaweza pia kutumia mfumo wa **“Build-Operate-Transfer rights” (BOT)**, kwa kutumia makampuni binafsi au taasisi zisizo za kiserikai kujenga vitega uchumi vikubwa na hatimaye wakisharudisha gharama zao, vitegauchumi hivyo vinakuwa vya Serikali au kama ambavyo Serikali inaweza kuamua vinginevyo. Kambi Rasmi ya Upinzani ina uhakika kuna makampuni yanayoweza kutekeleza program kama hizo ikiwa utaratibu utaandaliwa vizuri na kuyaonesha makampuni jinsi gani wakiwekeza kwenye miradi husika watakavyoweza kurudisha fedha zao, pale wakipewa fursa ya kujenga na kuanza kuuendesha mradi husika kwa kipindi kitakachokuwa kimefikiwa katika makualiano na baada ya kumalizika kipindi hicho mradi utarudi Serikalini au Serikali inaweza kuingia makubaliano mapya ya jinsi ya kuendesha mradi husika. Jambo kubwa ni kuwa tayari utakuwa unafanyakazi tayari na Serikali haitakuwa na jukumu la kukopa fedha kwa ajili ya ujenzi wa mradi husika.

**Mheshimiwa Spika,** utaraibu huu ndio kwa sehemu kubwa umeinua uchumi wa nchi za **Taiwan, India, Canada, Croatia, Australia, Japan, China, Malaysia, New Zealand na Philippines**. Utaratibu huu unatoa uhakika kuwa mradi utaendeshwa kwa faida, kutokana na mhusika atakavyokuwa anauendesha ili kurudisha gharama zake za ujenzi. Hoja ya msingi ni jinsi ya kuwa makini katika uingiaji wa mkataba baina ya pande mbili husika katika mazingira ya faida kwa wote ( win – win situation).

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba Serikali imeshindwa kutumia fursa ya sheria ya uendelezaji wa miradi kati ya Serikali na Sekta binafsi (PPP),

na kushindwa huko kunaweza kuelezewa na mambo yafuatayo:

- Inawezekana kwamba masharti yanayowekwa na Serikali yanakuwa magumu kiasi kwamba Sekta binafsi inaona itashindwa kufanya biashara na kurudisha gharama zake,

- Inawezekana pia kwamba, Serikali inataka kuwa ndiyo iwe imeshika mpini katika kila kitakachokuwa kinaendelea na mshirika mwenzake kukosa kauli katika ushirika, na

- Inawezekana pia kwamba, Serikali haitaki kuitekeleza kwa ubia miradi mikubwa ambayo ina uwezekano wa kurudisha gharama kwa haraka.

**Mheshimiwa Spika,** ni ukweli pia mitaji ya ujenzi wa miradi au fedha za kuongeza mitaji kwa makampuni ambayo hayafanyi vizuri kama Shirika letu la Umeme inaweza kupatikana kwa kusajili shirika husika kwenye soko la hisa "Initial Public Offerings". Hii itafanikiwa kama kutakuwa na uaminifu katika utayarishaji wa vitabu mahesabu ya Kampuni husika (Prospectus ya Kampuni). Mfumo huu ungeweza pia kutumika kwa shirika letu la Reli kwani kuna uhakika kwamba pale mradi utakapokamilika shirika litakuwa linatengeneza faida. Aidha, wanunuzi wa mwanzo wa hisa wanaweza kuziweka hisa hizo katika soko la pili na hivyo mtaji kuendelea kuendelea kukua.

## 14. VYANZO VYA MAPATO YA KODI

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwepo na kilio cha siku nyingi cha watanzania kuhusiana na kuongeza ufanisi wa makusanyo ya kodi kwa kuhuisha sera ya msamaha wa kodi na sheria zilizopo ambavyo kwa muda mrefu imekuwa ni kichaka cha kukwepa kodi. Aidha, Serikali imeshindwa kuifanyia ukaguzi misamaha inayotolewa na Serikali kwa wahusika.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kwamba fedha za misamaha ya kodi ni fedha halali za

walipa kodi, hivyo ni muhimu na lazima fedha hizo au miradi husika ifanyiwe Ukaguzi wa "value for money" na Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani sambamba na Kamati ya Mheshimiwa Spika Mstaafu ANNE MAKINDA (Chenge I Report) tulishauri kwamba ni muda mwafaka kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato badala ya kuongeza viwango vya kodi kwa vyanzo vile vile. Jambo hili linapelekea walipa kodi kutafuta njia mbadala za kukwepa kodi hiyo kwa kushirikiana na watendaji wa Mamlaka ya Kodi.

**Mheshimiwa Spika**, ni ukweli kwamba huwezi kuvuna pale usipowekeza, kauli hiyo ina ukweli mno katika muktadha wa sekta ya kilimo hapa Tanzania, Sekta hii kwa kwa takwimu zilizo katika nyaraka mbalimbali ni kwamba ndio uti wa mgongo wa uchumi wetu katika utoaji wa ajira kwa watanzania na ndio inaongoza kwa uchangiaji 29.7% kwenye Pato la Taifa na kutoa ajira kwa asilimia 56.5% na mchango wake kwa mauzo nje ni 24.9%, lakini kwa ukweli ni kwamba sekta hiyo inapokuja kwenye mchango wake katika mapato ya kodi-tax revenue (VAT, excise duty, corporation income tax and PAYE) ni 0.2% tu.

**Mheshimiwa Spika**, hii maana yake nini katika ukuaji wa uchumi wetu na maendeleo ya Taifa kwa ujumla? Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwa tafsiri rahisi ni kwamba uwekezaji wa kukifanya kilimo kuwa cha kisasa na endelevu kama ilivyoainishwa kwenye sera ya Kilimo ili waajiriwa katika sekta hiyo waweze kutambulika bado mkakati huo haupo.

Hata wawekezaji wanaowekeza katika kilimo bado wafanyakazi katika sekta husika kwa mtindo wa vibarua, jambo linalopelekea kuwa hawapo katika mfumo wa kulipa kodi ya mshahara (PAYE).

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Sekta ya Madini ambayo ukuaji wake umekuwa ni kama ifuatavyo 2012 - 6.7%, 2013 -

3.9%, 2014 -9.4%, 2015 -9.1% na 2016-16.6%[24] mchango wake katika Pato la Taifa ni 20.5%, lakini inachangia 3.7% tu kama kodi ya mapato ikiwa VAT 1.2% Kodi ya Makampuni 2.2% na PAYE 8.2% [25]. Kwa mwenendo huo wa mapato ni dhahiri kwamba wachangiaji wakubwa wa kodi ni wafanyakazi ambao wanalipa PAYE na sio kodi zingine zinazotakiwa kulipwa.

**Mheshimiwa Spika**, kodi zinazotakiwa kulipwa na Wamiliki wa migodi mikubwa kisheria ni:-

- Kodi ya makampuni,
- Kodi ya zuio (WHT)
- Kodi kwenye mishahara (PAYE)
- Ushuru wa stempu
- Kodi ya kuendeleza ufundi stadi (SDL)
- Ushuru wa barabara
- Ushuru wa forodha

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inataka kufahamu kati ya kodi hizo, ni kodi ngapi ambazo makampuni hayo yanazilipa kwa ukamilifu wake?

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa sheria zetu viwango vya mrabaha au tozo inayotozwa na kulipwa Serikalini kwa makampuni yote yanayozalisha na kuuza madini kabla ya kusafirisha madini hayo kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 ni:

- Vito, almasi na urani – 5%

---

[24]Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/18

[25] **L. RUTASITARA*, N. OSORO, J. AIKAELI AND G. KIBIRA- DEPARTMENT OF ECONOMICS, UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM - Domestic Resource Mobilization in Tanzania March, 2010**

- Vito iliyokatwa na kusanifiwa – 1%
- Chumvi na Madini ya Ujenzi – 3%
- Madini mengine ikiwemo dhahabu – 4%

**Mheshimiwa Spika**, ni wazi kwamba mchawi wa kutokunufaika kwetu na sekta ya madini ni sheria ambazo zimepitishwa na Bunge letu hili, ambalo toka uwepo wake limekuwa "dominated" na maamuzi ya chama kimoja ambacho kimeongoza nchi yetu tangu uhuru.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inasema ni muda mwafaka sasa sheria hii ya madini inayotoa viwango hivyo kufanya marejeo makubwa sambamba na sheria hiyo pia marejeo yafanyike kwenye sheria za mafuta na gesi zilizopitishwa mwaka 2015.

## 15. MAPATO YASIYO YA KODI

**Mheshimiwa Spika**, mapato yasiyo ya kodi (maduhuli) yanajumuisha; gawio, ada na tozo mbalimbali zinazotozwa na Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali. Vyanzo vya mapato haya ni pamoja na shughuli za utalii, bandari, viwanja vya ndege, uchimbaji madini (mirabaha), bidhaa zitokanazo na misitu, kodi ya ardhi, uvuvi.

Japokuwa kuna fursa kubwa ya kuongeza vyanzo vya mapato yasiyo ya kodi katika sekta kadhaa za kiuchumi, lakini vyanzo hivyo bado havijafanyiwa tafakuri kama ambavyo Kambi Rasmi kwa miaka yote imekuwa ikiishauri Serikali kufanyia kazi. Takwimu zinaonesha kwamba Serikali inapata chini ya 2% ya GDP kama mapato yasiyo ya kodi na mapato hayo ni chini ya 10% ya jumla ya mapato yote ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** kuna tafiti kadhaa zilizokwishafanyika ni kwa jinsi gani vyanzo vya mapato vinavyoweza kuongeza, urasimishaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi zinaweza

kufanyiwa kazi katika ngazi za Serikali za mitaa kwanza kwa kuwekewa utaratibu mzuri na ukishakubalika ni dhahiri Serikali itaanza kupata haki yake katika shughuli hizo za kiuchumi.

## 16. KODI YA MAJENGO KAMA CHANZO CHA MAPATO YA SERIKALI

**Mheshimiwa Spika**, Mwaka wa fedha unaokwisha mwezi Juni 2017 Serikali iliweka utaratibu wa kisheria kuondoa mamlaka ya Halmashauri kukusanya kodi ya majengo (property tax)na kuipa haki hiyo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) huku Serikali ikijua kuwa kodi hiyo ilikuwa sehemu muhimu sana ya mapato ya Halmashauri nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ililiona jambo hili kama mkakati wa kuondoa mapato kwa Halmashauri ili kuzipunguzia nguvu Halmashauri nyingi za Majiji ambazo zinaongozwa na Wapinzani. Ieleweke kuwa halmashauri hapa nchini zimekuwa zikikusanya mapato kwa ajili ya kuendesha miradi yake ya maendeleo na shughuli nyingine za kawaida kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato kwa mujibu wa sheria ya fedha ya Halmashauri (Local Government finance Act, 1982) Haukuwa uamuzi sahihi kutunga sheria ya kuondoa chanzo cha mapato cha kodi ya majengo kutoka katika halimashauri nchini .

**Mheshimiwa Spika**, Kufutwa kwa kifungu kilichokuwa kinazipa Halmashauri jukumu la kukadiria na kukusanya kodi za majengo na kulihamishia TRA kupitia sheria ya fedha ya mwaka 2016, kifungu cha 38 baada ya kufanya marekebisho kwa kuvifuta vifungu vya 31A na 31B vya sheria ya fedha ya Serikali ya Mitaa sura 290 kumeziyumbisha sana halimashauri katika kutekeleza majukumu yake kutokana na ukweli kwamba chanzo cha kodi ya majengo kilikuwa ni mojawapo ya chanzo kikubwa cha mapato ya Halmashauri.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wakati wa mjadala wa Ofisi ya Rais TAMISEMI tulieleza wazi kuwa

taarifa ya Serikali inaonyesha kuwa kodi ya Majengo iliyokusanywa ni shilingi milioni 4,762.37 kati ya mIlioni 29,004 sawa na asillmia 17.4 tu ambayo ilitarajiwa kukusanywa na TRA.

**Mheshimiwa Spika**, kwa takwimu hizo ni wazi kuwa TRA haina uwezo wa kufanya kazi ya kukusanya chanzo hiki cha mapato kwa ufanisi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili sababu za kuipa TRA mamlaka ya kukusanya kodi ya majengo wakati haikuwa imejipanga kimikakati na kimfumo kufanya kazi hiyo, aidha Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuleta tena marekebisho ya Sheria ya Fedha ili kurudisha chanzo hiki cha mapato katika ngazi ya Halmashauri kama ilivyokuwa awali.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo taarifa kuwa baada ya kuziondolea Halmashauri haki ya kutoza kodi ya majengo, Halmashauri nyingi hasa za Vijijini zimeanza kutoza kodi ya majengo kwa wananchi huko vijijini jambo ambalo limekuwa kero kwa wananchi wetu ambao kwa waliowengi hawana vipato vizuri.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge lako tukufu, ni kwa nini wameondoa kodi ya majengo kama chanzo cha mapato na kuruhusu Halmashauri kuanza kuwatoza wananchi wa vijijini kodi ya majengo yao.

**Mheshimiwa Spika**, Kama Serikali bado inang'ang'ania chanzo hiki, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri majengo yagawanywe kwenye madaraja kama vile majengo makubwa ya kibiashara, *residential apartments*, na majengo mengine makubwa kama itakavyoamuliwa kodi zao zikusanywe na Mamlaka ya Kodi Tanzania (TRA) lakini majengo madogo ya biashara na nyumba za makazi kodi yao ikusanywe na Halmashauri ili kuongeza ufanisi wa TRA katika ukusanyaji.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuhitimisha eneo hilo, Kambi Rasmi ya Upinzani ina mtazamo kwamba, kitendo cha Serikali hii ya awamu ya tano kuziondolea Serikali za Mitaa mamlaka ya ukusanyaji wa kodi ya Majengo na kurudisha mamlaka hiyo kwenye Serikali Kuu kupitia TRA, kunauwa kabisa dhana ya ugatuaji kamili wa madaraka (D by D) ambayo ilikuwa ndiyo kaulimbiu kubwa ya Serikali za awamu zilizopita na fedha nyingi zilitumika kutekeleza dhana hiyo. Kutokana na hali hiyo, uwepo wa Serikali za Mitaa hauna maana tena kwani madaraka yake ya msingi yamechukuliwa na Serikali Kuu, jambo ambalo litasababisha Serikali hizo zishindwe kujiendesha. Kwa maneno mengine ni kwamba Serikali Kuu inazifuta kinyemela kwa kuziondolea uwezo wa kufanya kazi na kujiendesha.

## 17. MCHANGO WA VIWANDA KATIKA UKUAJI WA UCHUMI

**Mheshimiwa Spika,** Ili Tanzania ifanikiwe kuwa ya uchumi wa kati kiviwanda ifikapo mwaka 2025 basi sharti sekta ya uzalishaji **(manufacturing) ichangie wastani wa chini wa asilimia 40 katika pato la Taifa ifikapo mwaka 2025.**

**Mheshimiwa Spika,** leo hii takaribani miaka 8 kabla ya mwaka 2025, sekta ya viwanda vya uzalishaji (manufacturing) inachangia **asilimia 5.2** tu ya pato la Taifa kwa mujibu wa kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Miaka mitano (National Five Year Development Plan, 2016/17 – 2020/21.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwenendo huo, hata kama Rais Magufuli akifanikiwa kukaa madarakani kwa miaka 8 ijayo mpaka kufikia mwaka 2025, yeye na Serikali yake yote hataweza kabisa kuigeuza Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati kiviwanda kwa sababu ili afanye hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inampa changamoto kuwa kila mwaka wa fedha ikiwamo mwaka huu wa 2017/2018, sekta ya uzalishaji (manufucturing) **inapaswa kukua kwa asilimia 4.35 kila**

**mwaka wa fedha mpaka ifikapo mwaka 2025 ili kufikia lengo la kuifanya 'manufacturing' ichangie asilimia 40 ya pato la Taifa na hatimaye Tanzania kuwa ya uchumi wa kati kiviwanda!**

**Mheshimiwa Spika,** ukisoma kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Miaka mitano (National Five Year Development Plan, 2016/17 – 2020/21 Serikali ilijipangia kutumia jumla ya Shilingi Trilioni 5.78 kwa ajili ya uwekezaji katika miradi mikubwa ya kimkakati kwenye sekta ya uzalishaji (manufacturing), wakati ahadi (commitment) ya Serikali pekee ikiwa ni bilioni 659 – angalia **Jedwali la 1 hapo chini.**

**Mheshimiwa Spika,** Miradi ya Uwekezaji wa Viwanda Kimkakati iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2017/ 2018 katika fungu Fungu 44, ilikuwa imetengewa jumla ya Shilingi Bilioni 2.38 ambayo ni sawa na asilimia 0.36 ya fedha zote za Maendeleo zilizotakiwa kutengwa na Serikali, kama sehemu ya ahadi yake katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka mitano. – angalia **Jedwali la 2 hapo chini.**

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaposema hoja ya Tanzania ya uchumi wa viwanda ni hoja hewa, inamaanisha inachokisema. Kwa kiwango cha 'facts' ambazo tayari tumezianisha katika jedwali la 1 na 2, ni wazi kabisa kuwa hakuna Tanzania ya viwanda inayoimbwa kila kukicha na Serikali ya CCM.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ya CCM kulielezea Bunge lako tukufu na Watanzania kwa ujumla inapojinasibu kuwa nchi yetu ni Tanzania ya viwanda, je Serikali itajenga uchumi wa viwanda kwa bajeti ipi?

**Jedwali 1:**

| Uwekezaji katika Sekta ya Uzalishaji (Manufacturing Sub Sector | | |
|---|---|---|
| Jina la Mradi | Mpango wa Bajeti 2017/2018 TZS Bilioni | Government Commitment 2017/2018 TZS Bilioni |
| Bagamoyo SEZ | 3,412 | 402.1 |
| Kurasini Logistics Center | 220 | |
| Mtwara SEZ (Freeport Zone) | 12 | 0.9 |
| Kigoma SEZ | 10 | 5 |
| Tanga SEZ | 5 | 2.7 |
| Ruvuma SEZ | 3 | 2.6 |
| Bunda SEZ | 3 | 2.8 |
| Morogoro - Star City SEZ | 337 | 13 |
| Industrial Park Interventions | 23 | 20.6 |
| MSMEs Parks Strategic Choices | 29 | 13.3 |
| Automotive industry Strategic Choices | 160 | 70.7 |
| Petro and Chemical Industries Strategic Choices | 1,144 | 30.5 |
| Development of Pharmaceutical Industries Strategic Choices | 27 | 5 |
| Textile and Clothing Industries | 10 | 9.5 |

**Jedwali 2:**

| Miradi ya Uwekezaji wa Viwanda Kimkakati iliyotengewa fedha 2017/2018 Fungu 44 | |
|---|---|
| **Jina la Mradi** | **Kiasi cha Fedha za Maendeleo kilichotengwa kwenye Bajeti, 2017/2018 TZS** |
| Lake Natron | 2,000,000,000 |
| Revival of General Tyre and Rubber Plant | 70,000,000 |
| Integrated Industrial Development | 10,000,000 |
| Mchuchuma Coal to Electricity Project | 100,000,000 |
| Liganga Vanadium Titanium | 100,000,000 |
| KAIZEN | 100,000,000 |
| **JUMLA** | **2,380,000,000** |

Chanzo: Volume IV - Public Expenditure Estimates Development Vote (PART A), Page 70 & 71

## 18. UNYANYAPAA WA SEKTA BINAFSI KATIKA KATIKA UKUAJI WA UCHUMI

**Mheshimiwa Spika,** Serikali hii ya awamu ya tano imeanzisha sera zisizo rasmi zenye msimamo mkali (extremist view) dhidi ya ukuaji wa sekta binafsi. Ni vema Serikali ikatambua kuwa nchi ya Tanzania katika ukanda wa Afrika Mashariki, Afrika na duniani kwa ujumla ina **uchumi dhaifu** unaokuwa taratibu ukitegemea ukuaji wa sekta binafsi katika kuufanya kuwa uchumi imara. Hivyo hatua zozote zenye misimamo mikali dhidi ya ukuaji wa Sekta binafsi ni hatua za kudhoofisha juhudi za ujenzi wa uchumi imara ulio shirikishi **(inclusive economic growth)**

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imemsikia Rais Magufuli akitoa ufafanuzi wa sera zisizo rasmi zenye msimamo mkali (extremist view) dhidi ya sekta binafsi nchini alipokuwa akifungua Kituo cha Kutunzia Taarifa (Data centre) na kuzindua Mfumo wa Ukusanyaji Mapato wa Serikali kwa Njia ya kielektroniki kwenye sherehe zilizofanyika Kijitonyama jijini Dar es salaam Juni 1, 2017, alinukuliwa

akisema kuwa ***"TCRA wanapotoa faini , faini ndogo tu sijui milioni mia tatu, sijui milioni ngapi, kwa mtu anayepata mabilioni ataacha kujirejista kwenye Dar es Salaam Stock Exchange kusudi uwe una mpiga faini, kwa sababu faida nyingi anabaki nayo, TCRA msipige faini, futeni haya makampuni"*** hii ni sera isiyo rasmi yenye mtazamo mkali (extremist view) ambao sio rafiki wa sekta binafsi nchini.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mtazamo huu, Rais anatuma ujumbe kwa sekta binafsi kuwa Serikali inakusudia kufuta makampuni nchini jambo ambalo sio sahihi kwa ukuaji wa uchumi wa Taifa. Rais anadhani njia rahisi ya kukusanya kodi kutoka sekta binafsi basi ni kutumia vitisho vya kufungia makampuni. Kulipa kodi sio jambo moja tu ambalo nchi inanufaika nalo, bali makampuni haya makubwa kwa madogo ndio yanayotoa ajira kwa maelfu ya Watanzania, ambao nao huilipa kodi ya mapato kwa Serikali (Pay As You Earn).

**Mheshimiwa Spika,** Moja ya njia ya kuboresha maisha ya Watanzania ni kwa Serikali kuweka mazingira rafiki ya makampuni katika Sekta binafsi kujiendesha kwa uhuru bila kuvunja sheria za kodi wala kukwepa kodi ili makampuni hayo yatoe ajira nyingi kwa Watanzania na mapato ya Serikali yaongezeke kutokana na tozo za kodi kwa makampuni. Lakini jambo la kustaajabisha ni kitendo cha Serikali kuwa na mawazo ya sera zenye msimamo mkali dhidi ya ukuaji wa Sekta binafsi nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutumia akili kukusanya kodi na sio matumizi ya nguvu na mabavu kama inavyoendelea kufanya Serikali ya awamu ya tano. Tanzania sio kisiwa na ni sehemu ya dunia haiwezi kujitenga na kujitegemea yenyewe inahitaji wawekezaji wa ndani ya nje ya nchi ili kunenepesha uchumi wa Taifa.

## 19. MWENENDO WA BIASHARA NCHINI NA JINSI UNAVYOATHIRI UKUAJI WA UCHUMI

### 19.1. Kushuka kwa Mauzo ya Bidhaa nje ya Nchi

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Biashara nchini inaongozwa na Sera ya Taifa ya Biashara ya mwaka 2003. Hata hivyo Seriali hii ya awamu ya tano inaonekana kutotekeleza Sera hiyo kwa ufanisi. Tafiti zinaonesha kuwa Sera hii haijafanikiwa kuendeleza sekta ya biashara hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Sera hii ya Taifa ya Biashara katika dira yake inaweka mkazo kwa Sekta nzima ya biashara kuwa ni kuugeuza uchumi kuwa wa uuzaji wa bidhaa nje ya nchi (export-led); Dira ya Sera hiyo inasema hivi:-

***"... to transform the economy from a supply constrained one into a competitive export-led entity responsive to enhanced domestic integration and wider participation in the global economy through national trade liberalisation"***

Kwa tafsiri isiyo rasmi ya Kiswahili ni kuwa:-
*"…kubadilisha uchumi kutoka katika vikwazo vya usambazaji kwenda kwenye ushindani wa mauzo ya bidhaa nje ya nchi yatakayowezesha maingiliano ya ndani na ushiriki mkubwa wa uchumi wa dunia kupitia biashara huria kitaifa"*

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imebaini kuwa msingi mkuu wa Sera ya Biashara ya Taifa ni **"mauzo ya bidhaa nje ya nchi"** yaani **"exports".** Msingi ambao ujenzi wake kwa vitendo umekuwa ni kitendawili kikubwa kutokana na Serikali hii ya CCM kushindwa kwa vitendo kuimarisha uzalishaji wa bidhaa na huduma ndani ya nchi ili hatimaye kuongeza mauzo ya bidhaa nje ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Ripoti ya Shirika la **Trading Economics** iliyochapwa mwaka 2017 katika takwimu zake zimeonesha kuwa mauzo ya bidhaa nje ya nchi (Exports) yameshuka kutoka **Dola za Kimarekani milioni 932.90** mwezi Januari, 2016 mpaka **Dola milioni 854** mwezi Disemba, 2016. Wastani wa mauzo ya bidhaa nje ya nchi uliendelea kubakia kuwa **dola milioni 549.16** kutoka mwaka 2006 mpaka mwaka 2017.

**Mheshimiwa Spika,** Ripoti ya Benki ya Dunia ya mwaka 2017 iitwayo **"Ease of Doing Business Tanzania"** (Wepesi wa Kufanya Biashara Tanzania) imeripoti kuwa Tanzania imeshika nafasi ya 180 kati ya 190 (nafasi ya 10 kutoka mkiani) katika wepesi wa kufanya biashara baina ya mipaka ya nchi na nchi (Trading Across Borders)

**Mheshimiwa Spika,** kukamilisha nyaraka za mauzo ya bidhaa nje ya nchi hapa kwetu Tanzania inachukua saa 96 (karibuni siku 4) wakati Botswana huchukua takribani saa 8 tu, na Kenya majirani zetu huchukua muda wa saa 21. Kushuka kwa mauzo ya bidhaa nje ya nchi kumeendelea kushika kasi hasa katika kipindi hiki ambacho Serikali ya awamu ya tano ipo madarakani.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kutoa taarifa mbele ya Bunge lako tukufu juu ya hatua inazozichukua kuhakikisha inaongeza kiwango cha mauzo ya bidhaa nje ya nchi (Exports) ili kukuza uchumi.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa inaboresha mazingira ya biashara katika mipaka ya nchi na nchi (Trading Across Borders). Ili nchi yetu iendelee kuaminiwa na wawekezaji wa ndani na nje, ni lazima sera na sheria zetu za biashara ziaminike, ziheshimiwe na ziwe shirikishi (Predictable and participatory).

### 19.2. Mazingira Magumu ya Kufanya Biashara Nchini

**Mheshimiwa Spika,** Ripoti ya **Ease of Doing Business Tanzania 2017** imeonesha kuwa Tanzania imeongeza ugumu zaidi katika hatua za kuanzisha bishara kwa kuongeza tozo za usajili. Jambo hili linaathiri juhudi za kuongeza ajira kwa vijana wetu. Tanzania imeshika nafasi ya 135 kati ya 190 katika wepesi wa kuanzisha biashara mpya. Unapokuwa na ugumu wa kuanzisha biashara, unawafanya wajasiriamali wasifanye shughuli rasmi ya kuingiza mapato yao na mapato ya Serikali, na hivyo kupunguza kiasi cha ajira zitokanazo na biashara rasmi.

**Mheshimiwa Spika,** ili mjasiriamali aanzishe biashara Tanzania anatakiwa kuruka vihunzi 9 vya utaratibu wa usajili ndani ya siku 26 na gharama ya asilimia 21.5 ya mapato ya Mtu mmoja kwa mwaka (per capital income). Biashara za ujenzi wa majengo ikiwemo uuzaji wa vifaa vya ujenzi unakabiliwa na changamoto kubwa ya muda mrefu unaotumiwa kutoa Kibali cha Ujenzi (Construction Permit). Utafiti wa ***'Ease of Doing Business 2017'*** unaonesha kuwa inachukua takribani siku 205 na taratibu 18 ili mfanyabishara apate kibali cha ujenzi. Kuingiza umeme kwenye biashara mpya kama vile kiwandani inachukua siku 109 na hatua 4 za ukamilishaji wa nyaraka mbalimbali. Kupata hati ya nyumba kwa ajili ya biashara mbalimbali inachukua hatua 8 ndani ya siku 67 kukamilisha mchakato wa kupata hati hizo.

**Mheshimiwa Spika,** nchini Rwanda, ambako ndiko Serikali ya awamu ya tano inapendelea sana kwenda kuchukua ushauri wa masuala mbalimbali ikiwemo jinsi ya kukusanya kodi, inachukua muda wa siku 1 tu kufungua Kampuni bila kulipia gharama zozote zile. Hapa nchini inachukua siku 4 kufungua kampuni na ada inayotozwa ni kati ya Shilingi 20,000 na 440,000 jambo linazuia biashara nyingi kurasimishwa, ajira kupotea na sekta binafsi kuendelea kudumaa.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na mazingira magumu ya kuanzisha na kuendeleza biashara nchini, utafiti uliofanywa na Wizara ya Viwanda na Biashara mwaka 2012, (National Baseline Survey Report – Micro, Small and Medium Enterprises in Tanzania) unaonesha kuwa asilimia 96.4 ya biashara za chini (Micro-Entprises) hazijasajiliwa na BRELA, na asilimai 84.4 ya biashara ndogo (Small Enterprises) hazijasajiliwa na BRELA, huku asilimia 63 ya wafanyabishara waliohojiwa wakisema hawajui chochote juu ya masuala ya usajili wa biashara.

**Mheshimiwa Spika,** hii ni ishara kuwa mazingira ya kuanzisha biashara nchini sio rafiki kiasi cha kuwa na kiwango kikubwa cha biashara zinazoanzishwa bila kusajiliwa rasmi. Ni ishara pia kuwa mipango ya Serikali haiwezi kuwafikia kundi hilo kubwa la wafanyabiashara nchini ili kuboresha mazingira yao

ya biashara na kuongeza mapato ya Serikali kwa namna itakayofaa.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuboresha mazingira ya kuanzisha biashara kwa kupunguza idadi ya siku mpaka kufikia siku moja na kuondoa tozo za usajili wa makampuni ili kuchochea wajasiriamali kufungua makampuni kwa wingi na kuongeza ajira kwa Watanzania.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuweka mazingira rafiki na yanayovutia wafanyabisahara wa kada zote kusajili biashara zao kwa namna itakayoiwezesha Serikali kubaini wafanyabishara walipo ili kuwapelekea Maendeleo kwa wepesi na haraka zaidi, tofauti na ilivyo hivi sasa, ambapo ni vigumu mipango ya Serikali kuzifika biashara ndogo ndogo zaidi ya asilimia 90 ambazo hazijasajiliwa na kutambuliwa.

## 19.3. Kufungwa kwa Biashara zaidi ya 2,000 Nchini

**Mheshimiwa Spika,** Waziri Uchumi na Mipango, Mhe. Dr. Philip Mpango alinukuliwa na gazeti la Mwananchi, tarehe 3 Januari, 2017 akikubali kuwa Serikali imebaini kuwa karibu wafanyabiashara 2,000 wamefunga biashara zao. Gazeti hilo hilo la Mwananchi, lilimnukuu mwenyekiti wa Wafanyabiashara nchini, Bw. Johnson Minja akidai kuwa kufungwa kwa biashara hizo kunatokana na Serikali kutosikiliza kilio cha muda mrefu cha wafanyabiashara, na kuwa Serikali imeweka mazingira magumu sana ya kufanya biashara hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Suala hili la kufungwa kwa biashara nchini limetolewa angalizo na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF). Ripoti ya IMF kuhusu utekelezaji wa Sera Tanzania (Policy Support Instrument for Tanzania) iliyotolewa tarehe 9 Januari, 2017 imeionya Tanzania kuwa moja ya masuala yanayohatarisha ukuaji wa uchumi ni pamoja na *"kuyumba kwa sekta binafasi kutokana na mikakati mipya ya Serikali ya*

*awamu ya tano"* (private sector uncertainty about the government's new economic strategies.)

**Mheshimiwa Spika,** kama biashara 2,000 zilizofungwa wastani kila biashara inaajiri watu 5, inamaanisha kuwa ajira 10,000 za Watanzania zimepotea kutokana na sera mbovu za uratibu wa biashara nchini zinazosimamiwa na Serikali ya awamu ya tano. Serikali imevuruga mazingira ya biashara nchini na hivyo kupelekea wananchi wengi kuishi maisha ya dhiki na taabu.

**Mheshimiwa Spika,** muendelezo wa sera hizi zinagharimu ajira na biashara nchini ni kinyume cha ushauri uliotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa – IMF tarehe 14 Aprili, 2017 Tanzania kuifikia malengo ya uchumi wa kati sharti iwe na sekta binafsi yenye nguvu na yenye mazingira bora ya biashara. Ni wazi kuwa kudorora huku kwa biashara na kuendelea kufungwa kwa biashara nchini ni ishara kuwa Serikali ya awamu ya tano haielewi inataka kulipeleka wapi Taifa letu kwa kuendelea kuharibu mazingira ya biashara nchini.

**Mheshimiwa Spika** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kutoa taarifa za kina kwanini biashara zaidi ya 2,000 zimefungwa nchini. Aidha, tunaitaka Serikali iseme kuwa ni hatua zipi inazozichukua ili kuondoa mdororo wa biashara nchini na hatua zilizochukuliwa kuzuia kuendelea kufungwa kwa biashara nyingine nchini.

### 19.4. Hali Duni ya Wafanyabiashara Wadogo

**Mheshimiwa Spika,** Taifa letu limekosa dira muafaka (a right vision) juu ya kuendeleza watu wake kupitia sekta isiyo rasmi iliyojaa wafanyabiashara wengi wa biashara ndogo ndogo maarufu kama wamachinga. Kwa ufupi, Tanzania kwenye sekta ya Biashara ni Taifa la wachuuzi, ambao kwa muda mrefu biashara zao zimekuwa zikiathiriwa na ukosefu wa dira muafaka ya Serikali kuhusu biashara ndogo ndogo.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni bado inaendelea kusisitiza kuwa 'Maendeleo ni ya watu na sio ya

vitu' hivyo ni jukumu la Serikali kuangalia Maendeleo ya kila mtu mmoja mmoja kwa makundi yao kama vile ilivyo kwa kundi la wafanyabiashara ndogondogo.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali pamoja na kufanya tafiti mbalimbali kupitia mashirika yake mbalimbali lakini inashindwa kuzitumia tafiti hizo kwa umakini wakati wa kupanga vipaumbele kwenye sekta ya ukuzaji wa biashara kwa ajili ya Maendeleo ya watu nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Moja ya tafiti ambazo hazitumiki ipasavyo na kwa kiwango cha kuridhisha katika kupanga Maendeleo ya wafanyabiashara ndogo ndogo ni pamoja na utafiti uliofanywa na Wizara ya Viwanda na Biashara mwaka 2012 juu ya Sekta ya Biashara za Chini, Ndogo, na Biashara za Kati (National Baseline Survey Report – Micro, Small and Medium Enterprises in Tanzania).

**Mheshimiwa Spika,** Utafiti huo ulibaini kuwa vijana wa Kitanzania wenye umri kati ya miaka 25 na 34 ndio kundi kubwa kwa asilimia 36 linalojihusisha na biashara ndogo ndogo nchini, wakati kwa ujumla wake asilimia 14.6 hawajawahi kumaliza elimu ya shule ya msingi, na asilimia 73.5 ndio wamemaliza elimu ya shule ya msingi na asilimia 72.1 katika maisha yao yote hawajawahi kabisa kupata mafunzo yoyote kabla hawajaanza biashara. Bila kuwa na 'picha kubwa' yaani maono makubwa ya kuliangalia taifa letu miaka 100 mbele, taifa haliwezi kupiga hatua za Maendeleo ya kibiashara kwa haraka, bali tutaenda kwa kusuasua kama ilivyo hivi sasa.

### 19.5. Hasara Benki za Biashara zinazochangiwa na Sera za Serikali

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ya awamu ya tano imendelea kuasisi sera mbovu ambazo zinaathiri sekta ya fedha inayotarajiwa kuimarisha sekta binafsi nchini. Sekta Binafsi imeendelea kuyumba kutokana na Sera ya Serikali ya kuzuia mashirika ya Serikali kutunza fedha katika mabenki ya kibiashara na kuondoa jumla ya Shilingi bilioni 5 kutoka mabenki ya biashara na kuzitunza katika akaunti maalumu zilizopo Benki Kuu (BoT).

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imebaini kuwa ongezeko la riba za mikopo katika benki za biashara linatokana na uamuzi wa Serikali ya awamu ya tano kuondoa fedha katika mabenki ya biashara jambo lililopunguza kiasi cha fedha 'liquidity' na kupelekea kupungua kwa amana katika benki hizo jambo linalolazimisha benki za biashara kuongeza kiwango cha riba ili kujipatia unafuu wa kibiashara.

**Mheshimiwa Spika,** uamuzi wa Serikali kuondoa fedha katika mabenki ya biashara ni hatua ya kuamua kuiangamiza sekta binafsi ambayo inauhusiano wa moja kwa moja na ukuaji wa pato la kila Mtanzania na pia ukuaji wa pato la Taifa. Mpaka sasa Benki kadhaa za kibiashara zimerekodi hasara katika hesabu zao kutokana na uamuzi huo. ***Gazeti la The Citizen, tarehe 11 mwezi Agosti, 2016***[26] liliripoti kuwa uamuzi wa Serikali kuhamisha fedha kwenye mabenki ya biashara kumesababisha benki kadhaa kupata hasara. Benki zilizorekodi hasara ni pamoja na ***Barclays Bank Tanzania (hasara ya Shilingi bilioni 8.2), TBI Development Bank (hasara ya Shilingi bilioni 6.27)***, ***Stanbic Bank Tanzania (hasara ya shilingi bilioni 2.40)***

**Mheshimiwa Spika,** Gazeti hilo hilo la The Citizen, tarehe 31 mwezi Oktoba, 2016[27] liliripoti benki kadhaa kuendelea kupata hasara iliyopelekewa na uamuzi wa Serikali kuondoa fedha katika mabenki ya biashara. Benki zilizorekodi hasara ni pamoja na ***CRDB Bank (hasara ya shilingi bilioni 1.9) na Amana Bank (hasara ya milioni 195)***

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kuanza kutekeleza sera za kutunza fedha za umma kwenye akaunti maalumu zilizopo Benki Kuu, sasa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka

---

[26] Banks hit by public entities' withdrawal of Sh500bn, imetolewa http://www.thecitizen.co.tz/magazine/businessweek/1843772-3340626-57jbnmz/index.html

[27]Tanzania's largest bank posts Sh2bn quarterly loss, **imetolewa:** http://www.thecitizen.co.tz/News/Tanzania-s-largest-bank-posts-Sh2bn-quarterly-loss/1840340-3435694-2cwx6vz/index.html

Serikali kulielezea Bunge lako tukufu kuwa ni hatua zipi inazozichukua ili kuhakikisha mifumo ya matumizi ya fedha za umma katika mashirika ya umma na Serikali kuu inaimarishwa ili kuzia ubadhirifu, wizi, ufisadi wa kimikataba na kuziba mianya ya rushwa kubwa kubwa za kimfumo zinazowanufaisha 'PEP' (Political Exposed Personalities) kama vile Wakurugenzi, Makatibu wakuu, na Mawaziri na viongozi wa ngazi za juu zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ya awamu ya tano kuelewa kuwa njia salama ya Serikali kuzuia wizi, ubadhirifu, ufisadi na matumizi mabaya ya fedha za umma sio kuzificha fedha katika akaunti maalumu zilizopo Benki Kuu; ***kwa kuwa, kwa vyovyote vile, lazima zitatolewa ili zikatumike kugharamia ujenzi wa miradi mbalimbali ya umma,*** njia sahihi ya kuzuia wizi ni ***kuimarisha usimamizi wa fedha (finance management) ndani ya mashirika ya umma na Serikali, kuimarisha sera za matumizi ya fedha kwenye miradi ya kimkakati na kuziba mianya ya rushwa katika mifumo rasmi ya matumizi ya fedha za umma.***
**Mheshimiwa Spika,** Mtindo unaotumiwa na Serikali ya awamu ya tano kutuza fedha za umma Benki Kuu badala ya kuziweka kwenye benki za biashara ili zisisimue uchumi wa nchi na kuimarisha sekta binafsi kwa kukuza biashara nchini ni njia za kizamani **(traditional methods),** zimepitwa na wakati na hazina tofauti na baba wa nyumba anayeficha fedha kwenye kibubu chini ya uvungu wa kitanda wakati angeweza kwenda kuzihifadhi katika amana za benki ili ziingizwe katika mfumo rasmi wa mzunguko wa fedha.

## 20. WINGI WA KODI KATIKA SEKTA YA UTALII NA ATHARI ZAKE KATIKA UCHUMI

**Mheshimiwa Spika,** ni masikitiko makubwa kuona kwamba serikali ya Chama cha Mapinduzi katika mapendekezo yake ya bajeti **haijazungumzia kwa namna yoyote uboreshaji wa sekta ya utalii**. Ni masikitiko makubwa kwa sekta binafsi zinazopambana kuhakikisha zinachangia pato la taifa yaani GDP kwa **17.5%** kama ilivyoonyeshwa kwenye ripoti ya Benki Kuu ya mwaka 2016, sekta inayotoa takribani ajira rasmi

**500,000** na jumla ya ajira zisizo rasmi **1,500,000** kwa mwaka kuona kuwa bajeti hii haijachukua mapendekezo yao licha ya sekta binafsi katika utalii kuonyesha vyanzo mbadala vya mapato. Wafanyabiashara katika sekta ya utalii ndio wanao kamuliwa kodi nyingi na kuwekewa mazingira magumu ya biashara. **Serikali ya CCM imesahau kabisa ili ng'ombe aweze kukamuliwa maziwa vizuri ni lazima aweze kulishwa vizuri.** Bajeti hii ya Serikali ya awamu ya tano haijawagusa kabisa maelfu ya wananchi wanaoishi na kujipatia riziki na kulipa kodi kwa kupitia sekta hii ya utalii. Hii ni bajeti ya ajabu kabisa ambayo haijawahi kutokea. Ni bajeti inayokwenda kuizika sekta ya utalii ambayo kihistoria imekuwa ni sekta ya pili baada ya kilimo katika kuchangia pato la taifa na kipato cha wananchi walio wengi.

**Mheshimiwa Spika,** ni ajabu kabisa bajeti hii ya serikali ya CCM haijaanisha vipaumbele vyake katika sekta ya utalii wala vyanzo vipya vya mapato vinavyotokana na utalii huku nchi yetu ikiwa na utajiri mkubwa wa rasilimali asili. Wakati nchi ya Kenya ikitoa kipaumbele katika sekta ya utalii ambayo uwekezaji wake ni mdogo na ikilinganishwa na faida (low investment - high return).Nchi hiyo imeainisha chanzo chake kipya cha mapato katika utalii ikiwemo utalii wa michezo (sport tourism), utalii wa fukwe (beach tourism) na utalii wa huduma ya afya (medical tourism) kama ilivyo kwa nchi ya India iliyowekeza zaidi katika huduma za matibabu ambapo wageni kutoka nchi mbalimbali hutembelea katika nchi hiyo kwa dhumuni la kununua huduma za kitabibu. Kwa mwaka 2012 nchi ya India iliingiza takribani dola za kimarekani bilioni 22.2 kwa huduma za kitabibu pekee. Pamoja na hilo nchi ya India imekuwa ikijipatia fedha nyingi za kigeni kwa kuuza visa za matibabu yaani (medical visas).

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka huu wa fedha 2017/2018 serikali ya Kenya imejikita katika ukarabati mkubwa wa ngome ya Yesu (Fort Jesus) ya Mjini Mombasa kama chanzo kikuu cha kuongeza mapato huku ikiboresha huduma katika viwanja vya ndege, maeneo ya kupumzikia na kutafuta masoko ya watalii.

**Mheshimiwa Spika**, kwa hapa Tanzania mambo ni tofauti kabisa kwani serikali imejikita kufanya siasa na hadaa kwa Watanzania kama ilivyozoea, kwani bajeti iliyowasilishwa na serikali imejikita katika kutoa ahuweni kwa watu wa tabaka la juu na kati huku zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania masikini waishio vijijini ikiwa haijawagusa ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, huko vijijini ndiko kuna mbuga mbalimbali za wanyama, ndiko wananchi wanapotunza hifadhi za misitu yetu, ndipo kwenye WMA's ambazo kimsingi ndizo zinazosaidia uharakishaji wa maendeleo katika vijiji vinavyozunguka hifadhi.Hivyo basi, kushindwa kutoa kipaumbele kwenye sekta ya maliasili na utalii ni dhahiri kuwa hakujawagusa moja kwa moja wananchi hawa.

**Mheshimiwa Spika**, kukumbuke kuwa kufutwa kwa ada ya mwaka ya leseni ya magari haina mguso wa moja kwa moja kwa mwananchi anayeishi katika lindi la umaskini vijijini. Lakini kwa kuboresha mazingira ya uwekezaji katika utalii wa asili (cultural tourism),kuboresha WMA's, kutoa kipaumbele cha ajira katika maliasili zetu ,kuwekeza katika mazingira ya hifadhi na misitu kuna faida ya moja kwa moja kwa wanachi hawa.

**Mheshimiwa Spika,** katika ukurasa wa tisa na kumi wa kitabu cha hotuba ya Waziri kifungu kidogo cha (iv) na (vii) vinaelezea kwamba serikali itahakikisha kwamba madini na maliasili zetu zinawanufaisha wananchi. Ni lazima hapa tujiulize wananchi hawa wananufaika vipi na maliasili endapo serikali hii haiwajali wala kuthamini mchango wa sekta binafsi. Jambo hili limejidhihirisha wazi katika ukurasa wa 22 na 23 wa hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya fedha 2017/18. Serikali imejinasibu kuwa inaamini sekta binafsi ndiyo injini ya uchumi na inathamini sana na kupongeza mchango mkubwa wa wafanyabiashara.

**Mheshimiwa Spika,** serikali imekwenda mbali zaidi na kujitutumua kuwa imendelea na jitihada za kuimarsiha utulivu wa uchumi, kupunguza urasimu, kuharakisha maamuzi, kuimaisha ulinzi na usalama na kuhakikisha upatikanaji wa

miundombinu ikiwemo umeme na mikopo. Mambo haya yanayosemwa na serikali hii ya CCM ni mambo ya ubabaishaji kabisa na usanii mtupu. Katika sekta ya utalii imeghubikwa na urasimu wa kutisha kuanzia kwenye kufungua kampuni na kulipa kodi, msururu wa tozo zinazowanyonya wafanyabiashara, rushwa ya kutisha, upendeleo kwa makampuni makubwa yale yanayolinda maslahi ya watu wachache, na kauli zinazokatisha tamaa zinazotolewa na viongozi wakubwa wa serikali ambazo kimsingi zina athari za moja kwa moja katika ukuaji wa sekta hii ya utalii.

**Mheshimiwa Spika**, mnamo Mwezi Julai 2016, Bunge hili lilipitisha Sheria ya Fedha 2016/2017 (Finance Act 2016/2017). Sheria hiyo ilianzisha kodi ya ongezeko la thamani yaani **VAT kwa asilimia 18** kwenye shughuli za utalii. Katika maelezo ya Waziri wa Fedha alieleza kwamba kuongeza kwa kodi hiyo ni mpango wa serikali wa kukusanya kodi na kuongeza mapato ili kuondokana na utegemezi,kuboresha huduma mbalimbali za kijamii na kupunguza athari za kimazingira zinazotokana na shughuli za utalii.

**Mheshimiwa Spika**, wakati huo huo katika bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii Mwaka wa fedha 2016/2017 ya nchini Kenya serikali iliamua kuondoa gharama ya **VAT ya 16%** katika huduma za utaliii. Kwa mujibu wa taarifa ya SATOA (www.satoa.com) ya tarehe 15/06/2016 yenye kichwa cha habari ***"Tanzania Tourism Industry worry about VAT on services"*** ambayo ilianisha kwa kina sababu hasa ya nchi ya Kenya kuondoa kodi hiyo ya VAT ambapo kimsingi iliondolewa ili kuisaidia nchi hiyo kuweza kumudu soko la ushindani ambalo lilikuwa limeathiriwa na changamoto za kisiasa na matishio ya ugaidi. Lakini zaidi ikiwa ni moja ya mbinu ya kibiashara katika kuwavutia watalii wengi zaidi ambapo wanaweza kupata huduma ya utalii kwa gharama nafuu na kwa ubora zaidi kuliko nchi nyingine yoyote Afrika Mashariki. Mwaka 2013 sekta ya utalii nchini Kenya ilianguka kwa **4.6 %** kutokana na matishio ya ugaidi na mpaka mwaka 2016 sekta ya Utalii nchini humo imekuwa kwa **15%** huku Tanzania ikikuwa kwa **11% pekee**.

**Mheshimiwa Spika,** ni dhahiri katika nchi za Afrika Mashariki nchi ya Kenya ndio mshindani hasa wa nchi yetu katika ushindani wa biashara ya utalii. Ni lazima tujue kuwa na mshindani katika biashara ni jambo zuri ambalo linatupa changamoto ya kubuni mbinu zaidi ili kuweza kuimarisha biashara hiyo. Kwa mantiki hiyo kama taifa tuna kila sababu za kuhakikisha tunakuwa na mbinu bora ili kuweza kuongeza idadi ya watalii.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Maliasili na utalii kwenye semina kuhusu umuhimu wa uhifadhi ya Mwezi Mei 2017, inaonyesha kwamba idadi ya watalii walioingia nchini kwa mwaka 2016 ni **1,284,279** ambapo kwa nchini Kenya waliingia watalii **1,307,351**. Hii inaonyesha kuwa kuna watalii **23,073** zaidi walioingia nchini Kenya. Ikumbukwe kuwa Tanzania ni nchi ya pili duniani kwa wingi wa vivutio vya maliasili lakini katika ushindani wa kibiashara ni nchi ambayo haifanyi vizuri ikilinganishwa na Kenya.

**Mheshimiwa Spika,** katika bajeti ya serikali ya Kenya 2017/ 2018 imeondoa VAT katika kuunda bodi za magari ya utalii ili kuwavutia wafanyabiashara wa utalii kuweza kuunda magari hayo maarufu kama (hardtop) kwa shughuli za utalii nchini humo kwa bei nafuu zaidi. ***(Kenya exempted locally assembled tourist vehicles in a move aimed at encouraging tour operators to buy locally assembled vehicles at a lower cost*****).** Hii ina maana kwamba hata wafanyabiashara wa sekta ya utalii kutoka Tanzania watavutiwa kwenda nchini Kenya kuunda magari yao kwa bei nafuu. Mpaka sasa biashara hii ya kuunda bodi za magari , pamoja na viti inafanyika sana hapa nchini.Kwa bei ya kuanzia shilingi milioni 50 kwa gari. Kwa tafiti mbalimbali za masoko ya magari zinaonyesha kuwa kwa sasa bei ya magari haya ya kitalii huanzia shilingi milioni 150 mpaka milioni 170. Hivyo basi kuondoa VAT kwenye kuunda magari haya ni msaada mkubwa sana kwa wafanyabiashara na hivyo ni wazi kuwa tutapoteza wateja ambao walikuwa wakiunda magari haya hapa nchini kutokana na gharama kubwa na hivyo serikali kupoteza mapato hayo kabisa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na hilo serikali imeshindwa kuwasaidia kabisa wawekezaji wa ndani na nje kwa kuwabebesha mzigo mkubwa wa kodi ambao hauendani kabisa na mapato wanayoyapata kutokana na shughuli za utalii. Pamoja na kuwa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imelizungumzia sana jambo hili na kutoa ushauri mara kwa mara bado Serikali ya CCM kwa mwendo ule ule wa kupuuza mambo imeendelea kuwatoza wafanyabiashara takribani kodi 36 ambapo kati ya kodi hizo 12 ni za usajili wa biashara na udhibiti wa leseni (business registration and regulatory license fees),11 zikiwa ni ada mbalimbali za usafiri na usafirishaji wa watalii (duties for tourist vehicles) na 13 zikiwa ni tozo nyinginezo (miscellaneous fees) na hivyo kuifanya Tanzania kuwa ni nchi yenye gharama kubwa zaidi katika huduma za utalii Afrika ya Mashariki kwa zaidi ya **25%** tofauti na miaka ya nyuma ambapo Tanzania ilikuwa na gharama zaidi kuliko nchi nyingine za Afrika Mashariki kwa **7%.**

**Mheshimiwa Spika,** tukirejea kauli ya Rais aliyoitoa tarehe 18 Julai, 2016 akiwaapisha Wakuu wa Mikoa alizungumzia suala la tozo za kodi katika shughuli za utalii alisema ***"ni bora waje awatalii wachache wanaolipa kodi kuliko kuja watalii wengi wasiolipa kodi".*** Ni dhahiri kuwa kwa kauli aliyoitoa Mheshimiwa Rais katika suala hili la kodi katika sekta ya utalii ni kuwa alipitiwa au hakuwa na maelezo ya kutosha kuhusiana na wingi wa kodi katika sekta hii ambayo wawekezaji wengi wameanza kuikimbia kutokana na mzigo mkubwa wa kodi unaowaumiza hasa wawekezaji wazawa.

**Mheshimiwa Spika,** Ongezeko kubwa la kodi katika sekta ya utalii limekuwa na madhara makubwa ya kibiashara kwa wawekezaji, madhara kwa uchumi wa nchi na hata uchumi binafsi wa wale wanaoitegemea sekta hii kwa ajili ya kujipatia kipato tofauti kabisa na maelezo ya Waziri aliyoyatoa tarehe 24 Mei 2017 alipokuwa akihitimisha hoja

**Mheshimiwa Spika**, mpaka sasa hoteli maarufu zilizokuwa zinategemewa na watalii wengi hapa nchini zimefungwa na nyingine kubadilisha matumizi yake kutokana na kushindwa kujiendesha kutokana na kuporomoka kwa soko.

Mfano kwa Mwaka 2016 pekee Hotel ya Land Mark ilibadilishiwa matumizi na kuwa hosteli za wanafunzi, kufungwa kwa hoteli zote za JB Belmont za Dar es Slaam na Mwanza zilifungwa kutokana na madeni na kushindwa kujiendesha, Impala hotel, Ngurdoto Arusha, Malindi hotel, Mtendele hotel , Mount Meru hotel Arusha pamoja na kampuni mbalimbali yakiwa na hali mbaya na hivyo kuamua kupunguza wafanyakazi.

**Mheshimiwa Spika,** kufungwa kwa hoteli , kubadilisha matumizi ya hoteli hizi za kitalii au kwa makampuni makubwa ya utalii ni ushahidi tosha kuwa sekta ya utalii nchini iko katika hali mbaya. Jambo hili la wazi kabisa halihitaji mbwembwe na kelele za kisiasa za kuendelea kuwadanganya Watanzania na tarakimu zisizo na tija. Hivyo ni lazima kutafuta mbinu mbadala za kibiashara ikiwa ni pamoja na mbinu ya kutafuta masoko na kuvutia wateja ikiwa ni pamoja na kupunguza kodi zisizo za lazima kwa wafanyabiashara ili waweze kuboresha huduma. Endapo wafanyabiashara hawa wataboresha huduma ni dhahiri kuwa watalii wengi zaidi watavutiwa kuingia Tanzania kutokana na kuwepo kwa maliasili za kipee kabisa.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali hii imekuwa ikitumia fedha nyingi kupitia Wizara ya Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu yenye Manaibu Mawaziri wawili katika kutafuta ajira kwa vijana. Tujiulize Wizara hii ina faida gani kama imeshindwa kumshauri Mheshimiwa Rais katika kuona umuhimu wa kutumia kauli itakayowatia moyo zaidi wafanyabiashara ili waboreshe huduma na kuwavutia watalii wengi zaidi na hivyo wananchi wapate ajira. Katika biashara ya ushindani **kauli ni mali.** Tunatambua kabisa kauli ya Mheshimiwa Rais ni **amri na hivyo ni sawasawa na sheria (presidential decree)** hivyo kutokana na uzito wa kauli zake ni vyema zikapimwa ili zisiwe na madhara katika uchumi na hivyo kuathiri jamii nzima.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na kuyumba kwa sekta hii ya utalii serikali ya CCM ituambie imejiandaaje kuhakikisha inakabilina na athari za wimbi kubwa la vijana kukosa ajira

ikiwa ni pamoja na matokeo yake kama vile kuongezeka kwa uhalifu nchini,utelekezaji wa familia,Watanzania hawa kushindwa kulipa kodi nyingine mbalimbali na kununua huduma kama vile afya, elimu, chakula, na nyinginezo ambazo ni muhimu kwa binadamu**.**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na hilo ni dhahiri kuwa serikali itapoteza mapato.Katika tafiti mbalimbali za utalii kwa wastani wageni wanaokuja nchini huja na fedha za ziada yaani **Pocket money** ambapo wengi huja na zaidi ya $ 6,000 kwa wastani . Fedha hizi huingia katika mizunguko mbalimbali ya kibiashara inayoinufaisha nchi pamoja na wananchi. Endapo wafanyabiashara wataelemewa na mzigo wa kodi na kushindwa kufanya biashara katika soko la kibiashara la ushindani basi ni dhahiri watalii watapungua na serikali itakosa mapato.

**Mheshimiwa Spika**, athari nyingine inayojitokeza ni uzoroteshaji wa wazi wa sera ya diplomasia ya kiuchumi. Mpaka sasa taifa letu lina tatizo kubwa la kushindwa kutekeleza sera ya diplomasia ya kiuchumi.Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikilizungumzia jambo hili kwa kina sana lakini ni wazi kuwa kukosekana kwa maono na watu wenye maono ndani ya serikali ya Chama cha Mapinduzi kunasababisha watu hao kushindwa kumshauri Mheshimiwa Rais ipasavyo ili kuona umuhimu wa kuwekeza katika sekta ya utalii kwa jicho pana zaidi. Mfano, Katika nchi ya Kenya ambayo ina vivutio vichache zaidi kuliko Tanzania inapokea wageni wengi zaidi kwa mwaka ikilinganishwa na Tanzania. Hii ni kwa sababu nchi ya Kenya kwanza inapeleka Mabolozi wenye ujuzi na **uwezo mkubwa wa kiakili ( great minds)** katika balozi zake ili kuweza kutafuta masoko ya kimataifa ya kibiashara ya utalii (foreign markets),wenye uwezo wa kiushawishi kwa wawekezaji wakubwa kwenye sekta hii (skills in sensitizing potential foreign investors), wenye uwezo mahususi katika lugha za kimataifa ( competent in key international languages) ambao wana uwezo wa kushikiri katika makongamo makubwa ya kibiashara ili sasa waweze kuwasaidia wawekezaji hasa wa ndani katika kuwapungumzia mzigo mkubwa wa kodi na tozo

mbalimbali ambazo serikali ya CCM inadhani kuwawekea mrundikano wa kodi serikali itapata mapato. Hii ni aibu kubwa kwa nchi na wachumi ambao humshauri Mheshimiwa Rais.

**Mheshimiwa Spika,** serikali ya awamu ya tano itambue kuwa nchi yetu imeingia katika mikataba mbalimbali ya kulinda haki za watalii na kanuni za utalii (tourism bill of rights and tourist code ).Moja ya mikataba hii ni ile iliyotokana na Azimio la Bulgaria la mwaka 1985 ambalo linatambua jukumu jipya la utalii ikiwa ni pamoja na kunyanyua maisha ya watu wote,kama njia ya kuleta amani na mahusiano bora duniani ***"it recognizes the new role of tourism as an appropriate instrument for improving the quality of life of all people and as a vital force for peace and International understanding and defines the responsibility of States for developing tourism and in particular ,for fostering awareness of tourism among the people of the world and protecting and enhancing the tourism resources which are part of mankind's heritage.***

**Mheshimiwa Spika,** hii ikiwa na maana kwamba biashara ya utalii ina kazi muhimu zaidi ya kuleta au kuboresha mahusiano baina ya nchi yetu na mataifa mengine. Hii ni pamoja na kuondoa dhana kuwa watalii wanaokwenda kwenye nchi nchi nyingine ni watu wenye fedha nyingi; bila kujali haki zao kimsingi ikiwa ni pamoja na kujifunza, kupumzika na kuburudika.Serikali ya CCM ielewe kuwa Watalii wanaotembelea nchi nyingi za Afrika ni wale wenye uchumi wa kati. Hivyo hujinyima na kujichanga ili waweze kuja kutembelea hifadhi na vivutio vingine katika nchi zetu.Hatuna budi kuhakikisha kuwa nchi yetu inanufaika na safari zao lakini pia serikali inapaswa kutokuwatoza tozo nyingi zenye kuwaumiza na kuwafanya watalii hao kushindwa kutembelea vivutio hivi ambavyo ndio fahari yetu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mustadha wa sekta hii ya utalii, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri serikali kufanya yafuatayo:

1. Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri Kamati ya Bajeti ihakikishe kuwa sekta ya utalii inatambuliwa katika bajeti hii hasa kwa kuzingatia umuhimu wake mkubwa katika kuchangia pato la taifa yaani GDP.Kwani kwa kupunguza kodi zizsizo za lazima na masharti magumu kwa wafanyabiashara katika sekta hii kutayafanya makampuni ambayo hayajasajiliwa (kampuni bubu) kujitokeza kufanya biashara kihalali kutokana na unafuu wa kodi. Kwani mpaka sasa kuna makampuni zaidi ya 700 ambayo hayajasajliwa kutokana na ugumu wa masharti ya kuanzisha biashara ikiwa ni pamoja na idadi ya magari na kodi ya leseni.Badala ya wafanyabaisha hawa kuanza kufanya biashara akiwa na gari tatu (3) ambapo kwa gari moja linagharimu milioni 150-200, na hvyo kufanya jumla ya milioni 450-600 kwa ununuzi wa magari pekee ambapo Mtanzania wa kawaida hawezi masharti haya, au kutoza dola 2000 kwa leseni ya kuanza biashara ambayo ni sawa na shilingi milioni 4,474,000, huku kukiwa na ada nyingine zaidi ya 35 ni uonevu mkubwa kwa wananchi wenye nia ya dhati ya kuwekeza katika sekta ya utalii.Hivyo ni muhimu masharti haya yakapunguzwa ikiwa ni pamoja na kuondoa VAT, na kodi zinazojirudia rudia bila ulazima wowote

2. Kuzingatia ushauri unaotolewa mara kwa mara na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, serikali ituambie ni nini kipaumbele chake katika sekta ya utalii nchini. Na je, inawekeza katika vyanzo vipi vya mapato ili faida (return of investment) iweze kupatikana na kuongeza pato la taifa na fedha za kigeni (foreign currency)

3. Katika Malengo ya Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2016/2017-2020/2021 serikali ilijiwekea lengo la kufikisha watalii milioni 2 na kuhakikisha kuwa mpaka mwaka 2020 Tanzania itakuwa na jumla ya vitanda 1,735,000 seikali ituambie inatumia mikakati gani kufikia ili sasa kama nchi tuweze kumudu soko hili la uhsindani ndani ya Afrika Mashariki kwani mpaka mwaka 2016 nchi ya Kenya ilikuwa na takribani vitanda milioni 3.6 ikiwa ni ongezeko la 14.6 %

ikilinganishwa na mwaka 2015 ambapo ilikuwa na vitanda 3.1huku Tanzania tulitaka kufikia idadi tajwa tu kwa mwaka 2020.

4. Serikali kuanzisha kituo kimoja mahususi cha kulipia tozo mbalimbali (onestop centre) kuliko ilivyo sasa ambapo huchukua takribani masaa 2,000 kwa mwaka katika ulipaji wa tozo mbalimbali katika sekta ya utalii kama ilivyoelezwa kwenye utafiti wa Dr.Sinare.

5. Serikali kuangalia upya utalii wa asili (cultural tourism) kwa kuwaalika wawekezaji katika maeneo hayo pamoja na kuvitambua vivutio mbalimbali kama jambo la kisera ili vivutio kama hot springs,maeneo ya camping, maeneo ya kihistoria, maeneo yenye jiografia na sifa za kipekee ambayo yanaweza kuendeshwa na halmashauri na kuwa sehemu ya mapato ya halmashauri.

## 21. KATIBA MPYA NA UCHUMI WA NCHI

**Mheshimiwa Spika,** sote tunatambua kuwa Katiba ndio sheria mama. Katiba ndio taswira hasa ya taifa katika masuala ya kiuchumi, kisiasa na hata katika mambo mbalimbali ya utoaji wa huduma kwa wananchi .Katiba ndio msingi wa utoaji haki na wajibu wa kila raia. Hivyo basi, kwa kutambua umuhimu mkubwa wa kuwa na Katiba Mpya inayokidhi matakwa ya wananchi na inayoendana na mabadiliko makubwa ya kiuchumi, kisiasa na hata kutatua kero mbalimbali za kijamii serikali ya awamu ya Nne iliona ni vyema ikatoa fursa kwa wananchi kuleta maoni yao kuhusu aina ya Katiba wanayoitaka ili kuweza kunufaika kwa pamoja kama taifa.

**Mheshimiwa Spika,** hakuna uchumi bora wa nchi kama hakuna Katiba bora. Katiba ndio chombo pekee cha kulinda uhuru wa kila raia, ni chombo cha kuonyesha dira ya kule tunapotaka kuelekea na miiko yetu kama taifa. ***(Constitution is the only safeguard of our liberties; it is a solid expression of our vision and values as a nation).*** Kwa mantiki hiyo ***hatuwezi kamwe*** kuendelea kiuchumi kama hatuna katiba inayotoa taswira ya kule tunapotaka kwenda.

**Mheshimiwa Spika,** katika mchakato wa Katiba mpya ;rasimu ya pili ya katiba imejadili mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kulisadia taifa hili kujikwamua kutoka katika lindi la umaskini wa kujitakia, maradhi na ujinga uliopindukia uliosababishwa na Chama cha Mapinduzi na serikali zake zote zilizotangulia Rasimu hii pia inazungumzia mchakato wa kupata viongozi katika ngazi mbalimbali, muundo wa tume huru ya uchaguzi ambapo inapendekeza tume hiyo iteuliwe na tume maalum kuliko ilivyo sasa ambapo tume huteuliwa na Mwenyekiti wa Chama tawala, Katiba pendekezwa ya wananchi inalenga maadili ya viongozi wa umma, mamlaka ya viongozi ambayo hayawezi kukiuka haki za binadamu, lakini zaidi rasimu hii ya pili ya katiba inaonyesha taswira ya taifa huru, lenye watu huru ,mawazo huru na yanayojikita kuheshimu maamuzi ya wananchi kuliko ilivyo sasa ambapo Katiba tuliyonayo inawapa viongozi wengine mamlaka yanayopitiliza kitendo ambacho kinaweza kuhatarisha haki za raia, vyama vya siasa, na kuingiza nchi yetu katika utawala wa kiimla au udikteta jambo ambalo ni hatari sana kwa amani na usalama wa nchi yetu na pia ni hatari kwa uchumi wa wetu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa umuhimu wa matamanio ya kuwa na katiba mpya; serikali ilitumia mabilioni ya fedha ikiwa ni sawa na fedha za maendeleo za Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Kilimo, Wizara ya elimu, Wizara ya maji na Umwagiliaji, Maliasili na Utalii, Wizara ya Afya,Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2016/2017 pekee kama ilivyoainishwa kwenye fedha za maendeleo za Wizara mbalimbali kwenye kitabu cha Matumizi ya Maendeleo Juzuu ya Nne kwa mwaka 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mabilioni hayo yaliyotumika serikali ilitumia muda mrefu wa takribani miezi mitatu ikijumuisha wajumbe zaidi ya 600 ambapo kila mjumbe alilipwa posho isiyopungua shilingi 300,000 kwa siku huku watendaji mbalimbali nao wakilipwa posho. Hii ikiwa na maana kwamba fedha za walipa kodi wa nchi hii ndizo zilizotumiwa na serikali ya CCM katika kutafuta Katiba mpya . Kwa umuhimu huo miradi ya huduma za kijamii kama maji,

hospitali, madawa, nishati ya umeme ambapo huduma hizi muhimu kwa kila mwananchi hazikupewa kipambele kwa wakati huo kama mchakato wa Katiba Mpya.

**Mheshimiwa Spika,** kila raia wa nchi hii alitambua umuhimu wa kuwa na katiba mpya ambayo ilikuwa tegemeo la matumaini mapya ya kuwepo kwa utawala bora ambao ungechochea kasi ya ukuaji wa uchumi na kujenga dhana ya uwajibikaji kwa kila raia na viongozi wao. Kinyume na mategemeo ya wananchi walio wengi mchakato wa upatikaji wa Katiba Mpya umekuwa na kiza kinene hasa katika serikali hii ya awamu wa Tano chini ya John Pombe Magufuli.

**Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 4, Novemba 2016, Mheshimiwa Rais alinukuliwa akisema ***hakuwahi kuzungumzia Katiba mpya wakati wa kampeni zake, kwa hiyo katiba siyo kipaumbele chake na kwamba anachotaka kwanza ni kunyoosha nchi***. Kauli hii ya Mheshimiwa Rais inataka kutuaminisha kuwa fedha zote zilizotumika katika mchakato huu ni kwamba zimekwenda kwenye mifuko na matumbo ya watu bure. Inaaminisha kuwa muda uliotumika katika kutafuta maoni ya wananchi umepotea bure, imenyang'anya sauti Mwenyekiti wa tume, na zaidi ya yote inaonyesha dhahiri kupuuzwa kwa sauti za wananchi ambapo ndio wenye mamlaka ya kuiweka serikali yoyote madarakani.

**Mheshimiwa Spika,** nchi hii haiwezi kunyooka kama ***hakuna Katiba mpya ambayo imezingatia maoni ya wananchi na sio ile iliyopendekezwa na kikundi fulani au iliyofanyiwa uhuni wa kuyaondoa yale yanayopendekezwa na wananchi wenyewe***. Nchi inaweza kunyooka tu pale ambapo Katiba yake inatoa taswira chanya ya namna bora ya kunufaika au kumiliki na kulinda rasilimali za nchi, na zaidi nchi inaweza kunyooka pale inapokuwa na katiba yenye kujenga umoja wa kitaifa, katiba yenye kuzingatia ugawaji wa mapato, mfumo mzuri wa kimaamuzi, fidia kwa shughuli za uwekezaji katika rasilimali hasa madini na gesi na zaidi katiba inayolinda matarajio ya wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Katiba ya sasa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, imeweka misingi ya uwajibikaji katika usimamizi wa maliasili ya Taifa kama inavyosomeka kwenye Ibara ya 27 (1) na (2) na Ibara ya 28 (1) ya Katiba.

(1) Kila mtu ana wajibu wa kulinda maliasili ya Jamhuri ya Muungano,mali ya Mmlaka ya Nchi na mali yote inayomilikiwa kwa pamoja na wananchi ,na pia kuiheshimu mali ya mtu mwingine

(2) Watu wote watatakiwa na sheria kutunza vizuri mali ya Mamlaka ya Nchi nay a pamoja ,kupiga vita aina zote za uharibifu na ubadhiifu, na kuendesha uchumi wa taifa kwa makini kama watu ambao ndio waamuzi wa hali ya baadaye ya taifa lao.

28 (1) Kila raia ana wajibu wa kulinda,kuhifadhi na kudumisha uhuru,mamlaka,**ardhi** na umoja wa taifa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na uwepo wa vifungu hivi katika Katiba ya Mwaka 1977 bado maliasili za nchi hii kama wanyamapori, misitu, madini, gesi, hewa, mafuta, maji na uvuvi, na hata mgawanyo wa ardhi umegubikwa na rushwa. Rasilimali zetu hususani madini na wanyapori yamekosa usimamizi mzuri kiasi kwamba wachache ndio wanaonufaika na wananchi wetu hususani wale wanaozunguka maeneo hayo wamebaki kuwa maskini wa kutupwa. Vijiji vinavyozunguka misitu ya hifadhi na migodi imekuwa ikikumbwa na mapigano ya mara kwa mara,manyanyaso makubwa kutoka kwa baadhi ya wawekezaji na hata vifo kwa raia wema wa nchi hii.

**Mheshimiwa Spika,**mfano dhahiri ni mauaji yaliyowahi kutokea katika mgodi wa Geita ambayo yamekuwa yakiripotiwa ikiwa ni pamoja na mauaji ya mwanafunzi wa darasa la tano katika shule ya Kivukoni marehemu Hoja Juma, vitendo vya mauaji, utesaji na kuwabambikizia kesi wanavijiji katika vijiji vinavyozunguka mgodi wa North Mara (NMGM), madhara ya kiafya pamoja na ucheleweshaji wa fidia katika maeneo mbalimbali ambayo serikali

imewakaribisha wawekezaji bila kujali mustakabali wa wananchi katika maeneo hayo. Katika bonde la Loliondo wananchi wa maeneo hayo wamekuwa wakiishi kama wakimbizi kutokana na manyanyaso makubwa wanayopata kutoka kwa baadhi ya wawekezaji wa kigeni huku serikali ikiyafumbia macho kutokana na rushwa kubwa kubwa zinazowanufaisha vigogo wa juu serikalini. Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikiipigia kelele kampuni ya Ortello Business Corporation (OBC) kutoka falme za kiarabu ambae amekuwa mwiba mkubwa kwa wananchi wa Loliondo na kuona kama wametengwa katika taifa lao.

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwepo kwa malalamiko makubwa kutoka kwa wananchi kuhusu ushirikishwaji katika maamuzi yanayohusu utumiaji wa maliasili katika maeneo yao. Wananchi katika maeneo mbalimbali yenye rasilimali wamekuwa wakiyatunza vizuri na bila uharibifu wowote lakini pale wanapoanza kuletwa wawekezaji **bila kuwashirikisha na kinyume na matarajio yao** basi wananchi hao wamekuwa wakileta vurugu jambo ambalo sio afya kwa wawekezaji na haileti taswira nzuri katika sekta ya uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na nje. Mfano, vurugu zilizowahi kutokea Mwezi Januari na Februari mwaka 2013 mkoani Mtwara.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani ilieleza kwa kina sana katika hotuba ya nishati na madini kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kuhusu katiba na mustakabali wa madini, mafuta na gesi asilia ikitoa mifano hai ya uzoefu wa nchi mbalimbali zilizofanikiwa baada ya kutatua changamoto mbalimbali za kikatiba, kisheria na kisera ili kulinda rasilimali za nchi. Mfano, nchi ya Norway imeweka mwongozo wa uwajibikaji katika matumizi ya maliasili kwenye Katiba yao Ibara ya 110 (b) ambapo ibara hiyo inasema ***“every person has a right to an environment that is conducive to health and to natural surroundings whose productivity and diversity are preserved. Natural resources should be made use of on the basis of comprehensive long-term considerations whereby this right will be safeguarded for future generations as well”***. Mwaka 2009 nchi ya Bolivia ilianza mchakato wa kupata

katika mpya ambao pamoja na mambo mengine katiba hiyo ililenga kuhakikisha kuwa mafuta na gesi asilia yanawanufaisha wananchi wa Bolivia.

**Mheshimiwa Spika,** hivyo basi ni dhahiri katiba ya sasa ya mwaka 1977 haitaweza kutuhakikisha kuwa rasilimali zetu zinatukomboa katika lindi la umaskini ambao umetukabili kwa takribani miaka 56 sasa hata baada ya uhuru. Msimamo wa katiba pekee ndio utakaoweza kufafanuliwa vizuri katika sheria zetu zinazolinda rasilimali zetu. Mfano, katika Katiba ya Bolivia imeeleza bayana kuwa serikali ya nchi hiyo itakapoingia ubia na makampuni binafsi katika utafutaji na uvunaji wa mafuta na gesi asilia itakuwa na hisa zisizopungua asilimia hamsini na moja (51%) ya hisa zote. Jambo hili limewekwa bayana ndani ya katiba.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mifano hii iliyo wazi ni kuwa Tanzania inakabiliwa na changamoto kubwa katika usimamizi wa rasilimali zetu na ili kujikwamua katika hili tunahitaji maoni ya rasimu ya pili ya katiba ambayo ilipendekeza namna bora ya kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali zetu ili ziweze kumnufaisha kila mwananchi.

**Mheshimiwa Spika**, tulipofika sasa kama taifa hatuhitaji kuwa na katiba yenye viraka viraka. Tunahitaji kuwa na katiba mpya inayoendana na kasi ya ukuaji wa uchumi na ushindani wa kibiashara, mabadiliko ya kimfumo katika teknolojia, mashirikiano ya nchi mbalimbali na misimamo ya taifa na utaifa wetu, utawala bora, inayozingatia demokrasia , haki za binadamu na utawala wa sheria. Hivyo, rasimu ya pili ya katiba imetoa maoni ya wananchi ambayo kimsingi yanashabihiana na uhitaji huo.

**Mheshimiwa Spika,** wananchi wanataka kuona katika ikiwashirikisha katika kumiliki faida zitokanazo na rasilimali zao ,ikiwa ni pamoja na michakato ya wazi ya utoaji wa leseni,katiba inayotoa mamlaka kwa Bunge kupitia na kuridhia mikataba mbalimbali inayohusu uvunaji wa maliasili ya Taifa ili kuongeza uwazi. Lakini pia, katiba itoe fursa kwa wananchi kuwa na sauti dhidi ya bunge lao, ikiwa ni pamoja

na kuhakikisha wanapata taarifa ya kila kinachoendelea ndani ya Bunge kwa kuwa Bunge ndio mkutano mkuu wa wananchi.
**Mheshimiwa Spika,** hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kurejesha mara moja mchakato wa rasimu ya pili ya katiba kwani katiba pendekezwa haikuzingatia maoni ya wananchi . Vilevile, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kutatua mkwamo wa mchakato wa katiba uliojitokeza katika serikali hii ya awamu ya tano bila sababu mahususi. Kuendelea kwa mkwamo huu kunatoa taswira hasi kwa serikali ya awamu ya tano sio tu ndani ya nchi bali pia katika medani za kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa umuhimu huu wa katiba mpya Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Pombe Magufuli kurejea katika Ibara ya kwanza ya Katiba ya Japan inayosema ***"The Emperor shall be the symbol of the State and of the unity of the People, deriving his position from the* will of the people *with whom resides sovereign power".*** Ikiwa na maana kwamba Mheshimiwa Rais azingatie matakwa ya wananchi katika kuwaletea kile walichokiomba kwa muda mrefu ambacho ni rasimu ya pili ya Katiba.

## 22. MCHANGO WA USAFIRI WA RELI KATIKA UJENZI WA UCHUMI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kitabu cha Mpango wa pili wa Maendeleo, kati ya mataifa 189 yanayotumia usafiri wa Reli duniani, Tanzania inashika nafasi ya 84 kiutendaji katika sekta hiyo. Hata hivyo, pamoja na Tanzania kuonekana kushika nafasi nzuri kwa wastani, bado kuna changamoto kubwa katika ukarabati na ujenzi wa miundombinu mipya ya reli.

**Mheshimiwa Spika,** ni ukweli kwamba mkakati wa ujenzi wa Reli ya kati kwa awamu ya kwanza kwa kujenga reli hiyo kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro. Hata hivyo, changamoto kubwa inaonekana ni upatikanaji wa fedha za kuhakikisha Reli hiyo inajengwa kwa ukamilifu wake kwa maana ya kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza.

**Mheshimiwa Spika**, Ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa (standard gauge) kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza, unatarajia kukamilika mwaka 2021 na utagharimu Sh trilioni 7.6. Aidha, awamu ya kwanza ya ujenzi huo inahusisha kipande cha kilomita 300 kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro, na tayari ujenzi huo umeshawekewa jiwe la msingi na unakadiriwa kugharimu dola za Marekani bilioni1.21 (Sh trilioni 2.6).

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa taarifa ya Ofisa Uhusiano kwa Jamii wa Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli Tanzania (RAHCO), ujenzi wa reli hiyo yenye urefu wa kilomita 1,011 (Dar es Salaam – Mwanza) umegawanyika katika awamu tano. Awamu ya kwanza ni kipande cha Dar es Slaam – Morogoro ambapo ujenzi umeshaanza; awamu nyingine itahusisha vipande vya Morogoro hadi Makutupora kilomita 336, Makutupora-Tabora (km 294), Tabora-Isaka (km 133) na Isaka-Mwanza (km 248); huku Serikali ikiwa imetenga kiasi cha shilingi trioni 1 katika bajeti yake kwa ajili ya ujenzi wa reli hiyo kwa kiwango cha standard gauge.

**Mheshimiwa Spika**, Sababu kubwa za kujenga reli ya kati kwa kiwango cha standard gauge ni sababu za kiuchumi ambazo lazima zizingatiwe kwa kiwango ambacho kitaliwezesha taifa kupata faida. Kwa mantiki hiyo bado, kuna sintofahamu katika tathimini ambazo mamlaka husika zimefanya na tathimini hizo zikapelekea kufanyika kwa maamuzi ya ujenzi wa reli ya kati kutoka Da es salaam hadi Mwanza badala ya kwenda Kigoma.

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Serikali kuanza kujenga Reli ya kati ya Dar es Salaam na Mwanza (kama taarifa inavyotolewa, japo kuwa Reli ya Kati ni Reli ya kutoka Dar es salaam kwenda mkoani Kigoma na si vinginevyo),unapaswa kuangalia vipaumbele vya maeneo ambayo shughuli za reli hiyo itasaidia kwa kuangalia takwimu ni wapi Serikali inapaswa kujenga reli ili mradi huu wa ujenzi wa reli uweze kuzalisha fedha za kujenga reli nyingine aukuliletea Taifa faida.

**Mheshimiwa Spika**, inavyoonekana tafsiri ya reli ya kati ambayo ilijulikana ni kutoka Dar es Salaam hadi Kigoma, reli nyingine inayounganishwa nayo inakuwa ni tawi la reli ya kaati na si vinginevyo. Kusema reli ya kati ni kutoka Dar mpaka Mwanza ni kupotosha tafsiri ya reli ya kati. Kwa muktadha huo Mheshimiwa Spika, ujenzi wa 'Standard Gauge' kwa hatua hizo za awali unaotoka Dar es salaam kwenda Mwanza ulipaswa kuwa ni ujenzi wa standard gauge kutoka jijni Dar es salaam kwenda mkoani kigoma.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa taarifa ya hali ya uchumi nchini ya mwaka 2015/2016, takwimu zinaonesha kwamba mizigo ambayo Tanzania inahudumia kwa nchi za maziwa makuu ni tani Milioni tano kwa mwaka. Katika hizo Zambia ni 34%, Kongo ni 34%, Rwanda12% Burundi 6% na Uganda ni 2.6%. Tafsiri yake ni kwamba Ujenzi wa ***'Standard Gauge'*** utakaotumia matrilion ya fedha wakati huo huo reli hiyo imeelekea Isaka na Mwanza maana yake ni kwamba reli hiyo itakayokuwa kwa kiwango cha standard gauge itahudumia 15% ya mizigo yote tunayoipitisha, kwa maana ya mizigo kutoka Rwanda na Uganda, wakati huo huo kama Taifa tumeacha kuhudumia mizigo 40% kwa maana ya mizigo inayotoka katika nchi za Kongo na Burundi ambayo yote inapita mkoani Kigoma.

**Mheshimiwa Spika**, mujibu wa aya ya 25 ya hotuba ya Waziri wa Fedha wakati akiwasilisha Bungeni Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2017/18 tarehe 8 Juni, 2017 ni kwamba nchi zinazofanya biashara na Tanzania kwa wingi katika bara la Afrika, ukiachilia mbali Afrika ya Kusini inayoongoza kwa asilimia 12.2; nchi inayofuatia ni Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ambayo ni asilimia 5.6 ikifuatiwa na Kenya kwa asilimia 5.5

**Mheshimiwa Spika,** kwa mantiki hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilitarajia Serikali ijenge reli ya Standard Gauge katika maeneo ya kimkakati kibiashara; na kwa maana hiyo reli ya kati ijengwe hadi Kigoma ili kuunganisha Tanzania na Congo DRC ambayo ni nchi ya kimkakati kibiashara, na pia

reli ya kaskazini ijengwe kwa standard gauge na iunganishwe na reli ya Mombasa – Nairobi iliyozinduliwa hivi karibuni kwa Kenya nayo ni nchi ya kimkakati kibiasahara.

Kambi Rasmi ya Bunge lako tukufu haipingi ujenzi wa reli ya kati kupitia Isaka – Mwanza, lakini inapendekeza Serikali ikamilishe kwanza ujenzi wa reli hiyo hadi Kigoma kwa kuwa kule kunza mzingo mwingi kutoaka DRC na kwa maana hiyo faida itapatikana haraka.

**Mheshimiwa Spika**, sambamba na ujenzi wa reli hii ya kati kwa kiwango cha standard gauge kuna fedha za Benki ya Dunia kwa ajili ya ukarabati wa reli, kiasi cha Bilioni 200, Kambi Rasmi ya Bunge lako Tukufu inasahauri kwamba, fedha hizi za ukarabati wa reli ambao upo kipindi hiki zipelekwe maeneo mengine ambayo ujenzi huu wa reli kwa kiwango cha standard gauge haufanyiki ili kuleta uwiano wa utekelezaji wa miradi hii ya reli.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani katika wasilisho lake la mwaka 2013 kuhusu bajeti ya Serikali ilipendekeza kuanzishwa kwa kodi maalum ***(Special Railways development levy)*** ya manunuzi na mauzo ya bidhaa nje. Tunapendekeza tozo ya asilimia moja (1 %) ya bei ya bidhaa zinazoagizwa toka nje na asilimia 0.5 (0.5%) ya thamani ya bidhaa kwa zile zinazouzwa nje. Mapato ya tozo hii maalumu yote yatumike kujenga miundombinu ya Reli hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, kitabu cha Mpango wa pili miaka mitano wa Maendeleo ukurasa wa 92 kuna wakfu(Fund) wa Maendeleo ya Reli ambao ulikadiriwa kwamba angalau asilimia 70 ya mtaji wake uwe ni kwaajili ya miradi ya Reli. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge ni kwa kiwango gani wakfu huo umeanza kazi na fedha zake zinatoka wapi na unaendeleaje kuongezeka?

## 23. MAMLAKA YA USAFIRI WA ANGA-TCAA

**Mheshimiwa Spika,** ni ukweli kwa mujibu wa sheria kwamba biashara yote ya usafiri wa anga hapa nchini inathibitiwa na kuongozwa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga. Mamlaka hii

iliundwa rasmi na kuanza kufanyakazi zake kwa mujibu wa sheria ya Bunge namba 10 ya mwaka 2003 ambayo ilifanyiwa marejeo mwaka 2006. Aidha, sheria hii ndiyo inaangalia kwa jinsi gani Sheria Namba 80 ya Usafiri wa Anga ya mwaka 1977 na kanuni zake zinazohusiana na masuala ya usafiri wa anga nchini zilizowekwa kwa lengo, hususan, kuhakikisha usalama katika matumizi ya vyombo vya usafiri wa anga sambamba na kulinda usalama wa umma na mali wakati wa matumizi ya vyombo husika.

**Mheshimiwa Spika,** kwa muktadha huu, ni dhahiri kwamba utendaji wa shirika letu la ndege unaathari za moja kwa moja na utendaji wa mamlaka hii ya usafiri wa anga. Kwani uendeshaji wa kampuni yoyote inayotoa huduma za usafiri wa anga ni lazima ithibitiwe na matakwa ya Mamlaka hiyo, hivyo kama mamlaka haina watendaji ambao wenye weledi wa kutosha katika tasnia ya usafiri na usafirishaji wa anga ni dhahiri hata kampuni inayotoa huduma itakuwa katika mtanziko wa kiutendaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali, katika kuhakikisha kuwa usafiri wa anga hapa nchini unaboreshwa ni lazima utendaji wa ofisi ya mdhibiti wa usafiri wa anga unakuwa na watu wanaoelewa kwa undani biashara nzima ya usafiri wa anga, na sio tu watendaji ambao walikuwa kwenye nafasi za juu katika wizara husika.

### 23.1. Kampuni ya Ndege Tanzania- ATCL

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa historia nzima ya uwepo wa shirika letu la ndege hadi sasa inafahamika vyema na kwa jinsi gani limehujumiwa na wale ambao ndio waliopewa dhamana na watanzania kuliangalia kwa niaba yao. Kwa muktadha wa hotuba hii itaweka zaidi wazi ni kwa jinsi gani uendeshaji wake ufanyike ili shirika letu liweze kuwa shindani katika medali za usafiri wa anga.

**Mheshimiwa Spika,** kabla ya kuangalia na kushauri naomba nitoe rejea kwa mashirika mengine ya usafirishaji ambayo yanafanya vizuri sana japokuwa yameanzishwa muda mfupi

kwa kulinganisha na shirika letu. Shirika la Ndege la Emirates, lilianzishwa rasmi mwaka 1985, hadi sasa shirika hilo lina jumla ya ndege 231 kati ya hizo ndege 68 ni aina ya Airbus, A.380 zinazobeba abiria 800. Lakini shirika lilianza biashara na ndege mbili (2). Katika kuonesha kuwa biashara ya ndege sio biashara ya kila mtu, wamiliki walimtafuta mtaalam wa uendeshaji masuala ya ndege raia wa Uingereza, Sir Maurice Flanagan ambaye ameliendesha shirika hilo hadi mwaka 2006 na akafariki May 2015.

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la ndege la Rwanda ambalo lilianza kufanyakazi rasmi mwaka 2002 na hadi sasa lina umri wa miaka 17 na lina jumla ya ndege 13 zinazofanyakazi na ndege nyingine moja inasubiriwa ili kuifanya idadi kuwa 14. Hoja ya msingi ni je wenzetu wamefanyaje mpaka shirika lao limefikia hapo lilipofikia?

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa shirika la ndege la Kenya ambalo muda wa uanzishwaji wake ni sawa na shirika letu. Hadi mwezi januari 2015 shirika hilo lilikuwa na ndege 6 Dreamliners B787-8 ambazo zinaenda kila siku Nairobi-London na hivyo kulifanya shirika hili kuongeza ndege zake kutoka 44 hadi kufikia 107 kwa kipindi cha miaka 10 kuanzia mwaka 2015, na hivyo shirika hilo kuwa na vituo (destinations) 115 kutoka vituo 62.

**Mheshimiwa Spika,** tukirudi kufanya ulinganisho na shirika letu la ndege ambalo lina umri sawa na wetu ni dhahiri kwamba bado tuna safari ndefu ili tuwakute wenzetu. Ni ukweli pia tunapanua uwanja wetu wa Julius Nyerere ili uweze kuwa shindani, lakini Kambi Rasmi ya Upinzani inasema ili Tanzania inufaike zaidi na uwanja huo ni lazima shirika letu liendeshwe kisasa zaidi, na mamlaka ya usafiri wa anga iwe na watendaji wenye taaluma na uzoefu wa kuendesha shughuli hizo.

**Mheshimiwa Spika,** ni ukweli pia wakati Mwalimu Nyerere anastaafu mwaka 1985 aliacha shirika likiwa na ndege 11 ikiwa ni; Douglas DC-9-32 ndege moja (1), Boeing 737 mbili(2), Fokker F 27 ndege nne(4), na Twin Otter DHC-6-300 ndege nne (4).

**Mheshimiwa Spika,** ndege hizo zote wajanja wamekunywa kama vijana wa mjini wanavyosema na hiyo itabakia kuwa ni historia kama ilivyoachwa na muasisi wa taifa hili.

### 23.2. Ukiukwaji wa Sheria katika Manunuzi ya Ndege

**Mheshimiwa Spika,** mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali kwa mujibu wa kitabu cha fedha za Maendeleo Volume IV Part A fungu 62 kasma **4294** ilitenga jumla ya shilingi **Bilioni 500** fedha za ndani kwa ajili ya kununua ndege za abiria kwa ajili ya shirika la Ndege la ATCL.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa hotuba ya waziri wa Fedha akiwakilisha taarifa ya hali ya uchumi ya mwaka 2016 na mpango wa maendeleo wa mwaka wa fedha 2016/17 ameeleza kuwa serikali imeshasaini mkataba wa ununuzi wa ndege nyingine 4 na malipo ya awali ya dola milioni 56.89 ambayo ni sawa na **shilingi 126,125,130,000.**

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inataka serikali itoe taarifa kamili juu ya masuala yafuatayo kuhusu ndege ambazo zimenunuliwa na zile zinazotegemea kununuliwa;

(i) Je mradi wa ununuzi wa ndege utagharimu kiasi gani cha fedha mpaka ndege zote zitakapowasili nchini?

(ii) Utaratibu upi uliotumika kuagiza ndege hizo kwa mujibu wa sheria ya manunuzi ya umma?

(iii) Je, kiasi cha dola milioni 56.89 kilichotumika kulipia malipo ya awali kilitengwa kutokana na fedha zipi za Bajeti kwa mujibu wa sheria?

(iv) Je, serikali ilitumia utaratibu gani mpaka kuamua kuchagua kampuni ambazo imeamua kuingia nazo mikataba ya ununuzi wa ndege?

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kutoa majibu ya mambo tuliyoyaainisha kwa sababu bila kutoa taarifa za kina kuhusu mradi huu wa ndege, mashaka

yatakuwa makubwa kuhusu matumizi hayo ya fedha nyingi za walipakodi.

**Mheshimiwa Spika**, utaratibu unaotumika kwa sasa duniani sio kununua ndege kwa fedha taslimu za walipakodi kama ambavyo serikali ya CCM inafanya, bali serikali huingia makubaliano na kampuni zinazozalisha ndege ambapo kwa kushirikiana na sekta binafsi ndege zinaanza kufanya biashara na kujilipa kutokana na faida inayopatikana. Utaratibu huu wa kuondoa mabilioni ya fedha kwenda nje ya nchi yetu unaathiri si mzunguko wa fedha ndani ya nchi bali pia huathiri miradi mingi ya huduma za jamii.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuweka wazi kuwa ni lazima ATCL iendeshwe kwa weledi na watu ambao wanajua kufanya biashara ya usafiri wa anga kuliko kutegemea kila mara kupokea maelekezo ya viongozi wa serikali ambao pengine hawana uelewa wa kutosha wa kuendesha biashara hiyo. Haitashangaza kuona ATCL inafanya biashara kwa hasara kuliko mategemeo ya sasa kwa sababu ya kuchanganya siasa na utendaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa ndege hizo ni mali ya Serikali na hivyo ndege hizo zinakodishwa kwa Kampuni ya ATCL na ATCL inatakiwa kulipa kiasi cha dolla za kimarekani 160,000 sawa na takriban shilingi 360,000,000/= kila mwezi na kwa mwaka shilingi 4,320,000,000/=, na kiasi kinachobakia kinauwezo wa kuifanya kampuni kurejea kwenye ushindani, kwa kuajili wataalam wabobezi wa masuala ya uendeshaji shughuli za usafiri wa anga au mambo ni yale yale ya Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kuteua anaohisi wanaweza. Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kwamba, kwa kuwa Kampuni ndio kwanza inaanza kutambaa ni kwani fedha hizo inazoilipa Serikali kila mwezi zisilipwe baada ya miaka mitano ambapo tayari itakuwa imesimama?

**Mheshimiwa Spika,** ni ukweli kwamba ATCL inakabiliwa na matatizo mengi sana. Miongoni mwa matatizo hayo ni pamoja na:-

**i. Kushindwa Kupata Vyeti Muhimu vya Usafiri wa Anga**
ATCL inatakiwa kuweke utaratibu wa kuwajengea uwezo watumishi au kuwajiri watumishi wapya wenye sifa stahiki pamoja na kuwa na mpango wa kurithishana ujuzi kwa nafasi muhimu za uongozi wa Shirika ili kuwa na watumishi wasomi, wazoefu, waliohamasika na wenye uwezo wa kukabiliana na ushindani katika soko linalokuwa kwa kasi la usafiri wa anga. Kwa njia hiyo ATCL inatakiwa kupata vyeti vyote kutoka Mamlaka ya Usafiri wa Anga ya Kimataifa (IATA) pamoja na ukaguzi wa usalama wa usafiri wa anga. Kulingana na taratibu na kanuni za uendeshaji wa makampuni yote ya ndege kufuata taratibu za usalama za usafiri wa anga.

**ii. Kukosekana kwa Mkakati Mahususi wa Kufufua Shirika**
ATCL inatakiwa kuwa na mkakati utakaoiwezesha kurudi katika hali nzuri ya kifedha kwa kufanya tathmini ya kina kubaini sababu na matatizo yaliyopelekea kuwa na matatizo ya hali ya kifedha iliyopo, pamoja na kuboresha mifumo na namna ya kuendesha biashara hiyo ili kuwa na Shirika jipya lenye ufanisi na kujiendesha kwa faida. Mwezi April, mwaka huu, Mkurugenzi Mtendaji wa ATCL, Ladislaus Matindi, alinukuliwa akisema shirika lake limefanikiwa kukusanya Sh Bilioni 9 kwa Miezi minne tu kwa kutumia ndege mbili za Bombardier.

**Mheshimiwa Spika,** hii inatokana na ukweli kwamba, ATCL hadi sasa bado halifanyi kazi kama Kampuni ya biashara badala yake linatoa huduma, mfano mzuri ni pale linaposhindwa kutunza muda wa ndege zake kuruka mapema au kuchelewa na kulazimika kuwakodishia abiria wake ndege zingine zenye gharama/bei au nauli kubwa kulinganisha na nauli inayotozwa na kampuni hiyo.

**24. UFANISI WA BANDARI NA MCHANGO WAKE KATIKA UCHUMI**
**Mheshimiwa Spika,** ni ukweli kwamba uwezo wa bandari yetu katika kuhudumia meli kubwa bado ni duni sana na jambo hilo halina ubishi kutokana na takwimu zilizopo.

Jambo hili linapelekea kwa kiasi kikubwa meli kubwa kushindwa kutia nanga hapa nchini kwetu na badala yake kwenda Bandari za Beira na Mombasa.

**Mheshimiwa Spika**, uwezo wa bandari yetu ni kupokea meli zenye uwezo wa deadweight tonnage (DWT) 4.1 million "dry cargo" na DWT 6.0 million "bulk liquid cargo". Kwa mujibu wa "Port master plan 2008-2028" inaonesha kuwa kulikuwa na mkakati wa kuongeza ufanisi na upitishaji wa mizigo kwa 30% toka tani 13.5milioni kwa mwaka 2013 hadi tani 18milioni mwaka 2015. Katika kufikia hapo uwekezaji mkubwa ulitakiwa kufanyika katika milango ya kuingizia meli na maegesho yake. Ukweli ni kwamba uwekezaji uliotakiwa hadi sasa haujafanyika.

**Mheshimiwa Spika,** bandari ya Dar es Salaam ni fursa muhimu ya kijiografia kwa nchi yetu, kutokana na mataifa yaliyotuzunguka kutokuwa na huduma hiyo wakati huo huo yanazo raslimali za kutosha kusafirishwa kwenda nje ya nchi. Tukumbuke kwamba biashara ni muda, ukishindwa kuupima muda basi muda huo utakupima wewe.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ya awamu ya nne kwa kuliona jambo hilo, iliingia makubaliano na Exim Bank ya China ili kupata mkopo kwa ajili ya kupanua lango na kujenga gati namba 13 na 14 lakini cha kushangaza hadi sasa ujenzi huo haujaanza. Wakati sisi tukishindwa kuchukua hatua, jirani zetu wa Kenya wamemaliza ujenzi wa gati namba 19 ya bandari ya Mombasa na bandari hiyo inafanyakazi. Katika kuonesha kuwa wako mbele zaidi kulinganisha na sisi Reli yao ya Standard Gauge ya kuanzia Mombasa kwenda Nairobi hadi Kampala imeanza kazi rasmi.

**Mheshimiwa Spika,** meli za mizigo zinaongezeka ukubwa na uwezo wa kubeba mizigo kulingana na imetengenezwa lini (Generations), hapa inaonesha jinsi muda wa utengenezaji meli unavyokwenda sambamba na ukubwa pamoja na uwezo wa kubeba mizigo. Bandari yetu inauwezo wa kuingiza meli za Generations 1 hadi 3.

| Generations | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Generation | Years | Type | Length | Draught | TEU's |
| 1st Gen. | 1956-1970 | Converted GCS/Tanker | 135-200 m | 9 m | 500-800 |
| 2nd Gen. | 1970-1980 | Cellular | 215 m | 10 m | 1000-2500 |
| 3rd Gen. | 1980-1988 | Panamax | 250-290 m | 11-12 m | 3000-4000 |
| 4rt Gen. | 1988-2000 | Panamax | 275-305 m | 11-13 m | 4000-5000 |
| 5th Gen. | 2000-2007 | Post-Panamax | 335 m | 13-15 m | 5000-8000 |

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kufahamu ni kwanini Serikali ya CCM inakuwa na kigugumizi kuanza ujenzi wa gati 13 na 14 wakati mradi tayari ulishapatiwa fedha tangu Mei, 2012, na hadi sasa utekelezaji haujaanza. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaka kufahamu inapotokea kuvunjwa kwa mkataba wa kupata mkopo pande husika inatakiwa kufidia vipi hasara iliyopatikana?

**Mheshimiwa Spika,** imetulazimu kuomba ufafanuzi huo kutokana na ukweli kwamba, mikataba inaingiwa na Serikali na baadae hatupatiwi mrejesho wa utekelezaji. Mfano mzuri ni ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo. Kuingiwa na kuvunjwa maana yake walioshiriki hawakuangalia maslahi ya nchi? Na kama ndivyo hivyo ni kwanini hatujasikia wakiwajibishwa kwa hilo?

**Mheshimiwa Spika,** juhudi zinazofanyika sasa hivi bandarini ni za kuongeza ufanisi wa kazi tu, jambo ambalo kwa upande wa kuingiza meli kubwa halitahusika, jambo hilo lilitakiwa kwenda sambamba na mpango wa upanuzi wa Gati na 13 na 14.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo juhudi za kuongeza ufanisi haziendani na uhalisia wa ushindani wa kibishara baina ya nchi yetu na washindani wetu katika miundombinu ya Bandari. Mfano:

1. Mgongano wa tozo za uhifadhi wa mzigo ambapo TRA wanatoza storage na TPA wanatoza Custom warehouse rent. Hiki ni kitu kile kile.

2. Tozo ya dola za kimarekani 23 kwa tani moja ya mzigo wa shaba ambapo bandari ya Durban kwa mzigo huohuo wa uzito huo wanatoza dola 17.86

3. Tozo kubwa kwa mizigo yote inayokwenda Zambia, kwa mfano kasha la urefu wa futi 40 linatozwa dolla 530, badala ya dolla 320 ambazo hutozwa kwa mzigo kwenye kasha la urefu wa futi hizo hizo kwa mzigo unaokwenda Rwanda na Burundi.

4. Single Custom Territory (Himaya ya Forodha) ambapo nchi ya DR-Congo (nchi na wafanyabiashara) inatumia bandari yetu kwa mizigo yote inayokwenda nchi hiyo. Lakini kitendo hicho wafanyabiashara wa DR-Congo wanaona kuwa ni gharama kwa biashara zao na hivyo kulazimika kuhama bandari na kuhamia bandari za Beira, Durban au Mombasa. Hii inatukosesha mapato ambayo yangelipwa na wafanyabiashara toka DRC kwa kigezo tu cha kufanya kazi ya mamlaka ya Mapato ya DRC.

5. Bandari yetu inatoa "grace period of transit of bulk liquid" fupi sana ya siku 30 kwa kulinganisha na washindani wetu wanaotoa siku 60 hadi 90.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuyafanyika kazi mapungufu hayo ya kimfumo ili ufanisi katika badari yetu uweze kuonekana. Kinyume cha hapo tutafukuza matendaji wote na kuleta wapya kwani matokeo hayatonekana.

**aidha,** kitendo cha kushindwa kupanua ukubwa wa maegesho kwa meli kubwa ni dhahiri hata ujenzi wa Reli kwa kiwango cha kimataifa bado **"economic viability"** yake inatia mashaka. Kwani ujenzi wa Reli kwa standard gauge lengo kubwa ni kuhakikisha inachukua mzigo mkubwa toka

ndani na nje ya mipaka ya nchi yetu, na mzigo huo uweze kuingizwa moja kwa moja kwenye meli zinazolingana na mizigo husika.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kutathmini upya mkakati wake wa uwekezaji katika Reli ya Kati ikienda sambamba na upanuzi wa bandari ya kisasa itakayokuwa na uwezo wa kuhudumia mizigo mingi, kwani gharama za ujenzi wa reli zitalipwa kwa reli kupokea mizigo mingi kupitia bandari.

## 25. MRADI WA UJENZI WA RELI YA KATIKA KWA KIWANGO CHA KIMATAIFA – STANDARD GAUGE:

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua umuhimu wa mchango wa usafiri wa reli katika kukuza uchumi wa taifa. Aidha, hapinngi ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha Kimataifa – Standard Gauge kutokana na umuhimu wake katika kuchochea ukuaji wa uchumi. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inapata shida kuelewa ni kwa nini Serikali kutekeleza mradi huo kwa kutumia kampuni yenye bei ya juu na kuacha iliyokuwa tayari kujenga reli hiyo kwa gharama za chini.

**Mheshimiwa Spika,** Ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa (standard gauge) kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza, unatarajia kukamilika mwaka 2021 na utagharimu Sh trilioni 17.6. Kwa kujenga jumla ya kilometa 2400 kwa mujibu wa mkataba na Wachina na ikalazimu Serikali kupata mkopo wa riba nafuu toka benki ya Exim ya China. Mkataba na Waturuki wa ujenzi wa kipande cha kilomita 205 kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro, na tayari ujenzi huo umeshawekewa jiwe la msingi na unakadiriwa kugharimu dola za Marekani bilioni1.21 (Sh trilioni 2.6).

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inataka majibu sahihi ni kwanini hasa mkataba nafuu wa Wachina wa trilioni 17.6 ambapo kilometa moja ilitakiwa kujengwa kwa dola bilioni 3.16 ulivunjwa na Serikali ikaingia mkataba na Waturuki

ambao ni ghali wa kujenga kilometa moja kujengwa kwa bilioni 5.8?

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hiyo ilieleza kuwa ujenzi huo utakamilika mwaka 2021 kutokana na mfumo unaotumika wa kutoa zabuni kwa vipande vipande badala ya kutoa zabuni yote kwa kampuni moja. Alisema mfumo huo unapunguza muda wa ujenzi kutokana na kampuni nyingi kufanya kazi hiyo kwa wakati mmoja, lakini ikitokea kampuni inayojenga ikaomba tenda na kushinda na ikabainika kuwa na uwezo wa kufanya shughuli hiyo kwa wakati, itapewa zabuni.

**Mheshimiwa Spika**, awamu nyingine itahusisha vipande vya Morogoro hadi Makutupora kilomita 336, Makutupora-Tabora (km 294), Tabora-Isaka (km 133) na Isaka-Mwanza (km 248). huku Serikali katika bejeti yake, serikali ikiwa imetenga kiasi cha shilingi trioni 1 kwa ajili ya ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha standard gauge.

**Mheshimiwa Spika**, Sababu kubwa za kujenga reli ya kati kwa kiwango cha standard gauge ni sababu za kiuchumi ambazo lazima zizingatiwe kwa kiwango ambacho kitaliwezesha taifa kupata faida. Kwa mantiki hiyo bado kuna sintofahamu katika tathimini ambazo mamlaka husika zimefanya na tathimini hizo zikapelekea kufanyika kwa maamuzi ya ujenzi wa reli ya kati kutoka Da es salaam hadi Mwanza badala ya kwenda Kigoma.

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa serikali kuanza kujenga Reli ya kati baina ya Dar es Salaam na Mwanza (kama taarifa inavyotolewa, japo kuwa Reli ya Kati ni Reli ya kutoka Dar es salaam kwenda mkoani Kigoma na si vinginevyo),unapaswa kuangalia vipaumbele vya maeneo ambayo shughuli za reli hiyo itasaidia kwa kuangalia takwimu ni wapi serikali inapaswa kujenga reli ili mradi huu wa ujenzi wa reli uweze kuzalisha fedha za kujenga reli nyingine ama kulíletea Taifa faida.

**Mheshimiwa Spika**, inavyoonekana serikali ni kama serikali imesahau tafsiri mpya ya reli ya kati, au inafanya kwa makusudi, kwa kuweka sawa kumbukumbu, ukisema reli ya

kati tafsiri yake ni kwamba unazungumzia reli ya kutoka mkoani Kigoma hadi jijini Dar es salaam au kutoka jijini Dar es salaam hadi mkoani Kigoma na maeneo mengine yote ni matawi ya reli ya kati. Kwa muktadha huo Mheshimiwa Spika, ujenzi wa 'Standard Gauge' kwa hatua hizo za awali unaotoka Dar es salaam kwenda Mwanza ulipaswa kuwa ni ujenzi wa standard gauge kutoka jijni Dar es salaam kwenda mkoani kigoma.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa taarifa ya hali ya uchumi nchini ya mwaka 2015/2016, takwimu zinaonesha kwamba mizigo ambayo Tanzania inahudumia kwa nchi za maziwa makuu ni tani Milioni tano kwa mwaka. Katika hizo Zambia ni 34%, Kongo ni 34%, Rwanda12% Burundi 6% na Uganda ni 2.6%. Tafsiri yake ni kwamba Ujenzi wa ***'Standard Gauge'*** utakaotumia matrilion ya fedha wakati huo huo reli hiyo imeelekea Isaka na Mwanza maana yake ni kwamba reli hiyo itakayokuwa kwa kiwango cha standard gauge itahudumia 15% ya mizigo yote tunayoipitisha, kwa maana ya mizigo kutoka Rwanda na Uganda, wakati huo huo kama Taifa tumeacha kuhudumia mizigo 40% kwa maana ya mizigo inayotoka katika nchi za Kongo na Burundi ambayo yote inapita mkoani Kigoma.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Bunge lako tukufu inataka kupata majibu kutoka serikalini, ni utaalamu gani na au upembuzi upi wa kiuchumi umetumika hadi kufikia maamuzi ya kujenga reli hii kwa kiwango cha ***standard gauge*** kwenda Isaka hadi Mwanza sehemu ambazo kwa takwimu za serikali yenyewe, zinaonesha kwamba haziwei kuleta faida kwa Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, sambamba na ujenzi wa reli hii ya kati kwa kiwango cha standard gauge kuna fedha za Benki ya Dunia kwa ajili ya ukarabati wa reli, kiasi cha Bilioni 200, Kambi Rasmi ya Bunge lako Tukufu inasahauri kwamba, fedha hizi za ukarabati wa reli ambao upo kipindi hiki zipelekwe maeneo mengine ambayo ujenzi huu wa reli kwa kiwango cha standard gauge haufanyiki ili kuleta uwiano wa utekelezaji wa miradi hii ya reli.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani katika wasilisho lake la mwaka 2013 kuhusu bajeti ya Serikali ilipendekeza kuanzishwa kwa kodi maalum ***(Special Railways development levy)*** ya manunuzi na mauzo ya bidhaa nje. Tunapendekeza tozo ya asilimia moja (1 %) ya bei ya bidhaa zinazoagizwa toka nje na asilimia 0.5 (0.5%) ya thamani ya bidhaa kwa zile zinazouzwa nje. Mapato ya tozo hii maalumu yote yatumike kujenga miundombinu ya Reli hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, kitabu cha Mpango wa pili miaka mitano wa Maendeleo ukurasa wa 92 kuna wakfu(Fund) wa Maendeleo ya Reli ambao ulikadiriwa kwamba angalau asilimia 70 ya mtaji wake uwe ni kwaajili ya miradi ya Reli. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge ni kwa kiwango gani wakfu huo umeanza kazi na fedha zake zinatoka wapi na unaendeleaje kuongezeka?

## 26. KUSAHAULIKA KWA SEKTA YA AFYA KATIKA MAENDELEO YA UCHUMI

**Mheshimiwa Spika,** katika bajeti hii ya serikali suala la afya halijapewa kipaumbele kabisa.Hii inaonyesha wazi kabisa bajeti hii ni ya ajabu kabisa na haijawahi kutokea. Ni ajabu kuona serikali hii haifahamu kuwa afya ndio msingi wa maendeleo ya taifa lolote duniani. Hakuna taifa lililowahi kuendelea kiuchumi pasipo kuwekeza kwenye afya ya wananchi wake.Hakuna uchumi bora bila kuwa na watu wenye afya bora. Maendeleo ya viwanda, kilimo, elimu,nishati, miundombinu na michezo yanaweza kufikiwa endapo tu nchi ina mifumo bora ya utoaji wa huduma za afya na wananchi wake wana uhakika wa maisha **.**

**Mheshimiwa Spika,** katika bajeti hii ambayo serikali imejigamba ni bajeti ya wananchi imeshindwa kuonyesha unaafuu katika suala la upatikanaji wa huduma ya afya ambalo ni suala linalogusa maisha ya kila Mtanzania wa kila rika, jinsia, rangi n.k. Afya huunganisha taifa. Lakini cha ajabu ni kuwa bei za vipimo mbalimbali kama vile CT-Scan vimekuwa ni vya gharama sana na hivyo kutokana na wananchi wengi kushindwa kumudu gharama za vipimo

hivyo wengi wamepoteza maisha.Nchi hii imekuwa na gharama kubwa sana katika ununuzi wa vifaa tiba jambo linalowafanya hata wawekezaji wa ndani kushindwa kuwekeza vya kutosha katika sekta hii ya afya. Vilevile, kumekuwa na urasimu mkubwa katika kufungua viwanda vya kutengeneza dawa hapa nchini pamoja na tozo nyingi zisizokuwa na tija badala ya kutoa unaafuu na kutengeneza mazingira wezeshi ili dawa hizi zipatikane moja kwa moja hapa nchini na kupunguza mzigo mkubwa kwa serikali katika kununua madawa nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika,tunapoteza nguvu kazi kubwa ya taifa kutokana na vifo visivyo vya lazima kwa sababu tu ya kukosekana kwa vifaa tiba,wataalamu na madawa. Mfano; kwa mujibu wa matokeo ya utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria wa Mwaka 2015-2016 (Tanzania Demographic and Health Survey and Malaria Indicator Survey) inaonyesha kuwa kati ya watoto 1,000 chini ya umri wa miaka mitano watoto 67 hufariki. Hii ina maana kwamba kati ya hao 67 wanaofariki tunapoteza nguvu kazi kama wataalamu,walipa kodi, tunapunguza pato la taifa na zaidi tunapunguza juhudi zetu katika kukuza uchumi.

**Mheshimiwa Spika**, sambamba na hilo bajeti hii haijagusa ipasavyo afya ya wanawake na watoto wa kike (women and girls) licha ya kuwa ndio kundi lenye wapiga kura wengi nchini . Kundi hili hukabiliwa na changamoto lukuki za kiafya ikilinganishwa na makundi mengine (most vulnerable group). Watoto wa kike wamekuwa wakitaabika sana wakati wa hedhi. Wengi wao wakilazimika kukatisha masomo, kupata msongo wa mawazo na hivyo kuathiri kabisa kiwango cha ufaulu kwa watoto wa kike. Wengi wa watoto hawa wamekuwa wakitumia vitu mbalimbali katika kujihifadhi na wengine wakilazimika kutumia vitambaa au matambara ambayo ni hatari kwa afya zao hususani kwenye via vya uzazi.

**Mheshimiwa Spika**, kupunguza kodi kwenye taulo za kike (sanitary pads) kungeweza kabisa kuwasaidia wanawake walio wengi kuendelea kufurahia uanamke wao,kujisikia huru na kufanya kazi za uzalishaji vizuri na hata kuongeza kiwango

cha ufaulu kwa walio mashuleni.Mpaka sasa bei ya taulo hizi za kike hugharimu kuanzia shilingi 2,500 mpaka shilingi 5,000. Wakati mwingine wanawake hulazimika kutumia pedi zaidi ya moja kutokana na wingi wa hedhi na hivyo kila mwezi anahitaji kuanzia 5,000- 8,000 /-ili kujisitiri.

**Mheshimiwa Spika,** gharama hii ni kubwa sana. Tafiti zinaonyesha ni 11 % tu ya wanawake waliofikia umri wa kupata hedhi wana uwezo wa kutumia taulo hizi maalum za hedhi, Kwa mujibu wa gazeti la the citizen la tarehe 10 June ,2017 lenye kichwa cha habari ***"Women decry levy on sanitary towels***" imeeleza kwa kina umuhimu wa serikali kupunguza kodi katika taulo za kike kwani pia taulo hizi zinategemewa sana na kina mama pale wanapojifungua.

**Mheshimiwa Spika,** badala ya Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kupiga makofi kishabiki ni lazima sasa kama taifa kuweka ukada pembeni na kuchambua kwa kina bajeti hii kwa kuangalia sekta muhimu zinazogusa maisha ya kila Mtanzania na makundi mbalimbali. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kupitia upya bajeti yake na kuzingatia mambo ya msingi hususani kwenye sekta ya afya kwani bila mfumo bora wa utoaji wa huduma na unaafuu wa upatikaji wa huduma za afya, tujue wazi hakuna nguvu kazi yenye afya na kwa maana hiyo uzalishaji utapungua na hivyo kuathiri ukuaji wa uchumi.

## 27. SEKTA YA MAFUTA NA GESI ASILIA

**Mheshimiwa spika**, katika historia ya Tanzania, tafiti za uchimbaji wa mafuta na gesi asilia zilianza mwaka 1952. Mafanikio ya shughuli za utafiti kwa mara ya kwanza yalipatikana miaka 22 baadaye ambapo mwaka 1974 gesi asilia iligunduliwa Songo Songo, katika mkoa wa Lindi. Baadaye, mwaka 1983 ugunduzi mwingine ulifanyika katika eneo la Mnazi katika mkoa wa Mtwara.Tokea wakati huo, shughuli madhubuti za utafiti wa uchimbaji ulikuwa ukiendelea na ilipofika Juni, 2015 ugunduzi wa gesi asilia ulikadiriwa kuwa trilioni za ujazo 55.08.

**Mheshimiwa spika**, mfumo wa udhibiti katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia hapa Tanzania unasimamiwa na Sheria ya Petroli ya mwaka 2015 ambayo imechukua nafasi ya Sheria ya Utafiti na Uzalishaji wa Petroli ya mwaka 1980 sura ya 328 kama ilivyorejewa mwaka 2002. Sheria zingine zinazotumika katika sekta ya mafuta na gesi kwa shughuli za uchimbaji kwenye mkondo wa juu ni Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, na Sheria ya Ushindani ya mwaka 2003.

**Mheshimiwa spika**, Hivi sasa, Tanzania imepitisha sheria tatu mpya ikiwa ni pamoja na Sheria ya Petroli ya mwaka 2015, Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi ya mwaka 2015 na Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika Shughuli za Utafutaji wa Mafuta, gesi asilia na madini Tanzania ya mwaka 2015, aidha ilielezwa kuwa lengo la sheria hizo ni kuboresha ubora wa usimamizi wa huduma, na shughuli katika sekta ya mafuta na gesi kwa maslahi ya Tanzania na watu wake.

**Mheshimiwa spika,** Sekta ya mafuta na gesi inajumuisha shughuli na taratibu mbalimbali ambazo kwa pamoja zinachangia mabadiliko ya rasilimali ya awali ya mafuta ya petroli na mwishowe kuwa bidhaa inayoweza kutumika na yenye thamani kwenye viwanda na watu binafsi. Shughuli hizi tofauti kwa asili yake zinahusiana (kinadharia, kimkataba, na/au kivitendo/kiutekelezaji), na mahusiano haya hutokea ndani ya makampuni binafsi, na pia ndani ya nchi au yanaweza kuvuka mipaka ya kitaifa.

### 27.1. Ushirikishwaji wa Wadau katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia Tanzania:

**Mheshimiwa spika,** Kuna wadau wakubwa kadhaa katika usimamizi wa sekta hii ya mafuta na gesi asilia Tanzania. Wadau hawa wamegawanyika katika makundi mbalimbali yakiwemo taasisi binafsi, makampuni ya kimataifa ya mafuta pamoja na taasisi zinazotoa huduma katika sekta hii. Aidha serikali kama mdau mkubwa kupitia Wizara ya Nishati na Madini, ina wajibu wa kusimamia sekta ya mafuta na gesi asilia nchini. Mbali na wajibu huu, Wizara ina kazi ya

kutengeneza na kupitia upya sera na kanuni katika sekta ya mafuta na gesi asilia nchini. Taasisi nyingine za uangalizi ni pamoja na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania, Baraza la Kitaifa la Usimamizi wa Mazingira, Mamlaka ya Usimamizi wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Hizi ni taasisi za serikali ambazo zina wajibu wa kusimamia shughuli za kila siku za makampuni ya kimataifa ya mafuta, mazingira, usalama na afya mahali pa kazi, pamoja na kusimamia mapato.

**Mheshimiwa spika**, kwa upande mwingine Makampuni ya Mafuta ya Kimataifa kama wadau mhimu kwenye sekta hii, hufanya shughuli zinazohusiana na mafuta katika maeneo ya mikataba kulingana na sheria zinazokubalika, pia kulingana na sheria za utendaji za kimataifa. Aidha kuna taasisi zinazotoa huduma katika Sekta hii kama vile Wizara ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia, na Wizara ya Kazi. Wizara hizi kwa kupitia taasisi zake za mafunzo kama vile vyuo, na vyuo vya ufundi na usanifu zina wajibu wa kujenga uwezo wa Watanzania ili waweze kushiriki na kujihusisha na uchumi wa mafuta na gesi asilia. Aidha, zinapaswa kulinda ushiriki wa wenyeji na kutekeleza sheria za kazi katika sekta hii.

## 27.2. Upotevu wa Fedha Zinazotokana na Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia.

**Mheshimiwa spika,** Taarifa ambazo kambi rasmi ya bunge lako tukufu inazo zinaonesha kwamba utekelezaji wa masharti ya ushirikishaji wa wazawa na uhakiki wa gharama rejeshwa katika makubaliano ya kugawana mapato ni hafifu na kuna hatari ya kutopata manufaa ya kutosha yatokanayo na ugunduzi wa mafuta na gesi asilia. Athari ya jambo hili mheshimiwa spika ni kupungua kwa mapato ya serikali kunakotokana na ushiriki hafifu wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) katika biashara ya mafuta na gesi asilia katika hatua ya uzalishaji. Taarifa zinaonesha kuna makubaliano ya mgawanyo wa mapato ambayo yanawapa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania fursa ya kushiriki katika biashara ya mafuta na gesi. Aidha makubaliano ya

Kugawana Mapato yanaruhusu ushiriki wa kati ya 5%-20% wakati wa kipindi cha uzalishaji na zaidi ya hapo ili mradi tu wachangie mtaji unaohitajika kuwekeza katika mradi husika.

**Mheshimiwa spika**, Ili kuhakikisha kwamba Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) linashiriki katika makubaliano yote ya kugawana mapato katika hatua ya uzalishaji, Shirika lilitakiwa kujumuisha kipengele hicho katika mikakati, mipango, na bajeti zake. Katika mantiki hiyo hiyo, Wizara ya Nishati na Madini kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha ilitakiwa kutoa msaada unaohitajika kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli ili kupata mtaji unaohitajika kuweza kujiingiza katika kila Makubaliano ya Kugawana Uzalishaji wakati uzalishaji wa kibiashara unapoanza.

**Mheshimia spika**, ushiriki wa TPDC usioridhisha kunako tokana na kutofanyika kwa uhakiki wa gharama rejeshwa kunasababisha kupotea kwa mapato yanayotokana na mafuta na gesi . Kulingana taarifa za Mkataba wa Makubaliano ya Mgawanyo wa Uzalishaji, Shirika la Maendeleo ya Mafuta (TPDC) linatakiwa kufanya uhakiki wa gharama rejeshwa za kila Mkataba katika kipindi cha ndani ya miaka miwili baada ya kufungwa kwa mwaka unaohusika. Pamoja na kutakiwa kufanya hivyo, taarifa ambazo kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo, zinaonesha kwamba, gharama rejeshwa zilizorekodiwa na makampuni ya mafuta na gesi zinazofikia kiasi cha dola za Kimarekani Bilioni 1.5 hazijahakikiwa hadi sasa.

**Mheshimiwa spika**, Uchambuzi zaidi unaonesha kwamba takribani dola za Kimarekani Bilioni 1.5 zilikuwa ni gharama rejeshwa zisizohakikiwa kwa kipindi kirefu, na hii maana yake mheshimiwa spika ni kwamba, gharama hizo ambazo hazihakikiwi zinasababisha serikali kupoteza mapato yatokanayo na mafuta na gesi, kwa sababu mapato hukusanywa baada ya marekebisho ya gharama rejeshwa kama sehemu ya gharama.

### 27.3. Madhaifu ya Mamlaka ya Mapato Kukadiria na Kukusanya Mapato katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia.

**Mheshimiwa spika,** yapo mapungufu yanayotokana na uwezo wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kukadiria na kukusanya mapato yatokanayo na kodi katika sekta ya mafuta na gesi asilia. Taarifa zinaonesha Mamlaka haina taratibu zinazowataka wakaguzi wa kodi kupima uhalali na uhakika wa taarifa kutoka vyanzo vingine mbali na taarifa kutoka kwa walipa kodi. Hii ni maana yake ni kwamba maafisa hao hulazimika kutumia taarifa anazotoa mlipa kodi mwenyewe bila kwa kuwa na utaratibu wa kutosha wa kutumia taarifa kutoka vyanzo vingine ili kujazia ushahidi ambao haukuonekana kwenye taarifa ya mlipa kodi.

**Mheshimiwa spika,** Kambi Rasmi ya Bunge lako tukufu inazotaarifa kuwa Mamlaka ya Mapato bado haijaunda mfumo wa taarifa ambao unasaidia katika ukaguzi wa kodi. Vilevile, taasisi hii haijabuni mfumo wa habari na mawasiliano ambao utasaidia wakaguzi wa kodi katika kutumia taarifa zinazopatikana ndani ya nchi hususani katika taasisi za serikali. Pamoja na hayo, Mamlaka yaMapato haina kanzidata yenye taarifa za kiasi cha hasara kilichopitishwa kutoka kwa makampuni ya mafuta na gesi asilia yaliyokadiriwa kodi .

**Mheshimiwa spika,** Mbali na uwepo wa taasisi mbalimbali za Serikali ambazo zinakusanya taarifa ambazo zinaweza kutumika kwa makadirio ya kodi za aina mbalimbali, Mamlaka ya Mapato haijawahi kufanya utafiti kuona njia zinazoweza kutumia vyanzo hivi katika makadairio ya kodi wanazokusanya. Taarifa ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo ni kwamba, mfumo wa taarifa uliopo umejikita zaidi katika kusaidia ukokotoaji wa kodi katika biashara za kunua na kuuza nje ya nchi pamoja na ukaguzi wa miamala ambayo haiakisi bei halisi ya soko. Huduma hii inatolewa na Kitengo cha Kodi za Kimataifa chini ya Idara ya Walipakodi Wakubwa.

**Mheshimiwa spika**, kambi Rasmi ya bunge lako tukufu inaona kwamba matatizo yaliyo ainishwa ni matokeo ya sera mbovu na mikakati isiyo endelevu ambavyo vinachangia kudidimiza sekta ya Gesi Asilia na Mafuta huku watanzaia wengi waliokwenye lindi zito la umasikini wakipewa matumaini hewa ya kunufaika na rasilimali hizi. Kwa mukitadha huo, Kamabi Rasmi ya Bunge hili inaitaka serikali kupitia taasisi zake kuacha uzembe unaosababisha Taifa kukosa mapato na kudidimiza uchumi wa nchi. Aidha mamlaka ya Mapato nchini lazima wawe na uwezo wa kufanya tathimini ya mlipa kodi kwa kuangalia pia taarifa nyingine nje na zinazotolewa na mlipa kodi mwenyewe.

**Mheshimiwa spika,** Pamoja na hayo, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini lazima iwe na miongozo ya ufuatiliaji na tathmini kwa lengo la kuelewa maeneo yanayohitaji maboresho zaidi katika utekelezaji wa mpango wa uendelezaji wa mtaji wa rasilimaliwatu. Hatuwezi kunufaika na rasilimali zetu ikiwa hatuna rasilimali watu wenye uwezo na weledi wa kutosha kwenye sekta ya Gesi asilia na Mafuta. Ikumbukwe kwamba uzalishaji wa wataalamu katika sekta ya mafuta na gesi asilia ni jambo moja lakini pia serikali kuhakikisha inaondoa tatizo la upungufu wa fedha na kuandaa miongozo ya ufuatiliaji ni jambo la pili, ili kuhakikisha kwamba shughuli za ufutiliaji na tathmini katika uendelezaji wa shughuli za kuwezesha ujuzi katika mafuta na gesi asilia zinafanyika kwa ufanisi, kinyume na hapa Taifa litaendelea kukosa mapato kama ambavyo bado hatujanufaika katika sekta ya Madini.

### 27.4. Maamuzi dhaifu kuhusu mradi wa ujenzi wa Bomba la Usafirishaji Gesi Asilia Kati ya Mtwara na Dar es Salaam

**Mheshimiwa spika**, ujenzi wa Bomba la kusafirisha Gesi asilia kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam lilijengwa na Kampuni ya China Petroleum and Technology Development Company (CPTDC) kwa gharama ya Dola za Kimarekani bilioni 1.283 ambapo kati ya hizo, dola za Kimarekani bilioni 1.225 zilipatikana kama mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Exim ya China. Marejesho ya mkopo huo yalitegemea

kupatikana kwenye mauzo ya gesi asilia baada ya kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa bomba na kuanza kutumika kibiashara.

**Mheshimiwa spika**, kwa masikitiko makubwa sana, taarifa zilizopo zinaonesha kwamba serikali ilikurupuka kufanya maauzi ya ujenzi wa bomba hilo,kabla ya kutafuta wateja na kusainiana mkataba wa mauziano ya gesi asilia kati ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na wateja lengwa wa gesi asilia. Matokeo yake mheshimiwa spika ni athari katika malipo ya mkopo kwa vile mauzo halisi ya gesi asilia yako chini ya kiwango cha makadirio ya awali cha futi za ujazo milioni 138.8 kwa siku (mmscfd). Aidha, kwa sasa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ndilo mteja pekee wa gesi asilia; ambapo anatumia wastani wa futi za ujazo milioni 46.61 kwa siku. Tafsili yake ni kwamba makubaliano ya awali ambayo ilikua TANESCO liweze kutumia takribani futi za ujazo milioni 80 kwa siku kama ilivyokuwa kwenye makubaliano ya mkataba wa mauziano ya gesi asilia (GA) ni tofauti na hali ilivyo kwa sasa.

**Mheshimiwa spika**, pamoja na maoni ya wadau kuhusu ama kuanza kujengwa kwa visima vya gesi au kuamua kujenga bomba la kusafirishia gesi, serikali iliamua kufanya maamuzi ya ajabu kwa kuanza kujenga bomba la gesi kuliko visima vya kuchimba gesi yenyewe, hali hiyo ilipelekea, mradi huu kujaribiwa kwa matumizi kwa kutumia kiwango cha wastani wa futi za ujazo milioni 46.61 kwa siku ikiwa ni kiwango cha chini sana ukilinganisha na ukubwa (capacity) halisi wa bomba. Maana yake ni kwamba, shirika la mafuta nchini TPDC itawajibika endapo itatokea hitilafu yoyote itakayotokana na majaribio ya upitishwaji wa gesi asili kufanyika chini ya kiwango cha bomba la gesi hilo. Hali inatokana na kipindi cha uangalizi wa bomba (defect liability period) kwa sehemu kubwa kuisha tangu mwezi Agosti mwaka 2016.

**Mheshimiwa spika**, Kambi Rasmi ya Bunge lako tukufu inashangaa kuhusu maamuzi haya ya kukurupuka yaliyofanywa na serikali hii ya chama cha mapinduzi kwa

kuwa maamuzi kama haya, hata kama yangetakiwa kufanywa na chombo kingine chochote chenye maamuzi, basi tunaamini chombo hicho kingeamua kuanza na ujenzi wa visima ili kuupatia mradi huo tija kama ambavyo wadau mbalimbali walitahadharisha. Katika mkitadha huo huo Kambi Rasmi inataka jitihada zaidi ziongezwe katika kuhakikisha wateja zaidi wa gesi asilia wanapatikana ili mkopo uweze kulipwa kabla ya marekebisho ya ulipaji ambayo yataongeza gharama kubwa kwa Serikali.

### 27.5. Matumizi ya Bomba la Gesi Asilia Chini ya Kiwango kwa 94%

**Mheshimiwa spika**, matokeo ya maamuzi ya kukurupuka yamepelekea Bomba la kusafirishia gesi asilia kutoka Mtwara hadi Dar es salaam lililojengwa ili kuwezesha usafirishaji wa gesi asilia kwa ajili ya matumizi ya kuzalisha umeme, viwandani, kwa ajili ya kupikia majumbani na kwa matumizi ya kwenye magari, sasa taarifa zinaonesha kwamba hapakuwa na maandalizi ya kupata wateja wa gesi hiyo na hadi sasa kwa mujibu wa taarifa ambazo kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo zinaoesha kuwa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ndilo mteja pekee aliyeunganishwa kwenye bomba la gesi asilia toka Mtwara.

**Mheshimiwa spika,** kuunganishwa kwa TANESCO kama mteja pekee wa gesi hiyo kumepelekea kutumika wastani wa futi za ujazo milioni 46.61 kwa siku sawa na asilimia sita (6%) tu ya ujazo wa bomba; ambapo, kiasi hicho ni pungufu futi za ujazo milioni 737.39 kwa siku ili kujaza bomba. Hali hii mheshimiwa spika, ni tofauti na taarifa za mkataba wa mauziano ya gesi asilia kati ya TPDC na TANESCO kuweka wazi kwamba TANESCO ingetumia gesi asilia kwenye mitambo yake sita (6) ya kuzalisha umeme ya Kinyerezi I, Kinyerezi II, Ubungo I, Ubungo II, Tegeta na Symbion kwa kima cha chini cha matumizi cha futi za ujazo milioni 80 kwa siku na futi za ujazo milioni 138.8 kwa siku kama kiwango cha juu.

**Mheshimiwa spika**, hadi sasa taarifa za Kambi Rassmi ya upinzani Bungeni zinaonesha kwamba mtambo wa kuzalisha umeme wa Kinyerezi I ndio pekee unaotumia gesi asilia kuzalisha umeme; na unatumia kiwango cha asilimia (34%) ya kiasi cha gesi yote iliyolengwa kutumiwa na TANESCO. Aidha mitambo mingine mitano iliyokuwa imekadiriwa kutumia kiasi cha futi za ujazo milioni 92.19 kwa siku, sawa na asilimi sitini na sita (66%) bado haijaanza kutumika; na haijulikani ni lini mitambo hiyo itaanza kutumia gesi asilia.

**Mheshimiwa spika**, TANESCO bado lina mikataba ya muda mrefu na wazalishaji wakubwa wa umeme ambao ni kampuni ya Independent Power Tanzania Ltd (IPTL) na Songas; ambapo mikataba yao inaisha mwaka 2022 kwa ule wa IPTL na mwaka 2023 kwa Songas. Hii inaiongezea TPDC na TANESCO ugumu kwenye kutimiza vifungu walivyokubaliana kwenye mkataba wa mauziano gesi asilia (GA).

**Mheshimiwa spika,** kama kweli serikali hii ya chama cha mapinduzi inadhamira ya kuliepusha taifa hili na malipo ya mkopo huo ambao kimsingi haufanyi kazi kama livyokusudiwa kwa matokeo ya vitendo vya serikali yenyewe kukurupuka, nilazima sasa TPDC iwasiliane na TANESCO na Wizara ya Nishati na Madini ili wajadiliane ni kwa namna gani mitambo ya uzalishaji umeme ya TANESCO itaweza kumalizika kwa wakati ili bomba la gesi litumike kwa ufanisi na kuweza kulipa mkopo wa bomba la gesi kutoka Benki ya Exim ya China kwa wakati. Kwa upande mwingine, nguvu zaidi zielekezwe kwenye kutafuta wateja zaidi wa gesi asilia ili kuongeza mapato ya gesi na kuiwezesha TPDC kutimiza wajibu wa kulipa madeni inapostahili.

### 27.6. Uzembe wa Wizara ya Nishati na Madini, TRA na FCC na kuisababishia serikali hasara ya takribani dola mil 700.

**Mheshimiwa spika**, kampuni ya ORPHIR ilipouza shares zake kwa kampuni ya PEVELION kwa vitalu 3 vya mtawara serikali ilivuna zaidi ya dola 230m mwaka 2013 kutokana na malipo

ya capital gain tax iliyopo kwa mujibu wa sheria ya fedha ya 2012.

Mheshimiwa spika, kampuni ya Shell iliponunua shares za BG kwenye soko la mitaji London, ilikuja nchini na kufanya uhamishaji wa shares za BG kwenda shell kuptia mamlaka za wizara ya Nishati na Madini, FCC na TRA kabla ya kodi kulipwa na kusababisha serikali kupoteza kodi ya takribani dola 700m. Matokeo yake mheshimiwa spika, Leo hii TRA inahangaika kuidai Shell kwenye tribunal kutokana na uzembe wake na hakuna uhakika wa kulipwa kutokana na uzembe wenye kila sura ya ufisadi.

**Mheshimiwa spika**, kutokana na uzembe huo, ambao umesababisha serikali imepoteza kodi ya takribani kiasi cha mil 700 dola za kimarekani, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka maelezo ni lini itawatumbua wahusika wa wizara ya nishati na madini, TRA na FCC kutokana na uzembe huu wenye sura ya ufisadi hasa ukizaingatia ukweli kuwa sheria hii ya fedha imekuwepo tangu 2012 na imepata kutumika mara kadhaa, iweje katika hili la Shell mamlaka hizi zifanye maamuzi bomu kama haya.

### 27.7. Kiasi cha Gesi iliyogunduliwa na Maeneo ilikopatikana

**Mheshimiwa spika**, Sekta ya Gesi na mafuta hapa Tanzania ni sekta ambayo kama ikitumika vizuri italitoa taifa hapa lilipo na kutuweesha kupiga hatua nyingi mbele za kimaendeleo ikiwa tutakuwa na utashi wa kisiasa wa kufanya hivyo. Hadi sasa, kwa takwimu za mwaka 2015 kwa mfano, gesi ilikuwa imekwishapatikana sehemu mbalimbali nchini ikiwemo Mkuranga 2007 (0.2 TCF), Kiliwani 2008 (0.07 TCF), Songo Songo 1974 (2.5 TCF), MnaziBay 1982 (5 TCF), Ntorya 2012 ( 0.178 TCF), Deep Sea 2010-12 (44.8 TCF), Ruvu Basin 2015 (1.9) TCF ) ambapo jumla ya kiasi cha gesi kilichogunduliwa nchini kwa kipindi hichi ilikuwa ni futi za ujazo Trilioni 55.05 .

**Mheshimiwa spika,** nchi yetu imejaliwa utairi wa gesi asilia katikati ya lindi la umasikini wa wananchi na Taifa letu lina

fursa ya kuwa nchi kiongozi katika gesi Afrika na kushindana kimataifa kama tutaweka mstari wa mbele upeo, umasikini na uadilifu katika sekta ndogo ya gesi na mafuta.katika miaka ya nyuma imekuwepo miradi inayohusu shughuli za uendelezaji, uzalishaji na usafirishaji wa gesi asilia hapa Tanzania.

**Mheshimiwa spika**, kwa mujibu wa ripoti ya BMI, (Business Monitor International Ltd) kuhusu ***"Tanzania and Gas Report –Q4-2016"***, ripoti inayohusu pia matarajio kwa miaka 10 ijayo, miradi inayohusika na sekta ya Gesi na Mafuta hapa Tanzania ambayo bado iko kwenye utafiti ni 10, makampuni yaliyoko kwenye hatua ya Appraisal ni 5 na makampuni yaliyofikia hatua ya ugunduzi ni 5, kampuni 1, ilikuwa katika hatua ya uendelezaji, na kampuni 1 pia ilikuwa katika hatua ya uzalishaji.

**Mheshimiwa spika,** kwa mujibu wa ripoti hiyo, makampuni hayo ya uwekezaji yana kumbwa na tishio kubwa la hali ya sintofahamu kuhusu sheria za nchi zinazohusu sekta ya Gesi na Mafuta. Sintofahamu hiyo inakwamisha na kupunguza shauku ya wawekezaji na hivyo kusababisha kudorola kwa miradi husika. Aidha ripoti hiyo inasema, ukosefu wa miundombinu na hali ya mazingira ya sintofahamu dhidi ya sekta hii ni kikwazo kikubwa dhidi ya wawekezaji kwenye sekta hii.

## 27.8. Changamoto katika sekta ya Gesi na Mafuta Nchini

**Mheshimiwa spika**, Serikali ilipaswa kuiangalia sekta ya Gesi na Mafuta rikali ili kuhakikisha kuwa inakuwepo mipango na mikakati na inatekelezwa kikamilifu. Taarifa zinaonesha kwamba vyombo vya serikali vyenye wajibu katika sekta ya mafuta na gesi havitekelezi vya kutosha mipango na mikakati iliyopangwa kama ipo au havjapanga kabisa mipango ama mikakati yeyote. Aidha mipango kama ya kuendeleza rasilimali watu, katika sekta ya mafuta na gesi asilia; kufanya au kuwezesha kufanyika kwa utafiti kwenye petroli na gesi; na kutoa ushauri kuhusu teknolojia sahihi na

mbinu muhimu za utendaji mzuri katika sekta ya petroli ilipaswa kufanyika na inaonekana kutofanywa na serikali hii ya chama cha mapinduzi.

**Mheshimiwa spika**, taarifa ambazo kambi rasmi ya bunge lako tukufu inazo ni kwamba kumekuwepo na kushindwa kufikia malengo ya manunuzi na utoaji wa mikataba na leseni. Taarifa ambazo KRUB inazo zinaoesha kwamba malengo ya serikali kupitia TPDC kuhusu usimamizi wa mchakato wa uandaaji na utoaji wa mikataba na leseni za utafutaji wa gesi asilia halikufanikiwa kutokana na ukosefu wa mwongozo wa muda maalumu; na kukosekana kwa sera sahihi, mikakati na miongozo. Aidha taarifa hizo zinaonesha kwamba, malengo yaliyopangwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli yalifikiwa kwa kiasi kwa sababu ya matarajio madogo ya sekta nchini, na uwezo mdogo wa kiufundi na kifedha.

**Mheshimiwa spika**, Mapungufu mengine yaliyoonekana ni katika uwasilishaji wa majibu ya zabuni zilizotangazwa kuwa chini ya matarajio. Katika mzunguko wa nne wa leseni, kati ya zabuni za vitalu nane (8) zilizotangazwa, vitalu sita havikuguswa ambayo ni sawa na asilimia 75 ya jumla ya zabuni za vitalu vyote. 25% tu ya zabuni za vitalu iliwavutia wawekezaji. Hali hii ilibainika katika mizunguko yote minne ya leseni, ambapo jumla ya zabuni za vitalu 32 zilitangazwa, lakini ni mikataba ya vitalu 5 tu ndiyo ilifanikiwa kutolewa ambayo ni sawa na 16%. Aidha taarifa zinaonesha kwamba kulikuwa na upungufu katika utoaji wa zabuni kwa makampuni ya kimataifa ya mafuta na gesi asilia. Mapungufu haya yalisababishwa na lengo la manunuzi halikukidhi vigezo kama gharama za kuendesha shughuli na mapato yanayotarajiwa, pamoja na muda utakaotumika kukamilisha kazi au hata uzalishaji, ubora, na utaalamu wa makampuni yaliyonunuliwa.

**Mheshimiwa spika**, katika ule mwendelezo wa wawekezaji kuendelea kuzifaidi rasilimali za watanzania chini ya sera ambovu za chama cha mapinduzi, sekta ya Gesi na mafuta nayo inaonesha kukumbwa na tatizo la utelekezaji duni wa

masharti ya mkataba wa ugawanaji wa mapato yatokanayo na uzalishaji na uhakiki wa urejeshaji wa gharama za uendeshaji. Taarifa za mikataba hiyo zinaonesha kwamba Mkataba wa Ugawanaji wa Mapato yatokanayo na Uzalishaji ambao ulitiwa saini kati ya Serikali ya Tanzania, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania pamoja na Makampuni ya Kimataifa ya Mafuta; Wizara ya Nishati na Madini ilikuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa kipengele cha Ushiriki wa Wazawa kimewekwa kwenye Mkataba wa Ugawanaji wa Mapato yatokanayo na Uzalishaji pamoja na Sheria ya Uzalishaji na Utafutaji wa Petroli ya mwaka 1980 zinatekelezwa kwa ufanisi.

**Mheshimiwa spika,** katika kuonesha kwamba yanayotokea kwenye sekta ya Gesi na mafuta siyo ajali, kama ambavyo bajeti kuu haitaji ni ajira kiasi gani serikali inakusudia kuongeza, huenda ni kutokana na serikali kupuuza dhamira ya kuhakikisha wananchi wanapata ajira. Kwenye sekta ya Gesi na mafuta pia, wajibu wa utoaji Ajira kwa Watanzania hautekelezwi. Hii inasababishwa na upembuzi hafifu wa kutambua nafasi za ajira katika sekta ya mafuta na Gesi asilia na pia ukosefu wa mipango mkakakati ambayo ingehakikisha kupatikana kwa ajira kwa Watanzania katika makampuni ya kimataifa ya mafuta ya na gesi asilia na ukosefu wa miongozo na utaratibu wa kutoa ajira kwa wafanyakazi wa kigeni.

**Mheshimiwa spika**, hali hii ya watanzania kushindwa kupata ajira katika sekta hii, kunasababishwa na mapungufu ya kisheria, udhibiti, na mfumo wa kitaasisi kwa ajili ya usimamizi wa utekelezaji wa kipengele cha Ushiriki wa wazawa katika Mkataba wa Ugawanaji wa Mapato yatokanayo na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia. Aidha kuna ushiriki usioridhisha Katika Biashara ya Mafuta na Gesi Asilia, kwa mfano Shirika la Maendelelo ya Petroli Tanzania lilipaswa kushiriki katika mradi wa Songosongo pamoja na mradi wa Mnazi Bay ambayo ni miongoni mwa mikataba michache ambayo ilishafikia katika hatua za uzalishaji, lakini taarifa zilizoo ni kwamba TPDC ilishiriki katika mradi wa ghuba ya Mnazi pekee.

**Mheshimiwa spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa mbadala ufuatao dhidi ya sekta ya Gesi na mafuta hapa nchini.

i. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ingehakikisha inashirikisha wadau mbalimbali zikiwemo sekta binafsi katika michakato ya utafiti, uchimbaji na usambazaji wa gesi asilia ili kuhakikisha kwamba sekta binafsi zinapewa nafasi ya kushiriki katika kujenga uchumi wa Taifa hili.

ii. Kambi Rasmi ya upinzani bungeni ingehakikisha inaondoa mazingira yote yanayoonesha viashiria vya sintofahamu ili kuruhusu wawekezaji wakubwa kufanya maamuzi ya mwisho katika uwekezaji ili kuinusuru miradi ambayo inachechemea kutokana na sintofahamu ya sheria na viashiria vya hofu.

iii. Kambi rasmi ya upinzani Bungeni ingehakikisha , sekta ya gesi na mafuta inatoa ajira kwa watanzania waliowengi ili kupiunguza tatizo la ukosefu wa ajira nchini, kuweka miongozo na kusimamia sheria kwa ukaribu ili kuhakikisha wazawa wanapewa ajira na makampuni ya kigeni yanayowekeza katika sekta hii. kwa kufanya hivyo, vipato vya wananchi vingepanda, lakini pia serikali ingepata kodi inayolipwa kutokana na vipato vya mishahara yaani (PAYE)

iv. Kambi Rasmi ya upinzani Bungeni ingehakikisha kuna fungamanisho la sekta ndogo ya gesi asilia na sekta nyingine ili kuongezeka na kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Tunaposisitiza fungamanisho la sekta ndogo ya gesi asilia na sekta nyingine, hapa tunataka gesi iwe kichocheo cha ukuaji wa sekta nyingine hapa nchini kama Ajira, kilimo, viwanda, Nishati na uvuvi.

## 28. USAWA WA JINSIA KATIKA BAJETI (GENDER BUDGETING)

**Mheshimiwa Spika,** JINSIA ni dhana inayoelezea tafsiri ya jamii kuhusu wajibu na haki za KE na ME katika jamii, tofauti na JINSI ambayo ni dhana inayoelezea tofauti za kimaumbile

au kibaiolojia – yaani hali ya kuzaliwa mwanamke au mwanaume. Kwa kuwa jinsia inahusika zaidi na wajibu au shughuli wanazofanya wanaume au wanawake, basi kwa vyovyote vile shughuli hizo zitakuwa na uhusiano wa moja kwa moja au vinginevyo katika kujenga na kukuza uchumi wa taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Taifa letu linatambua umuhimu wa mchango wa jinsia zote mbili katika kulijenga taifa na ndio maana waasisi wa taifa letu waliafiki kuweka picha au taswira ya mwanaume na mwanamke katika Nembo ya Taifa wakimaanisha kwamba taifa litajengwa na wanaume na wanawake katika kazi zao na nafasi zao mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** ili wanaume na wanawake waweze kutekeleza jukumu hilo la kujenga taifa, ni lazima wapatiwe fursa sawa ili waweze kutumia maarifa yao na uwezo walio nao kutoa mchango wao katika ujenzi wa taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali katika kuhakikisha hakuna ubaguzi wa kijinsia, ili watu wote waweze kupata fursa sawa za kushiriki katika shughuli za kiuchumi na hivyo kutoa mchango wao katika ujenzi wa uchumi wa taifa. Miongoni wa hatua hizo ni pamoja na kuridhia mikataba ya kimataifa na kikanda inayohusu kuleta usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake ikiwemo:

i. Mkataba wa Kuondoa Aina Zote za Ukatili Dhidi ya Wanawake (CEDAW 1979)

ii. Maazimio ya Beijing

iii. Ajenda ya Umoja wa Afrika Kuhusu Usawa wa Jinsia au Katika Mkakati wa AGENDA 2063

iv. Itifaki ya Usawa wa Jinsia wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) (2007)

v. Malengo Makuu ya Milenia na Sasa Malengo 17 Endelevu ya Dunia (SDGs) nk

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na dhamira hiyo njema ya Serikali, bado kuna changamoto kubwa katika kuzingatia usawa wa kijinsia katika sekta mbali mbali za kiuchumi. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo:

i. Wanawake na wasichana wengi hapa nchini hawana fursa na haki sawa katika takriban maeneo yote ya jamii ikiwemo kufikia, kutumia na kumiliki rasilimali zikiwemo ardhi, fedha, taarifa, teknolojia nk. Kwa mfano utafiti wa TDHS 2010 ulibaini kuwa ni asilimia 8 tu ya wanawake wanamiliki ardhi yao peke yao ikilinganishwa na asilimia 30 ya wale wanaomiliki katika mfumo wa pamoja. Aidha, utafiti uliofanywa na Oxfam, 2012 ulibaini kwamba ni asilimia 5 tu ya wanawake wanaofanya kazi za kilimo wenye kumiliki ardhi yao, na asilimia 44 wanafanya shughuli za kilimo kwenye ardhi inayomilikiwa na waume zao na asilimia 35 wanafanya kilimo katika ardhi inayomilikiwa na ukoo. Katika utafiti huo, ilibainika pia kwamba ni asilimia 13 tu ya kaya zinazoongozwa na KE wanapata mikopo ikilinganishwa na asilimia 33 ya kaya zinazoongozwa na wanaume. Hali hii inazuia wanawake kupata fursa za kujiendeleza kiuchumi.

ii. Wanawake na wasichana bado hawana fursa sawa na wanaume kufikia huduma bora za kijamii zikiwemo elimu, afya, maji , nishati na huduma za ugani. Kwa mfano Demographic Health Survey 2010 ilibainisha kuwa asilimia 19.1 ya wanawake wenye umri kati ya miaka 20 – 24 hawana elimu kabisa ikilinganishwa na asilimia 10.5 ya wanaume.

iii. Wanawake hawana fursa sawa na wanaume katika maamuzi kuhusu maslahi yao kuanzia ngazi ya familia hadi taifa. Utafiti wa DHS 2010 ulibaini pia kwamba katika uongozi wanawake katika ngazi za wilaya na serikali za mitaa wanawake walikuwa ni asilimia 10tu au pungufu.

**Mheshimiwa Spika,** ukiachilia mbali ubaguzi huo wa kijinsia katika fursa mbalimbali bado kuna ongezeko kubwa la ukatili dhidi ya wanawake na watoto, vitendo vya ubakaji kwa wanawake, mimba za utotoni kwa wasichana na mila

kandamizi dhidi ya wanawake hususan ukeketaji, utakasaji, nyumba ntobhu, nk.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya manyanyaso wanayopata wanawake, imebainika kwamba wao ndio nguvu kazi kubwa inayotegemewa katika ukuzaji wa uchumi. Kwa mujibu wa sensa ya Watu na Makazi ya 2012, zaidi ya nusu ya watanzania ni Wanawake katika makundi yote ya jamii ambao fursa zao katika uchumi ni ndogo zaidi ikilinganishwa na wanaume. Wachambuzi wa masuala ya kiuchumi wanasema kwama Usawa wa kijinsia ukizingatiwa katika shughuli mbalimbali za kiuchumi utasaidia kufikia haraka malengo ya uchumi wa ngazi ya kati – ambao kwa sasa ni uchumi wa viwanda.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hali hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kutekeleza mambo yafuatayo:

i. Kuweka lengo mahusi la kuzingatia usawa wa kijinsia ili lielekeze jinsi ya kutafsiri jinsia katika malengo/ vipaumbele vingine vyote na pia kuendeleza juhudi zilizokwishakufanyika kaitka kufikia usawa wa kijinsia katika ngazi mbalimbali za jamii.

ii. Kuweka mazingira ya kuwajengea uwezo wasichana katika kujenga wataalam wenye ujuzi maalum.

iii. Kuweka mfumo wa bajeti unaozingatia usawa wa kijinsia.

## 29. SEKTA YA FEDHA
### 29.1. Mikopo ya Kibiashara na Riba

**Mheshimiwa Spika,** kabla ya Mwezi machi, 2017 riba katika mikopo ya kibiashara ilifikia kati ya 18-26% jambo ambalo lilipelekea kushuka kwa kiwango kikubwa cha mzunguko wa fedha katika uchumi wetu. Hali ya ongezeko la riba katika mikopo hiyo kulitokana na kuongezeka kwa hali ya uhaba wa fedha katika mabenki pamoja na ku-discourage wananchi kukopa ili kukabiliana na kupungua kwa ukwasi wa fedha katika taasisi za kifedha.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Benki Kuu kupunguza kiwango cha mabenki ya kibiashara kukopa katika benki kuu ya Tanzania toka kiwango cha awali cha 16% mpaka 12% na pia kupunguza amana za mabenki ya kibiashara (statutory minimum reserve requirement) toka 10% mpaka 8% bado hali ya riba na mikopo ya kibiashara ni ngumu kwa wananchi kwa kawaida. Kwani bado riba zipo juu na wananchi wa kawaida hawawezi kumudu.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuchukua hatua ya kuwaeleza mabenki ya kibiashara kupitia BOT kupunguza riba kama ambavyo na wao wamepunguziwa ili wananchi waweze kukopa.

**29.2. Serikali Kukopa Mikopo ya Ndani na Athari zake katika Biashara**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha miaka 3 mfululizo Serikali imekuwa na tabia ya kuendelea kukopa katika mabenki ya ndani kwa masharti ya kibiashara ili kuhudumia malipo ya madeni ya amana. Kitendo hicho kimepunguza uwezo wa mabenki na taasisi za kifedha kukopesha wananchi kutokana na kukabaliwa na ushindani wa serikali kukopa kwenye mabenki. Mfano katika mwaka huu wa fedha 2017/2018 serikali inatarajia kukopa ndani tril 7.7 fedha ambazo haziendi katika uwekezaji wa miradi ya kimaendeleo na badala yake ni mkopo wa kulipa mkopo. Hali hii imeathiri sana mzunguko wa fedha katika mabenki na kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani bungeni inaishauri serikali kurudi katika utaratibu wa awali wa kukopa nje mikopo yenye riba nafuu (concessional loans) kwa kukubali kutengeza utaratibu mzuri wa kidiplomasia.

**29.3. Wafanyabiashara Kushindwa Kulipa Mikopo**

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hali ya kibiashara kuwa mbaya hali ya marejesho ya mikopo katika mabenkI kwa wafanyabiashara imekuwa mbaya katika historia ya nchi yetu kwani imevuka kiwango cha chini cha 5% kinachoruhusiwa.

Mpaka sasa mikopo chechefu imefikia 10.3% ya watu kushindwa kulipa madeni kutokana na mikopo iliyokuwa imechukuliwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuchukua hatua za haraka kupitia BOT kunusuru hali hii ili mabaenki yetu yasije kufilisika.

## 30. VYANZO MBADALA VYA MAPATO

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani kwa takriban miaka kumi (10) imekuwa ikitoa ushauri na mapendekezo kuhusu njia mbadala za kuongeza mapato ya Serikali. Bunge, kwa kuona mapungufu yaliyopo Serikalini katika kubuni vyanzo vipya au vilivyopo kutokuwa na uthibiti navyo, lililazimika kuunda kamati maalum ili kuishauri Serikali jinsi ya kuongeza mapato badala ya kuongeza viwango vya kodi kwa vyanzo vile vile.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa kuna baadhi ya vyanzo tumeishauri Serikali kuvifanyia kazi na imeshindwa inatulazimu kurudia tena, na vyanzo hivyo pia vilifafanuliwa vyema na ***kamati maalum ya Spika Mstaafu -Anne Semamba Makinda*** kwenye "***taarifa ya mapendekezo kuhusu mapato na matumizi ya serikali",***vyanzo hivyo ni vifuatavyo:

### 1. Mapato Yatokanayo na Uvuvi katika Bahari Kuu

**Mheshimiwa Spika**, takwimu zinaonesha kuwa mbali ya kutoza fedha kidogo za leseni kwa ajili ya meli zinazofanya uvuvi katika bahari kuu (deep sea fishing) bado Serikali haipati hata shilingi moja ya mrabaha wa samaki zinazovuliwa na meli hizo.

**Mheshimiwa Spika,** takwimu zinaonesha kuwa wastani wa meli 41 zinapatiwa leseni kwa mwaka kwa ajili ya kufanya uvuvi katika bahari kuu. Kwa ujumla ni kwamba kiwango cha chini cha ada ya leseni na kukosa mrabaha pamoja na biashara nyingine ambazo zingefanyika kama kungekuwa na bandari ya samaki. Tanzania inapoteza mapato ya dola

za Kimarekani milioni 220 sawa na Tshs. **492,140,000,000**/- kila mwaka kutokana na uvuvi haramu.

**2. Mapato Yatokanayo na Sekta ya Madini ya Vito**

**Mheshimiwa Spika,** eneo hili la madini ni chanzo kikubwa sana cha mapato, lakini ukweli ni kwamba toka hujuma ilisababisha kufa kwa minada ya vito pale Arusha. Baada ya minada kufa, wafanyabiashara hawa, wakaja kwa sura za wawekezaji lakini kiuhalisia walikuwa ni wachuuzi (*traders*) na waliweza kupata haki zote za kukaa na kufanya biashara mpaka kufikia kutawala soko la ndani na nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa ya Kamati maalum ya Spika Mstaafu - Makinda inaonesha kuwa kuna ofisi zisizopungua hamsini (50) za wageni mjini Arusha zinazonunua *Tanzanite* na kwamba Wizara ya Nishati na Madini inatoza dola za Kimarekani 200 kwa kila leseni kwa mwaka. Bei hii ni ndogo sana ikilinganishwa na ilivyo katika nchi za jirani zenye vito vyenye thamani ya chini ikilinganishwa na Tanzanite. Kwa mfano Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo leseni hutolewa kwa dola za Kimarekeni 50,000 kwa mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** kwa takwimu hizo za kampuni za kigeni ada ya leseni ikiwa dola za Kimarekani 50,000 kwa mwaka maana yake mapato yatakuwa dola 2,500,000 ukitumia kiwango cha USD 1 =Tshs 2,237. Mapato yanakuwa **Tshs. 5,592,500,000/-**

**Mheshimiwa Spika**, mbali ya ada ya leseni ni kwamba ilikwisha kubalika kwamba madini hayo yasiuzwe nje ya nchi bila ya kusafishwa/ kuchongwa. Lakini kwa sababu ambazo haziko wazi bado madini ya vito yanasafieishwa yakiwa ghafi na hivyo ajira kubwa kuhamishwa na kupelekwa nje ya nchi, katika mchakato huo mapato mengi yanapotea.

**Mheshimiwa Spika,** India, Jaipur Germs imeajiri vijana/ wafanyakazi wapatao laki moja kwa ajili ya kukata na

kusafisha madini ya Tanzanite yanayotoka Tanzania, lakini kwetu vijana walioajiriwa ndani hawazidi elfu tano. Unaweza kuona ni kiasi gani cha TANZANITE kinachokwenda India kwa njia ambazo Serikali haizifahamu. Hii yote ni kukosa uthibiti wa madini hayo.

**Mheshimiwa Spika,** kitendo cha kuwa na mitambo au vifaa vya kusafisha TANZANITE hapa ni kuzidisha uthibiti wa madini hayo, jambo linalozidisha thamani yake katika soko la kimataifa. Bei nzuri ya madini ya PARAIBA TOURMALINE yanayotoka Nchini Brazil inatokana na udhibiti makini unaofanywa na Serikali ya Brazil. Hivyo kuyafanya yauzwe kwa bei ghali kwa sababu ya uadimu wake katika soko tofauti na Tanzanite ambayo haijafanyiwa udhibiti makini na umiliki wake (branding) halali haujulikani. Mfano kuna Tanzanite-Tanzania, Tanzanite- Kenya, Tanzanite- India, Tanzanite- Sri lanka, Tanzanite- South Africa, nk. Kama Tanzanite ingefikia thamani ya PARAIBA TOURMALINE mauzo yake yangefika dola za kimarekani bilioni moja kwa mwaka (dola za Kimarekani 1,000,000,000).

**Mheshimiwa Spika,** hali hii huifanya Tanzanite kuuzwa kwa bei ya chini sana ikilinganishwa na PARAIBA TOURMALINE ya Brazil inayouzwa mara kumi ya bei ya Tanzanite ambayo ni kati ya Dola za Kimarekani 1,500-20,000 kwa Karati wakati Tanzanite huuzwa kati ya dola za Kimarekani 150-300 kwa Karati.

**Mheshimiwa Spika,** kwa muktadha huo ni dhahiri mapato yatokanayo na mrabaha ambayo ni asilimia 5 na asilimia 1 kwa kodi ya kukata na kusanifu vito ukiweka na kodi ya PAYE. Hivyo basi, mapato yanakadiriwa kuwa **shilingi 270 bilioni.**

**3. Mapato Kutokana na Dhahabu na Madini Mengine**

**Mheshimiwa Spika,** takwimu zinaonesha kuwa kuna makampuni 12 ya uchimbaji wa madini nchini na makampuni hayo mbali ya kulipa mrabaha kwa dhahabu inayochimbwa kwa kiwango cha asilimia 4 tu, lakini bado

makampuni hayo hayalipi kodi ya makampuni (corporate tax) kwa ukamilifu wake. Hivyo fedha ambazo hazijalipwa na hivyo zinatakiwa kulipwa ni takriban kiasi cha dola za kimarekani 265,687,434.9 (Tshs 425,099,895,840/=). Hizi fedha ni mapunjo yanayotakiwa kulipwa, lakini kodi stahiki kwa mwaka .

**4. Kupunguza misamaha ya kodi kuwa 1% ya pato la Taifa**

**Mheshimiwa Spika,** misamaha ya kodi kwa sasa ni 1.14% ya pato la taifa na ili kufikia kiwango ambacho kitaleta tija katika uchumi inatakiwa misamaha iwe asilimia 1 au chini ya pato la Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kwamba 0.14% iliyoongezeka ya pato la Taifa la shilingi milioni 103,744,606 kuwa ni mapato ya Serikali. Hivyo basi kiasi cha shilingi **145,242,448,400/-** kitapatikana.

**5. Uuzaji wa Hatifungani za Kimataifa (EURO BOND FLOATS)**

**Mheshimiwa Spika,** kama tulivyoeleza hapo awali kwamba, miradi ya kimkakati kama vile, ujenzi wa mradi wa umeme wa Stigler's Gorge, Ujenzi wa Reli ya Kati n.k inaweza kujengwa kwa fedha kwa Serikali kutoa hatifungani kimatifa. Katika chanzo hiki ni dhahiri zinaweza kupatikana shilingi **2.2 trilion.**

**6. Mapato kutoka katika Sekta ya Utalii**

**Mheshimiwa Spika,** katika sekta ya utalii, kampuni zinazojihusisha na shughuli za utalii takwimu zinaonesha kuwa ni 1050, lakini kati ya kampuni hizo zilizosajiliwa kwa biashara hiyo ni kampuni 350 na hivyo kuziacha kampuni 700 bila ya

kusajiliwa. Kama kampuni hizo zikilipa TALA license ya USD 500 inayotakiwa kulipwa na kuacha kodi zingine. Kambi Rasmi ya Upinzani inatarajia kukusanya kiasi cha shilingi **782,950,000/** = ikiwa dola moja ni sawa na shilingi 2237.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa kuna makampuni 1,050 na tukichuulia kuwa kila kampuni ina wastani wa magari 20 na kila gari moja la kubeba watalii mbugani linalipiwa dola 100 kama vehicle fee. Hapa tutapata jumla ya shilingi **4,697,700,000/-.**

**Mheshimiwa Spika,** kuna utalii wa kiasili ambao hadi sasa kivutio hiki hakija rasimishwa, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba hapa itaweza kupata mapato ya shilingi **bilioni 300.**

**Mheshimiwa Spika,** takwimu zinaonesha kuwa kwa mwaka 2016 watalii walioingia nchini ni 1,284,275 na tunatarajia idadi hiyo itaendelea kuwa hiyo au zaidi kwa mwaka wa fedha unaokuja na kila mtalii akilipa Visa fee ya dola 100, maana yake kiasi cha **shilingi 287,293,212,300/-.**

**Mheshimiwa Spika,** hivyo basi kwa sekta ya Utalii itatoa mapato ya jumla **shilingi 592,773,862,300/-.**

### 7. Mapato kutoka kwenye sekta ya michezo ya kubahatisha-Gaming.

**Mheshimiwa Spika,** mchezo wa kubahatisha ni mchezo ambao hapa nchini unakua kwa kasi kubwa sana na hivyo mchezo huu kama ukiwekewa utaratibu mzuri na mazingira ya kuridhisha kama nchi za wenzetu ni dhahiri ni chanzo kingine cha mapato kwa Serikali. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kwa chanzo hiki kitatoa kiasi cha ziada ya shilingi **bilioni 30.59.**

## 31. MUHTASARI WA VYANZO VIPYA YA MAPATO MBADALA

| NA | MAELEZO | KIASI (TSHS) | KIASI(TSHS) |
|---|---|---|---|
| 1. | Mapato yatokanayo na uvuvi katika bahari kuu | 492,140,000,000. | |
| 2. | Mapato yatokanayo na sekta ya madini ya vito;<br>**a)** Kutokana na Leseni | 5,592,500,000. | |
| | **b)** Kodi, Mrabaha na PAYE | 270,000,000,000. | |
| 3. | Kupunguza misamaha ya kodi kuwa 1% ya pato la Taifa | 145,242,448,400. | |
| 4. | EURO BOND FLOAT | 2,200,000,000,000. | |
| 5. | Mapato kutoka katika sekta ya Utalii | 592,772,862,300. | |
| 6. | Mapato kutoka kwenye sekta ya michezo ya kubahatisha-Gaming | 30,000,000,000.59 | |
| | **JUMLA YA VYANZO VYA MAPATO VYA NYONGEZA** | | **3,735,747,810,700.59** |

## 32. SURA YA BAJETI MBADALA KWA MWAKA WA FEDHA

| | MAELEZO | KIASI KATIKA SHILINGI (TZ) | | |
|---|---|---|---|---|
| | **MAPATO** | | | |
| **A** | Mapato ya Ndani | | **20,725,442,810,700.59** | |
| | i. Mapato ya Kodi | 17,521,578,448,400.00 | | |
| | ii.Mapato yasiyo ya kodi | 3,203,864,362,300.59 | | |
| **B** | Mapato ya Halmashauri | | **387,306,000,000.00** | |
| | **JUMLA YA MAPATO YOTE YA NDANI** | | | **21,112,748,810,700.59** |
| | | | | |
| **C** | Mapato na mikopo nafuu kutoka nje | | **5,071,103,000,000.00** | |
| | | | | |
| **D** | Mikopo toka nje masharti ya kibiashara | | **3,794,985,000,000.00** | |
| | **JUMLA YA MAPATO YOTE(A+B+C+D)** | | | **29,978,836,810,700.59** |

**MUHIMU:**

1. Serikali yetu mbadala itafanya "CREDIT RATING" ili iweze kuaminika kimataifa kwa minajili ya kukopeshwa mikopo yenye riba nafuu na pia mikopo ya kibiashara toka nje.
2. Mapato ya mikopo ya kibiashara kutoka nje yataongezeka kufikia trilioni 3.794t kutoka trillion 1.594 ya Serikali ya sasa kwa sababu, Serikali mbadala itatoa EURO BOND zenye thamani ya DOLA BILLION 1 kimataifa ili kupata fedha za kugharamia bajeti.
3. Kutokana na kuaminika huko, tutapata mikopo nafuu kutoka nje ya thamani ya shilingi trilioni 5.071
4. Mapato ya Halmashauri yatashuka kufikia shilingi bilioni 387 kutoka shilingi bilioni 687 ya sasa ili kuziwezesha halmashauri kufanya miradi yake ya maendeleo.

## 18. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, nimalizie kwa kuwakumbusha watanzania kuwa Serikali hii ya CCM inayoongozwa na Mwenyekiti wa CCM John Pombe Magufuli imekuwepo

madarakani miaka mingi toka taifa letu lipate uhuru na hivyo matatizo tuliyonayo kama Taifa yana unasaba wa moja kwa moja na serikali hii.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha niwakumbushe pia kuwa Rais aliyepo sasa alikuwepo kwenye serikalini kwa zaidi ya miaka ishirini iliyopita na kwa hiyo masuala ya ufisadi, sheria mbovu za uwekezaji, sheria za madini na zingine zinazoratibu matumizi ya rasilimali zilitungwa yeye akiwa sehemu ya serikali na kwa hiyo kuwahadaa watanzania kuwa anajenga Tanzania mpya ni mchezo wa kuigiza na propaganda ambazo hazitatujenga kama Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania mpya tunayoiona ni Tanzania ambayo serikali inaziba wananchi midomo kwa kutumia sheria ya makosa ya kimtandao, Tanzania ambayo wananchi wake hawana haki ya kuona Bunge live ili kuona wawakilishi wao wakitekeleza majukumu yao, Tanzania ambayo vyama vya siasa haviruhusiwi kufanya mikutano ya hadhara kueneza sera zao kwa wananchi tofauti na utaratibu tuliojijengea kwa miaka takribani 25 ya vyama vingi, Tanzania ambayo Katiba ya nchi inakanyagwa kwa kauli na matendo ya baadhi ya viongozi wa serikali, Tanzania ambayo wafanyakazi katika mwaka wa pili wa bajeti hawajashuhudia ongezeko la mishahara yao, Tanzania mpya ambayo watumishi wa umma wanafukuzwa kwenye mikutano ya hadhara kinyume cha sheria ya utumishi wa umma, Tanzania ambayo wasimamizi wa uchaguzi hawatakiwi kuwa na itikadi za vyama lakini sasa wameteuliwa wakurugenzi na makatibu Tawala wa CCM, Tanzania ambayo vyombo vya dola badala ya kulinda mali na raia vinashiriki kwenye matukio ya utekaji na utesaji.

**Mheshimiwa Spika**, kweli serikali ya awamu ya tano inajenga Tanzania mpya ambayo ni Tanzania biashara zinafungwa, Tanzania ambayo Mamlaka ya Kodi inatisha walipa kodi kwa mitutu ya Bunduki, Tanzania ambayo mauaji yanaendelea huko Kibiti bila jitihaa za dhati za serikali, Tanzania ambayo inaendekeza ubaguzi wa itikadi za kisiasa, Tanzania ambayo vyombo vya habari vinavamiwa na kiongozi wa serikali na mteule wa Rais akiwa na silaha za moto.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Davidi Ernest Silinde (Mb)
**Kny: MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**
12 Juni, 2017

**KIELELEZO A**
MCC Statement on Decision of Board of Directors to Suspend Partnership with Tanzania March 28, 2016

Washington, D.C. — In December 2015, the Millennium Challenge Corporation's (MCC) Board of Directors deferred a vote on the reselection of Tanzania for compact eligibility, citing the nullification of election results in Zanzibar and the need for a prompt, fair and peaceful conclusion of the electoral process. The Board also sought assurances from the Government of Tanzania that the Cybercrimes Act would not be used to limit freedom of expression and association, in light of arrests made during the elections. These concerns were repeated on a number of occasions, including in a statement of Ambassador Mark B. Childress.

On March 20, 2016, Tanzania moved forward with a new election in Zanzibar that was neither inclusive nor representative, despite the repeated concerns of the U.S. Government and the international community. The Government of Tanzania has also not taken measures to ensure freedom of expression and association are respected in the implementation of the Cybercrimes Act.

MCC's model has a partner country's commitment to democracy and free and fair elections at its core. The elections in Zanzibar and application of the Cybercrimes Act run counter to this commitment. As a result, while the United States and Tanzania continue to share many priorities, the MCC Board of Directors determined that the Government of Tanzania has engaged in a pattern of actions inconsistent

with MCC's eligibility criteria, and voted to suspend the agency's partnership with the Government of Tanzania. MCC will therefore cease all activities related to the development of a second compact with Tanzania.

**KIELELEZO B**

**Statement on Election Re-Run in Zanzibar**[28]

The High Commissioners and Ambassadors to Tanzania of Belgium, Canada, Denmark, the European Union, Finland, France, Germany, Ireland, Italy, the Netherlands, Norway, Spain, Sweden, Switzerland, the United Kingdom and the United States, today issued the following statement regarding the election re-run which took place in Zanzibar on March 20th, 2016:

"We regret the Zanzibar Electoral Commission's decision to hold a re-run of the 25 October 2015 election, without a mutually acceptable and negotiated solution to the current political impasse.

"In order to be credible, electoral processes must be inclusive and truly representative of the will of the people.

"We reiterate our call on the Government of Tanzania to exercise leadership in Zanzibar, and to pursue a negotiated solution between parties, with a view to maintaining peace and unity in the United Republic of Tanzania.

"We commend once again the population of Zanzibar for having exercised calm and restraint throughout this process, and call on all parties and their supporters to re-start the national reconciliation process to find an inclusive, sustainable and peaceful resolution."

By U.S. Embassy Dar es Salaam | 21 March, 2016 | Topics: Press Releases

---

[28] https://tz.usembassy.gov/statement-election-re-run-zanzibar/

**MWENYEKITI:** Naendelea, tunaanza kazi kubwa ya kuchangia ambayo ndio muhimu, na kwa sababu ya muda tulionao naanza na Mheshimiwa...

Waheshimiwa Wabunge tusikilizane nitaweza kuwatoa mkacheke vizuri nje.

Naanza na Mheshimiwa Kasuku Samson Bilago atakuwa wa kwanza, lakini kwa sababu ya muda sidhani kama tutapata mtu wa pili lakini mchana tutaanza na Mheshimiwa Mwambalaswa, tutaendelea na Mheshimiwa Almas Maige, na kwa upande wa Kambi ya Upinzani tutaanza na Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali, hao ndio wa jioni lakini sasa tunaanza na Mheshimiwa Kasuku.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote kwanza niseme ripoti ya leo ya makinikia nasikitika kwamba imewataja Wabunge wengi katika Bunge letu hili Tukufu. Kwa hiyo, sijajua hatima yake itakuwaje, niwape pole wote kwa pamoja watakaokuwa wameguswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupewa nafasi ya kwanza kabisa ni upendeleo wa pekee na Mtemi kwa hili nakupongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo tulilonalo katika nchi hii, tunalo tatizo kubwa la namna ya kukusanya mapato ya nchi yetu. Tuna tatizo na mapato na kwa kweli tusipojikita kutafuta vyanzo vya mapato vilivyo imara, hata vile tulivyonavyo tukaviimarisha na vikatoa fedha inayoweza kuendesha nchi hii tutaendelea kuimba wimbo wa maendeleo ya nchi hii bila kufika mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tulikuwa na bajeti ya shilingi trilioni 29 ambayo haikutekelezwa; bajeti ya maendeleo ilitekelezwa kwa asilimia 34. Leo hii tunakuja na bajeti ya shilingi trilioni 32 huu ujasiri tunaupata wapi? Yaani shilingi trilioni 29 zimeshindikana unakwenda shilingi trilioni 32, wakati fulani unaweza ukasema ni ujasiri wa kujifunika

shuka moja na nyoka, nimuujiza gani tutakaoufanya tufike shilingi trilioni 32 wakati shilingi trilioni 29 ilishindikana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe wito kwa Mawaziri mnaohusika. Hebu tukae chini tupitie chanzo kimoja kimoja, tuone ni kwa nini hatufikii makusanyo ya asilimia 100 kwa kila chanzo tulichonacho? Nchi zinatucheka! Una dhahabu, unakuwa wa tatu katika Afrika lakini ni nchi maskini! Tuna utalii, tuna wanyama wa kutosha, tuna milima na vivutio vingi vya watalii, lakini bado nchi ni maskini. Tuna ardhi nzuri yenye rutuba na mabonde mazuri, lakini nchi bado ni masikini. Tuna kila kitu ambacho tumepewa na Mwenyezi Mungu, lakini bado ni maskini. Jamani ndugu zangu, nani katuroga nchi hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake bajeti iliyoletwa ambayo watu wanashangilia sana, ni bajeti tegemezi na hatuna uhakika hata wa *collection* za ndani kama tutafika hizo fedha ambazo tumetenga. Hao wafadhili ambao tunategemea watuletee shilingi trilioni 11 tuna mkataba nao? Wasipoleta, tutawafanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wabunge wote tutakaochangia bajeti hii tujikite kuielekeza Serikali namna ya kukusanya mapato na kuzuia uvujaji wa mapato. Upotevu wa fedha za Serikali ni mkubwa mno. *CAG* na kitabu chake kinene chote kile kimeeleza namna fedha za Tanzania zinavyopotea na waliopoteza wote hakuna yeyote aliyeko jela. Wote wako nje wanakula *chips* na kuku wanaendelea kuishi na wengine wako humu humu wanaendelea kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite kwenye suala la kufutwa kwa *Annual Motor Vehicle* ambayo sisemi ni kufutwa, ni kubadilishwa ipatikane kwenye chanzo kingine. Wamiliki wa vyombo vya moto yaani magari wana uwezo kiuchumi, leo hii wanafutiwa kulipa shilingi 150,000 mpaka shilingi 250,000 mzigo ule anakwenda kubeba mkulima wa kijijini kule kwangu Kakonko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi 40 inayoongezeka kwenye lita moja ya mafuta, italigharimu Taifa hili na itaendelea kuwadidimiza Watanzania walio maskini. Mimi natoka Mkoa wa Kigoma, nadhani ni mbali kuliko Tanzania yoyote. Bidhaa itakayotoka Dar es Salaam au Dodoma, ije imfikie mwananchi wa Kakonko, itakuwa imepanda bei kwa sababu ya kuongeza bei ya mafuta na Wabunge tunashangilia! Nani Mbunge hana uwezo wa kulipa shilingi 250,000 hapa ya *motor vehicle?* Matokeo yake *motor vehicle* anakwenda kulipa mama anayewasha kibatari kijijini kwangu Kasuga. Bila hata kufanya tathmini wala huhitaji kwenda kusoma sana uwe na madigrii kwamba ukiongeza mafuta umeongeza gharama za maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashine za kusaga zinatumia mafuta. Kwa hiyo, mama aliyekuwa anasaga debe moja kwa shilingi 1,000 atakwenda kuisaga kwa shilingi 2,000 au shilingi 3,000, mwananchi wa kijijini kabisa. Tumejiangalia sisi wenye uwezo tukashangilia, tume-*save* shilingi 250,000 bila kuangalia wapiga kura wetu wataathirika kiasi gani kwa kuongeza shilingi 40 kwa lita? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, siungi mkono kabisa suala la kusema hiyo imefutwa na watu wanashangalia. Tena bahati mbaya walisimama na kushangilia kabisa kufutwa kwa *motor vehicle* halafu akaongezewa aliyempigia kura kumleta huku Bungeni. Mimi nilipata wakati mgumu sana na ni hatari sana! Ni lazima tufike hatua tuwe na uchungu na huruma kwa watu maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kuishauri Serikali, tutafute namna bora ya kushughulika na *motor vehicle.* Tuachane na wananchi kuwabebesha mzigo wa *motor vehicle,* wazilipe kupitia mafuta ya taa ambayo yameongezwa na yanatumiwa na asilimia zaidi 70 ya Watanzania walioko vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie haki na maslahi ya wafanyakazi. Nimepitia kitabu cha kaka yangu

Mheshimiwa Mpango, chote hakuna kilipotaja maslahi ya wafanyakazi; hakuna walipotaja nyongeza ya mishahara kwa wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2016 wafanyakazi hawakuongezwa mishahara, wakatoka patupu. Mbaya zaidi kwa mujibu wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, hata ile *Statutory Annual Increment* hawakupewa. Iko pale! Kwenye Waraka wa Mishahara ukiangalia kule mwishoni kuna nyongeza ya kila mwaka. Nyongeza ya kila mwaka haihitaji kuja Bungeni, wala haihitaji kujadiliwa, ni *automatic,* kila mwaka unapewa. *Annual increment* hawakupewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu tena imekuja pako kimya. Wafanyakazi wanaambiwa chapeni kazi tu; hapa kazi tu! Kazi ipi? Ni kazi ipi ya bila kula? Kazi ipi wafanyakazi wana-*starve,* wana maisha magumu, mshahara walioupata ni ule ulioachwa na Serikali ya Awamu ya Nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Awamu ya Nne hawajawahi kuongezwa mshahara mwingine. Haya maisha tunakwendaje na wafanyakazi? Matokeo yake wakidai haki zao ni vitisho. Mtafukuzwa, utaondoka, tutakutumbua na kadhalika. Haitalisaidia Taifa hili. Wafanyakazi waongezwe mishahara ili waweze kuongeza tija. Kama hakuna mshahara, hakuna tija hata mngepeleka vitisho vya namna gani, haitasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madai ya wafanyakazi hayajazungumzwa popote namna ya kuwalipa. *Plan* ya kulipa iko wapi?

Pamoja na kiasi kidogo kilichotajwa, shilingi bilioni 156, ambazo mimi nasema ni za uongo, kwa sababu walimu tu wanadai shilingi trilioni 1.06 na zenyewe hakuna *plan* ya kuwalipa, bajeti haijataja. Mnadhani wafanyakazi hawa wataipongeza hii bajeti? Mfanyakazi atakayeipongeza hii bajeti atakuwa na roho ngumu na ujasiri wa kujifunika shuka moja na nyoka. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira mpya hazikutajwa popote. Tuliambiwa kuna wafanyakazi 52,000 wataajiriwa mwaka huu, kwenye bajeti imetajwa ukurasa wa ngapi? Hawa wasomi wanaosomeshwa kwa fedha za Serikali, tena wengine wamepita vyuo vikuu na tumewakopesha fedha kupitia kwenye *Loan Board,* tunatarajia waje walipe hiyo mikopo wakishapata ajira. Ajira ziko wapi ili walipe fedha za *Loan Board* na wengine waendelee kukopa? Tusishangilie wasomi kuendelea kutembea mitaani, kuzurura mitaani na vyeti vimejaa kwenye *briefcase,* ni hatari kubwa. *Batch* zinatoka, vyuo vikuu wanamaliza, vyuo vya kati wanamaliza, wapo tu na hakuna anayeshtuka kwamba hawa hawana ajira. Mpango wa kuwaajiri uletwe hapa na Mheshimiwa Waziri atakaposimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee vyanzo vya mapato ya Halmashauri. Nina bahati mbaya, rafiki yangu Mheshimiwa Simbachawene hayupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mtu ambaye nimekuwa nikilalamikia *D by D* na wanasema iko bomba. Sasa leo *D by D* imemalizwa na Serikali Kuu. Ni jambo jema, kwa sababu kuna jambo ambalo nilikuwa najiuliza, kwa nini Wizara ya Elimu isitoke kule ikawa inajitegemea isiingie kule Halmashauri? Wakasema mambo ya *D by D.* Sasa *D by D* imeliwa na Serikali Kuu. Vyanzo vyote vya mapato vimechukuliwa na Serikali Kuu na sisi tunashangilia, Halmashauri zinakwenda ku-*starve*, Halmashauri zinakwenda kufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Property Tax* mmebeba ambayo iliwashinda kukusanya mwaka 2016. Tumetoka hapo, kama vile haitoshi, tumeenda kwenye mabango; mpaka mabango mnayafuata kwenye Halmashauri, nayo yameshindikana huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima Mheshimiwa Waziri wa Fedha aje na mbadala wa vyanzo alivyoviondoa kwenye Halmashauri. Aje na mbadala, ni chanzo gani kitakachoendesha Halmashauri kule chini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Kakonko ni changa sana. Ukiondoa vyote hivyo vinavyoondolewa, Halmashauri ya Kakonko haitafanya kazi yoyote; mwisho mtaifunga. Maana nasikia kuna utaratibu wa kutaka kuzifunga baadhi ya Halmashauri ambazo hazitafikia uwezo wa makusanyo, wanakusanya kutoka wapi, wakati vyanzo vyote vya makusanyo mmebeba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la miundombinu, bado...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kasuku.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nawashukuru sana kwa kufanya kazi ya Kibunge hasa katika kupiga makofi. *(Makofi/Kicheko)*

Pili, niseme tu, someni hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha vizuri, lakini kuhusiana na suala la *Property Tax,* hii Kodi ya Majengo ambayo ni ya Halmashauri kwa mujibu wa sheria, kilichofanyika siyo kwamba wananyang'anywa, wanataka tu kazi hiyo ya kukusanya ifanywe na *TRA...*

*(Hapa baadhi Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Ndiyo! Wameshaanza, ili sasa mje mwiambie Serikali kwamba makusanyo ya *TRA* kwa kipindi hiki hayakidhi malengo ambayo...

*(Hapa baadhi Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Ndiyo kazi yetu hapa! Eeh!

Kwa hiyo, tulieni tu mtayapata maelezo mazuri. Nimeshawasema wa kwanza mchana ili muwe na uhakika

tu. Mheshimiwa Mwambalaswa, Mheshimiwa Almas Maige na Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali. Baadaye tutajipanga upya tena, mtachangia tu. Ahsanteni sana.

Nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10. 00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2016 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Nilitaja wale wa kwanza watatu. Kwa hiyo, tunaanza na Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, atafuatiwa na Mheshimiwa Almas Maige na Mheshimiwa Riziki Mngwali, ajiandae. Mheshimiwa Mwambalaswa!

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *sandiangu wa ukulu* kabisa, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia hoja hii iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuunga mkono hoja hii mia kwa mia. Nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu na wataalam wote waliotayarisha Bajeti ya mwaka huu. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia, kuna jambo moja dogo linanikera sana, naomba niliseme hapa hewani. Terehe 2 Juni, kwenye Bajeti ya Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Saed Kubenea alisimama hapa akinituhumu mimi Mwambalaswa kwamba kwanza ni Mkurugenzi kwenye Kampuni ya Umeme ya Upepo ya Singida na kwamba Ukurugenzi wangu huu nina mgongano wa maslahi *(conflict of interest)* kwa sababu nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na vilevile nilikuwa Mjumbe wa Bodi ya *TANESCO. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna *project* nyingine ya umeme wa upepo, kule kuna *concept,* kuna *idea* na *idea* hii imeanza mwaka 2000. Mimi nimekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati mwaka 2013, hii imeanza mwaka 2000. Mgongano wa maslahi unatoka wapi? Nimekuwa Mjumbe wa Bodi ya *TANESCO* mwaka 2008. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kubenea aliienda mbali zaidi, akasema Mheshimiwa Mwambalaswa alizuia kutekeleza Ripoti ya *Richmond* ya Mheshimiwa Mwakyembe. Mimi Mbunge nitazuiaje ripoti? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huyu Mheshimiwa ananisemea maneno ya uwongo bila sababu yoyote. Ananishambulia bila sababu! Kule kuna *concept, is not a company! Is not a project, is a concept.* Ni ya waswahili fulani, sisi na walimu wa Chuo Kikuu tumeacha wazo hilo, lakini linapigwa vita na watu kama yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani yeye Mheshimiwa angeona hii *concept* ni ya mzungu angeunga mkono kama vile ambavyo Mheshimiwa Rais amezuia makontena ya makinikia, amempinga, lakini angezuia mzungu, angemuunga mkono. Jamani tusitembee na *Ph.D* mifukoni za mitaani. *Ph.D (Pull him Down).* Tuinuane waswahili kwa waswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kubenea namfahamu sana, ni mdogo wangu, rafiki yangu wa miaka

mingi. Alipoanzisha Kampuni ya Jarida lake la Mwanahalisi, mimi na wenzangu tulimchangia *computer* yake ya kwanza tulinunua sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulimnunulia, lakini unaona anakonipeleka! Mheshimiwa Kubenea alimwagiwa tindikali machoni; amelazwa hospitali, Mheshimiwa Rais Kikwete, Rais wa Awamu ya Nne ameenda kumwona hospitali na amemchangia pamoja na sisi aende akatibiwe India, akageuka na magazeti yake anamshambulia Mheshimiwa Kikwete. Huyo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya, Mheshimiwa Kubenea amechukua miaka kama nane anamshambulia Mheshimiwa Lowassa kila siku, ona! Lowassa katika kashfa mpya, hilo hapo; Rostam Hajaandika, hilo hapo; Wanaomsafisha Lowassa Hawa Hapa, hii hapa; Genge Laundwa Kumkabili JK, hili hapa; Rostam Aziz Hashikiki, hili hapa; Mabilioni Yatengwa Kumsafisha Lowassa, hili hapa; Lowassa Kutinga Kortini, hili hapa; kila siku! Leo anamsujudia Mheshimiwa Lowassa, huyo huyo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi lile ni wazo, sina *conflict of interest* yoyote, ni wazo. Kama ana matatizo na mimi aje tuongee. Mimi ni rafiki yangu, namfahamu huyu kijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, nasema hivi, sijui kama anatumwa na dhamira yake au analipwa. Sijui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwapongeza Wataalam na Mheshimiwa Waziri kuhusu bajeti iliyo mbele yetu, bajeti nzuri sana, mti wowote wenye matunda unapigwa mawe. Kwa hiyo, mawe tunayategemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahi sana kwamba barabara yangu ya Mbeya - Chunya - Makongolosi imefika Chunya kilometa 72, ahsante sana Serikali ya JK na Serikali ya Mheshimiwa Magufuli ahsanteni sana. Nimefurahi kwamba kwenye bajeti hii ambayo iko mbele yetu, sasa wanaanza

kujenga Chunya kwenda Makongolosi na Mkola na wanafanya kama alivyoagiza Mheshimiwa Rais kwenye kampeni kwamba tuanze Makongolosi kuja Chunya. Wataalam wako pale kwenye manunuzi, ninashukuru sana na nimefurahi sana. Najua huku kutoka Mkiwa kwenda Itigi iko kwenye bajeti, itaanza kujengwa ili baadaye tukutane katikati hii barabara ambayo zamani ilikuwa *the Great North Road* iwe kwa kiwango cha lami barabara nzima. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli ya *TAZARA,* kama ilivyo reli ya kati ambayo sasa inaboreshwa na Serikali hii ili tutumie uchumi wetu wa jiografia, tutumie nchi yetu kijigrafia kuweza kuzihudumia nchi ambazo ziko *landlocked,* ili tuweze kuinua kipato na uchumi wa nchi yetu; na reli ya *TAZARA* iko hivyo hivyo. Reli ya *TAZARA* yenyewe iko zaidi ya *meter gauge,* ndiyo maana matreni ya Afrika Kusini yanaweza kupita kwenye reli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haihitaji maboresho ya makubwa sana, inahitaji tu labda kuweka umeme ili treni za umeme zipite. Ile ya Kati inapokuwa imekamilika na ya *TAZARA* nayo iwe imekamilika tuweze kuihudumia Zambia, Zimbabwe, Malawi na Kongo ya Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja wa ndege wa Songwe, nashukuru sana Serikali za awamu zote kwa kujenga uwanja wa ndege pale Songwe, Mkoa wa Mbeya. Uwanja ule uko *very strategic* kwa kutega uchumi kwenye Mikoa yote ya Nyanda za Juu Kusini na nchi zote majirani zetu, lakini sasa hivi taa hazipo za kuongoza ndege. Ndiyo maana mara moja, mbili, tatu ndege inakwenda, inakuta ukungu, inarudi Dar es Salaam hasa wakati wa mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba bajeti ya mwaka huu hii ambayo iko mbele yetu, najua fedha imo, tukamilishe kuweka taa kwenye uwanja ule ili tuweze kupata fursa zote za kiuchumi kwenye uwanja huo wa Songwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii bajeti ni nzuri mno, siyo ya kuisemea sana, ni ya kuunga mkono moja kwa moja. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea, Mheshimiwa Maige Almas.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru sana kuniruhusu nichangie hoja hii iliyoko Mezani kuhusu Bajeti na hasa mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite kwenye madini. Madini popote duniani ndiyo inayotoa tathmini ya utajiri wa nchi. Kwa hiyo, kabla ya mafuta, madini yalikuwa ndiyo kipimo cha utajiri wa nchi. Kwa hiyo, matapeli na waaminifu wamejikita kwenye madini. Kwa hiyo, Serikali yetu ijue kwamba kwenye migodi yetu hapa kuna makundi ya aina mbili; wako watu waaminifu sana na wako wahalifu. Hawa wahalifu wanangojea fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uelewa wangu mdogo, biashara hii ya madini, hasa kwa wenye migodi, wana malengo yao na malengo yao ni kuwa matajiri. Utajiri huo wanaupata kwa aina mbili. Kwanza kwa kuuza madini yenyewe, lakini pia kufanya biashara na migodi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa makampuni haya, aidha yananunua mitambo kutoka kwenye kampuni tanzu au kampuni mama, kwa hiyo, matumizi ya mitambo ambayo kwa mfano mgodi ulianza kuchimba uwekezaji mkubwa wakapata na *holiday* ya kutolipa kodi, lakini wakanunua mitambo ya kuchimba labda mita 100; kwa kipindi chote hicho watapata hasara. Gharama ya mitambo na dhahabu wanayoitoa, hawalipi kodi. Baada ya mita 100 watawekeza tena kutoka mita 100 na kuendelea na hivyo hivyo hawatapata faida, watapata hasara. Kwa hiyo, kodi haiwezi kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo matatu ambayo ni muhimu sana ili nchi iweze kufaidika na madini, la sivyo itabaki na mashimo ya madini. Madini yote yataondoka. Mambo haya matatu, la kwanza, ni lazima Serikali iwe na hisa kwa niaba ya wananchi wake katika kila mgodi ambao unafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa kuwa na hisa, Serikali itakuwa na Wajumbe wake wa Bodi, lakini pia itakuwa na wafanyakazi wa Bodi, kwa hiyo, watajua kiasi gani madini yanachimbuliwa na kiasi gani yanauzwa nje. Kwa sisi kuwa nje, tunawaachia wale wote madini ya kwetu na wachimbe wapeleke nje, hatujui kiasi gani cha madini kinachimbuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala la pili, nalo ni ulinzi. Sasa hivi migodi yetu yote ina viwanja vya ndege na ndege zinatua pale na kuondoka na madini na haziji Dar es Salaam wala haziendi Mwanza wala Tabora, zinakwenda nje ya nchi. Matokeo yake tunabaki na mashimo makubwa ya madini kule, lakini hatuyaoni madini yale.

Katika taarifa ya Tume iliyotolewa leo na tunashukuru leo karibu Watanzania wote tuna msiba baada ya kujua kiasi gani tumeibiwa, hata furaha ya kuchangia inakuwa taabu kidogo. Madini yote yameenda nje, tumebakia na mashimo, lakini hatuna chochote tulicholipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu ambayo ni mbaya zaidi ni hii ya kutofuata *local content.* Makampuni haya yote yanakuja kutoka nje, yanakuja na makampuni ya ulinzi, kazi ambayo ingefanywa na makampuni ya nchini hapa. Wanakuja na makampuni ya ulinzi kwa sababu hawataki Watanzania tujue ulinzi ule, kiasi gani mali inatoka? Kwa kufanya hivyo, miaka yote hii ambayo makampuni haya yamechimba yamekuwa na makampuni yao ya ulinzi na kwa hiyo, mali iliyotoka nje hatujui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, ni manunuzi. Manunuzi imekuwa ndiyo unapofanya mizania ya kulipa kodi

ili uonekane kama unapata faida, wanajaribu kupanga kiasi gani tumepata na kiasi gani tumetumia na miaka yote miradi mingi ya migodi imeonesha kwamba wamepata hasara badala ya faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kungojea sisi tupate mapato, kampuni zioneshe mapato, ndipo tudai kodi *TRA* waende, tumekuwa tunapata hasara badala ya kupata faida. Manunuzi haya kama sisi tungekuwa na nafuu ya kujua kiasi gani gari moja la kuchimbia mgodini linauzwa; na je, *dumper* lile shilingi ngapi? Tungeweza kujua kwamba tunadanganywa. Kwa vile tuko nje, hatuwezi kujua kiasi gani tunadanganywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la ulinzi wa mali migodini lipo kisheria. Makampuni haya na siyo haya tu, hata ya gesi na mafuta yamekataa katakata kutumia makampuni ya Tanzania na wWanazo sababu. Mimi nimekuwa Mwenyekiti wa Makampuni ya Ulinzi kwa miaka 15 na nimejitahidi sana kupata makampuni ya Tanzania yakalinde kwenye migodi, imeshindikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu kubwa ni kwamba wanasema Kampuni za Tanzania hazina viwango, hazina sheria, hazina kanuni na hazina miongozo. Ndiyo maana nilipokuja Bungeni humu jambo la kwanza nililolifanya ni kuleta Muswada Binafsi wa Sheria ya Sekta ya Ulinzi Binafsi ili hiyo Sheria iunde Mamlaka ya Kampuni za Ulinzi Binafsi, ambapo mamlaka hiyo ndiyo itakayodhibiti uwezo wa kampuni. Kampuni ambazo zinalinda migodini, nyingine hazina uwezo kuliko kampuni za Tanzania, lakini hatuna mizania ya kupimia kwa sababu hatuna Mamlaka ya Kampuni za Ulinzi Binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo, ni lazima tusonge mbele. Serikali iliniomba mimi rasmi kwamba, tunaomba Muswada wako huo tuulete sisi, lakini huu ni mwaka wa pili, na mimi naona kama tunachelewa. Yaliyosemwa leo katika taarifa ile ya Tume ya Pili ya Mheshimiwa Rais inasikitisha, ni kama vile mali imechukuliwa

wenyewe wamelala au hawapo. Tungekuwa na macho yetu kule, tungekuwa na Sheria ya Ulinzi ya Binafsi, maana haiwezekani tukapeleka majeshi kwenda kulinda migodi ya watu binafsi au polisi kulinda migodi ya watu binafsi. Duniani kote migodi hii inalindwa na kampuni za Sekta ya Ulinzi Binafsi, lakini kwa kufuata sheria iliyopo na mamlaka iliyopo. Umefika muda sasa Serikali ilete Muswada hapa utakaosaidia sisi kuweza kudhibiti migodi yetu kwa macho ambayo tunayaamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nirudi Jimboni kwangu. Tunayo matatizo makuwa sana Jimboni kwangu, hakuna maji. Tunakubali kwamba kutakuwa na Mradi wa kutoka Ziwa Victoria, lakini nikisemea Mkoa mzima, huo mradi haufiki Urambo, haufiki Kaliua, haufiki maeneo yote ya Jimbo langu; na chini ya ardhi ya Jimbo langu kuna mwamba. Kwa hiyo, visima vingi vilivyochimbwa vimekufa, zimebakia sehemu chache zenye chemchem kama vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yangu, nimegharamia kwenda kuchunguza wapi maji yapo? Pale maeneo machache ambayo tumepata maji, Serikali iniunge mkono ije ichimbe maji kwa faida ya wananchi wangu. Tuna taabu ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kusimama hapa kila siku nagombana na Waziri wa Maji, nagombana na kaka yangu Mheshimiwa Kamwelwe. Naomba nipate ahadi sasa kwamba watakuja kuchimba vile visima hata vitatu, vinne kwa faida ya Jimbo langu. Wananchi wangu wananishangaa sana, kama nimegharimia mamilioni kuwaleta watu wapime maji, maji yakapatikana, kuchimba imekuwa taabu! Mimi napata taabu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni upande wa mawasiliano. Wilaya yangu ni mpya, haina barabara za ndani. Ili uje Tabora Mjini lazima uende Nzega ukapite kule kwenye barabara ya lami ndiyo uje mjini. Imekuwa gharama kubwa; watu wanapanda baiskeli, halafu wanaacha baiskeli wapande magari kwenda mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili suala la barabara za ndani liangaliwe sana katika bajeti. Ipo barabara moja tu ya Tabora - Mambali ambayo ilikuwa iwekewe lami kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, sasa imewekewa iwe *TANROADS,* lakini barabara zote ndani hakuna. Tunatembea kwa miguu kama mwaka *BC* huko!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali yangu inisikie na haya ambayo nimeyasema kuhusu madini, yachukuliwe kwamba ni mambo muhimu sana. Mambo matatu; manunuzi, ulinzi, kwamba ije Sheria ya Sekta ya Ulinzi Binafsi, lakini pia mambo yanayohusu hisa za Watanzania ndani ya migodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyeki, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali, atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Ndassa na Mheshimiwa Anna Lupembe ajiandae.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Niruhusu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, muumba mbingu na ardhi, aliyetujalia sote uhai, afya na uzima na kutuwezesha kuwa hapa tukijadili hili suala tunalojadili kwa mara ya pili sasa katika kipindi hiki au awamu hii ya uongozi tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nifuatilize kwa jambo jema kabisa ambalo limewahi kutendwa hapa duniani ambalo ni kuhusiana na kuusia mema na hasa kuusia kumcha Mwenyezi Mungu. Basi na mimi niwausie kama ninavyousia nafsi yangu kumcha Mwenyezi Mungu kwa namna inavyopasa kumcha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni chini ya uongozi thabiti wa Mheshimiwa Mbowe, akisaidiwa na mimi hapa ndugu yake, lakini pia chini ya usaidizi mkubwa kabisa wa Mwenyekiti Mwenza, kaka

yangu mpenzi, Mheshimiwa James Mbatia. Ama timu ya UKAWA inafanya kazi na kwenye ukweli siku zote uongo hujitenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika pongezi ambazo ningependa kuzitoa leo hii kwa uzito wa kipekee kabisa, nimpongeze kiongozi wangu mwadilifu, mcha Mungu, muungwana, mpenda amani na yeye mwenyewe ni kipenzi cha watu; huyu sio mwingine ni Katibu Mkuu Mwenza wa UKAWA, Mheshimiwa Maalim Seif Sharrif Hamad ambaye yeye siyo tu ana dhamira ya kuendeleza amani, bali anafanya kwa kitendo. Anatekeleza suala hili, anaendeleza amani na maelewano katika nchi hii na kwa kweli penye ukweli pasemwe. Laiti Maalim Seif angekuwa kama viongozi wengine wa Afrika wale ambao wana maslahi binafsi au wana ubinafsi, basi Bunge hili inawezekana ingekuwa saa hizi tunajadili mengine au nchi hii kwa ujumla wake ingekuwa katika hali tofauti na hii tunayoiona sasa hapa. Nampongeza sana, namwomba Mwenyezi Mungu amzidishie subira na ucha Mungu na kwa hakika yeye ni miongoni mwa wenye kufaulu duniani na akhera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi wala si mtaalam sana wa takwimu lakini masuala mengine yamekuwa *tabled* hapa wiki iliyopita na kwa vigelegele kabisa mpaka watu wakasimama wima mimi nilikuwa nashangaa na naamini ulikuwa unaniona, nilikuwa nashangaa hivi kweli hotuba hii inastahiki kusimamiwa, kwa lipi lililomo mle jipya? Walichojitahidi sana ni kucheza na maneno, *semantics genetics* tu, sarakasi za maneno lakini hazina jipya lilotuletea hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, semeni kwa ukweli wa dhati wa mioyo yenu Waheshimiwa hivi unapoongeza tozo kwenye mafuta ya taa nia yako hasa ni nini? Wapiga kura wetu walio wengi lile wenyewe wanaita jiko la mchina ndiyo gesi yao na ndiyo *electric cooker* yao. Hivi unavyowaongezea hiyo gharama ya kununua mafuta ya taa unataka waende wapi? Unaongeza bei ya mafuta wakati ambapo tunakaza nati kwenye masuala ya mazingira na kuwazuia kukata miti, hao

wananchi waishi maisha ya namna gani hebu niambieni Waheshimiwa? Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri ukija hapa tuambie hawa walala hoi wa Tanzania wewe unataka waishi maisha ya aina gani mwaka huu wa 2017/2018? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesahau yule Malkia wa Ufaransa alikuwa wa mwaka gani lakini katika kituko chake cha ile kuonyesha kiasi cha yeye kuwa mbali na *realities* na uhalisia wa mambo, wananchi walipoandamana wakasema hatuna mikate akawaambia *why don't you eat cake,* hamna mkate kuleni keki. Kumbe wenzie wanasema hawana mkate yaani hawana hata kile cha kuendesha maisha ya kawaida, sasa ndiyo tunachokifanya hapa. Tumeshindwa kutafuta shilingi trilioni zile pungufu 29 leo tunasema tunataka shilingi trilioni 32 tunazitoa wapi kwa hali halisi? Halafu hatuonyeshi mbadala ulio mahsusi na makini wenye kueleweka kwamba hivi ndiyo vyanzo ambavyo vinakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani nakusihi sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, hebu soma kwa uadilifu bila hiyana maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ambayo *Masha Allah* leo kijana wangu Silinde kaya-*present* yakiwa kwenye fomu yake hasa. Yapitie kwa umakini kabisa, utaona mapendekezo gani yamo mle kuhusu vyanzo vya mapato, lakini pia kuhusu ipi iwe ndiyo *budget figure* yetu. Tuache kucheza na maneno hapa, tuache kuwadanganya walimwengu lakini mwisho wa yote tunajidanganya sisi wenyewe. Hivi unaposema nitakimbia kilometa saba ukashindwa ukaishia mbili na nusu halafu unakuja tena unasema sasa mara hii nataka kukimbia kilometa kumi, inatokea wapi mambo hayo? Jamani kwa nini tunajidanganya hivi? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Wanakula madawa.

**MHE. RIZIKI S. MNGWALI:** Mheshimiwa Mwalimu Bilago pale kauliza huyo aliyeturoga nani huyu? Sisi kule kwetu wanasema ukiona hali kama hii huyo aliyekuroga kafa

maana angekuwa hai angekuhurumia. Laiti yule aliyeturoga Watanzania angekuwa hai akatuona tunavyodhalilika humu, tunavyosema mambo ambayo hayana kichwa na miguu wala hayana mbele wala nyuma angetuhurumia. Basi akapunguza, wanasema anapunguza ile dozi, basi na sisi tungepata ahueni. Waheshimiwa Wabunge nawasihi sana tumwogope Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwalimu wangu mmoja wa jiografia nilipokuwa *O-level, Mrs. Seif,* Mwenyezi Mungu ambariki sijui yuko wapi sasa hivi, katika ufundishaji wake mzuri sana wa *geography* ya maeneo alikuwa anatupandisha ndege na meli lakini tuko Kisutu Sekondari. Anatuambia fumba macho leo tunaondoka Zanzibar kwa boti namba fulani tumeingia baharini, mawimbi yanafanya vile, fumba macho na kweli tunafumba macho tuna-*internalize* ile safari yote mpaka lile aneo jipya tunalokwenda. Hebu na sisi tufumbe macho tu-*internalize* haya mambo, tu-*internalize* hii bajeti *process* yetu kila *figure,* tumvute kwenye picha hii kubwa kila mtu ambaye anaguswa na bajeti hii, tusijifikirie sisi wenyewe tu Waheshimiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mambo ambayo mimi naamini au katika vitu ambavyo ninajua kabisa bila hata kufundishwa wanasema, *I am spill of effect* au *trickling down effect* ni masuala ya mafuta. Unapoongeza tozo kwenye *diesel* na *petrol* unatarajia hao wenye mabasi yao akina Mheshimiwa Shabiby watawacha nauli ile ile, si watapandisha? Madaladala si watapandisha nauli? Mwalimu Bilago kasema hapo unadhani bidhaa itakayotoka Dar es Salaam mpaka ikafika huko Kakonko sijui itakuwa bei ile ile, itakuwa bei juu. Sasa sisi tunafanya nini jamani mbona tunagusa mahali sipo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunafanya jambo kama hili wakati tunadai eti tunataka kuwasaidia walalahoi, hatuwasaidii walalahoi. Labda mniambie mmekuja na *system* ambayo mtatengeneza kwenye vile vituo vya mafuta ile gari ikienda inakuwa *detected,* hii ni ya Mheshimiwa Ashatu mkate huyu, hii ni gari la daladala usikate labda iwe hivyo lakini

kama tunaweka hii *blanket amount* halafu kwa *system* hii ya kawaida kwa kweli tunakwenda kuwaumiza watu wetu na walio wengi wataanza sasa kutumia hii tunaita *TZ eleven,* watatembea kwa miguu badala ya kutumia vyombo vya usafiri kwa sababu hawatamudu kutoa gharama hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waswahili wanasema kama ilivyo dawa ya jipu kulitumbua dawa ya deni kulipa. Msitumie maneno lihahimilika, linavumilika, linahamishika, linakwenda wapi? Bado linabaki ni deni letu la taifa, tulilipe, tuwe na *clean slate* halafu tunaanza upya. Watu tumelalamika hapa na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti kasema kuhusu riba, riba tena inatuning'inia rohoni hapa hatujiwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitawaambia jambo lakini ninyi mtakasirika kwa sababu lilishaingia Bungeni humu likaleta siasa na chuki, *go OIC* ambapo tunapata mikopo haina riba. Kama *OIC* mnaiona ina ukakasi, mimi naamini kama hiyo *economic diplomacy* yetu tungeitumia vizuri wangetutafutia *partners* ambao wangeweza kutupa mikopo kwa bei nafuu kabisa. Naamini hao watu wapo, hizo nchi zipo kwenye Bara la Ulaya tungeweza kupata hao *partners* ambao wangetupa *arrangements* zenye unafuu sana na mikopo ambayo kweli tungeweza kuhimili. Siyo hii mikopo ambayo tunaenda kukopa kibiashara kwenye *arrangements* ambazo zinatutoza riba kubwa mwisho wa yote *capital* hatulipi na wala hiyo riba inayoongezeka kila mwaka hatulipi, tunaendelea kubadilisha maneno hapa mara leo linahimilika, kesho sijui litavumilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri husika hebu atuambie vizuri haya maneno hasa mwisho wake nini na nini anapotuambia tunaweza kuhimili deni ili mwisho wake iwe nini. Atuambie tu hii bajeti yake inajibu vipi vilio vile ambavyo tulivisikia hapa wakati tunajadili *Sectorial Ministries.* Tulipokuwa tunasema maji, kila mtu hana maji na Mheshimiwa kaka yangu Almas anamalizia

hiyo imekwisha, Wizara ya Maji ilishapita na hii bajeti haina hata maji humu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejadili hapa kila kitu elimu matatizo, afya mtihani, maji ndiyo hayo, barabara hazisemeki, kila kitu kila kitu hakipo. Hii bajeti hii hapa hii ukiondoa hiyo dhamira ya kuendeleza amani ambayo wala haipo mnafanya nini ku-*address* vilio vyote vile ambavyo vimesemwa katika Bunge lako hili Tukufu kuhusu maisha ya Watanzania kwa mustakabali wa nchi yetu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Anna Lupembe na Mheshimiwa Sixtus Mapunda ajiandae.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa nafasi hii. Nianze kwa kuiunga mkono bajeti ya Serikali, lakini pia niunge mkono taarifa ya Kamati ya Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza sana mwasilishaji wa upande wa pili, anasema bajeti ni mbaya sana haijawahi kutokea, lakini humu mimi ni wa muda mrefu kidogo bajeti hii ni bajeti ya karne haijawahi kutokea, bajeti ni nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashauri tu wenzangu, tunaweza tukawa wavivu wa kusoma, ni vizuri twende tusome ukurasa kwa ukurasa mtari kwa mstari kwa mstari. Tusirukie kusema kwamba bajeti hii ni mbaya, siyo mbaya hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna msemo wa kiswahili unasema ukiwaona adui zako wanachukia jambo lako endelea nalo, lakini ukimwona analifurahia liache haraka iwezekanavyo. Kwa hiyo, hii ni jambo jema sana Mheshimiwa

Waziri wa Fedha na timu yako. Bajeti hii haijawahi kutokea, ni bajeti nzuri nzuri nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini waswahili wanasema kama una shughuli mahali, kuna harusi au kuna jambo fulani unaalika akina mama kwenda kuchambua mchele. Katika kuchambua mchele unaondoa zile chuya na michanga midogo midogo unabakiza mchele. Sasa wenzangu wanachagua mpaka na mchele badala ya kuchagua mchanga na chuya. Ni vizuri tukajitahidi kwenye bajeti hii tukachagua yale mabaya ambayo ndiyo yanatakiwa yaboreshwe lakini ninyi mnachukua yote kwa pamoja. Tujifunze hii ni bajeti ya Serikali yetu na ninyi mmekuja na mbadala yetu lakini hizo *figure* mlizotaja hazina uhalisia hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri nikuombe labda safari nyingine vitabu hivi tuwe tunavipata mapema kidogo kwa sasa hatuwezi kulinganisha kwa sababu imesomwa pale lakini hatuwezi kuona popote pale. Kwa hiyo, niombe sana bajeti hii Waziri wa Mipango sisi kama CCM ni bajeti yetu, lazima tuiunge mkono kwa sababu ina mambo mengi sana kuhusu wananchi wetu na hata wananchi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanakimbilia kusema unajua hii tozo ya shilingi 40 kwenye magari, nilikuwa naongea na Mheshimiwa Shabiby hapa kuna mama mmoja ametoka kumtaja Mheshimiwa Shabiby, anasema katika ongezeko hili la shilingi 40 kwa lita moja, yeye ndiyo mwenye mabasi, hakuna hata senti tano itakayoongezeka. Sasa wewe humiliki hata bajaj au baiskeli unasema itaongezeka, itaongezeka wapi? Mwenye mabasi yake anasema hakuna senti tano itakayoongezeka. Kwa utaratibu wa Chama cha Mapinduzi, bajeti iliyopikwa vizuri ongezeko la shilingi 40 kwa lita moja ingekuwa ni vizuri zaidi tungeshauri badala ya kulalamika kama ambavyo sasa mimi nashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu liko suala la kuwatua ndoo akina mama kuhusu suala la maji, nishauri na nikuombe kwenye tozo tuna shilingi 50 tuchukue hii shilingi

40 tuiongeze kwenye shilingi 50 ili tupate shilingi 90 ziende zikahudumie maji vijijini. Hii shilingi 50 tayari ipo na sababu kuna ongezeko hili la Sh.40 kwa lita moja, shilingi 50 na shilingi 40 unapata shilingi 90, tuziweke pamoja hizi ziende zikahudumie maji vijijini na hiyo ndiyo itakuwa suluhisho la kuwatua ndoo akina mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maeneo mengi, nakumbuka asubuhi katika swali namba 368, 369, 370, haya maswali yalikuwa yanahusu maji, kila Mbunge alisimama mpaka ukawa unatuhesabu lakini ukashindwa kutuchukua wote kwa sababu wengi tulikuwa tunataka kuuliza kuhusu swali la maji. Kwa hiyo, niombe sana Waziri wa Fedha, Waziri wa Maji, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti mtakapokwenda kule kwenye *Finance Bill* tafadhalini sana sana muangalie suala hili kwa sababu bila maji tutakuwa hatujawasaidia akina mama. Nikushauri sana sana na naomba nirudie hii, kwetu sisi kama wana CCM na hili nalisema wazi kwa sababu maji vijijini kwa akina mama ndiyo kete yetu ya CCM lazima tuibebe. Hamsini, arobaini, tisini naomba tuziunganishe tuzipeleke kwenye maji ili kusudi tupate maji kwa ajili vijiji vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyo vijiji vingi kule kwangu vinahitaji maji na suluhisho kubwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha haipendezi sana tunalo Ziwa Tanganyika, Nyasa, Victoria lakini ukienda Kigoma na wilaya zake zingine hazina maji lakini maji yako Ziwa Tanganyika, ni wakati sasa tuamue. Vivyo hivyo kwa Ziwa Nyasa, Victoria lazima tuweke nguvu. Vilevile tunayo mito mingi imetuzunguka, naomba tuamue sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini Serikali ya Chama cha Mapunduzi chini ya Jemedari Mkuu, John Pombe Magufuli ambaye leo amewaonesha Watanzania, wapo watu walikuwa wanadhani kwamba anatania, sasa leo wamesikia na wameona kwa macho yao kwamba watalishughulikia suala hili. Sisi kama Watanzania, Waheshimiwa Wabunge hapa nafikiri kitu ambacho tungefanya ni kuomba Serikali kama navyoiomba sasa kama kuna mikataba ambayo

haitunufaishi sisi tuilete hapa haraka iwezekanavyo ili tuirekebishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kwa mapato yale kwa kiasi kile kilichotajwa na kama sikosei Waziri wa Fedha sijui ndiyo yule pale Dkt. Mpango nafikiri ulikuwepo umesikia wale wataalam wanasheria wamesema kwamba hapa tunapunjwa badala ya kumi tunachukua mbili. Kama mikataba hii ina matatizo, mimi nashauri tena Waheshimiwa Wabunge wa itikadi zote na vyama vyote tumuunge mkono Mheshimiwa Rais kwa sababu pesa zile zikipatikana, matrilioni yale yanayotajwa ambayo yanaweza kusaidia bajeti tano mara moja mbali ya hizi, miundombinu ya barabara, maji, reli, vitu vyote nafikiri vitakamilika kwa sababu tunaweza hata kukopesha nje. Niombe sana Waheshimiwa Wabunge...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Anna Lupembe atafuatiwa na Mheshimiwa Mapunda.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia bajeti yetu muhimu sana kwa ajili ya Watanzania. Naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuumba ametupa uhai na uzima leo tumekuwa hai na tunaendelea na wale wote wanaofunga nawatakia funga njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nimpongeze Rais wa Muungano wa Tanzania John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya kwa ajili ya Watanzania. Leo Watanzania wameona jitihada za Mheshimiwa Rais za kutetea maslahi ya Watanzania.

Naomba Watanzania wote tumuunge mkono Rais kwa kazi kubwa anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya. Vilevile naomba nimpongeze Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kuwa makini sana na kuchukua yale mahitaji yanayotakiwa na Wabunge na mnachukua mawazo, mmechukua mambo mengi kwa Wabunge ambayo mmeyafanyia kazi na mmeweka kwenye bajeti, naomba niwapongeze sana. Wananchi wote wanaunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. Ina maana leo kama kungekuwa kuna uchaguzi CCM ingepata asilimia mia moja. *(Vigelegele/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono bajeti ya Serikali kwa asilimia mia moja kwa sababu bajeti hii imeeondoa kero za wananchi kwa asilimia mia moja. Leo hii mimi mtu wa Mpanda ukiniambia bajeti haijawasaidia wananchi siwezi kukuelewa kwa sababu nilikuwa najua kero za wanachi wa Mpanda hususani Mkoa wa Katavi. Mkoa wa Katavi ni wa kilimo, leo hii tani moja yule mfanyabiashara mdogo mdogo anasafirisha mazao yake bure ina maana kuwa bajeti hii imemkomboa mfanyabiashara mdogo na mkulima nayetoa mahindi yake Mlele, Mpimwe magunia kumi anayaleta mjini anakuja kuyauza, mmemkomboa kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze sana Serikali kwa hilo ndiyo maana na wenyewe wameiunga mkono asilimia 100 bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niipongeze Serikali kwa kuanza kujenga *standard gauge* kwa sababu inafika Mkoa wangu wa Katavi. Reli hii itaturahisishia sana sisi wa kanda hii kwa sababu usafiri wetu mkubwa ni reli ya kati. Sasa kwenye reli ya kati mnatupitishia sasa reli ya kisasa ambayo ni *standard gauge,* naomba niipongeze sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba niipongeze Serikali kwa kununua ndege mbili ambazo zipo tayari na vilevile mmenunua tena ndege zingine tatu ambazo zitasaidia na uchumi wa nchi yetu utaongezeka mara mbili, tatu. Naomba sana niipongeze Serikali, leo ni kuipongeza kwa sababu haijawahi kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba niipongeze Serikali kwa kufuta leseni za magari. Leo wananchi wengi walikuwa wame-*park* magari yao, walikuwa hawana pesa za kulipia lakini mmewaondolea mzigo magari yote sasa yatatembea barabarani. Naomba niipongeze sana Serikali kwa kazi kubwa mliyoifanya kwa kuwaondolea adha wananchi kwani sasa watatembea na magari yao na watafanya biashara. Wengi walipaki magari, walikosa hela za kulipia lakini leo watatembeza magari, wataenda kufanya shughuli zao mbalimbali ili uchumi wao uweze kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na vilevile naunga mkono mapendekezo ya Kamati ya kupeleka fedha za tozo ya shilingi 40 kwenye maji itakayotoka kwenye dizeli, petroli na mafuta ya taa. Najua kabisa hii pesa ikienda Hazina siyo lazima ifanye jambo lingine inaweza kupendekeza hizi pesa shilingi 40,000 zikaenda kwenye maji kwa sababu akina mama wengi sana wanateseka na ukosefu wa maji. Naomba hii tozo ya shilingi 40,000…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ni shilingi 40.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni shilingi 40, si unajua tena, raha imezidi kutokana na bajeti nzuri sana, nzuri mno. Sasa hii shilingi 40 itaenda kwenye maji ili wananchi waweze kutatuliwa matatizo mazito tuliyonayo. Naomba Serikali, najua Waziri upo makini sana tunaomba hii tozo ya shilingi 40 iende kwenye maji ili wananchi sasa waweze kupata unafuu kwa sababu vijijini akina mama wanapata taabu sana kwa ajili ya maji. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mambo mengi yanayofanyika katika Serikali hii ni makubwa na mazuri sana.

Naomba tuendelee kuiunga mkono kwa sababu mnaiona jinsi gani inavyofanya kazi kwa ajili ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja upande wa kilimo. Mkoa wa Katavi sisi ni wakulima, naomba sasa tuweke mikakati mizuri, wale wananchi wa Katavi waweze kupelekewa mbolea kwa ukaribu zaidi na mapema ili kilimo chao kiwe na tija. Naomba Serikali yangu sikivu sasa hivi twende kwenye mbolea tuweke mikakati ya mbolea kwa mikoa yote inayolima ya Katavi, Rukwa, Mbeya na Ruvuma. Naomba Serikali yangu mbolea iwe kipaumbele, wapelekewe mbolea mapema na ukizingatia Mkoa wa Kigoma wenyewe wanalima mapema basi iwekwe mikakati mizuri ya kupelekea mbolea wakulima mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mkoa wangu wa Katavi tuna shida sana ya maji. Tuna Ziwa Tanganyika ambalo lina kina kirefu, tukilitumia ziwa hili nafikiri Mkoa wa Katavi matatizo ya maji yataisha kabisa. Naomba Serikali yangu sikivu tutumie Ziwa Tanganyika. Tumepata mafanikio makubwa sana kwenye Ziwa Victoria, tumeilisha Mwanza, Shinyanga na sasa tunaelekea kuilisha Tabora na bado hapo hapo hata watu wa Mkoa wa Singida wanatamani maji ya Ziwa Victoria yafike. Tukiilisha maji Mkoa wa Katavi kupitia Ziwa Tanganyika tutakuwa tumeondoa kero kubwa sana ya maji kwa sababu yale maji yatapita kwenye maeneo mengi na kwenye vijiji vingi na hatma yake maji yatakuwa mengi katika Mkoa wetu wa Katavi na shida ya maji itakwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja asilimia mia moja bajeti hii ya historia ya Chama cha Mapinduzi. Chama cha Mapinduzi tuna raha sana. Unajua ukifanya kitu kizuri lazima ujisifie, naunga mkono hoja asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Anna Lupembe kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Sixtus Mapunda atafuatiwa na Mheshimiwa Josephat Kandege na Mheshimiwa Musa Ntimizi ajiandae.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie bajeti hii ya kihistoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Comrade Senator* Ndassa amesema kwa uzoefu wake wote aliokaa katika Bunge hili, hajawahi kuiona bajeti iliyoshiba na yenye matumaini kama hii. Na mimi pamoja na umri wangu huu mdogo, toka nimeanza kupata ule ufahamu kuweza kujua redio, *tv* na kuweza kusoma na kuandika sijawahi kuiona bajeti iliyosheheni matumaini kama hii. Bajeti hii ni bajeti ya wananchi, bajeti hii inawagusa wakulima wote, wafugaji, wafanyabiashara wa kada zote na bajeti hii inawagusa wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba bajeti hii ni bajeti ya pili ya Serikali ya Awamu ya Tano ambayo imejipambanua kwamba inakwenda kuitengeneza Tanzania ya viwanda na kumuondoa Mtanzania angalau ifikapo mwaka 2025 tufike katika *level* ya kati ya uchumi. Kwa namna yoyote ukitizama bajeti hii, imefanikiwa kutujibu swali la siku zote la tafsiri ya maendeleo, maendeleo ni nini? Bajeti hii imetujibu *development should be people centered*. Kwa namna yoyote utakapoingalia inakuonyesha bajeti hii ni bajeti ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi bajeti hii imejikita katika kuwasaidia watu wa uchumi wa chini, uchumi wa kati, wafugaji, wakulima, wafanyabiashara na wawekezaji. Ili twende vizuri na tuelewane katika hili kuwaambia kwamba bajeti hii ni bajeti ya kihistoria, naomba niwapeleke kwenye mambo kumi muhimu yaliyopo kwenye bajeti hii. Kwa lugha nyingine naweza kuyaita *ten tenants. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, Taifa lolote unaweza kulipima kama lina matumaini kuhusu kesho baada ya miaka kumi na miaka 50 ijayo kwa namna gani inajikita kwenye miradi mizito ya vielelezo, miradi ya maendeleo. Bajeti hii imeanza pasipokuwa na shaka lolote kutekeleza miradi ya vielelezo zaidi ya saba*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kwanza ni ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge.* Ni watu tu ambao hawafikiri dunia inakwendaje wanaweza wakahoji hili. Kwa miaka yote tumelalamika kwamba reli ya kati kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma kwamba bidhaa zinakwenda shida, maendeleo hayawezekaniki, tumetoka sasa tunakwenda kwenye *standard gauge*. Dola bilioni 300 zimekwishatengwa na tayari zimekwenda kwenye kuandaa karakana na kufanya upembuzi yakinifu ili ndani ya hii miaka michache, mtu anatoka Dar es Salaam mpaka anafika Kigoma akiwa amelala usingizi, anasoma gazeti lake kwa muda wa saa saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuboreshwa kwa Shirika la Ndege Tanzania. Hili kuna watu hawalielewi, wakiambiwa Serikali imenunua ndege huwa haelewi. Unaponunua ndege hatuangalii mapato yanayopatikana kwa wewe kupanda ndege kutoa hapa kwenda Kigoma, Songea na sehemu nyingine. Tunaangalia vitu vingine vinavyosababisha kukua kwa uchumi lakini kwa sababu umetumia saa chache sana barabarani, uchumi unakua. Hii ni hatua kubwa sana ya nchi yoyote inayotaka kwenda kwenye uchumi wa kati lazima iimarishe shirika lake la ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa tatu, tumezungumzia sana suala la Mchuchuma na Liganga, hii imewekwa katika mpango huu. Tushukuru sana Serikali tumeipigia kelele sasa tunakwenda ile hoja mliyokuwa mnalalamika chuma sasa kinatoka Liganga na makaa ya mawe yatatoka Liganga. Utaratibu wa reli sasa haitakuwa ya kati tu, kwa chuma cha Liganga tunao uwezo wa kuuza chuma nje, tunao uwezo wa kutandaza reli kwenye Wilaya zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa nne ni ununuzi na ukarabati wa meli kwenye maziwa makuu. Juzi tulipokuwa tunaongelea hapa Wizara ya Uvuvi, ndugu yangu Ulega alisema hatutumii vizuri ile bahari kuu kwa sababu hatuna meli za kisasa zenye uwezo wa kuvua, sasa Serikali imeiona

hili na imeliweka. Sasa nashangaa watu wanaosema hawaoni basi yawezekana ni vipofu tuwasaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tano ni ule wa gesi kimiminika *(liquefied natural gas).* Hili ni jambo kubwa ambalo sasa litakwenda kujibu matatizo mengi. Ile gesi ikishafika tunaiboresha sasa itakaa kwenye mitungi ni hatua ya baadae hata yule aliyekuwa anatia mashaka mafuta ya taa yamepanda bei, huko sisi tunataka kutoka, mafuta ya taa kwanza yanaleta *air pollution*, ni adha na ukipika na chakula nacho kinanuka, tunataka tumtoe mtu huyo huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mama yangu ulinifundisha siwezi kukusema sana ila ili kuweka tu kumbukumbu sahihi, siyo sawa unaposema kuhusu mafuta ya taa. Hesabu zote za kiuchumi zinatuonyesha tunatoka kwenye mafuta ya taa tunakwenda kwenye gesi. Mwalimu wangu wataalam wanasema *you can not strengthen the weak by weakening the strong.* Hoja ya msingi ni kumfanya yule *weak* awe *strong* siyo kwa kumdhoofisha yule ambaye ni *strong.* Kupeleka bei ya mafuta kwa wale watu wenye magari hakumaanishi kuwa tunamfanya huyu asiyekuwa na uwezo awe *weak,* tunajaribu kumuimarisha kwa njia nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili katika mambo yangu yale kumi, hili lilikuwa la kwanza tu, la pili ni Kodi ya Majengo. Sheria ya Fedha ya mwaka 2016 ndiyo kwa mara ya kwanza iliyoipa mamlaka *TRA* kukusanya mapato kwenye majengo. Safari hii imefanya maboresho tu kwa sababu ilikuwa haieleweki watu wanakadiriwa vipi, Serikali imekuja sasa na ukomo, nyumba ya kawaida iwe shilingi 10,000, ya ghorofa shilingi 50,000, tatizo liko wapi hapa sasa? Unaona sasa tunataka tupate mapato katika njia inayoeleweka, kila nyumba itatoa Sh.10,000 kila ghorofa shilingi 50,000, Serikali inayotabirika katika maendeleo ndiyo inakuonyesha namna gani itatutoa hapa tulipo itupeleke sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wafugaji, Serikali imeondoa *VAT* kwenye mayai ya kutotolesha vifaranga *(fertilized eggs for incubation),* jambo hili ni kubwa sana.

Ndugu yangu Mwita pale atakuwa shahidi kule Kitunda, walishaacha sasa kuleta mayai pale mjini kwa sababu gharama za chakula na kutotolesha vifaranga ilikuwa kubwa kutokana na kodi hii. Kwa kuiondoa kodi hii sasa unamsaidia mtu wa kawaida wa chini, wale vijana na akina mama watakuwa wanafuga kuku na kutotolesha mayai. Hapa sasa ndiyo hatua ya kwanza ya kutengeneza viwanda vidogo vidogo vya kusindika nyama na ku-*process* mayai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni viwanda na uwekezaji. Serikali imeondoa *VAT* kwa uagizaji wa bidhaa za mitaji yaani *capital goods,* hili jambo linasaidia kwanza kuwa-*encourage* Watanzania wawe *export oriented.* Huwezi ukapata pesa za kigeni kama hau-*export* lakini vilevile tukumbuke *Tanzania it's a strategic area,* tuna-*control* hizi *land locked countries,* tukiwa na mfumo mzuri wa kuondoa hizi kodi na kupeleka malighafi nje...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, naendelea kuwakumbusha upande huu naona watu wanaendelea kutumia vitabu kupiga makofi, piga tu kwenye kitabu chako lakini tumia mikono yako hivi. Ndiyo Kanuni za Kibunge na Kanuni zetu. Tunaendelea na Mheshimiwa Josephat Kandege atafuatiwa na Mheshimiwa Ntimizi halafu nitahamia tena huku.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi leo kupata nafasi jioni hii ili kuweza kuchangia katika hotuba ya bajeti. Mengi yamesemwa na naomba niishukuru Serikali, nina kila sababu ya kuishukuru Serikali kwa sababu mawazo mengi ambayo yalitolewa na

Kamati ya Bajeti na kutolewa na Bunge yamezingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyopata fursa ya kuongea *ITV* nilisema hivi, kwa nchi zetu zinazoendelea, bajeti kama hii iliyoandaliwa utategemea iandaliwe kipindi ambacho nchi inaenda kufanya uchaguzi mwaka unaofuata. Hata hivyo, kwa Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli uchaguzi wala hatutarajii kwamba upo mwakani, kwa hiyo, ni bajeti ambayo inaenda kuwakomboa Watanzania kwa nia ya dhati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maboresho mengi tumetoa na Serikali imezingatia, naomba nisitumie nguvu katika kuchangia kwa sababu naamini Serikali ni sikivu. Naomba niboreshe baadhi ya maeneo machache ambayo yapo kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango ili waweze kuyatilia mkazo na marekebisho yaweze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo ambalo naomba nijikite kwa kuanzia ni kuhusiana na *VAT* katika huduma uwindaji. Asilimia 18 inatozwa pale ambapo muwindaji anaenda kulipia *block (block fee)* eti nayo anatozwa *VAT.* La kushangaza zaidi hata pale anapolazimika kusafirisha *trophy* kupeleka nje ambayo amekatia leseni na ameruhusiwa awinde, wakati kwa mujibu wa sheria *VAT on export* hakuna kitu kama hicho, lakini kwa mwindaji tunataka atozwe asilimia 18, naomba Serikali mkatizame. Kama hiyo haitoshi hata pale ambapo ametozwa *penalty* lakini katika *penalty* hiyo nayo tunaweka na 18% *VAT,* sheria hiyo haipo. Kwa hiyo, naomba Serikali kwa ujumla wakalitizame kuanzia mwanzo mpaka mwisho ili marekebisho yafanyike twende kwa mujibu wa sheria inavyotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusiana na taasisi na mashirika ya umma. Ni takwa la kisheria kwamba wanatakiwa kuchangia asilimia 15 ya *growth revenue* kwenda Serikali Kuu. Kinachoshangaza, kwa mujibu wa Sheria ya Kodi kwa maana ya *Income Tax,* anapoandaa hesabu zake anatakiwa aoneshe kile kiasi ambacho alishatoa

kupeleka Serikalini lakini jambo la ajabu ni kwamba akiandaa hesabu ikifika *TRA* wanasema hawatambui, kama vile Serikali haijapata hata senti tano, wanairudisha kama siuo *allowable deduction,* kwa hiyo, kunakuwa na *double taxation.* Naomba Serikali mkalitazame hili, halina tija kwa mashirika yetu, inaua mashirika yetu bila sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hii hoja ya shilingi 40 ya tozo ambayo Kamati na naamini na Wabunge wote hata upande wa pili wanalitamani kimya kimya kwa sababu inakwenda kupunguza kero kubwa ya maji na hasa maji vijijini. Kwenye Kamati yetu ya Bajeti tumependekeza kwamba asilimia 70 ya pesa hizi ambazo zinakwenda kupatikana zikatibu kero ya maji vijijini na asilimia 30 ndiyo iende kutibu kero ya maji mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini hili halina mjadala, naamini hata upande wa pili wakiulizwa watapigia kura ya kuunga mkono suala hili. Kwa sababu hakuna hata mmoja, awe anatoka mjini, awe anatoka vijijini, tatizo la maji ni tatizo la kitaifa. Kwa hiyo, tukubaliane ndugu zangu kwamba ni vizuri katika hili tukaungana, hii tozo ambayo inapatikana ikatatue kero ya maji vijijini na mijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niiombe Serikali, wakati Mheshimiwa Waziri anawasilisha bajeti yake amesema kwamba anaondoa *road license* lakini katika ile *sticker* ya *road license* kuna kiasi fulani cha *fire extinguisher* aje atuambie, nayo imeondolewa? Maana kama haijaondolewa itakuwa ni kero, kwa sababu ninyi wenzangu wote mashahidi, hakuna hata siku moja ambapo eti hiyo *fire extinguisher* imeweza kusaidia, sanasana ni *stickers* tu zinatolewa inakuwa ulaji. Naomba nayo iondolewe, ni kero kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama hiyo haitoshi, kuna zile *stickers* za Wiki ya Nenda kwa Usalama. Lengo lilikuwa zuri kwamba tunataka magari ambayo yanatembea barabarani yawe ni yale magari ambayo ni *road worthy,* lakini sisi sote ni mashahidi, tumekuwa tukiuziwa *stickers* gari

hazikaguliwi. Kwa hiyo, nayo ni vizuri iondoke, ni kero, haitusaidii chochote, inasaidia wachache ambao ni wajanja wajanja, ikiondoka hiyo itakuwa imetusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika wasilisho la Mheshimiwa Waziri anasema kwamba *excise duty* ya ngano inapungua kutoka asilimia 35 kwenda asilimia kumi. Naomba tuulizane Mheshimiwa Waziri, hali ya sasa ikoje, kwa sheria ilivyo leo hii asilimia 10 hiyo anatozwa yule ambaye anaagiza ngano anakuja kuisaga tukijua kwamba wananchi watanufaika. Sasa kwa kuondoa kwa hawa wengine *brokers,* huisaidii Serikali wala humsaidii mwananchi wa kawaida. Ni kama vile tunataka wawepo *middlemen* ambao watakuwa wanaagiza ngano halafu wanakuja wanawauzia wenye viwanda waende kusaga. Mheshimiwa Waziri, naomba ulitizame, ni bora hiyo ibaki vilevile iwe chanzo cha mapato ila wale ambao wanaagiza kwa ajili ya kuja kusaga tukijua kwamba bei ya mkate itakuwa imeshuka itatusaidia lakini hiki chanzo kiendelee kwa sababu kinasaidia katika kuongeza mapato kwa upande wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linalosemwa kuhusu suala la *property tax,* ni vizuri tukakumbushana Waheshimiwa Wabunge, sisi sote tulikuwa tunalalamika kwamba chanzo kisichotokana na kodi makusanyo yake yamekuwa hafifu, tukakubaliana kwamba ni vizuri kama *TRA* wanakusanya hawakusanyi pesa hiyo iende Mfuko Mkuu, ni wajibu wa *TRA* ikikusanya pesa hizo zizirudie Halmashauri maana ndiyo wenye hayo majengo, ndiyo msingi wake upo hapo, lakini si kwamba eti Serikali Kuu ichukue kama ni chanzo chake, la hasha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tukubaliane tangu mwanzo kwamba pesa hiyo ikikusanywa inatakiwa irudi kwenye Halmashauri husika ili yale majukumu ambayo Halmashauri inatakiwa iyafanye yaendelee kufanywa na Halmashauri. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri hili upigie mstari kabisa isije ikaonekana kwamba sasa tunanyang'anya vyanzo upande wa Serikali za Mitaa kwenda Serikali Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la ushuru wa mazao, nimefarijika sana ilikuwa kutoka asilimia tano sasa inakwenda asilimia tatu. Naomba nisisitize, asilimia tatu hii iwe kwa mazao yote, isiwe kwamba eti kuna mazao ya biashara na mazao ya chakula maana itakuwa ni vigumu sana kuweza kujua ni wakati gani mahindi yanakuwa zao la biashara na wakati gani mahindi yanakuwa zao la chakula, hapo tutakuwa tunatengeneza mwanya wa rushwa bila sababu. Kwa hiyo, kimsingi ni vizuri hicho kiasi kikapungua lakini iwe sawa kwa ama mazao ya biashara au mazao ya chakula na tafsiri iko rahisi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Waheshimiwa wengine wanasema kwamba tunaipunguzia Halmashauri uwezo wa kukusanya, lakini ukiipunguzia Halmashauri uwezo wa kukusanya hicho ambacho kingekusanywa na Halmashauri kikawa kwa mwananchi wa kawaida, mwananchi huyu wa kawaida maana yake *disposable income* inakuwa imeongezeka, atakwenda kufanya *spending* katika mambo mengine na kodi yetu tutaipata. Ni nani asiyependa wananchi wetu wakawa wana pesa mifukoni mwao? Kwa hiyo, ni wazo jema mimi naliunga mkono sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni shahidi kwamba hatukulala mpaka saa nane na naamini na mengine tutaendelea kushauriana na Serikali, yale ambayo hawakuyachukua wataendelea kuyachukua kwa sababu naamini Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla ni wasikivu na naamini na wenzetu wa upande wa pili hakuna sababu ya kuja na *pages* 200, tuje na *pages* chache...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kandege kwa mchango wako.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Musa Ntimizi.

**MHE. MUSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia mawazo ya Wanaigalula katika bajeti hii ambayo ni nzuri, ambayo Wanaigalula wanaiunga mkono kwa sababu kwa asilimia kubwa inatatua matatizo na mambo ambayo wanadhani ni shida kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri ambayo wameifanya katika bajeti ya mwaka huu. Yako mambo ambayo tuliyashauri mwaka jana tulidhani hayajafanyiwa kazi kumbe walikuwa wanajipa muda wa kutafakari na sasa wameyaweka na kuyafanyia kazi katika bajeti ya mwaka huu. Mimi nataka niungane na wale wote wanaoipongeza bajeti hii kwa sababu yale yote yaliyozungumzwa katika bajeti ya mwaka huu mengi tuliyashauri katika bajeti ya mwaka jana na mengi tumekuwa tukiyashauri siku hadi siku. Nina hakika kwa asilimia kubwa yamefanyiwa kazi na yamewekwa katika bajeti ya mwaka huu. Natoa pongezi kubwa sana kwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi nzuri mnayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mwizi wa fadhila nisipompongeza Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ambaye ni Rais msikivu. Wamekaa pamoja na Waziri wa Fedha wamekubaliana na wametuletea bajeti ambayo nina uhakika kama itatekelezwa vizuri itakwenda kutatua kero na changamoto nyingi tulizonazo katika majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ni nzuri lakini yapo mambo ambayo tunaendelea kuishauri Serikali yetu iyafanyie kazi ili kuendelea kuiboresha zaidi bajeti yetu iwe nzuri zaidi. Kwanza kabisa nianze kuzungumzia reli. Naipongeza Serikali kwa uamuzi wa kujenga *standard gauge,* reli ambayo itatusaidia sisi wana-Igalula na mikoa mingine katika usafiri na usafirishaji wa mazao yetu. Tulikuwa tunasafirisha tumbaku

yetu kwa malori kwa gharama kubwa, sasa nina uhakika *standard gauge* ikikamilika usafiri wa tumbaku yetu toka Tabora kuja sokoni utakuwa ni wa rahisi na kutusaidia kuongeza faida katika zao letu la tumbaku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maendeleo yoyote changamoto lazima ziwepo. Wakati tunaanza kujenga *standard gauge,* kuna wananchi maeneo mengi wanalalamika wanaanza kuvunjiwa nyumba zao bila utaratibu. Niombe Wizara husika ikakae na wananchi wetu katika maeneo itakapopita reli hii ambapo wananchi wote wanakubali ujenzi wake ili waelimishwe wafanye uhakiki mzuri ili wale wanaostahili kuvunjiwa maeneo wavunjiwe wakiwa wanajua taratibu zimekamilika na ziko sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu barabara. Naomba niipongeze Serikali baada ya kusikia kilio chetu sisi wana-Igalula cha barabara ya Chaya - Nyahua, tumepata shilingi bilioni 110 kutoka *Kuwait Fund* itakayoenda kujenga barabara ile. Barabara hii kwa asilimia 100 inapita katika Jimbo la Igalula lakini inaunganisha Mikoa ya Tabora na Singida, Tabora na Kigoma na Tabora na Katavi, barabara hii ni muhimu sana. Unapozungumzia kipande hiki cha barabara cha kilometa 89 kitasaidia sana usafiri na usafirishaji katika maeneo ya mikoa hii niliyoitaja lakini sisi wana-Igalula tutanufaika kwa asilimia kubwa kwa sababu asilimia 100 barabara hii inapita katika Jimbo la Igalula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukipata kikubwa na kidogo pia unaomba, tuna barabara tuliomba ipandishwe hadhi ya kutoka Buhekela - Miswaki - Loya ambapo tuna kilimo kikubwa cha mpunga. Tunaposema wananchi wetu wawe wakulima wazuri, tusipowatengenezea miundombinu iliyo bora ya kufanya wapate faida ya mazao yao tunakuwa hatujawasaidia. Barabara hii haipitiki kipindi kikubwa kwa sababu ni mbovu. Tuliomba ipandishwe hadhi ili wananchi wa kule wanaolima mpunga waweze kupata faida kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la maji. Sisi Mkoa wa Tabora tunaipongeza tena Serikali kwa uamuzi wake wa kuyatoa maji toka Ziwa Victoria kuyaleta katika Mkoa wetu wa Tabora. Najua kuna baadhi ya maeneo mradi huu wa Ziwa Victoria hautafika ikiwemo Urambo, Kaliua, Ulyankulu na sisi Igalula. Najua ipo mipango inafanyika kupata maji ya uhakika katika maeneo haya lakini kipindi hiki ambacho tunasubiri mipango hiyo, tunaomba taratibu za kupata maji ikiwemo kuchimbiwa visima virefu, mabwawa ili tuweze kupata maji ya uhakika katika baadhi ya maeneo yetu ifanyike. Sisi Igalula tuliahidiwa kujengewa bwawa kubwa katika Kata ya Goweko na Loya lakini mwaka wa fedha uliopita havikutekelezeka. Naomba katika mwaka huu wa fedha tuweze kusaidiwa kupata maji katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na mawazo ya Mheshimiwa Ndassa aliyesema zile shilingi 40 ziongezwe na shilingi 50 ya mwaka jana ziwe shilingi 90 zikatatue kero ya maji katika maeneo yetu. Bajeti kubwa ya mwaka jana ya Wizara ya Maji ya kutekeleza miradi mingi ya maendeleo ilitokana na shilingi 50 tuliyoipitisha sisi hapa ndani. Kama ikiongezwa shilingi 40 ile, nina uhakika miradi mingi ya maji katika maeneo yetu itakwenda kutekelezeka. Wale wanaopinga kuongezeka shilingi 40 nadhani hawawatakii mema wananchi wetu wanaopata taabu ya maji katika maeneo yetu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda nizungumzie kidogo suala la kilimo cha tumbaku, tunashukuru juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali yetu katika kutatua kero za tumbaku katika maeneo yetu. Unapozungumzia tumbaku ni uchumi wa wananchi wetu wa Igalula na Mkoa wa Tabora. Unapozungumzia tumbaku, ni uchumi wa nchi kwa sababu nchi inapata kodi kubwa katika zao la tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo yanatakiwa yaendelee kufanyiwa kazi ikiwemo soko la tumbaku na tuondolewe *grades* mbalimbali katika zao la tumbaku ili iweze kupata bei nzuri, lakini kikubwa Serikali sasa ifikirie

kujenga kiwanda cha tumbaku katika Mkoa wa Tabora linapozalishwa zao hili la tumbaku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hotuba ni nzuri, naomba na mimi niungane na wale wote wanaosema bajeti hii ni nzuri. Tunachoshauri sasa yakatekelezwe yale yote ambayo yameahidiwa katika bajeti hii ikiwemo na mawazo sasa ya Waheshimiwa Wabunge ambayo wanaongezea katika kuiboresha zaidi bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ntimizi kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, nitumie fursa hii kutambua wageni na tuna wageni muhimu sana leo hapa ambao ni wageni wa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Profesa Joyce Lazaro Ndalichako ambao ni wanafunzi waliofanya vizuri katika mitihani yao ya kumaliza masomo katika ngazi mbalimbali kwa mwaka 2016. Wanafunzi hawa wameambatana na baadhi ya walimu wao na wazazi lakini pia na wanafunzi wenzao ambao wamewasindikiza kwenye tukio hili la kutambulishwa humu Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, naomba wanafunzi ninapowataja mnasimama, kwa upande wa watahiniwa kumi bora kitaifa kwa mitihani ya kumaliza elimu ya msingi mwaka 2016 ni kama ifuatavyo; Ndugu Japhet Elia Stephano, Shule ya Kwema Mkoani Shinyanga; Ndugu Jamal Ally Athuman, Kwema Shinyanga; Ndugu Enock Daud Bundala, Kwema Mkoa wa Shinyanga; Ndugu Justina Pius Gerald, Tusiime Dar es Salaam; Ndugu Shabani Hussein Mavunde, Tusiime Dar es Salaam; Ndugu Jacob Thadeous Wagine, Kwema Shinyanga, Ndugu Isaac John Isaac, Kwema Shinyanga; Ndugu Daniel Manase Kitundu, Kwema Shinyanga; Ndugu Benjamin Benevenuto, Kwema Shinyanga na Ndugu Azad Feruz Ayayullah, Kaizirege Kagera. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao watahiniwa kumi bora kitaifa kwa mitihani ya kumaliza elimu ya sekondari, tunaanza na Ndugu Alfred Shauri – *Feza Boys,* Dar es Salaam; Ndugu Cynthia Nehemiah Mchechu - *St. Francis Girls* Mbeya; Ndugu Erick Mamuya - *Marian Boys* Pwani; Ndugu Jigna Kalpesh Chavda - *St. Mary Goreth* Kilimanjaro; Ndugu Naomi Tundui - *Marian Girls* Pwani; Ndugu Victoria Alexender Changa - *St. Francis Girls* Mbeya; Ndugu Brian Johnson - *Marian Boys,* Pwani; Ndugu Esther Emmanuel Mndeme – *St. Mary's,* Mazinde Juu Tanga; Ndugu Ally Hassan Koti - ALGP Kilasara, Kilimanjaro na Ndugu Emmanuel Kajege - *Marian Boys,* Pwani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuna wanafunzi tisa waliopata zawadi za Kitaifa kwa kidato cha sita ambao ni Ndugu Hassani Bakari Gwaay – *Tabora Boys,* Tabora; Ndugu Mohamed Ally – *Feza Boys* Dar es Salaam; Ndugu Joshua Zumba – Uwata Mbeya; Ndugu Japhet S. Lawrence – Tusiime Dar es Salaam; Ndugu Juliana Elias Mwalupindi - Weruweru Kilimanjaro; Ndugu Arnold James – Umbwe Kilimanjaro; Ndugu Edith C. Msenga – *St. Mary's,* Mazinde Juu Tanga; Ndugu Boniface Edward Kajaba – *Manao Lutheran Junior Seminary* Mbeya na Ndugu Elikana Simo – Runzewe Mkoani Geita. *(Makofi)*

Walimu na wanafunzi tunawapongeza sana kwa heshima hiyo, kwa ushindi huo lakini kubwa zaidi ni kwa kubahatika kutangazwa humu Bungeni. Ni wazo zuri la Wizara, ni kama motisha kwa wengine pia katika siku zijazo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na michango Waheshimiwa Wabunge, sasa namtambua Mheshimiwa Susan Jerome Lyimo atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipatia fursa hii ili na mimi niweze kuchangia kwenye hoja muhimu sana ya bajeti kwa sababu bajeti ni suala la kisera na ndiyo sababu huwa tunakuja kuitungia Sheria ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme tu kwamba bajeti hii kwa kweli kama ambavyo wamesema ni ya kihistoria, kihistoria kwa maana gani? Wote tunajua kwamba Wabunge ni wawakilishi wa wananchi lakini jambo linalosikitisha wananchi hao wameachwa holela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwa misingi ifuatayo. Nimeona Wabunge wa CCM wakishangilia sana bajeti hii na kubwa wanalozungumzia ni suala la kuondolewa kwa kodi ya barabarani yaani *motor vehicle.* Hata hivyo, ukiangalia kimsingi *motor vehicle* ni vyombo vinavyotumia moto lakini leo mwananchi wa kawaida anayetumia mafuta ya taa, kibatari kijijini anatakiwa akatwe shilingi 40 kila anaponunua mafuta. Kuna Mheshimiwa mmoja hapa amezungumza akasema sasa hivi tunataka kuondokana na *air pollution* kwamba leo wazazi wetu waliotulea kwa vibatari kijijini tunawaona hawafai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme Serikali basi ingeondoa kwanza mafuta ya taa wahakikishe kwamba wananchi wanajengewa nyumba bora na wapinzani tumekuwa tukiongea muda mrefu kwamba vifaa vya ujenzi vipunguzwe ushuru ili wananchi wengi waweze kujenga nyumba bora na nyumba hizo ziweze sasa kuwekewa umeme, ziweze kuwekewa gesi. Leo mwananchi wa kawaida hata nyumba ya tembe anaenda kukatwa kodi. Inaelekea labda wengine tunatoka maeneo mengine tofauti kwamba hatujui wapiga kura wetu ni wa namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Ndassa ambaye najua ni *very senior* Mbunge humu ndani, anatuambia kwamba Mheshimiwa Shabiby amesema nauli hazitapanda, sasa najiuliza hivi Mheshimiwa Shabiby yeye ndiye mpangaji wa nauli au ni soko huru? Soko ndiyo lina *determine* kama nauli itapanda au siyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, *simple arithmetic,* basi lilikuwa linalipa shilingi 300,000 kwa mwaka hiyo *motor vehicle* leo basi linalotumia lita 400 kutoka *let say* Mara mpaka Dar es Salaam ina maana lita hizo 400 akiongeza

shilingi 40 kwa kila lita atalipa shilingi 16,000. Ina maana kwa mwezi mmoja tu ni shilingi 480,000, kwa mwaka gari linaloenda na kurudi ni zaidi ya shilingi milioni tano. Ndiyo sababu Serikali imeonyesha wazi kwamba watapata faida. Kwa hiyo, hili suala kwamba wenye magari mabovu watayaleta barabarani siyo hoja kwa sababu haiwezekani watu wote wenye magari mimi naamini wana uwezo hatuwezi ku-*justify* sisi wenye magari kuongeza shilingi 40 kwa kuwatesa wale ambao hawana magari na hawategemei hata siku moja kununua gari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumeambiwa na Mheshimiwa Ndassa sijui kama yupo amesema kwamba tusome

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Taarifa.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Taarifa ya nini?

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Lyimo kaa kidogo kwa taarifa, Mheshimiwa Kandege taarifa.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimuongezee taarifa ili wakati anachangia nalo aliweke. Sisi ni mashuhuda kwamba bei ya mafuta ilishuka kufika shilingi 1,400 na hakuna nauli iliyoshuka na wala pesa ambayo ilitakiwa isaidie kwenda kutatua tatizo la maji hatukuiona. Kwa hiyo, ni vizuri akaunganisha na hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lyimo unasemaje na taarifa hiyo?

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza siipokei na kwamba ananipotezea muda tu. Mimi nazungumzia suala la kupanda sijazungumzia suala la kushuka, kwa hiyo, aendelee na Umakamu wake kama ameshindwa kuweka bajeti yake vizuri atulie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niende kwenye hoja yangu ya pili, Mheshimiwa Ndassa amezungumza hapa suala la kwamba wapinzani hatusomi vizuri, hatusomi *between lines* nikategemea anatuletea *facts* ni mambo gani ambayo ameona katika bajeti yetu hatujazingatia. Nataka kuwaambia tu kwamba pamoja na kwamba Serikali ina wataalam wa kutosha, sisi wapinzani tumegundua kwamba vitabu vyao vyote vina makosa. Pamoja na kuwa na wataalam wengi wenye *Ph.D* tunaona vitabu *Volume I, II, III and IV* ukija ku-*totalize* ni trilioni 23, ukija kwenye matumizi ni trilioni 26.9, ukija kwenye bajeti ya Waziri ni shilingi trilioni 31, sasa tunajiuliza kama mna wataalam wa kutosha kwa nini kuna hizi *variance* kubwa namna hii?

Kwa hiyo, nadhani Mheshimiwa Waziri utakapokuja utuambie inakuaje mapato na matumizi yanatofautiana lakini vilevile bajeti yako kuu uliyotusomea nayo ina tofauti kubwa ya trilioni tatu, mtuambie hizi ziko wapi, mmezitoa wapi. Kwa hiyo, nadhani mtusifu kwamba sisi wapinzani tumesoma kwa kina, tukachambua kwa kina na tukaja na *facts. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la *property tax* ambalo umelizungumza Mwenyekiti umesema kwamba *TRA* sasa wanazikusanya, lakini nataka niwaambie, naomba nitoe mfano wa *Kinondoni Municipality* ambayo mimi natoka. Mwaka 2015/2016 tulikuwa tumepanga kukusanya shilingi bilioni kumi na tukaweza kukusanya shilingi bilioni 7.5. Sasa hivi *TRA* wametuambia watatuletea shilingi bilioni mbili kwa mwaka huu unaoisha, lakini hawajaleta. Kwa hiyo, suala la *own source* ni la muhimu sana na tunasema kwamba *own source* ile *five percent* ya vijana na wanawake inatakiwa itoke mule sasa kama tunakausha hivi vyanzo vya mapato hawa wanawake na vijana wanapata wapi fedha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo hivyo tu, tunaongelea suala la *D by D,* kama tunagatua madaraka, tunataka Serikali za Mitaa nazo ziweze kufanya kazi sawasawa na kule ndiko kuna wananchi, leo tunakausha vyanzo vyao tunategemea nini? Nataka nijiulize, nadhani

labda Serikali tuelewane, kuna *Decentralization by Concentration* na *Decentralization by Devolution,* sasa tunaomba tujue sisi Tanzania ni *D by D* ipi tunayoitumia? Kwa sababu mimi ninayoiona tunafanya *Decentralization by Concentration* yaani tumeamua kupeleka mambo yote kule lakini hatupeleki fedha, tunanyang'anya tena kile kidogo ambacho walikuwa wanakipata, maana yake ni nini? Ndiyo sababu tunasema ni kweli hii bajeti ni ya ajabu, ni ya kihistoria sijui ni ya kijiografia nadhani tuongeze pia na ya jiografia siyo kihistoria tu kwa sababu inatisha yaani ni tishio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kumekuwa na hoja ya kujisifia sana kwa suala la *standard gauge.* Nasema mimi kama Mtanzania ni kweli ningependa sana tuwe na *standard gauge* nchi nzima lakini naomba nije kwenye mahesabu maana yake twende kwa mahesabu. Hii *standard gauge* wakati tumefunga mkataba na Wachina ilikuwa watujengee kilometa 2,190 kwa dola za Kimarekani bilioni 7.6. Hii ina maana kila kilometa moja ingekuwa ni sawa na dola za Kimarekani milioni 3.4. Leo mkataba ule haupo, tumeenda kwenye mkataba na Waturuki na Wareno kwamba Wareno hawa na Waturuki ambao wanatujengea hiyo kilometa 205 kwa dola za Kimarekani bilioni 1.2 maana yake ni nini? Maana yake ukigawanya, *simple mathematics* ni kwamba kila kilometa moja itagharimu dola za Marekani milioni 6. *(Makofi)*

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa *Engineer* Ngonyani, Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu wala Wizara yetu haijawahi kuingia mkataba wowote na Wachina.

**MWENYEKITI:** Haya, taarifa unaikubali, unaikataa?

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa iko kwenye maandishi, labda anazungumzia Serikali ya Awamu ya Tano, lakini nazungumzia Serikali iliwahi, hii taarifa niliyonayo labda nitaileta baadaye lakini natambua kwamba tayari kulikuwa na mkataba huo wa Wachina. Nilichotaka kuzungumza ni kwamba tulikuwa na mkataba zamani sasa hivi tunao huu wa Waturuki, hoja ya msingi, kama ilikuwa ni bilioni 3.4 leo ni bilioni sita maana yake ni kwamba tuna-*save* au tunapoteza? Hiyo ndiyo ilikuwa hoja yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee, nchi hii ni ya wakulima na wafanyakazi. Nimeangalia Kitabu cha Hali ya Uchumi ni jambo la kusikitisha. Ukiangalia suala la kilimo tumesema kwamba kilimo ndicho ambacho kinaweza kusaidia viwanda lakini leo hii ukisoma kitabu hiki cha Serikali yaani mazao ya biashara karibia yote isipokuwa kahawa na mkonge tu ndivyo ambavyo havijashuka kwa asilimia ya uzalishaji. Sasa kama mazao yetu yameshuka kwa kiwango kikubwa namna hiyo, tunategemea viwanda vyetu vitapata wapi malighafi kwa ajili ya viwanda hivyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wanasema kabisa bila hata aibu kwamba Tanzania eneo lake la umwagiliaji hatujafikia hata asilimia kumi ya umwagiliaji na wanatoa sababu kwamba kwa nini kilimo kimeshuka, wanasema ni kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi.

Mimi nilikuwa naomba niulize Serikali mabadiliko ya tabianchi yapo siku zote, ukame upo siku zote lakini Tanzania ni nchi ambayo ina vyanzo vikubwa vya maji. Leo nchi ya Misri inategemea maji kutoka katika Ziwa letu Victoria inakuwaje tunashindwa kutumia maji yetu wenyewe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, tuna vyanzo vingi mno vya mito lakini hatuvitumii. Leo kuna mvua kunakuwa na mafuriko kila mahali lakini tunashindwa ku-*tap* yale maji ili yaweze kusaidia kwenye kilimo chetu halafu tunasema asilimia zaidi ya 80 ya wanawake wa Tanzania ni

wakulima, wanalimaje kama hakuna maji? Halafu hii ni nchi wanasema ni ya viwanda, hivyo viwanda ni vya namna gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika yote wanatuambia kwenye kilimo wameweza kupeleka asilimia tatu tu ya bajeti halafu tunategemea nini katika nchi hii? Kwa hiyo, kwa kweli bado nasema hii bajeti ni ya kihistoria kwa sababu imeacha kabisa wananchi wake, imeacha kabisa kilimo, imeacha kabisa masuala ambayo yanawagusa wananchi moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la elimu. Ukiangalia kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, mara zote wamesema huu ni wakati wa kuboresha elimu yetu lakini ukiangalia hakuna uboreshaji wa aina yoyote. Huwezi kuwa na elimu bora kama huna ukaguzi. Wenyewe wamekiri katika kitabu hiki, ukurasa wa 260 kwamba katika shule zao hakuna ngazi hata moja wameweza kufikia asilimia 50. Kwa maana hiyo bado elimu yetu itaendelea kuporomoka wakati tunajua kipaumbele cha Tanzania ni elimu na bila elimu bora hatuwezi kufika mahali popote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo nataka kuzungumza ni suala la hosteli za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Sijaona limezungumzwa popote na nataka Mheshimiwa Waziri atakapokuja aje atuambie, tunataka kujua mabweni yanayoitwa *Magufuli Hostel* ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam yamejengwa kwa gharama za kiasi gani kwa sababu taarifa alizozitoa Mheshimiwa Waziri wa Elimu alisema ni shilingi milioni 500 kwa jengo la ghorofa nne jambo ambalo mimi binafsi sikubaliani nalo. Nilisema kama ni kweli ni shilingi milioni 500 niko tayari kutoa shilingi milioni tano...*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siungi hoja hii mkono. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso atafuatiwa na Mheshimiwa Catherine Nyakao Ruge.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja ambayo imewasilishwa na Serikali hapa Bungeni. Kwanza naunga mkono maoni ya Kambi ya Upinzani ambayo yamechambua na kutoa mapendekezo mengi. Hapa ndani ya Bunge upande wa pili mmekuwa na mtazamo wa kuona kwamba hatushauri lakini kuna ushauri mwingi sana umetolewa na mapendekezo mengi, naamini Serikali mtaichukua na kuifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kutoa maoni yangu kuhusu utekelezaji wa bajeti ambayo tunaimalizia. Bajeti ya mwaka 2016/2017 tulipitisha shilingi trilioni 29 kama bajeti ya jumla lakini katika hizo shilingi trilioni 29 mpaka tunapoongea ni takribani asilimia 38 tu ya fedha zote ndiyo imeenda kwenye miradi ya maendeleo. Katika fedha hizi za miradi ya maendeleo ambayo Serikali mmepeleka ni kama ifuatavyo kwa ufupi kwa mujibu wa kitabu cha Waziri. Ujenzi na ukarabati wa barabara imepelekwa shilingi bilioni 675, miradi ya uzalishaji wa umeme shilingi bilioni 441, malipo ya awali ya ujenzi wa reli shilingi bilioni 300, usambazaji wa maji vijijini shilingi bilioni 186 na huduma za afya ni shilingi bilioni 170.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunajiuliza hata hizi fedha tu za miradi ya maendeleo ambayo imepelekwa kwa asilimia chache kiasi hiki, zile ambazo ni muhimu kwa afya za Watanzania ikiwemo afya, maji imepelekwa kidogo ukilinganisha na hizo nyingine za ujenzi na ukarabati wa barabara. Kwa hiyo, unaona kabisa hata umuhimu wa kuwapa Watanzania hizi huduma muhimu za maji na afya haupo na wala hazipewi kipaumbele.

Kwa hiyo, Waziri sasa hivi tunaposema hata hii pia hamtaweza kutekeleza tunamaanisha kwa sababu ya maneno yenu ambayo mmeyaandika humu kwenye hivi vitabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ya 2017/2018 ambayo sasa tunaitarajia kuanza, mnakisia maoteo ya bajeti itakuwa shilingi trilioni 31.7. Kama hii tunayoimaliza ya shilingi trilioni 29 haijatekelezwa hata kwa asilimia hiyo, je, hii tunayoiendea itatekelezwa? Mnawahadaa Watanzania kwa kuwaambia kwamba hii bajeti haijawahi kutokea, ni bajeti ya karne, mimi naamini ni kweli itakuja kuwaumiza Watanznaia kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati mnafanya bajeti hii kufikia shilingi trilioni 31 maana yake bajeti hii ni shirikishi kuanzia Serikali za Mitaa, watu wamepanga kwa mfumo wa *O&OD,* wakaibua, wakapanga, tukapitisha kwenye Halmashauri zetu, zikapita kwenye *process* nzima za kibajeti mpaka Serikali mkaja Bungeni mkasema kwamba bajeti ni shilingi trilioni 31. Sasa muone mnavyojikanganya, hii shilingi trilioni 31 ni pamoja na mapato ya ndani ya Serikali za Mitaa kwa sababu bajeti imeanzia kule chini. Halmashauri zetu zimesema zitakusanya ushuru mbalimbali kama mapato ya ndani baadaye mkafanya *compilation* mkatuletea bajeti ya shilingi trilioni 31 lakini mnatuletea bajeti ya shilingi trilioni 31 huku nyuma mnafuta vyanzo vingi vya Serikali za Mitaa ambavyo tayari mmeshaweka kwenye bajeti yenu. Mheshimiwa Waziri hiki unachokisema shilingi trilioni 31 hautakaa utekeleze kwa sababu umesahau vyanzo vingine umevifuta wakati viko kwenye bajeti ya Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo unatuambia bajeti zimefutwa, kwanza kuanzia miaka ya 2000-2010 Serikali mlifanya maboresho ya Serikali za Mitaa kwa kuziboresha kwa kuweka mfumo ya *O&OD,* mkasema mnagatua madaraka, mnaziachia Serikali za Mitaa ziwe na madaraka kamili, zikusanye mapato yake, zijiendeshe, leo mmegeuka baadhi ya mapato mnayachukua, mengine mnayafuta bila kuzishirikisha Serikali za Mitaa, hamtambui umuhimu wa Serikali za Mitaa? Mheshimiwa Waziri Serikali za Mitaa ziko kwa mujibu wa Katiba ya nchi kwanza mnavunja hata hii Katiba ya nchi. Leo umekuja unatuambia umefuta ushuru wa huduma *(service levy),* Halmashauri zetu nyingi jamani

zinategemea ushuru wa hizi *guest house* na zimeshaweka kwenye bajeti yake. Leo unafuta ada ya machinjio, Halmashauri zetu ndiyo zinategemea ipate hizo ada, umefuta ada ya makanyagio minadani Halmashauri nyingi za vijijini ndiyo zinategema hii ada, umeondoa kodi ya mabango umeichukua umepeleka *TRA* halafu unasema utazirudisha, hamrudishagi mnatudanganya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnasema mmepunguza ushuru wa mazao kutoka asilimia tano mpaka asilimia mbili kama ni mazao ya chakula na biashara lakini Mheshimiwa Waziri unasahau kwamba Halmashauri zetu tayari zilishaweka fedha hizi kwenye bajeti yao kwa nini mnawadanganya Watanzania? Halafu nitashangaa sana Waheshimiwa Wabunge wa CCM mkiendelea kusema mnaunga mkono hoja, Halmashauri zenu mtaona tukianza mwaka wa fedha hazitakuwa na fedha kwa sababu vyanzo vingi vimefutwa na Serikali Kuu na tayari walishaweka kwenye bajeti zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri mnaenda kuua Serikali za Mitaa au basi mseme kwamba Serikali za Mitaa hazipo tena, mfanye vitu vyote. Mmekuwa mkiahidi mara zote kwamba mtarudisha hizo fedha na hamjawahi kurudisha. Mheshimiwa Susan Lyimo amesema hapa Kodi ya Majengo tu, mliahidi mtarudisha hamrudishi hata senti tano. Sasa Serikali za Mitaa zitawezaje kwenda kujitegemea na kufanya shughuli zake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie Kodi ya Majengo. Serikali ya Awamu ya Tano mlichukua kodi hii ya majengo mkasema *TRA* inakusanya. Juzi niliuliza swali la nyongeza hapa Bungeni kwa Mheshimiwa Waziri Simbachawene, nikataka kujua kauli ya Serikali ni majengo yapi hasa ambayo yanatozwa kodi hii kwa sababu kwenye Wilaya zetu mpaka nyumba za tembe, nyumba za udongo zinatozwa kodi hii. Mheshimiwa Simbachawene akanijibu hapa akasema majengo yatakayotozwa kodi ni yale yanayotengeneza faida kwa maana ya nyumba zinazofanya biashara. Mheshimiwa Waziri wa Fedha ukasimama

ukaniambia kuwa subiri bajeti yangu tutasoma, sasa hii bajeti yako ukurasa wa 48 inasema hivi; "Serikali itatoza Kodi ya Majengo kwa nyumba zote kwa viwango vitakavyopangwa na Waziri na Fedha na Mipango. Nyumba ambazo hazijafanyiwa uthamini zitatozwa kwa kiwango maalum *(flat rate)* cha shilingi 10,000 kwa nyumba na shilingi 50,000 kwa nyumba za ghorofa kwa kila ghorofa." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni zile ambazo hazijafanyiwa uthamini, kati ya shilingi 10,000 mpaka shilingi 50,000, acha zile zingine ambazo zitafanyiwa uthamini. Mheshimiwa Waziri hamuoni ninyi wenyewe mnajikangaya kwenye kauli zetu? Mheshimiwa Simbachawene amesema ni zile ambazo zinaingiza faida, akasema unaweza kwenda vijijini ukakuta mtu ana *guest house* na kadhalika huyo sawa atozwe kodi lakini wewe unasema nyumba zote, maana yake unasema hata za tembe nazo zitozwe kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu mnasema hii ni bajeti ya kuwakomboa Watanzania au kuwanyonya Watanzania? Mnathubutu kusema kwamba hii bajeti haijawahi kutokea ni bajeti ya karne, hii haiwezekani hata kidogo. Nitawaomba sana Waheshimiwa Wabunge wa CCM mkasome tena upya hii bajeti yenu ambayo mnasema eti inaenda kumkomboa Mtanzania wakati siyo kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la *Road License.* Wamepongeza sana hapa Wabunge wenzetu wa upande wa pili lakini tunajiuliza hivi ni Watanzania wangapi kati ya Watanzania milioni 40 ambao wana *own* magari? Inawezekana ni asilimia tano ya Watanzania wote, sasa asilimia tano ya Watanzania wote hawa leo mmewaondolea *Road License* ambayo watalipa kwa mwaka, mnasema mnapeleka kodi hii kwenda kutozwa kwa shilingi 40 kwa kila lita moja ya mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunafahamu ukiweka ongezeko lolote kidogo kwenye kila lita ya mafuta nchi hii, kila kitu kinapanda bei. Kwa sababu mafuta yanahusiana moja kwa moja na masuala mengine, utakuta bidhaa

zinapanda sokoni, ukisafirisha mazao bei inapanda na kila kitu. Sasa kwa nini tuwaadhibu Watanzania wengine walio wengi ambao hawamiliki vyombo vya moto kwa sababu hawalipii *Road License* halafu tunawaacha hawa asilimia 5 tu tunawapa msamaha huu wakati itawagharibu Watanzania walio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Serikali ya Awamu ya Nne ya JK...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana muda wako ndiyo huo. Tunaendelea na Mheshimiwa Catherine Nyakao Ruge.

**MHE. CATHERINE N. RUGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Bajeti Kuu ya mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Kambi Rasmi ya Upinzani kwa hotuba nzuri. Niiombe Serikali iweze kuchukua muda kusoma hotuba hii na kuangalia mambo mazuri ambayo tumeishauri ili waweze kuifanyia kazi kwa mustakabali wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba hii nitajikita kwenye mambo makuu matano. Bajeti hii imekuja wakati kama Taifa tukiwa na changamoto nyingi, mojawapo ikiwa ni ukame ambao umesababisha njaa katika maeneo mbalimbali nchini lakini pia kuyumba na kufungwa kwa biashara nyingi ambapo zimeathiri uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kufungwa na kuyumba kwa biashara nyingi nchini mwaka 2016/2017. Wakati Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango akiwasilisha hotuba ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2016/2017 alikiri katika kipindi cha mwezi Agosti na Oktoba, 2016 biashara 1,872 zilifungwa katika Mikoa miwili ya Dar es

Salaam na Arusha. Kama kwa kipindi cha miezi mitatu, biashara zaidi ya 1,000 zinaweza kufungwa basi ndani ya mwaka mzima ni zaidi ya biashara 7,488 zinaweza kufungwa kwa mikoa miwili tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii maana yake ni nini? Tunakwenda kupoteza ajira zaidi ya 15,000 kwa maana ya wastani wa wafanyakazi wawili katika kila biashara. Hii haiathiri wafanyakazi tu, lakini pia familia zao ambazo zinawategemea ukizingatia utamaduni wetu wa nchi yetu tunaishi kwa kutegemeana *(extended families). (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango alikuwa anatoa mifano ya jinsi gani kumekuwa na mdororo wa uchumi kwa nchi mbalimbali miaka mingi iliyopita. Nadhani ni vizuri Mheshimiwa Waziri ungejikita katika kuangalia sababu zilizofanya kufungwa kwa biashara hizi na suluhisho ili kuzuia na sisi tusije tukapata mdororo wa uchumi kama nchi ambazo ulizitolea mfano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara wengi wamekuwa wakilalamika kwamba kuyumba kwa biashara zao kumetokana na jinsi ambavyo *TRA* wamekuwa wakiwakadiria mapato. Niishauri Serikali iweze kuangalia ni jinsi gani inaweza kujenga mazingira rafiki ya wafanyabiashara kulipa kodi na kufanya biashara zao na isiwe chanzo cha wafanyabiashara kufunga biashara zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo napenda kuchangia ni *import and export.* Uchumi wa nchi yoyote hauwezi kukua kama mauzo ya biashara tunayozalisha nchini yanapungua siku hadi siku. Kwa mujibu wa Jarida la Uchumi la Benki Kuu ya Tanzania Machi, 2017, linaonyesha kwamba uwezo wetu wa kuuza bidhaa tunazozalisha nchini kwenda masoko ya nje umepungua kwa asilimia 34.6 ukilinganisha na kipindi kama hicho Machi, 2016. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo ambalo inabidi tulitazame kwa jicho la tatu na inabidi Serikali ijiulize maswali

yafuatayo. Je, ni kwa sababu bidhaa zetu hazina ubora wa kuweza kushindana na bidhaa za mataifa mengine au ni kwa sababu bidhaa tulizokuwa tunaziuza nje kwa mwaka 2016 na miaka iliyopita zimekosa masoko na hivyo basi inabidi tufikirie bidhaa mbadala ili tuweze kuendelea kuuza nje na kuongeza pato la Taifa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauzo ya nje yakiwa yameshuka kwa kiwango hicho nilichokitaja lakini pia manunuzi yamepanda kwa asilimia 33.5 kwa mwaka 2016/2017. Hii inanipa wasiwasi kwa kuwa tunaelekea Tanzania ya Viwanda kwamba tunanunua zaidi kuliko tunavyouza na hivyo kunakuwa na *unfavorable balance of payments.* Ili tuweze kuvilinda viwanda vyetu, inabidi tu-*promote* viwanda vya ndani lakini pia tuweze kuzalisha zaidi na kukidhi masoko ya ndani pia kuweza kuuza zaidi nje ya nchi ili tuweze kuongeza pesa za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu ambalo napenda kuzungumzia ni ajira. Suala hili limeendelea kuwa changamoto *especial* kwenye kipindi hiki cha Awamu ya Tano ambapo tumekuwa na wahitimu wengi wakiwa wanatoka vyuoni zaidi ya 10,000 kila mwaka, lakini Serikali hii imesitisha ajira pia kuna mazingira magumu ya kufanya biashara na hivyo kampuni nyingi zimepunguza wafanyakazi. Hii imekuwa ni changamoto *especial* kwa vijana, wamekuwa wakirandaranda mitaani na *degree* zao na vyeti vyao na kukosa matumaini ya kesho yao na kujiona kwamba wamepoteza muda kusoma *degree* zao za miaka mitatu mpaka mitano. Mheshimiwa Waziri nikuombe wakati unakuja kuhitimisha hotuba yako uwaeleze vijana wa Kitanzania katika bajeti ya mwaka 2017/2018 unakwenda kuajiri vijana wangapi katika Taifa hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ukisoma kitabu cha bajeti Serikali inaonyesha imelipa madeni ya shilingi bilioni 67.6. Naomba niipongeze Serikali kwa kulipa madeni hayo. Tatizo langu nataka kujua *definition* ya watumishi katika Taifa hili kwa sababu madeni haya yote ya shilingi bilioni 67.6 wamelipwa walimu. Nikuombe

Mheshimiwa Waziri, kuna watumishi wengine ambao siyo walimu wanadai *arrears* zao za mishahara, stahiki zao za kupanda vyeo, stahiki zao za uhamisho ili uweze kuwalipa kwa sababu kwenye kitabu chako hujaonesha kama kuna ongezeko lolote la mshahara. Hata ile *increment* ambayo ni kwa mujibu wa sheria wafanyakazi hawa hawajongezewa mishahara yao, namaanisha *statutory annual increment* kwa wafanyakazi ambayo ipo kwa mujibu wa *Labor Laws. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala la *PAYE* kwa maana ya *Pay As You Earn*. Wafanyakazi wamekuwa wakilipa kodi kwa asilimia 100 kwa sababu hawana *loopholes* za kukwepa hii kodi ukilinganisha na wafanyabiashara. Kama kuna watu wanalipa kodi *genuine* katika Taifa hili basi ni wafanyakazi, lakini wafanyakazi wanakatwa kodi kwenye *gross pay* na siyo *net pay.* Tukumbuke wafanyakazi pia wana matumizi au *expenses* mfano na wao pia wanalipa kodi, wanalipa nauli, wanakula chakula pamoja na matumizi mengine katika kutimiza wajibu wao wa kwenda kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfanyakazi ambaye yupo kwenye *band* ya milioni moja na zaidi analipa asilimia 25 au zaidi ya *PAYE*. Ukiangalia kwa makampuni au *corporate companies* ambao wanalipa *30 percent* kwa *net profit* kwa maana kuna *allowable expenses* nyingi ambazo wanakuwa hawazilipii kodi. Kwa hiyo, tunaona kuna *burden* kubwa sana kwa mfanyakazi wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe Mheshimiwa Waziri, kama Serikali haiwezi kupunguza *Pay As You Earn* basi *PAYE* ikatwe kwa *net pay* baada ya kutoa *housing allowance, food allowance, fuel allowance... (Makofi/Vigelegele)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kwa mujibu wa kanuni ambazo zinatuongoza, Kanuni ya 68(1) na (8) na Kanuni ya 64(1)(a), nilitaka kuliweka vizuri jambo ambalo limetokea leo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumbukumbu za kikao chako cha leo ziondoke hapa zikijua kwamba jambo lililosemwa na Mheshimwia Susan kwamba Tanzania ilishaingia mkataba halisi wa kujenga reli kwa gharama alizozisema haziko sawasawa, si kweli.

Kwa hiyo, naomba tunapoondoka hapa leo, *Hansard* iwe imerekodi kitu ambacho ni sahihi kilichosemwa na Naibu Waziri kwamba mkataba huo baina ya nchi ya Tanzania kwa maana ya Serikali yetu ya Tanzania na China hakuwa ni mkataba na tulikuwa hatujaingia mkataba na Serikali hiyo ya nchi ya China.

Kwa hiyo, ujenzi wa reli yetu unaendelea kwa utaratibu ambao umesemwa na Waziri mwenye dhamana ya Mipango na Fedha katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niliona tusiondoke hapa tukiwa tumefanya mapokeo ya mchango uliotolewa na Mheshimiwa Susan Lyimo, mchango halisi na taarifa halisi ambazo ziko sahihi ni zile ambazo ziko kwenye taarifa za Serikali kupitia Waziri wa Fedha na Mipango katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Jenista unachangia.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, umenitajia Kanuni ya 68 kwenye eneo la Mwongozo, bahati mbaya hukunifikisha huko lakini kwa uendeshaji bora wa shughuli zetu za Bunge na kwa kuzingatia Kanuni za Bunge, la kwanza hilo ulilolisema ni sahihi kwamba rekodi kwa upande wa Serikali mnataka ikae hivyo na lazima ikae hivyo, lakini kwa vile tunaendelea kujifunza Kanuni hizi Waheshimiwa Wabunge, wakati Mheshimiwa Susan Lyimo alipotamka hayo aliyodai, ilitakiwa tu aidha Waziri au Mbunge mwingine asimame Kuhusu Utaratibu na akajaribu kuelezea kwa kiwango cha kuweza kuliridhisha Bunge ukweli wa jambo hili ambalo ni zito kweli ili sasa *burden of proof* ihame baada ya maelezo hayo kwake sasa, atakiwe kuthibitisha hayo aliyoyasema. Huo ndiyo utaratibu ambao ningependa sana Waheshimiwa Wabunge tuwe tunazingatia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lakini *for the purpose* ya *record,* kwa sababu wote tunafahamu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haijawahi kuwekeana mkataba kwa ujenzi wa reli kati ya Serikali yetu na Jamhuri ya Watu wa China. Na mimi nilishtuka kidogo na nilitegemea upande huu na hasa upande wa Serikali kwamba wangeliona hili haraka na wakasema Utaratibu lakini baada ya maelezo hayo limekaa vizuri. Kama Mheshimiwa Lyimo unataka kuliendeleza kwa njia nyingine unaweza kuliendeleza ili tupate ukweli, mimi najua si kweli. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, sina matangazo hapa, niwashukuruni sana kwa kazi nzuri mliyofanya *so far,* mnafanya vizuri sana kwa michango ya pande zote. Tuisaidie Serikali kwa kutoa ushauri, tusilalamike

tu. Ndiyo maana kitabu cha Waziri wa Fedha mnaona anasema kuhusu mapendekezo ya Serikali, ninyi ndio Bunge, ninyi ndiyo mtakaoamua haya ni mapendekezo ya Serikali, kwa hiyo, tuisaidie Serikali katika michango yetu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.00 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 13 Juni, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*